# MAANDIKO *ya* AWALI

Ellen White



**Jumbe za kwanza za unabii walizopewa Waadventista wa Sabato**

Mwito kwa Mpendwa Msomaji

Jiunge na darasa la Uandishi, Ukalimani, Kutafsiri na Uhariri WhatsApp!

Hitaji letu kuu katika huduma hii ya Machapisho Uhamishoni ni Roho Mtakatifu , ushauri, na kisha Maombi yako msomaji. Kumbuka pia huduma zingine za machapisho kwa kila lugha, taifa na jamaa. Toka mtambo wa kuchapa ubuniwe kule Ujerumani mwaka 1456 na Johannes Gutenberg, Neno la Mungu limefikia mabilioni, ila bado kuna makundi 6000 hayajafikiwa, angalia Joshugaproject.org na habari za '1040 window' Sambaza Biblia popote ndiyo kauli mbiu ya muumini, Sambaza Neno la Mungu kote. Jiunge nasi katika kuandika vitabu vya kuboresha watu, kutafsiri, kuhakiki, na kuhariri. Ombi letu, ni unapochapa, usibadilishe chochote labda typos tu, tuwasilane kama kuna kosa la dhana au lugha! Sasa umefika wakati wa kuandika vitabu ambavyo vinaendana na muktadha wa rasilimali, mazingira na utamaduni wetu, kwani ulimwengu wa Kikristo sasa umehamia Afrika na Amerika ya Kusini. Ila hapa Kwetu Afrika Mashariki, sisi tumekuwa wazito kuandika kuhusiana na Mada mbalimbali ambazo zinaendana na mazingira yetu kwenye mada za afya, lishe, mahusiano kati ya wazazi au ndoa, kilimo na mazao yake, kulea na kukuza watoto, aina za biashara zinazoendelea, hali ya kisiasa na muumini, utendaji wa kufikia watu na kujenga makanisa, nyimbo zetu na noti zake, haya yote tunayasoma na kuyaiga kwenye vitabu na mitandano ya magharibi na ni mema tu, ila kama ulimwengu wa Kikristo umehamia kwetu, tunabidishwa pia kuwa waandishi kwasababu tunajua hali yetu katika kufikia wengine au kuboresha afya na jamii kuliko mtu mwingine. Kwanini nyimbo zetu nzuri zenye ujumbe mzito zisichaguliwe kwa makini, nyimbo zilizoimbwa miaka 50 hivi na kuwekwa kwenye vitabu na kisha watu waimbe. Tenzi tunazoimba za magharibi ni nzuri, ila nasi hapa tuna nyimbo nzuri na zinaendana na utamaduni wetu, kwanini tusijiongeze nasi, ili tuongeze kwenye maktaba yetu ya nyingine, vizuri vingine, tuna wataalamu wengi wa nyimbo sasa.

Na hata vitabu vya watoto, tunahitaji watu wanaopenda watoto kufanya kazi hii kwa kushirikiana. Pia umefika wakati wa 'Reverse Mission' Watu wa Amerika ya Kusini sasa ni wainjilisti kila mahali duniani, ikiwemo magharibi kama vile Ulaya, Marekani na hata, Asia, Australia, Mashariki ya kati na Afrika! Sisi Afrika tuna Wauminin wengi kuliko Amerika ya kusini, ila bado tunaona kwamba tupate waandishi kutoka nchi zenye Wakristo wachache kuliko sisi ambao hawaandiki kwa muktadha wa mazingira yetu na watoto wetu wanaona pengine wawe na vile vitu walivyo navyo nchi zingine au wawe na mwenendo kama ule, mfano mdogo sana utakuwa, wanafikiri sisi ni lazima tule kimchi, taco, panzit, empanada, manicotti, tortellini, sushi, falafel, je viwanda vyetu vinatengeneza vitu hivi? Kila chakula duniani kinacholimwa hufanana tu, ila jinsi ya kukitengeneza hupishana, Mwafrika atatumia ngano kupika ugali, Mhindi chapati, Mchina Noodle, Mzungu mkate au makaroni, nk. Ni kweli Kiswahili ilikuwa lugha ya kuzungumzwa na siyo ya Maandishi, ila wakati umefika maandishi kuongezwa kwenye mambo mazuri! Naelewa kwamba si utamaduni wetu kuandika, ila si utamaduni wetu kufanya mambo mengi ambayo sasa tunayafanya! Nategemea tunaiga mazuri tu! Na si kila kitabu tunachoandika ni lazima kiuzwe, vingine ni vya kusaidia jamii, wewe hautaweza kuuza kila kitu katika dunia hii kama unataka kufanya uinjilisti au kubariki watu, vingine vitakudodea. Watu husema utamaduni wa mtu mweusi ni kusaidia jamaa na ndugu zake wa damu tu na wala sio taasisi. Yawezekana ni kweli ila tuna la kujifunza kutoka kwa kila mwanadamu. Wenzetu wa Nigeria wameanza kuweka vitabu vyao vya kuboresha jamii mtandaoni ili watu wasome na kufaidika katika nyanja mbalimbali kama vile uchumba, maombi ya kuondoa laana kwenye familia nk. Joel Nanauka ni mfano mzuri katika Ulimwengu wa Kiswahili kwenye kuandika na kugawia watu ujuzi wake, tumevisoma vitabu vyake vizuri ambavyo ametubariki kwa mamilioni kwenye ujasiliamali nk. Ukiwa na chochote, hata ni kama senti mbili za Mjane, ujuzi, uwezeshaji wa aina fulani tafadhali usisite kutufikia na pia kama una ujuzi wa kuandika vitabu au kufundisha wengine kuandika vitabu, tuwasiliane, maana ulimwengu wa Kiswahili una umasikini wa ***Maandishi*** yaliyoandikwa kwa muktadha wa utamaduni, nyenzo, na maisha yetu ya kila siku, tunaomba mashauri pia kwa kutumia email UhamishoniUghaibuniMtandaoni@gmail.com au simu -1 -908-343-3022- Bwana atubariki sote ili tukae Ndani Yake

YESU Anarudi! Roho na Bibi arusi waseme, "Njoo!" Kila mtu asikiaye hili, na aseme, "Njoo!" Aliye na kiu na aje; anayependa, na achukue maji ya uzima bila malipo. Amina. Njoo BWANA!

SHUKRANI KWA MWENYEZI MUNGU

WA MBINGUNI

TABARUKU

Watafsiri, Waombezi, Wahariri, Washauri, Wahakiki, Wataalamu wa Teknolojia, na watia moyo wote -wapita njia, Marafiki na Ndugu, na hakika wasomaji wote, kwa vile najua mnaendelea kuombea huduma ya machapisho duniani kote, maana tunaambiwa 'Watu 1000 siku moja wataamini kwa ujumbe wa kimya'. Endeleeni kuombea huduma hii na zingine zote zinazosambaza machapisho kwa kila lugha, jamaa taifa

1. Grace Momadi-Masaka-New Jersey, Marekani

2. Daniel Nyangaresi Masaka-Kisii, Kenya

3. James Ongoso-Mara, Tanzania

4. Musa Budodi-Shinyanga, Tanzania

5. Elias Luwela-Sumbawanga, Tanzania

7. David Masaka -Pennslyvania, Marekani

8. John na Judi Mugane-Boston, Massachusets

9. Mbusi Mpagalushu- Bariadi, Tanzania

10. Kombeo ya Umishenari-Arusha, Tanzania

11. Isaac Msusu-Kigoma, Tanzania

12. Gerard Saakumi Nyafanga-Ukerewe, Tanzania

13. Ezekiel Ojwang-Tarime, Tanzania

14. Niwaeli Mburuja-Kilimanjaro Tanzania

15. Manase Kefa Omuga-Iringa, Tanzania

16.Gerard Saakumi Nyafanga-Rorya, Tanzania

17. Denis Momadi Masaka-Oklahoma, Tanzania

18. Nhandi Masunga, Iringa, Tanzania

19.Emmanuel Oola-Rorya, Tanzania

20.Sandra Barron, North Carolina, Marekani

21. Mohammed Mboi-Kisii, Kenya

Jiunge nasi Kuandika Vitabu na Kuhakiki, Asante sana

Huduma ya Vitabu Uhamishoni Ughaibuni Mtandaoni Majumbani

Tukishirikianana na Huduma ya 'Mungu Anajali' ya Dr Mtango na Mwinjilisti Oola

Tuko Njiani kuingia kwenye Youtube tukisaidiwa na Dr Mtango kwa Maelezo ya tiba sahili.

Samaritan Laymen Ministries of New Jersey

**Dibaji- (Takribani p.4 mpaka p.62)**

Ni nadra hasa katika nyakati hizi zinazobadilika-badilika kwamba kitabu kistahimili kuwepo kwa karne na huku kuhitajika kwake kukiwa kunaongezeka siku zote na kuwa miongoni mwa vitabu vinavyosomwa sana kwa upande wa vitabu vinavyohusika na masuala ya leo/sasa. Na bado hiyo ndio rekodi ya kufanikiwa sana ya kitabu *Early Writings* cha Ellen G. White. Katika miaka mingi hadi sasa, kumekuwapo na machapisho mengi ya matoleo mbalimbali. Hivi sasa kinaonekana katika toleo la tano la Kimarekani. **{EW iii1}**

Kitabu hiki kidogo maarufu kimeitwa kama inavyotakiwa, kikiwa ni uchapishaji upya wa vitabu vitatu vya kwanza vya Ellen G. White - *Christian Experience and Views of Mrs. E. G. White (Uzoefu wa Kikristo na Maoni ya Mama Ellen G. White)*, kilichochapishwa kwa mara ya kwanza mnamo mwaka 1851; A *Supplement to Experience and Views (Nyongeza ya Uzoefu na Maoni)*, kilichotolewa mnamo mwaka 1854; na *Spiritual Gifts (Karama za Roho)*, Gombo la kwanza, ambalo lililotolewa mwaka 1858. **{EW iii2}**

Umaarufu mpana na wa kudumu wa *Early Writings (Maandiko ya Awali)* unaweza kufikiriwa kuwa ni matokeo ya shauku isiyopungua ya kumiliki na kujifunza ujumbe wa kutaarifu na kutia moyo ambao ulikuja mapema kwa kanisa kupitia kipawa cha unabii.

Chapisho la pili la jambo hili lilifanyika mnamo mwaka 1882 katika magombo mawili—*Experience and Views (Uzoefu na Maoni)* na *Suppliment* (Nyongeza) inayojumuisha ya kwanza, na *Spiritual Gifts* (*Karama za* Roho) cha pili. Kama nyongeza fulani katika ya kwanza ya kazi hizi za awali mabadiliko madogo ya uhariri yaliyofanywa wakati ule, dibaji ya mchapishaji inasema: **{EW iii4}**

"Maelezo ya chini yanayotoa tarehe na maelezo, na kiambatisho kinachotoa ndoto mbili za kuvutia sana, ambazo zilitajwa lakini hazikusimuliwa katika kazi ya awali, hizi zitaongeza thamani ya toleo hili. Mbali na haya, hakuna mabadiliko kutoka katika kazi ya awali yaliyofanywa katika toleo la sasa, isipokuwa matumizi ya maneno mapya hapa na pale, au mabadiliko katika muundo wa sentensi, ili kuelezea wazo vizuri zaidi, na hakuna sehemu ya kazi ambayo imeachwa. Hakuna kivuli cha mabadiliko kilichofanywa katika wazo lolote au

mawazo ya kazi ya awali, na mabadiliko ya maneno yamefanywa mwandishi mwenyewe akiona, na kwa idhini yake kamili.” **{EW iii4}**

Vitabu hivi viwili vya rejea vilitolewa tena kama kitabu kimoja mnamo 1882 chini ya jina *Early Writings (Maandiko ya Awali)*. Mnamo 1906 herufi za kupigia chapa zilipangwa upya ili kufanya toleo la tatu la Amerika, ambalo limesambazwa sana, kukidhi mahitaji ambayo yanadumu kuongezeka. Kurasa za toleo hili zikawa ndio kiwango kwa ajili ya kazi zote za kurejelea na faharasa zilizofuatia kuchapishwa kuhusu maandiko ya Bibi White. **{EW iv1}**

Toleo la nne la *Early Writings (Maandiko ya Awali*) lilichapishwa mnamo mwaka 1945. Miaka arobaini ya uchapishaji na kuchapisha upya ilifanya iwe ni muhimu kuwa na pleti mpya ya uchapishaji (printing plates). Wakati herufi zilipobadilishwa maudhui yalishikiliwa ukurasa kwa ukurasa kulingana na toleo lililotangulia. Tahajia za kisasa na mitindo ya sasa za uakifishaji ilitumiwa na dibaji mpya ilipitia historia ya kitabu hiki kwa ufupi. **{EW iv2}**

Toleo hili la tano linajulikana kwa utangulizi wa

kihistoria, ulioongezwa ili kumpa msomaji ufahamu wa nyakati na mazingira ya sehemu mbalimbali za kitabu na kwa maelezo kadhaa ya kiambatisho yaliyotolewa kuelezea maneno na hali ambazo hazieleweki vizuri sasa kama ilivyokuwa wakati wa kuandikwa kwa kitabu hiki. Hakujakuwa na mabadiliko ya maandishi ya E. G. White wala mabadiliko katika uwekaji wa namba za kurasa kutoka toleo la nne ambalo toleo hili linafuatia, kwa hiyo linakubaliana *na Comprehensive Index to the Writings of Ellen G. White (Faharasa Pana kwa Maandishi ya Ellen G. White.)* **{EW iv3}**

Katika *Experience and Views (Uzoefu na Maoni)* imewasilishwa muhtasari wa kwanza wa wasifu wa Bi White, ukifuatilia kwa ufupi uzoefu wake kupitia vuguvugu la Ujio wa 1840-44. Kisha yanafuatia maono kadhaa ya awali, ambayo mengi yalikuwa yameonekana kwanza kuchapishwa katika karatasi pana au katika namna ya makala ya kwenye majarida. **{EW iv4}**

*Supplement (Nyongeza)* inaelezea virai fulani vya kazi ya awali ambayo haikueleweka vizuri au

iliyoeleweka vibaya, na inatoa ushauri wa ziada kwa Kanisa. Uchapishaji wake ulikitangulia kwa mwaka mmoja kijitabu cha kwanza kilicho na jina la Ushuhuda kwa Kanisa (Testimony for the Church).**{EW v1}**

*Spiritual Gifts (Karama za Roho)*, Kitabu cha 1, kikiwa ni kisa cha kwanza kilichochapishwa cha pambano linaloendelea kwa muda mrefu kati ya Kristo na malaika Zake na Shetani na malaika zake, kinathaminiwa sana kwa sababu ya maelezo yake ya wazi na kwa ufupisho wake, kikigusa tu mawazo au mambo muhimu zaidi. Katika miaka iliyofuata kisa hiki kifupi cha pambano kilikuzwa sana katika vitabu vinne vya *Roho ya Unabii (Spirit of Prophecy)*, vilivyochapishwa mnamo 1870-84. Baada ya kusambazwa kwa wingi, seti hii yenye vitabu vinne ilibadilishwa na ile inayojulikana sana na kusomwa sana yaani Mfululizo wa Pambano la Vizazi Vyote (Conflict of the Ages Series-five books), ikiwasilisha maelezo hayo kwa kinaganaga zaidi, kama yalivyowasilishwa kwa Bibi White katika maono mengi. Ijapokuwa magombo kamili – *Wazee na Manabii, Manabii na Wafalme, Tumaini la Vizazi Vyote, Matendo ya Mitume*, na *Pambano Kuu* -

Huwasilisha kisa cha pambano hili kwa namna iliyo kamili zaidi, maandishi ya awali ya kisa hiki kama yalivyowasilishwa hapa kwa jinsi yake ya muhtasari, iliyo wazi, sahili, pamoja na *Experience and Views* (*Uzoefu na Maoni*), daima vitahitajika kwa uhitaji mkubwa. **{EW v2}**

Wadhamini wa Maandishi ya Ellen G. White, Washington, D.C.

Machi, 1963

## Utangulizi kwa Toleo la Kwanza la "Uzoefu na Maoni"

Tunafahamu vizuri kwamba watafutaji wengi waaminifu wa Ukweli na utakatifu wa Biblia wanafanya upendeleo dhidi ya maono. Sababu kubwa mbili zimejenga upendeleo huu. Ya kwanza ni ushupavu wa kidini, unaoambatana na maono na utekelezaji bandia, umekuwepo kwa kiasi fulani karibu kila mahali. Hili limewaongoza wengi ambao ni wakweli kuwa na shaka kuhusu chochote kinachofanana na hicho. Pili, maonesho ya kiinimacho, na kile kinachojulikana kwa kawaida

kama “kuwasiliana na roho za waliokufa,” yamekusudiwa kikamilifu kudanganya, na kusababisha kutokuamini kuhusiana na karama na utendaji wa Roho wa Mungu. **{EW v3}**

Lakini Mungu habadiliki. Kazi yake kupitia kwa Musa mbele ya Farao ilikuwa kamilifu, ingawa Yane na Yambre waliruhusiwa kufanya miujiza kwa uwezo wa Shetani, ambayo ilifanana na miujiza iliyofanywa na Musa. Bandia pia ilionekana katika siku za mitume, lakini bado karama za Roho zilidhihirishwa ndani ya wafuasi wa Kristo. Na si kusudi la Mungu kuwaacha watu Wake katika enzi hii ya udanganyifu ulio karibia kila mahali,bila vipawa na udhihirisho wa Roho Wake. **{EW vi1}**

Mpango wa kilicho bandia ni kuiga kitu halisi kilichopo. Kwa hiyo udhihirisho wa sasa wa roho ya makosa ni uthibitisho kwamba Mungu anajidhihirisha kwa watoto Wake kwa uweza wa Roho Mtakatifu, na kwamba anakaribia kulitimiza Neno Lake kwa utukufu. **{EW vi2}**

“Itakuwa siku za mwisho, asema Mungu, nitawamwagia watu wote Roho Yangu, na wana

wenu na binti zenu watatabiri; na vijana wenu wataona maono; na wazee wenu wataota ndoto." (Matendo ya Mitume 2:17- (Linganisha na Yoeli 2:28.) **{EW vi3}**

Kuhusiana na kiinimacho (mesmerism, animal magenetism, hyponotism), daima tumeifikiria kuwa ni hatari, kwa hiyo hatuna uhusiano wowote nao. Hatujawahi kamwe hata kuona mtu aliyelala usingizi wa kiinimacho na hatujui chochote juu ya sanaa hiyo kwa uzoefu. **{EW vi4}**

Tunatuma kazi hii ndogo kwa matumaini kwamba itawafariji watakatifu. **{EW vi5}**

James White.

*Saratoga Springs*, N.Y., Agosti, 1851.

Early Writing Study Guide. A Complete chapter by chapter guide with questions to aid in your reading and Understanding the book. **{EW vi6}**

## Utangalizi wa Kihistoria

(*Early Witings*) Maandiko ya Awali ni kazi ya kudumu na yenye manufaa ya pekee kwa Waadventista wa Sabato, kwa kuwa inajumuisha vitabu vya awali kabisa vya Ellen G. White. Haya

yaliandikwa na kuchapishwa kwa mara ya kwanza katika miaka ya 1850 kwa ajili ya ujenzi wa maadili na kuwafundisha wale ambao pamoja na mwandishi walikuwa wamepitia uzoefu wa Waadventista watunza Sabato katika miaka ya 1840 na mapema miaka ya 1850. Mambo yakiwa hivyo, mwandishi alichukulia kwa upande wa msomaji kuwa ana uzoefu na historia ya, uamsho wa marejeo ya Kristo na maendeleo ya vuguvugu la Waadventista wa Sabato iliyojitokeza mwaka 1844. Kwa hiyo, matukio yaliyoeleweka vizuri wakati huo yanadokezwa tu, na maneno yanatumika ambayo ili yapate kueleweka kwa usahihi, ni lazima yafikiriwe katika mfumo wa historia ya Waadventista watunzao Sabato katika miaka hiyo ya awali. **{EW vii1}**

Katika mwaka wa 1858, katika kuandika juu ya kutangazwa kwa ujumbe wa malaika watatu wa Ufunuo 14, Ellen White anashughulika na uzoefu wa wale walioshiriki katika kazi hii na kuchukua masomo kutokana na uzoefu huu, badala ya kutoa kama vile ambavyo mtu angeweza kutarajia, uwasilishaji wa wazi wa tabia ya ujumbe huu. Tazama ukurasa wa 232-240; 254-258. Mara kwa mara maneno anatumia ambayo kwa sasa si ya

kawaida kama vile

"Waadventista wa jina," "Mlango uliofungwa," "Mlango uliofunguliwa," na kadhalika. **{EW vii2}**

Leo tunatengwa na zaidi ya karne moja kutoka nyakati hizo za kishujaa. Msomaji inabidi aliweke hili wazi akilini. Historia ambayo ilikuwa inajulikana sana kwa watu wa wakati wa Ellen White sasa tutaipitia, tukigusa baadhi ya mambo makuu ya uzoefu wa Waadventista wa Sabato wakati wa muongo mmoja au miwili iliyotangulia uchapishaji wa kwanza wa taarifa zinazoonekana hapa.**{EW vii3}**

Katika aya za mwanzo Bibi White anarejelea kwa ufupi juu ya uongofu wake na uzoefu wake wa awali wa Ukristo. Pia anasimulia juu ya kusikia hotuba kuhusu mafundisho ya Biblia juu ya marejeo binafsi ya Kristo, ambayo yalidhaniwa kuwa yako karibu sana. Mwamko mkuu wa Marejeo ambao umerejelewa hapa kwa ufupi tu, ulikuwa ni vuguvugu la ulimwengu wote katika ufikiaji wake watu. Liliibuka kama matokeo ya kuchunguza kwa uangalifu Maandiko ya unabii kwa upande wa wengi, na kupokelewa kwa habari njema ya kuja kwa Yesu kwa idadi kubwa ya watu ulimwenguni kote. **{EW viii1}**

## Mwamko Mkuu wa Marejeo

Lakini ilikuwa ni nchini Marekani ambapo ujumbe wa Marejeo ulitangazwa na kupokelewa sana. Pale unabii wa Biblia unaohusu kurudi kwa Yesu ulipokubaliwa na wanaume na wanawake wenye uwezo wa imani nyingi za kidini, kundi kubwa la wafuasi waumini wa dhati Waadventista lilitokea. Ikumbukwe, hata hivyo, kwamba hakukuwapo mfumo wa kidini uliojitenga na ulio dhahiri ulioanzishwa. Tumaini la Marejeo liliongoza katika uamsho wa kina wa kidini ambao uliyapa faida Makanisa yote ya Kiprotestanti na kuwaongoza wale wenye kushuku na makafiri wengi kukiri hadharani imani yao katika Biblia na kwa Mungu. **{EW viii2}**

Wakati vuguvugu lilipokaribia kufikia kilele chake mapema katika miaka ya 1840, mamia kadhaa ya wachungaji waliungana katika kuutangaza ujumbe huu. Katika nafasi ya kwanza alikuwapo William Miller, ambaye aliishi katika ukingo wa mashariki wa Jimbo la New York. Alikuwa mtu mashuhuri katika jamii yake na alijishughulisha na kazi ya kilimo. Licha ya usuli

mzuri wa kidini, katika ujana wake alitokea kuwa mtu wa kushuku/mashaka (skeptical). Alipoteza imani katika Neno la Mungu na kupokea mtazamo wa wale wanaoamini juu ya uwepo wa Mungu lakini wakikataa ufunuo wa Kiungu kufuata nuru ya asili na *fikra* kama mwongozo pekee wa mafundisho na desturi, hawa waliamini kwamba Mungu aliumba dunia na kuiacha ijiendeshe yenyewe, watu hawa waliitwa Deists. (Deism ni theolojia ya kimantiki na msimamo wa kifalsafa ambao unasisitiza matumizi ya akili na uchunguzi wa maumbile ili kuelewa Mungu na ulimwengu. Waumini wanaamini kwamba Mungu aliumba dunia na kuiweka ijiendeshe yenyewe, kwamba Mungu haingilii na uendeshaji wa dunia. Waumini hawa pia wanaamini kwamba wanadamu ni mawakala huru ambao wanaweza kuchagua matendo yao na kwamba maadili ndiyo wajibu mkubwa zaidi wa kidini). Alipokuwa akisoma hubiri katika Kanisa la Kibaptisti Jumapili moja asubuhi, Roho Mtakatifu aliugusa moyo wake, naye aliongozwa kumkubali Yesu Kristo kama Mwokozi wake. Miller alianza kujifunza Neno la Mungu, akidhamiria kupata katika Biblia jibu la kuridhisha kwa maswali yake yote, na kujifunza mwenyewe Kweli zilizowekwa katika

kurasa zake. **{EW viii3}**

Kwa miaka miwili alitumia muda wake mwingi kujifunza Maandiko kwa mtindo wa aya moja moja. Aliamua kutokuendelea na aya inayofuata mpaka alipohisi kwamba amepata maelezo ya kuridhisha ya ile Aya aliyokuwa akiisoma. Mbele yake alikuwa na Biblia yake tu na itifaki ya Biblia (Bible Concordance) - mpangilio wa kialfabeti wa maneno muhimu. Punde katika uchunguzi wake alifikia unabii wa ujio wa pili wa Kristo ulio halisi, katika nafsi Yake mwenyewe. Pia alishughulikia utabiri wa matukio ya muda mrefu, hasa unabii wa siku 2300 wa Danieli 8 na 9, ambao aliuhusisha na unabii wa Ufunuo 14 na ujumbe wa malaika anayetangaza saa ya hukumu ya Mungu (Ufunuo 14:6, 7). Katika kitabu hiki, kwenye ukurasa wa 229, Bibi White anasema kwamba “Mungu alimtuma malaika Wake kuugusa moyo” wa William Miller, “kumwongoza kuchunguza unabii.” **{EW ix1}**

Katika kipindi chake cha usichana Bibi White alimsikia Miller akitoa mifululizo miwili ya mahubiri katika mji wa Portland, Maine. Hisia ya kina na ya kudumu iliwekwa moyoni mwake. Tutamruhusu Ellen aweke mbele yetu hesabu ya unabii, kama Mzee Miller alivyouwasilisha kwa hadhira yake. Kwa

ajili ya hili tunakigeukia kitabu cha baadaye cha Bibi White, *Pambano Kuu:* **{EW ix2}**

## Kuhesabu Vipindi vya Unabii

"Unabii ambao ulionekana wazi kabisa kudhihirisha wakati wa ujio wa pili ulikuwa ni ule wa Danieli 8:14: 'Hata nyakati za jioni na asubuhi elfu mbili na mia tatu; ndipo Patakatifu patakapotakaswa.' Kufuatia kanuni yake ya kufanya Maandiko yajifafanue yenyewe, Miller alijifunza kwamba siku katika unabii wa mfano inawakilisha mwaka (Hesabu 14:34; Ezekieli 4:6); aliona kwamba kipindi cha siku 2300 za unabii, au miaka halisi, kingeenea mbali kupita mwisho wa kipindi cha Wayahudi, hivyo kisingekuwa kinarejelea Patakatifu pa kipindi hicho. Miller aliukubali mtazamo wa jumla uliopokelewa kwamba katika zama za Ukristo dunia ndio Patakatifu, na kwa hiyo alifahamu kuwa kutakaswa kwa Patakatifu kulikotabiriwa katika Danieli 8:14 kuliwakilisha kutakaswa kwa dunia kwa moto katika ujio wa pili wa Kristo. Hivyo, basi, kama mwanzo sahihi ungepatikana kwa ajili ya siku hizi 2300, alihitimisha kuwa wakati wa ujio wa pili

ungeweza kuhakikishwa bila shida. Hivyo ungeweza kudhihirishwa wakati ule wa ukamilisho mkuu, wakati ambapo hali ya sasa, pamoja na 'kiburi na uwezo, fahari na ubatili, uovu na uonevu vyote vingekoma;' wakati ambapo laana 'ingeondolewa duniani, mauti kuangamizwa, thawabu kutolewa kwa watumishi wa Mungu, manabii na watakatifu, na wao wanaolicha jina Lake, na kuangamizwa kwa wale wanaoiharibu dunia' (S. Bliss, *Memoirs of William Miller,* uk. 76).**{EW ix3}**

Kwa bidii mpya na ya kina zaidi, Miller aliendelea na uchunguzi wa unabii, akitumia muda wote wa usiku na vile vile wa mchana ukiwa umewekwa wakfu kwa ajili uchunguzi wa kile ambacho sasa kilionekana kuwa cha umuhimu mkubwa sana na chenye shauku ya kushughulisha sana. Katika sura ya nane ya Danieli hakuweza kupata kidokezo chochote cha mwanzo wa siku 2300; malaika Gabrieli, ingawa aliamriwa kumfanya Danieli ayafahamu maono hayo, alimpa sehemu tu ya maelezo. Wakati mateso ya kutisha ambayo yalikuwa yatokee kwa kanisa yalipooneshwa kwenye maono ya nabii, nguvu za kimwili zilitoweka. Hakuweza kuvumilia zaidi, na malaika akamwacha

kwa muda. Na mimi, Danieli ‘nikazimia, nikaugua siku kadha wa kadha.’ “Nami naliyastajabia yale maono,” anasema, “ila hakuna aliyeyafahamu.” **{EW x1}**

“Lakini Mungu alimwambia mjumbe Wake, ‘Mfahamishe mtu huyu maono haya.’ Utume ule ni lazima utimizwe. Katika kuutii, malaika, muda fulani baadaye, alirudi kwa Danieli, akisema, ‘Nimetokea sasa, ili nikupe akili upate kufahamu;’ ‘basi itafakari habari hii, na kuyafahamu maono haya.’ (Danieli 8:27, 16; 9:22, 23, 25-27). Kulikuwa na jambo moja muhimu katika maono ya sura ya nane ambalo lilikuwa limeachwa bila kuelezewa, yaani, lile linalohusiana na wakati, -kipindi cha siku 2300; kwa hiyo malaika, katika kurudia tena maelezo yake, anaeleza sana juu ya mada ya wakati: **{EW x2}**

“‘Muda wa majuma sabini umeamriwa juu ya watu wako, na juu ya mji wako mtakatifu.... tangu kuwekwa amri ya kutengeneza na kuujenga upya Yerusalemu hata zamani zake Masihi aliye Mkuu; kutakuwa na majuma saba; na katika majuma sitini na mawili utajengwa tena pamoja na njia kuu zake na handaki, naam, katika nyakati za taabu. Na

baada ya yale majuma sitini na mawili, masihi atakatiliwa mbali, naye atakuwa hana kitu; na watu wa mkuu atakayekuja watauangamiza mji, na Patakatifu; na mwisho wake utakuwa pamoja na gharika, na hata mwisho ule vita vitakuwapo; ukiwa umekwisha kukusudiwa.

...Naye atafanya agano thabiti na watu wengi kwa muda wa juma moja; na kwa nusu ya juma hiyo ataikomesha sadaka na dhabihu.’ **{EW xi1}**

“Malaika alikuwa ametumwa kwa Danieli kwa ajili ya kusudi la wazi la kumweleza jambo ambalo alishindwa kulielewa katika njozi ya sura ya nane, taarifa inayohusiana na wakati—“Hata nyakati za jioni na asubuhi elfu mbili na mia tatu; ndipo Patakatifu patakapotakaswa.” Baada ya kumwambia Danieli ‘nimetokea sasa, ili nikupe akili upate kufahamu,’ Maneno ya kwanza kabisa ya malaika ni, ‘Muda wa majuma sabini umeamriwa juu ya watu wako, na juu ya mji wako mtakatifu.’ Neno lililotafsiriwa hapa ‘umeamriwa,’ hasa linamaanisha ‘kukatwa.’ Majuma sabini, yanayowakilisha miaka 490, yanatangazwa na malaika kuwa yamekatwa, hasa yakifungamana na Wayahudi. Lakini yalikatwa kutoka wapi? Kwa kuwa siku 2300 zilikuwa ndicho kipindi pekee cha wakati

kilichotajwa katika sura ya 8, ni lazima kiwe ndicho kipindi ambacho kutoka kwake majuma sabini yalikatwa; majuma sabini kwa hiyo lazima yawe ni sehemu ya siku 2300, na vipindi hivi viwili lazima vianze pamoja. Majuma sabini yalitangazwa na malaika kuwa ni kuanzia tangu kutolewa kwa amri ya kurejesha na kujenga Yerusalemu. Kama tarehe ya amri hii ingepatikana, basi mahali pa kuanzia kwa kipindi kikuu cha siku 2300 kingeweza kuhakikishwa. **{EW xi2}**

Katika sura ya saba ya Ezra amri hii inapatikana. (Aya 12-26). Katika hali yake kamilifu kabisa ilitolewa na Artashasta, mfalme wa Uajemi, 457 K.K. Lakini katika Ezra 6:14 nyumba ya Bwana iliyoko Yerusalemu ilikuwa imejengwa "kwa amri ya Koreshi, na Dario, na Artashasta mfalme wa Uajemi." Wafalme hawa watatu, katika kuanzisha, kuthibitisha tena, na kukamilisha amri hii, waliileta katika ukamilifu unaotakiwa na unabii huu kwa ajili ya kuashiria mwanzo wa miaka 2300. Tukichukua 457 K.B., wakati ambapo amri hii ilikamilishwa, kuwa tarehe ya amri, kila taarifa ya unabii kuhusu majuma sabini zilionekana kuwa zimetimizwa. **{EW xi11}**

"Tangu kuwekwa amri ya kutengeneza na

kuujenga upya Yerusalemu hata zamani zake masihi aliye mkuu; kutakuwa na majuma saba, na katika majuma sitini na mawili”—yaani, majuma sitini na kenda, au miaka 483. Amri ya Artashasta ilianza kutumika katika majira ya kupukutisha ya 457 K.K (fall season). Kuanzia tarehe hii, miaka 483 inafikia majira ya kupukutisha ya mwaka 27 B.K. Wakati huo unabii huu ulitimia. Neno ‘Masihi’ lina maana ya ‘Mtiwa-Mafuta.’ Mnamo majira ya kupukutisha ya mwaka 27 B.K. Kristo alibatizwa na Yohana na kupakwa mafuta na Roho. Mtume Petro anashuhudia kwamba “Mungu alivyomtia mafuta [Yesu wa Nazareti] kwa Roho Mtakatifu na nguvu.” [Matendo ya Mitume 10:38.] Naye Mwokozi Mwenyewe alisema: “Roho wa Bwana yu juu yangu, kwa maana amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema. [Luka 4:18.] Baada ya kubatizwa Kwake alikwenda Galilaya, ‘akihubiri habari njema ya Mungu, akisema, Wakati umetimia.’ [Marko 1:14, 15.] **{EW xii1}**

"Naye atalithibitisha agano na watu wengi kwa muda wa juma moja." “ Juma” linalooneshwa hapa ni lile la mwisho kati ya yale sabini; ni miaka saba ya mwisho ya kipindi kilichotengwa hasa kwa Wayahudi. Wakati huu, kuanzia mwaka 27 B.K. hadi

34 B.K., Kristo, mara ya kwanza Yeye binafsi na baadaye kupitia kwa wanafunzi Wake, alitoa mwaliko wa injili hasa kwa Wayahudi. Mitume waliposonga mbele wakiwa na habari njema ya ufalme, maelekezo ya Mwokozi yalikuwa: "Katika njia ya Mataifa msiende, wala katika mji wo wote wa Wasamaria msiingie; Afadhali shikeni njia kuwaendea kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli." [Mathayo 10:5, 6.]

"Kwa nusu ya juma hiyo ataikomesha sadaka na dhabihu." Katika mwaka wa 31 B.K., miaka mitatu na nusu baada ya ubatizo Wake, Bwana wetu alisulubiwa. Kwa dhabihu kuu iliyotolewa pale Kalvari, mfumo ule wa matoleo ambao kwa miaka elfu nne ulikuwa umeelekeza mbele kwa Mwana-Kondoo wa Mungu ulikoma. Halisi ilikuwa imekutana na mfano, na dhabihu zote na matoleo ya mfumo wa sherehe zilikuwa zikome pale (type had met the antitype). **{EW xii1}**

"Majuma yale sabini, au miaka 490, iliyotengwa hasa kwa Wayahudi, iliisha, kama tulivyoona, mnamo mwaka 34 B.K. Wakati huo, kwa kupitia hatua ya Baraza Kuu la Wayahudi—Sanhedrin, taifa lilitia muhuri kukataa kwake injili kwa kuuawa kwa Stefano na mateso ya wafuasi wa Kristo. Ndipo

ujumbe wa wokovu, ambao haukuwa umewekewa mipaka tena kwa ajili ya wateule peke yao, ukatolewa kwa ulimwengu. Wanafunzi, wakilazimishwa na mateso kukimbia kutoka Yerusalemu, 'wakaenda huko na huko wakilihubiri neno'. 'Filipo akatelemka akaingia katika mji wa Samaria, akawahubiri Kristo.' Petro, kwa uongozi wa kiungu, alifungua injili kwa akida wa Kaisaria, Kornelio mcha Mungu; na Paulo mwenye bidii, aliyeongolewa katika imani ya Kristo, alipewa utume wa kupeleka habari njema "mbali kwa watu wa Mataifa." [Matendo 8:4, 5; Matendo 22:21.] **{EW xii2}**

"Hadi hapa kila ainisho la unabii linatimizwa kwa namna ya kuvutia sana, na mwanzo wa majuma sabini unaamuliwa bila shaka kuwa ni mwaka 457 K.K., na kumalizika kwake ni mwaka 34 B.K. Kutokana na data hii hakuna ugumu katika kupata mwisho wa siku 2300. Yale majuma sabini—siku 490—zikiwa zimekatwa kutoka katika zile 2300, kuna siku 1810 zilizobakia. Baada ya mwisho wa siku 490, siku 1810 bado zilipaswa kutimizwa. Kuanzia 34 B.K., miaka 1810 inafikia mwaka 1844. Kwa hiyo zile siku 2300 za Danieli 8:14 zinakoma katika mwaka 1844. Mwishoni mwa kipindi hiki kikuu cha unabii, kwa ushuhuda wa

malaika wa Mungu, ‘Patakatifu patakapotakaswa.’ Hivyo wakati wa kutakaswa kwa Patakatifu—ambao uliaminika karibu na wote kuwa ungetoke wakati wa kuja kwa mara ya pili—ulioneshwa waziwazi. **{EW xii3}**

“Miller na washirika wake mwanzoni waliamini kwamba siku 2300 zingeisha katika majira ya kuchipua ya 1844, ambapo unabii unaelekeza katika majira ya kupukutisha ya mwaka huo. Kutokueleweka kwa jambo hili kulileta masikitiko na fadhaa kwa wale ambao walikuwa wameweka tarehe ya awali kama wakati wa kuja kwa Bwana (walibainisha siku maalum). Lakini hilo halikuathiri hata kidogo nguvu ya hoja inayoonesha kwamba zile siku 2300 zilikoma katika mwaka wa 1844, na kwamba tukio kuu lililowakilishwa na kutakaswa kwa patakatifu lazima litendeke. **{EW xiv1}**

“Akiingia katika kujifunza Maandiko kama alivyokuwa amefanya, ili kuthibitisha kwamba hayo yalikuwa ni ufunuo kutoka kwa Mungu, Miller, mwanzoni, hakuwa ametazamia hata kidogo kufikia hitimisho ambalo alikuwa amelifikia sasa. Yeye mwenyewe hakuweza kusadiki matokeo ya uchunguzi wake. Lakini ushahidi wa maandiko ulikuwa wazi na wenye nguvu mno kuweza

kupuuzwa.**{EW xiv2}**

“Alitenga muda wa miaka miwili kwa ajili ya kujifunza Biblia, ambapo, mnamo mwaka 1818, alifikia usadikisho wa dhati kwamba ndani ya takriban miaka ishirini na mitano Kristo angetokea kwa ajili ya ukombozi wa watu wake.” — *The Great Controversy*, 324-329. **{EW xiv3}**

## Kukatishwa tamaa na Matokeo Yake

Ilikuwa ni kwa matarajio ya bidii sana kwamba waumini wa Marejeo waliikaribia siku ile iliyotazamiwa ya ujio wa Bwana wao. Waliona kuwa majira ya kuchipua ya1844 kuwa ndiyo wakati ambao unabii wa Danieli ulielekeza. Lakini waumini hawa waliojiweka wakfu walipaswa kupatwa na kukatishwa tamaa kukali. Kama vile wanafunzi wa zamani walivyoshindwa kuelewa sifa bainifu halisi ya mambo yaliyopaswa kutokea katika utimizwaji wa unabii uliohusiana na ujio wa kwanza wa Yesu walivyovunjika moyo, ndivyo Waadventista katika mwaka 1844 walivyovunjika moyo kuhusu maendeleo ya unabii unaohusiana na ujio wa pili wa Kristo uliotarajiwa. Kuhusu hili, Ellen White aliandika ndani ya kitabu hiki: **{EW xv1}**

“Yesu hakuja duniani kama vile kundi lililosubiri, lenye furaha lilivyotarajia, kupatakasa Patakatifu kwa kuitakasa dunia kwa moto. Niliona kuwa walikuwa sahihi katika hesabu yao ya nyakati za unabii; wakati wa unabii ulimalizika mnamo 1844, na Yesu aliingia katika Patakatifu pa Patakatifu kutakasa Patakatifu mwishoni mwa siku. Kosa lao lilikuwa katika kutokuelewa Patakatifu hapo palikuwa ni wapi na namna ya kutakaswa kwake.” - Ukurasa 243. **{EW xv2}**

Mara tu baada ya kukatishwa tamaa ya Oktoba 22, waumini wengi na wachungaji ambao walikuwa wamejihusisha na ujumbe wa Marejeo waliondoka. Baadhi ya hawa walijiunga na vuguvugu hili kwa kiasi kikubwa kutokana na hofu, na pale muda wa matarajio ulipopita ya kuja kwa Yesu kwenye tarehe waliyoipanga ulipopita, waliliachia tumaini lao na kutoweka. Baadhi walikumbwa na ushupavu wa dini. Kama nusu ya kundi la Waadventista, waliendelea kushikilia imani yao kwamba punde Kristo angeonekana katika mawingu ya mbinguni. Katika uzoefu wa kejeli na dhihaka zilizolundikwa kwao na ulimwengu, walidhani kuwa walikuwa wameona ushahidi kwamba siku ya neema kwa ajili ya ulimwengu ilikuwa imepita. Watu hawa waliamini

kwa dhati kwamba kurudi kwa Bwana kulikuwa kumekaribia mno. Lakini kadiri siku zilivyosogea na kuwa majuma na Bwana hakutokea, mgawanyiko wa maoni uliibuka, na kundi hili likagawanyika. Sehemu moja, iliyokuwa kubwa kwa idadi, ilichukua msimamo kwamba unabii haukutimizwa mnamo 1844, na kwamba lazima kulikuwako na kosa katika kuhesabu nyakati za unabii. Walianza kukaza usikivu wao juu ya tarehe fulani mahususi ya baadaye kwa ajili ya tukio hilo. Walikuwapo wengine, kundi dogo, waasisi wa Kanisa la Waadventista wa Sabato, ambao walikuwa na uhakika sana wa ushahidi wa utendaji kazi wa Roho wa Mungu katika uamsho mkuu wa Marejeo kiasi kwamba kukataa kwamba vuguvugu hili lilikuwa si kazi ya Bwana, waliamini, kungeweza kutenda kinyume na roho ya neema. Waliona kuwa wasingeweza kufanya hivyo. **{EW xv3}**

## Njonzi Yatolewa kwa Ellen Harmon

Uzoefu wa kundi hili la waumini, na kazi waliyopaswa kuifanya, walikuta kuwa umeoneshwa katika aya za mwisho za Ufunuo 10. Matarajio ya Marejeo yalipaswa kuamshwa tena. Mungu alikuwa

amewaongoza. Bado alikuwa akiwaongoza. Miongoni mwao alikuwapo kijana mwanamke, Ellen Harmon kwa jina, ambaye mnamo Desemba, 1844, miezi miwili tu baada ya kukatishwa tamaa, alipokea ufunuo wa unabii kutoka kwa Mungu. Katika maono haya Bwana aliomwonesha safari za watu wa Marejeo kwenda Yerusalemu Mpya. Ingawa maono haya hayakuelezea sababu ya Kukatishwa tamaa kule, ambako maelezo yake yangeweza kupatikana kutoka katika kujifunza Biblia, yaliwapa uhakikisho kwamba Mungu alikuwa akiwaongoza na angeendelea kuwaongoza wakisafiri kuelekea katika mji wa mbinguni. **{EW xvi1}**

Mwanzoni mwa njia ya mfano iliyofunuliwa kwa kijana Ellen kulikuwa na nuru angavu, iliyotambulishwa na malaika kuwa ni kilio cha usiku wa manane, usemi uliohusishwa na mahubiri ya kilele katika majira ya joto na ya kupukutisha ya 1844 ya Ujio wa Pili wa Yesu, uliokuwa karibu. Katika maono haya alimwona Kristo akiwaongoza watu kwenda kwenye mji wa Mungu. Mazungumzo yao yalionesha kuwa safari hiyo ingekuwa ndefu kuliko walivyotarajia. Wengine waliacha kumwona Yesu na kuanguka kutoka katika njia, lakini wale

waliokaza macho yao kwa Yesu na kwa mji ule walifika kwenye kituo chao cha mwisho kwa usalama (mbinguni). Ni hili ndilo tunalokuta limeelezwa katika "Njozi Yangu ya Kwanza" kwenye ukurasa wa 13-17. **{EW xvi2}**

## Makundi Mawili ya Waadventista

Mwanzoni ni wachache tu walitambulishwa na kundi hili ambao walikuwa wakisonga mbele katika kuiendeleza nuru. Kufikia mwaka wa 1846 idadi yao ilikuwa takriban watu 50. **{EW xvii1}**

Kundi lile kubwa zaidi ambalo liliacha kuwa na imani katika utimilizaji wa unabii katika mwaka wa 1844 lilikuwa idadi ya watu takriban elfu thelathini. Viongozi wao walikutana pamoja mnamo mwaka 1845 katika mkutano uliofanyika mjini Albany, New York, Aprili 29 hadi Mei 1, wakati ambapo walichunguza upya misimamo yao. Kwa hatua rasmi waliandika kama onyo dhidi ya wale wanaodai kuwa na "nuru maalum," kuwa ni wale wanaofundisha "hadithi za kubuniwa za Kiyahudi," na wale wanaoanzisha "majaribio mapya" (*Advent Herald*, Mei 14, 1845). Hivyo walifunga mlango kwa ajili ya nuru ya Sabato na Roho ya Unabii. Waliamini

kuwa unabii haukutimizwa mnamo mwaka 1844, na baadhi waliweka muda kwa ajili ya kumalizika kwa kipindi cha siku 2300 katika siku zijazo. Nyakati kadhaa ziliwekwa, lakini mmoja baada ya mwingine ulipita. Watu hawa, wakiwa wameshikamanishwa pamoja na tumaini la Marejeo, mwanzoni walijiunga katika vikundi kadhaa ambavyo havikushikamana vizuri vyenye tofauti kubwa kuhusu misimamo juu ya mafundisho fulani. Baadhi ya makundi hayo punde yalitoweka. Kundi lililoendelea kuwapo likaja kuwa Kanisa la Kikristo la Marejeo. Watu kama hao wanatambulishwa katika kitabu hiki kama "Waadventista wa siku ya kwanza" au "waadventista wa jina tu." **{EW xvii2}**

## Mapambazuko ya Nuru Kuhusu Patakatifu

Lakini lazima sasa turudi kwa wale ambao walishikilia sana imani yao kwamba unabii ulikuwa umetimizwa mnamo Oktoba 22, 1844, na ambao kwa akili na mioyo iliyo wazi walisonga mbele katika Kweli za Sabato na Patakatifu kwa kadiri ambavyo nuru ya mbinguni ilivyoangaza njia yao. Watu hawa hawakuwa katika sehemu moja maalum

bali walikuwa ni mtu mmoja mmoja au vikundi vidogo vidogo hapa na pale kote katika sehemu ya kaskazini kati na kaskazini-mashariki mwa Marekani (Massachusets, Maine, New York, Connecticut, Vermont nk).**{EW xviii1}**

Hiram Edson, mmoja wa kundi hili, aliishi katikati ya Jimbo la New York huko Port Gibson. Alikuwa kiongozi wa Waadventista katika eneo hilo. Waumini walikutana nyumbani kwake siku ile ya tarehe 22 Oktoba 1844, wakisubiri kuja kwa Bwana. Kwa utulivu na subira walilingojea tukio hili kubwa. Lakini ilipofika saa ya usiku wa manane nao wakatambua kuwa siku ya matarajio ilikuwa imepita, ikawa dhahiri kwamba Yesu hangekuja mapema kama walivyokuwa wamefikiri. Ulikuwa wakati wa masikitiko makubwa. Asubuhi na mapema Hiram Edson na wengine wachache walitoka kwenda ghalani kwake kuomba, na walipokuwa wakiomba, alihisi kuhakikishiwa kuwa nuru ingekuja. **{EW xviii2}**

Baadaye kidogo, Edson na rafiki yake walipokuwa wakivuka eneo la shamba la mahindi kwenda kuwatembelea Waadventista wenzao, ilionekana kana kwamba mkono fulani uligusa bega lake. Alitazama juu apate kuona—kana kwamba alikuwa katika maono—mbingu zilifunguka, na

Kristo katika Patakatifu pa mbinguni akiingia katika Patakatifu pa Patakatifu, mle kuanza kazi ya huduma kwa niaba ya watu wake, badala ya kutoka katika Patakatifu pa Patakatifu ili kuisafisha dunia kwa moto, kama walivyokuwa wamefundisha. Uchunguzi makini wa Biblia wa Hiram Edson; F.B. Hahn, daktari; na O. L. Crozier, mwalimu wa shule, punde ulidhihirisha kwamba Patakatifu pa kutakaswa mwishoni mwa miaka 2300 haikuwa dunia bali hema lililoko mbinguni, Kristo akihudumu kwa niaba yetu katika Patakatifu pa Patakatifu. Kazi hii ya upatanisho ya Kristo ilijibu Wito wa "saa ya hukumu ya Mungu" uliotangazwa katika ujumbe wa malaika wa kwanza (Ufunuo 14:6, 7). Bwana Crozier, mwalimu wa shule, aliandika matokeo ya uchunguzi huu. Haya yalichapishwa katika eneo hilo mahalia, na kisha kwa namna kamilifu zaidi lilichapwa katika jarida la Waadventista lijulikanalo kama *The Day-Star*, lililochapishwa Cincinnati, Ohio. Nambari maalum ya Februari 7, 1846, ilitumiwa kabisa katika somo hili la Biblia kuhusu suala la Patakatifu. {**EW xviii3**}

## Kweli Zathibitishwa na Njozi

Wakati uchunguzi huu ulipokuwa ukiendelea, na kabla ya kazi yao haijajulikana, mbali kuelekea mashariki katika jimbo la Maine, maono yalitolewa kwa Ellen Harmon ambapo alioneshwa kuhama kwa huduma ya Kristo kutoka mahali Patakatifu kwenda mahali Patakatifu pa Patakatifu mwishoni mwa siku 2300. Kumbukumbu ya njozi hii inapatikana katika *Early Writings*, 54-56. **{EW xix1}**

Kuhusu njozi nyingine muda mfupi baada ya hii, kama ilivyorejelewa na Bibi White katika taarifa iliyoandikwa mnamo Aprili, 1847, anaandika kwamba "Bwana alinionesha katika njozi, zaidi ya mwaka mmoja uliopita, kwamba Ndugu Crozier alikuwa na nuru ya Kweli juu ya kutakaswa kwa Patakatifu, na kadhalika; na kwamba ilikuwa ni mapenzi yake kwamba Ndugu Crozier alipaswa kuandika mtazamo ule aliotupatia katika toleo la *The Day-Star Extra*, Februari 7, 1846. Ninahisi kupewa mamlaka kikamilifu na Bwana kupendekeza toleo hilo la nyongeza kwa kila mtakatifu.” -— *A Word to the “Little Flock,“ 12 (Neno kwa “Kundi dogo,”)*. Kwa jinsi hiyo matokeo ya wasomi wa Biblia yalithibitishwa na njozi ya mjumbe wa Mungu. **{EW xix2}**

Katika miaka iliyofuata Ellen White aliandika sana kuhusu Ukweli wa Patakatifu na umuhimu wake kwetu, na kuna rejea nyingi kuhusu hili katika *Maandiko ya Awali*. Angalia hasa sura inayoanzia ukurasa wa 250 yenye kichwa "Patakatifu." Ufahamu wa huduma ya Kristo katika Patakatifu pa mbinguni ulionekana kuwa ndio ufunguo uliofungua fumbo la Kukatishwa Tamaa Kukuu (*The Great Dissapointment*). Waasisi wetu waliona waziwazi kwamba unabii unaotangaza kuwa saa ya hukumu ya Mungu imekaribia ulitimilizwa katika matukio yaliyotokea mnamo mwaka 1844, lakini kwamba kulikuwako na kazi ya huduma iliyopaswa kukamilishwa katika Patakatifu pa Patakatifu katika hekalu la mbinguni kabla ya Yesu kuja duniani. {**EW xix3**}

Ujumbe wa malaika wa kwanza na ujumbe wa malaika wa pili ulikuwa umetangazwa katika kuhubiriwa kwa ujumbe wa Marejeo, na sasa ujumbe wa malaika wa tatu ulianza kusikika. Chini ya ujumbe huu umuhimu wa Sabato ya siku ya saba, yaani  Jumamosi ulianza kufahamika (Genesis 2:2–3).Exodus

20:8-11, **Matthew 28:1, Luke 24:1** Luke 4:16). {EW xx1}

## Mianzo ya Utunzaji wa Sabato

Tunapofuatilia kisa cha mwanzo wa utunzaji wa Sabato miongoni mwa Waadventista wa awali, tunakwenda kwenye kanisa dogo katika mji wa Washington katikati ya New Hampshire, jimbo ambalo linapakana na Maine upande wa mashariki na ambalo mpaka wake wa magharibi uko ndani ya maili sitini kutoka mstari wa jimbo la New York. Hapa washiriki wa kanisa huru la Kikristo mnamo 1843 walisikia na kuyakubali mahubiri ya ujumbe wa Marejeo. Lilikuwa ni kundi lenye bidii sana. Miongoni mwao alikuja Rachel Oakes Mbaptisti wa Siku ya Saba, ambaye alisambaza vipeperushi vilivyoelezea madai ya lazima, na yenye mashiko ya amri ya nne. Baadhi ya watu katika mwaka wa 1844 waliuona na kuukubali Ukweli huu wa Biblia. Mmoja wao akiwa William Farnsworth, katika ibada moja ya Jumapili asubuhi, alisimama kwa miguu yake na kutangaza kwamba alikusudia kuitunza Sabato ya Mungu ya amri ya nne. Wengine kadhaa walijiunga

naye, wakiweka msimamo wao thabiti juu ya amri zote za Mungu. Hawa walikuwa ndio Waadventista wa Sabato wa kwanza. **{EW xx2}**

Mchungaji aliyekuwa akilitunza kundi hili la kanisa, Frederick Wheeler, punde aliikubali Sabato ya siku ya saba na alikuwa ndiye mchungaji wa kwanza wa Waadventista kufanya hivyo. Mwingine kati ya wahubiri wa Marejeo, T. M. Preble, aliyeishi katika jimbo hilo moja, aliukubali Ukweli wa Sabato na mnamo Februari, 1845, alichapisha makala katika jarada la *Hope of Israel,* mojawapo ya majarida ya Waadventista, akiweka madai ya ambayo ni lazima kufuatwa ya amri ya nne.  Joseph Bates, mchungaji maarufu wa Waadventista aliyeishi Fairhaven, Massachusetts, alisoma makala ya Preble na kuikubali Sabato ya Siku ya Saba. Muda mfupi baadaye, Mchungaji Bates alisafiri kwenda Washington, New Hampshire, ili kujifunza Ukweli huu mpya uliopatikana pamoja na Waadventista walioitunza Sabato wanaoishi huko. Aliporejea nyumbani kwake, alikuwa ameridhishwa kabisa kuhusu Ukweli wa Sabato. Bates hatimaye aliamua kuchapisha kipeperushi kinachoweka madai ya lazima ya amri ya nne. Kijitabu chake cha Sabato chenye kurasa 48 kilichapishwa mnamo

Agosti, 1846. Nakala yake ilifika mikononi mwa James na Ellen White wakati wa karibu na ndoa yao mwishoni mwa Agosti. Kutokana na ushahidi wa Maandiko uliowasilishwa ndani yake, walikubali, na kuanza kuitunza Sabato ya siku ya saba. Kuhusu hili Ellen White baadaye aliandika: "Katika majira ya kupukutisha ya 1846 tulianza kuitunza Sabato ya Biblia, na kufundisha na kuitetea."—*Testimonies for the Church*, 1:75. {**EW xx3**}

## Umuhimu wa Sabato Wadhihirishwa

James na Ellen White walichukua msimamo wao kutokana na ushahidi wa Maandiko tu yale ambayo akili zao ziliwaelekeza katika kipeperushi cha Bates. Kisha Sabato ya kwanza mnamo Aprili, 1847, miezi saba baada ya kuanza kuitunza na kufundisha Sabato ya siku ya saba, Bwana alitoa njozi kwa Bibi White huko Topsham, Maine, ambapo umuhimu wa Sabato ulisisitizwa. Aliziona mbao za torati ndani ya sanduku katika hekalu la mbinguni, na duara ya nuru ikiizunguka amri ya nne. Angalia ukurasa wa 32-35 kwa ajili ya simulizi ya njozi hii. Msimamo uliochukuliwa hapo awali kutokana na

uchunguzi wa neno la Mungu ulithibitishwa. Njozi hii pia ilisaidia kupanua mawazo ya waumini juu ya utunzaji wa Sabato. Katika ufunuo huu, Bibi White alipelekwa hadi mwisho wa wakati na kuona Sabato kama Ukweli mkubwa wa kupimia watu, ambao kwa huo watu wanaamua ama kumtumikia Mungu au kuitumikia mamlaka iliyoasi. Akiangalia nyuma katika mwaka 1874 katika uzoefu huu, aliandika: **{EW xxi1}**

"Niliamini Ukweli juu ya suala la Sabato kabla sijaona chochote katika maono kuhusiana na Sabato. Ilichukua miezi kadhaa baada ya kuanza kuitunza Sabato kabla sijaoneshwa umuhimu wake na nafasi yake katika ujumbe wa malaika wa tatu." - E. G. White *Letter* 2, 1874. **{EW xxii1}**

## Mikutano Muhimu Kuhusu Sabato

Kwa majaliwa ya Mungu wachungaji kadhaa waliokuwa wakitunza Sabato ambao waliongoza katika kufundisha Ukweli huu mpya kwa kushirikiana na baadhi ya wafuasi wao, walikutana

pamoja mnamo mwaka 1848 katika mikutano mitano ya Sabato. Kupitia vipindi vya kufunga na kuomba walilichunguza Neno la Mungu. Mzee Bates, mtume wa Ukweli wa Sabato, aliongoza katika kutetea madai ya lazima ya Sabato. Hiram Edson na washirika wake, ambao walihudhuria baadhi ya mikutano hii, walikuwa hodari katika uwasilishaji wao wa nuru ya Patakatifu. James White, mwanafunzi makini wa unabii, alielekeza umakini wake juu ya matukio ambayo ni lazima yatokee kabla ya Yesu kuja tena. Katika mikutano hii mafundisho yanayoongoza na yanayoshikiliwa leo na Waadventista wa Sabato yaliletwa pamoja. **{EW xxii2}**

Akiangalia nyuma katika uzoefu huu, Ellen White aliandika: **{EW xxii3}**

"Wengi wa watu wetu hawatambui jinsi msingi wa imani yetu uvyowekwa imara. Mume wangu, Mzee Joseph Bates, Baba Pierce, Ndugu wakubwa miongoni mwa waasisi walikuwapo hapa hivyo wakirejelewa kwa kumbukumbu. "Baba Pierce" alikuwa ni Stephen Pierce, ambaye alitumika katika kazi ya huduma na utawala katika siku za awali.] Mzee [Hiram] Edson, na wengine ambao walikuwa na bidii, wanyofu, na wakweli, walikuwa miongoni

mwa wale ambao, baada ya kupita kwa wakati mnamo mwaka 1844, waliutafuta Ukweli kama hazina iliyositirika. Nilikutana nao, nasi tulijifunza na kuomba kwa bidii. Mara nyingi tulibaki kuwa pamoja hadi usiku wa manane, na wakati mwingine hadi usiku mzima, tukiomba kwa ajili ya nuru na kulichunguza neno. Mara kwa mara ndugu hawa walikusanyika ili kujifunza Biblia, ili waweze kujua maana yake, na kuwa tayari kuifundisha kwa nguvu. Walipofikia mahali katika masomo yao ambapo wangesema, "hatuwezi kufanya chochote zaidi," Roho wa Bwana angekuja juu yangu, ningechukuliwa katika maono, na ningepewa maelezo ya wazi ya mafungu ambayo tulikuwa tukiyasoma, pamoja na maagizo ya jinsi ambavyo tulipaswa kufanya kazi na kufundisha kwa ufanisi. Hivyo nuru ilitolewa ambayo ilitusaidia kuelewa maandiko kuhusu Kristo, utume Wake, na ukuhani Wake. Mfuatano wa Ukweli kutoka wakati huo hadi wakati ambapo tutauingia mji wa Mungu, iliwekwa wazi kwangu, nami nikawapa wengine maagizo ambayo Bwana alikuwa amenipa. **{EW xxii4}**

“Wakati wote huu sikuweza kufahamu fikira za ndugu wengine. Akili yangu ilikuwa imefungwa, kama ilivyokuwa, na sikuweza kuelewa maana ya

maandiko tuliyokuwa tukijifunza. Hii ilikuwa ni mojawapo ya huzuni kubwa kabisa katika maisha yangu. Nilikuwa katika hali hii ya akili hadi hoja zote kuu za imani yetu zilipowekwa wazi kwa akili zetu, kwa upatanifu na Neno la Mungu. Ndugu walijua kwamba wakati sikuwa katika maono, sikuweza kuyaelewa mambo haya, na waliukubali kama nuru ya moja kwa moja kutoka mbinguni ufunuo uliotolewa." - *Selected Messages* 1:206, 207. {**EW xxiii1**}

Hivyo msingi wa mafundisho ya Kanisa la Waadventista wa Sabato uliwekwa katika kujifunza neno la Mungu kwa uaminifu, na pale ambapo waasisi hawakuweza kuendelea, Ellen White alipewa nuru ambayo ilisaidia kuelezea ugumu wao na kufungua njia kwa ajili ya uchunguzi kuendelea. Njozi hizi pia ziliweka muhuri wa kibali cha Mungu juu ya hitimisho sahihi. Hivyo karama ya unabii ilitenda kazi kama mrekebishaji wa makosa na mthibitishaji wa Ukweli. (Angalia *Gospel Workers*, 302.) {**EW xxiii2**}

## Waasisi Wanaanza Kuchapisha

Ilikuwa ni muda mfupi baada ya mkutanowa

tano wa Sabato uliofanyika mnamo mwaka 1848 ambapo mkutano mwingine uliitishwa nyumbani kwa Otis Nichols huko Dorchester (karibu na Boston), Massachusetts. Ndugu walikuwa wakijifunza na kuomba juu ya jukumu lao la kutangaza nuru ambayo Bwana alikuwa amesababisha iangaze kwenye njia yao. Walipokuwa wakichunguza, Ellen White aliochukuliwa katika maono, na katika ufunuo huu alioneshwa wajibu wa ndugu kuichapisha nuru hii. Analisimulia tukio hilo katika *Life Sketches*.{**EW xxiv1**}

"Baada ya kutoka katika maono nilimwambia mume wangu: 'Nina ujumbe kwa ajili yako. Unapaswa kuanza kuchapisha kijizuu na kukisambaza kwa watu. Hebu na kiwe kidogo tu mwanzoni; lakini watu watakapokisoma, watakutumia fedha za kuchapisha, nacho kitakuwa na mafanikio tangu cha kwanza. Kutoka katika mwanzo huu mdogo ilioneshwa kwangu kuwa kingekuwa kama miali ya nuru iliyokwenda bila kuzuiwa kote ulimwenguni.'" - Ukurasa 125. {**EW xxiv2**}

Hapa palikuwapo na wito wa kuchukuliwa hatua. James White angelifanya nini? Alikuwa na mali

chache sana za dunia hii. Lakini maono hayo yalikuwa ni maagizo ya Mungu, alihisi nguvu ya kusonga mbele kwa imani. Hivyo, kwa Biblia yake iliyonunuliwa kwa senti sabini na tano pamoja na concordance/itifaki ya Biblia ambayo majalada yake yote yalikuwa yamechanika, James White alianza kuandaa makala juu ya ukweli wa Sabato na mada zingine za namna hiyo ili zipate kuchapishwa katika gazeti ndogo. Yote haya yalichukua muda, lakini hatimaye aliwasilisha nakala hiyo kwa mchapishaji huko Middletown, Connecticut, ambaye alikuwa tayari kumwamini kwa ajili ya agizo la uchapishaji. Herufi zilipangwa, uhakiki ulifanyika na kusahihishwa, na nakala elfu moja za gazeti hilo zilichapishwa. James White alizisafirisha kutoka ofisi ya uchapishaji ya Middletown hadi nyumbani kwa Belden ambapo yeye na Ellen walikuwa wamepata makazi ya muda. Kijitabu hiki kidogo kilikuwa na ukubwa wa inchi sita kwa tisa na kilikuwa na kurasa nane. Kilibeba jina la *Present Truth* –(*Ukweli wa Sasa)*. Ilikuwa Julai, 1849 ambapo Rundo dogo la karatasi lililazwa sakafuni. Kisha ndugu na dada wakakusanyika karibu nalo, na kwa machozi machoni mwao, walimsihi Mungu apate kuibariki karatasi hii ndogo itakapotumwa

kwenda kwa watu. Kisha makaratasi hayo yalikunjwa, yakafungwa na anwani kuandikwa juu yake, na James White akayapeleka umbali wa maili nane kwenye ofisi ya posta ya Middletown. Hivyo ndivyo kazi ya uchapishaji wa Kanisa la Waadventista wa Sabato ilivyoanza. {**EW xxiv3**}

Matoleo manne yalitumwa kwa njia hii, na kila moja liliombewa kabla ya karatasi kupelekwa katika ofisi ya posta. Punde barua zilipokelewa zikieleza kuhusu watu ambao walikuwa wameanza kutunza Sabato kutokana na kusoma majarida hayo. Baadhi ya barua hizi zilikuwa na pesa, na James White, mnamo Septemba, aliweza kumlipa mchapishaji wa Middletown **$**/dola 64.50 kwa ajili ya matoleo manne. {**EW xxv1**}

## Kuanzisha Review and Herald

Kadiri James na Ellen White walivyosafiri kutoka sehemu moja hadi nyingine, kukaa miezi michache hapa na miezi michache pale, walipanga kuchapisha matoleo kadhaa ya gazeti hili. Hatimaye toleo la kumi na moja na la mwisho lilichapishwa huko Paris, Maine, mnamo Novemba, 1850. Bibi White alichangia uandishi wa makala kadhaa katika

*Present Truth (Ukweli wa Sasa)*. Mengi ya haya yanapatikana katika sehemu ya kwanza ya *Early Writings* (*Maandiko ya Awali)*, 36-54. {**EW xxv2**}

Pia, mnamo Novemba, kongamano lilifanyika jijini Paris, na ndugu waliichunguza kazi ya uchapishaji iliyokuwa ikikua. Waliamua kulikuza gazeti hilo na wakabadilisha jina lake kuwa *The Second Advent Review na Sabbath Herald*. Lilichapishwa kwa miezi michache huko Paris, Maine, kisha Saratoga Springs, New York. Limechapishwa tangu siku hiyo hadi leo kama gazeti la kanisa la Waadventista wa Sabato. {**EW xxv3**}

## Kazi ya Uchapishaji Yakua

Wakati akiishi Saratoga Springs, James White alipanga mnamo Agosti, 1851, kuchapisha kitabu cha kwanza cha Bibi White kilichoitwa *A Sketch of the Christian Experience and Views of Ellen G. White*, Ambacho kwa sasa ni ukurasa wa 11-83 wa kitabu hiki. Kikiwa na kurasa zake 64, kilikuwa ni kijitabu tu.

**{EW xxvi1}**

Katika majira ya kuchipua ya mwaka 1852, familia ya White walihamia Rochester, New York, na pale walianzisha ofisi ambayo wangeweza kufanya uchapishaji wao wenyewe. Ndugu waliungana katika ombi la kupata pesa kwa ajili ya kununua mashine ya kupiga chapa na dola mia sita zilichangishwa kwa ajili ya kukipata kifaa hicho. Ni furaha iliyoje waumini wa awali walikuwa nayo pale machapisho yetu yalipoweza kutolewa kwenye kiwanda cha uchapishaji cha watunza Sabato! Kwa muda zaidi kidogo ya miaka mitatu, waliishi Rochester na kuchapisha ujumbe huko. Mbali na majarida ya *Review and Herald* na *Youth's Instructor* yalivyoanzishwa na James White mnamo mwaka 1852, pia, mara kwa mara, walichapisha vijuzuu. Kijitabu cha pili cha Ellen G. White, *Supplement to the Christian Experience and Views of Ellen G. White*, kilichapishwa Rochester Januari 1854. Hiki sasa kinapatikana katika *Early Writings*, Ukurasa 85-127**{EW xxvi2}**

## Battle Creek Inakuwa Kituo cha Uchapishaji

Mnamo Novemba, 1855, James na Ellen White na wasaidizi wao walihamia Battle Creek, Michigan.

Mashine ya kupiga chapa pamoja na vifaa vingine vya uchapishaji viliwekwa katika jengo lililojengwa na Waadventista Watunzao Sabato kadhaa ambao walikuwa wametoa pesa za kuanzisha ofisi yao wenyewe ya uchapishaji. Kadiri kazi yao ilivyoendelea katika mji huo mdogo, Battle Creek ikawa makao makuu halisi ya Kanisa la Waadventista wa Sabato. Lakini ilikuwa ni kwa shida sana kwamba James White alidumisha kazi ya Uchapaji wa vitabu. **{EW xxvi3}**

Tunapouchunguza usuli wa *Early Writngs* (*Maandiko ya Awali*), inapaswa izingatiwe kwamba Waadventista wa kwanza watunzao Sabato mwanzoni walikuwa na mzigo wa kuwafikia tu ndugu zao wa zamani katika Mwamko Mkuu wa Marejeo kwa Ukweli wa Sabato; yaani, wale ambao walikuwa pamoja nao katika ujumbe wa malaika wa kwanza na wa malaika wa pili. Kwa hiyo, kwa takriban miaka saba baada ya 1844, kazi zao zilikuwa kwa sehemu kubwa kwa ajili ya Wanamarejeo wale ambao walikuwa hawajachukua msimamo juu ya ujumbe wa malaika wa tatu. Kwa mtu anayeifahamu hali ilivyokuwa, hii inaeleweka hakika.**{EW xxvii1}**

## "Mlango Uliofungwa" na "Mlango Ulio Wazi"

Katika juhudi maalum zilizofanywa katika kuutangaza ujumbe wa Marejeo katika majira ya joto ya 1844, viongozi katika vuguvugu hii waliuona uzoefu wao wenyewe katika mfano wa wanawali kumi walioandikwa katika Mathayo 25. Kulikuwa na "wakati wa kukawia" uliofuatiwa na kilio, "Haya bwana arusi; tokeni mwende kumlaki." Hii ilikuwa inajulikana kama "kilio cha usiku wa manane." Katika njozi yake ya kwanza, hii ilioneshwa kwa Bibi White kama nuru angavu iliyowekwa nyuma ya Waadventista mwanzoni mwa njia. Katika mfano huo, walisoma kwamba wale waliokuwa tayari waliingia ndani pamoja na bwana-arusi katika arusi, “mlango ukafungwa.” (Angalia Mathayo 25:10.) Kwa hiyo walihitimisha kwamba tarehe 22 Oktoba 1844, mlango wa rehema ulifungwa kwa wale ambao walishindwa kuukubali ujumbe ule ambao ulikuwa umetangazwa kwa upana kiasi kile. Miaka michache baadaye Ellen White aliandika kuhusu hili: **{EW xxvii2}**

“Baada ya kupita kwa wakati ule ambapo Mwokozi alitarajiwa, wao [waumini wa Marejeo] bado waliamini kuwa kuja Kwake ni karibu; walishikilia kwamba walikuwa wamefikia pambano muhimu, na kwamba kazi ya Kristo kama mwombezi wa mwanadamu mbele za Mungu, ilikuwa imekoma. Ilionekana kwao kufundishwa katika Biblia kwamba mlango wa rehema wa mwanadamu ungefungwa muda mfupi kabla ya ujio halisi wa Bwana katika mawingu ya mbinguni. Hili lilionekana kuwa dhahiri kutoka katika maandiko yanayoelekeza katika wakati ambapo watu watatafuta, watabisha na kulia kwenye mlango wa rehema na hautafunguliwa. Na lilikuwa swali kwao kama tarehe ile ambayo walikuwa wametazamia kuja kwa Kristo isingeashiria mwanzo wa kipindi hiki ambacho kilikuwa kinatangulia ujio Wake. Baada ya kutoa onyo juu ya hukumu iliyo karibu, walihisi kwamba kazi yao kwa ajili ya ulimwengu ilikuwa imekwisha na walipoteza wajibu wao kwa roho kwa ajili ya wokovu wa wenye dhambi, huku dhihaka thabiti na za kukufuru za wale wasiomcha Mungu zikionekana kwao kama ushahidi mwingine kwamba roho ya Mungu ilikuwa imeondolewa kutoka kwa watu wanaoikataa rehema Yake. Haya

yote yaliwathibitisha katika imani kwamba rehema ilikuwa imekwisha, au kama walivyoielezea wakati huo, ‘mlango wa rehema ulikuwa umefungwa.’ ”—*The Great Controversy,* 429. {**EW xxvii3**}

Kisha Bibi White anaendelea kuonesha jinsi ambavyo nuru ilianza kupambazuka juu ya suala hili:{**EW xxviii1**}

“Lakini nuru iliyo wazi zaidi ilikuja kutokana na uchunguzi wa mada ya Patakatifu. Sasa waliona kwamba walikuwa sahihi kwa kuamini kwamba mwisho wa siku 2300 katika 1844 uliashiria zahama muhimu. Lakini wakati ambapo ilikuwa kweli kwamba mlango huo wa matumaini na rehema ambao watu walikuwa nao kwa miaka elfu moja na mia nane kwa ajili ya kumfikia Mungu, ulikuwa umefungwa, mlango mwingine ulifunguliwa, na msamaha wa dhambi ulitolewa kwa wanadamu kupitia kwa maombezi ya Kristo katika Patakatifu pa Patakatifu. Sehemu moja ya huduma Yake ilikuwa imefungwa, ili kuipa nafasi nyingine. Bado kulikuwapo na “mlango uliofunguliwa” wa kuingia katika Patakatifu pa mbinguni, ambapo Kristo

alikuwa akihudumu kwa niaba ya wenye dhambi. **{EW xxviii2}**

“Sasa ilionekana matumizi ya maneno yale ya Kristo katika Ufunuo, yaliyosemwa kwa Kanisa lililopo katika wakati huu hasa: ‘Haya ndiyo anenayo yeye aliye mtakatifu, aliye wa Kweli, aliye na ufunguo wa Daudi, Yeye Mwenye kufungua wala hapana afungaye, Naye afunga wala hapana afunguaye. Nayajua matendo yako. Tazama, nimekupa mlango uliofunguliwa mbele yako, ambao hapana awezaye kuufunga,.’ (Ufunuo 3:7, 8.) **{EW xxviii3}**

“Ni wale ambao kwa imani wanamfuata Yesu katika kazi kuu ya upatanisho, ndiyo wanaopokea faida za upatanisho Wake kwa niaba yao; huku wale wanaoikataa nuru inayoweka wazi kazi hii ya huduma hawanufaiki nayo.—*The Great Controversy*, 429, 430.**{EW xxix1}**

## Njia Mbili za Kutoka katika Mkanganyiko

Kisha Bibi White anazungumza juu ya jinsi makundi mawili ya waumini wa Marejeo walivyojihusisha na uzoefu wa kukatishwa tamaa wa Oktoba 22, 1844 (*The Great Dissapointment of 1844*): **{EW xxix2}**

"Kupita kwa wakati mnamo 1844 kulifuatiwa na kipindi cha majaribu makubwa kwa wale ambao bado walikuwa wameishikilia imani ya Marejeo. Msaada wao pekee, kuhusu kuhakikisha msimamo wao wa Kweli, ulikuwa ni nuru ile ambayo iliyelekeza akili zao kwenye Patakatifu pa juu. Wengine waliiacha imani yao juu ya hesabu yao ya awali ya nyakati za unabii na kudhani kuwa ilikuwa ni nguvu za wakala wa kibinadamu au wa kishetani zilizoliosababisha mvuto ule wenye nguvu wa Roho Mtakatifu ambao uliambatana na vuguvugu lile la Marejeo. Kundi lingine lilishikilia kwa uthabiti kwamba Bwana alikuwa amewaongoza katika uzoefu wao uliopita; na kadiri walivyokuwa wakingoja na kukesha na kuomba ili wapate kuyajua mapenzi ya Mungu waliona kwamba Kuhani Mkuu alikuwa ameingia katika kazi nyingine

ya huduma na wakimfuata Yeye kwa imani, waliongozwa kuona pia kazi ya mwisho ya kanisa. Walifahamu kwa uwazi zaidi ujumbe wa malaika wa kwanza na wa malaika wa pili, na walikuwa tayari kuupokea na kuutoa kwa ulimwengu onyo lile makini la malaika wa tatu wa Ufunuo 14."—*The Great Controversy*, 431, 432.{**EW xxix3**}

Rejea fulani zinatokea katika kazi hii, kwenye ukurasa wa 42-45, kuhusu "mlango uliofunguliwa" na "mlango uliofungwa." Hii inaeleweka kwa usahihi kwa kuzingatia historia ya uzoefu wa waumini wetu wa kwanza peke yake. {**EW xxix4**}

Si muda mrefu sana baada ya Kukatishwa tamaa, waasisi waliona kwamba japokuwa palikuwapo na wale ambao kwa kuikataa kabisa nuru walikuwa wamefunga mlango kwa ajili ya wokovu wao, walikuwapo watu wengi ambao walikuwa hawajausikia ujumbe huu na hawakuwa wameukataa, na hawa wangeweza kufaidika kutokana na majaliwa yaliyotolewa kwa ajili ya wokovu wa mwanadamu. Katika miaka ya 1850 hoja hizi zilijitokeza waziwazi. Kisha pia, njia za kuwasilisha ujumbe wa malaika watatu zilikuwa zinaanza kufunguka. Chuki ilianza kufifia. Ellen White, akiangalia nyuma katika uzoefu wao baada

ya Kukatishwa tamaa aliandika: **{EW xxx1}**

"Wakati huo ilikuwa haiwezekani kupata fursa ya kuingia kwa wasioamini. Kukatishwa tamaa mnamo mwaka 1844 kulikuwa kumechanganya akili za wengi, na hawakuwa tayari kusikiliza maelezo yoyote juu ya jambo hilo.'" — *The Review and Herald*, Novemba 20, 1883. **{EW xxx2}**

Lakini katika mwaka wa 1851 mzee White aliweza kuripoti kwamba: "'Sasa mlango uko wazi karibu kila mahali kwa ajili ya kuwasilisha Ukweli, na wengi wako tayari kusoma machapisho, ambao hapo awali hawakuwa na shauku ya kuchunguza.'" —*The Review and Herald*, Agosti 19, 1851. **{EW xxx3}**

## Wito kwa Ajili ya Kupanga au Kuweka Mfumo wa Kanisa (Church Organization)

Lakini pamoja na fursa hizi mpya, na kwa idadi kubwa ya watu kuukubali ujumbe, dalili chache za kutopatana zilikuja miongoni mwao. Kama hizi zisingezuiwa, kazi ingedhurika sana. Lakini hapa tena tunaona majaliwa ya Mungu katika kuwaongoza watu wake, kwa kuwa mnamo Desemba 24, 1850, katika njozi aliyopewa Ellen White, anatuambia: **{EW xxx4}**

"Niliona jinsi Mungu alivyokuwa mkuu na mtakatifu. Malaika alisema, "Tembeeni kwa uangalifu mbele Yake, kwa maana Yeye Yuko juu na ameinuliwa, na vazi la utukufu Wake linaijaza hekalu." Niliona kwamba kila kitu kilichokuwa mbinguni kilikuwa katika utaratibu kamili. Malaika akamwambia, "Tazameni, Kristo Ndiye kichwa, enendeni kwa utaratibu, enendeni kwa utaratibu. Muwe na maana kwa kila jambo." Malaika alisema, "Tazameni, nanyi mjue ni jinsi gani utaratibu wa mbinguni ulivyo mkamilifu, na ulivyo mzuri; nanyi ufuateni huo." - Ellen G. White *Manuscript* 11, 1850. **{EW xxx5}**

Ilichukua muda kuweza kuwaongoza waumini kwa ujumla kufahamu hitaji la utaratibu na thamani ya utaratibu wa injili. Uzoefu wao wa zamani katika makanisa ya Kiprotestanti ambayo walikuwa wamejitenga nayo uliwaongoza kuchukua tahadhari. Isipokuwa katika maeneo yale ambapo hitaji la kiutendaji lilikuwa dhahiri sana, hofu ya kukaribisha utaratibu rasmi iliwafanya waumini kusita kuhusu utaratibu wa kanisa (waliogopa kuwa na urasmi, au desturi kavukavu zisizohusisha moyo, au kuwa dhati). Haikuwa hadi muongo mmoja baada ya njozi ya 1850 ndipo mipango kamili zaidi ya mfumo

hatimaye ilitekelezwa. Bila shaka sababu ya msingi ya umuhimu katika kuleta juhudi hizi kuzaa matunda ilikuwa ni sura ile pana yenye kichwa “Utaratibu wa Injili,” Iliyochapishwa katika *Supplement to the Christian Experience and Views of Ellen G. White*. Hii inaonekana katika kazi hii kama ukurasa wa 97-104. {**EW xxxi1**}

Mnamo mwaka wa 1860, kuhusiana na uandaaji wa kazi ya uchapishaji, jina lilichaguliwa. Baadhi walidhani kwamba “Kanisa la Mungu au Church of God” lingefaa, lakini hisia ilienea kwamba jina hilo lingepasa liakisi mafundisho bainishi yanayolitofautisha kanisa. Walikubali “Waadventista wa Sabato au Seventh-Day Adventists” kama jina lao. Mwaka uliofuata baadhi ya makundi ya waumini yalijipanga kuwa makanisa, na makanisa ya Michigan yaliunda konferensi ya Jimbo. Punde kulikuwapo na konferensi kadhaa za kitaifa. Ndipo mnamo Mei, 1863, Konferensi Kuu ya Waadventista wa Sabato ilianzishwa. Hii inatuchukua miaka mitano ng’ambo ya wakati wa *Maandiko ya Awali (Early Writings)*. {**EW xxxi2**}

## Njozi ya Pambano Kuu

Rejea zimetolewa juu ya kuhamishwa kwa kazi ya uchapishaji kutoka Rochester, New York, kwenda Battle Creek, Michigan, mnamo Novemba, 1855. Mzee na Bibi White walifanya makao yao huko Battle Creek na baada ya kazi kuanzishwa vizuri huko, waliweza kuendelea na safari zao katika Shamba la Bwana-maeneo tofautii-tofauti. Ilikuwa ni kuhusiana na ziara ya Jimbo la Ohio mnamo Februari na Machi, 1858, ambapo njozi muhimu ya pambano kuu ilitolewa kwa Bibi White katika nyumba ya shule ya umma kule Lovett's Grove. Maelezo ya njozi hii iliyochukua saa mbili yanapatikana katika *Life Sketches*, Kurasa 161, 162. Mnamo Septemba 1858, Pambano Kuu kati ya Kristo na Malaika Zake na Shetani na Malaika zake lilichapishwa. Kitabu hiki kidogo cha kurasa 219 kinajumuisha mgawanyiko wa tatu na wa mwisho wa *Maandiko ya Awali (Early Writings)*. {**EW xxxi3**}

Machapisho madogo ya miaka kumi na mitano ya kwanza ya kazi ya Bibi White yalikuwa yafuatwe na vitabu vingi vikubwa vinavyohusu mada nyingi muhimu kwa wale wanaozishika amri za Mungu na

kuwa na imani ya Yesu Kristo. Hata hivyo maandiko ya awali kabisa daima yatakuwa ni ya kupendwa sana na mioyo ya Waadventista wa Sabato wote. **{EW xxxii1}**

—Wadhamini wa Machapisho ya Ellen G. White

Washington, D.C.

Machi, 1963.

**Yaliyomo**

Dibaji . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .

Dibaji ya Toleo la Kwanza la "Uzoefu na Maoni"… 5

Utangulizi wa Kihistoria. . . . . . . . . ……. . . . . . . . . . . . . . 7

Mwamko Mkuu wa Marejeo. . . . . . . . . . . . . . … . . .8

Kuhesabu Nyakati za Unabii……………………… 9

Kukatishwa Tamaa na Matokeo Yake……………..15

Maono Yatolewa kwa Ellen Harmon . . . . . . . . . . . 16

Makundi Mawili ya Wanamarejeo . . . . . . . . . . . . . 17

Kupambazuka kwa Nuru ya Patakatifu . . . . . . . . . 18

Kweli Zinathibitishwa na Njozi . . . . . . . . . . . . . . . . 19

Mwanzo wa Utunzaji wa Sabato. . . . . . . . . . . . . …20

Umuhimu wa Sabato Wafunuliwa. . . . . . . . . . . …. 21

Mikutano Muhimu Juu ya Sabato. . . . . . . . . . . 22

Waasisi Waanza Kuchapisha. . . . . . . . . . . .. . . . . . . 24

Kuanzishwa kwa *Review and Herald* . . . . . . . . . . 25

Kazi ya Uchapishaji Inakua . . . . . . . . . . . . . . . . . . 26

Battle Creek Inakuwa Kituo cha Uchapishaji . . . . 26
“Mlango Uliofungwa” na “Mlango Ulio Wazi” . . 27
Njia Mbili za Kutoka Katika Mkanganyiko……. 29
Wito kwa Ajili ya Mfumo wa Kanisa. . . . . . . . . . . 30
Njozi Kuhusu Pambano Kuu … . . . . . . . . . . . . . . . 31
**Yaliyomo.** . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . ………………….7

**Uzoefu na Maoni** ………………………………….11
Njozi Yangu ya Kwanza . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 13

Maandiko Yaliyorejelewa kwenye Ukurasa

Uliotangulia .. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 24
Njozi za Baadaye. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 32

Kutiwa Muhuri . . . . . . .. . . . . . . . . . . . . . . . . . 36
Upendo wa Mungu kwa Watu Wake . . . . . . . . 39
Kutikiswa kwa Nguvu za Mbingu . . . . . . . . . . .. 41
Mlango Ulio Wazi na Uliofungwa. … . . . 41
Kujaribiwa kwa Imani Yetu. . . . . . .. 46

Kwa “Kundi Dogo” . . . . . . 48
Mapigo ya Mwisho na Hukumu……52
Mwisho wa Zile Siku 2300. . . . . . . . . 54
Wajibu kwa Kuzingatia Wakati wa Taabu . . . . .
56
Wajumbe . . . . . ……..61
Alama ya Mnyama . . . .  . . . . . 64
Kipofu Kumwongoza Kipofu . . . . .  . . 68
Maandalizi kwa Ajili ya Mwisho . . . .. . . . . . . . . .
69
Maombi na Imani . . . . . . . . . . . . . . .…..72
Muda wa Kukusanyika. . . . . . . . . . . . . 74
Ndoto za Bibi White. . . . . . . . . .. .  ….78
Ndoto ya William Miller…………………………… 81
**Nyongeza** ……………………85
Sura ya 20--Maelezo .. . . . . . .  . . . . . . . . 85
Sura ya 21--Utaratibu wa Injili. . . . 97
Sura ya 22--Matatizo ya Kanisa. . . . . . 104
Sura ya 23--Tumaini la Kanisa . . . .107
Sura ya 24--Maandalizi kwaajili ya Ujio wa

Kristo . .111

Sura ya 25--Uaminifu Katika Mikutano ya Kijamii. . . .114

Sura ya 26--Kwa Wasio na Uzoefu .. . .. 118

Sura ya 27--Kujikana Nafsi .......... 121

Sura ya 28--Kutokuheshimu Vitu Vitakatifu . .. 122

Sura ya 29--Wachungaji wa Uongo . . . . 122

Sura ya 30--Karama ya Mungu kwa Mwanadamu . . .125

**Karama za Roho, Kitabu cha 1** ................133

Utangulizi . . . . . . . . 133

Sura ya 31-Anguko la Shetani . . . . . . . . . . 145

Sura ya 32-Anguko la Mwanadamu .. . . . . 147

Sura ya 33-Mpango wa Wokovu. .. . . . . . . . . . 149

Sura ya 34-Ujio wa Kwanza wa Kristo . . . . . . . 153

Sura ya 35-Huduma ya Kristo . . . . . 158

Sura ya 36-Kubadilika Sura . . . 162

Sura ya 37-Kusalitiwa kwa Kristo . . 165

Sura ya 38-Sura ya Kuhukumiwa kwa Kristo . . 169

Sura ya 39-Kusulubiwa kwa Kristo . . . 175

Sura ya 40-Kufufuka kwa Kristo . . . . . 181

Sura ya 41-Kupaa kwa Kristo . . 190

Sura ya 42-Wanafunzi wa Kristo . . .192

Sura ya 43-Kifo cha Stefano . . . . 197

Sura ya 44-Kuongoka kwa Sauli . . . 200

Sura ya 45-Wayahudi Waamua Kumuua Paulo . . 202

Sura ya 46-Paulo Atembelea Yerusalemu . . . 206

Sura 47-Uasi Mkuu . . . . .. . . 210

Sura ya 48-Siri ya Uovu . . ......213

Sura ya 49-Kifo si Uzima wa Milele katika Mateso . . . . . 218

Sura ya 50-Matengenezo. . . . 222

Sura ya 51-Umoja wa Kanisa na Dunia. . 226

Sura ya 52-Sura ya 50-William Miller . .. . . . . .

229

Sura ya 53-Ujumbe wa Malaika wa Kwanza....232

Sura ya 54-Ujumbe wa Malaika wa Pili. . . . . . . 237

Sura ya 55-Vuguvugu la Wana marejeo Laoneshwa kwa Mfano . ...... 240

Sura ya 56-Mfano Mwingine. . . 245

Sura ya 57-Patakatifu. . . .. . . . . 250

Sura ya 58-Ujumbe wa Malaika wa Tatu. . . . . . 254

Sura ya 59- Jukwaa Imara. ... ...258

Sura ya 60-Umizimu . . . . . 262

Sura ya 61Tamaa . . . . 266

Sura ya 62-Kutikiswa ......-......... . 269

Sura ya 63-Dhambi za Babeli . . . . . . . . . 273

Sura ya 64-Kilio Kikuu . . . . . . . . . . . . . 277

Sura ya 65-Ujumbe wa Tatu Wafungwa . . . . . . . 279

Sura ya 66-Wakati wa Taabu . . . . . . . . . 282

Sura ya 67-Kukombolewa kwa Watakatifu . . . 285

Sura ya 68-Thawabu ya Watakatifu . . . . . . . 288

Sura ya 69-Dunia Yabaki Ukiwa . . 289

Sura ya 70-Ufufuo wa Pili. . . .. . 292

Sura ya 71-Mauti ya pili. .... 294

**Kiambatisho** ................................ 297

## SEHEMU YA KWANZA

## Uzoefu na Maoni

Kwa maombi ya marafiki wapendwa nimekubali kutoa muhtasari mfupi wa uzoefu na maoni yangu, kwa tumaini kwamba utawachangamsha na kuwaimarisha watoto wa Bwana walio wanyenyekevu, wenye kumtumaini.{EW 11.1}

Nilipokuwa na umri wa miaka kumi na moja niliongoka, na nilipokuwa na umri wa miaka kumi na miwili nilibatizwa, na kujiunga na Kanisa la

Wamethodisti. [Bibi White alizaliwa Gorham, Maine, Novemba 26, 1827.] Nilipokuwa na umri wa miaka kumi na tatu nilimsikia William Miller akitoa mfululizo wake wa pili wa mahubiri huko Portland, Maine. Wakati huo nilihisi kwamba sikuwa mtakatifu, sikuwa tayari kumwona Yesu. Na pale mwaliko ulipotolewa kwa washiriki wa kanisa na wenye dhambi kuja mbele kwa ajili ya maombi, nilikubali kwa moyo fursa ile ya kwanza, kwa maana nilijua kwamba ilibidi kazi kubwa ifanyike kwa ajili yangu ili kuniandaa kwa ajili ya mbingu. Roho yangu ilikuwa na kiu ya wokovu kamili unaotolewa bure, lakini sikujua jinsi ya kuupata. {EW 11.2}

Katika mwaka wa 1842, nilihudhuria mikutano ya Marejeo huko Portland, Maine mara kwa mara, na niliamini kabisa kwamba Bwana alikuwa anakuja. Nilikuwa na njaa na kiu ya wokovu mkamilifu, kupatana kabisa na mapenzi ya Mungu. Mchana na usiku nilikuwa nikijitahidi kuipata hazina hii yenye thamani kubwa sana, ambayo utajiri wote wa dunia haungeweza kuinunua. Nilipokuwa nimeinama mbele za Mungu nikiomba kwa ajili ya baraka hii, wajibu wa kwenda kuomba katika mkutano wa maombi wa hadhara uliwasilishwa mbele yangu. Sikuwahi kuomba kwa sauti katika mkutano, nami

nilirudi nyuma kutoka katika wajibu huu, nikiogopa kwamba ikiwa ningejaribu kuomba ningefadhaishwa. Kila wakati nilipokwenda mbele za Bwana kwa ajili ya maombi ya faragha wajibu huu usiotimizwa ulijitokeza, hata nikaacha kuomba, na kutulia katika hali ya huzuni, na hatimaye nikawa katika hali ya kuvunjika moyo sana. {**EW 11.3**}

Akili yangu ilibaki katika hali hii kwa muda wa majuma matatu, bila kuwa na hata mwale mmoja wa nuru wa kupenya haya mawingu mazito ya giza yaliyonizunguka. Ndipo nilipopata na ndoto mbili ambazo zilinipa mwali hafifu wa nuru na tumaini. [Ndoto zinazorejelewa hapa zitapatikana kwenye ukurasa wa 78-81.] Baada ya hapa nilifungua akili/mawazo yangu kwa mama yangu aliye mwaminifu. Mama aliniambia kwamba sikuwa nimepotea na akanishauri niende kumwona ndugu Stockman, ambaye wakati ule aliwahubiria Wanamarejeo katika eneo la Portland. Nilikuwa na imani kubwa kwake, kwa kuwa alikuwa mtumishi mwaminifu na mpendwa wa Kristo. Maneno yake yalinigusa moyo na kunipa matumaini. Nilirudi nyumbani na tena nikaenda mbele ya Bwana, na kuahidi kwamba ningefanya lolote linalowezekana na kuteseka kwa chochote kile ikiwa ningeweza

kupata tabasamu za Yesu. Wajibu ule ule uliwasilishwa kwangu. Mkutano wa maombi ulikuwa unaenda kufanyika jioni ile, ambao nilihudhuria, na wakati wengine walipopiga magoti kuomba, nilisujudu pamoja nao huku nikitetemeka, na baada ya wawili au watatu kuomba, nilifungua kinywa changu kwa maombi kabla sijatambua kwamba nimefanya hivyo, na ahadi za Mungu zilionekana kwangu kama lulu nyingi za thamani ambazo zingepokelewa kwa njia pekee ya kuomba kwa ajili yake. Nilipokuwa nikiomba, mzigo na uchungu wa roho ambao nilikuwa nimeuhisi kwa muda mrefu uliniacha, na baraka za Mungu zilinijia kama umande mtulivu. Nilimpa Mungu utukufu kwa kile nilichohisi, lakini nilitamani sana zaidi. Sikuweza kuridhika hadi nilipojazwa na utimilifu wa Mungu. Upendo usioelezeka kwa Yesu ulijaza roho yangu. Wimbi baada ya wimbi la utukufu lilipita juu yangu, mpaka mwili wangu ukakamaa. Kila kitu kilikuwa kimefungwa kwangu isipokuwa Yesu na utukufu, na sikujua chochote kuhusu kile kilichokuwa kikipita karibu nami. **{EW 12.1}**

Nilibaki katika hali hii ya mwili na akili kwa muda mrefu, na nilipotambua kile kilichokuwa karibu nami, kila kitu kilionekana kuwa kimebadilika.

Kila kitu kilionekana kuwa na utukufu na kipya, kana kwamba kinatabasamu na kumsifu Mungu. Wakati huo nilikuwa tayari kumkiri Yesu kila mahali. Kwa miezi sita hakuna wingu hata moja la giza lilipita katika akili yangu. Roho yangu ilikuwa ikinywa mafunda mengi ya wokovu kila siku. Nilidhani kwamba wale waliompenda Yesu wangependa ujio Wake, kwa hivyo nilienda kwenye mkutano wa darasa na kuwaambia kile Yesu alichokuwa amenitendea na utimilifu nilioufurahia kupitia kuamini kwamba Bwana alikuwa anakuja. Kiongozi wa darasa alinikatiza, akisema, "Kupitia Umethodisti"; lakini sikuweza kutoa utukufu kwa Umethodisti wakati ilikuwa ni Kristo na tumaini la ujio Wake, uliokuwa karibu, ndivyo vilikuwa vimeniweka huru. {EW 12.1}

Wengi wa familia ya baba yangu walikuwa waumini kabisa wa marejeo, na kwa kushuhudia mafundisho haya matukufu, saba kati yetu kwa wakati mmoja tulifukuzwa kutoka katika Kanisa la Wamethodisti. Wakati huu maneno ya nabii yalizidi mno kuwa ya thamani kwetu: "Ndugu zenu wawachukiao ninyi, waliowatupa kwa ajili ya Jina Langu, wamesema, Na atukuzwe Bwana, tupate kuiona furaha yenu; lakini watatahayarika." Isaiah

66:5. {EW 13.1}

Kuanzia wakati huu, hadi Desemba, 1844, furaha, majaribio, na masikitiko yangu yalikuwa kama ya marafiki wangu wapendwa Wanamarejeo walionizunguka. Wakati huu nilimtembelea mmoja wa dada zetu wa Kiadventista, na asubuhi tulisujudu kuzunguka madhabahu ya familia. Hakukuwa na uchangamfu mahali hapa, na kulikuwapo na watu watano tu, wote wanawake. Nilipokuwa nikiomba, uweza wa Mungu ulinijia kwa jinsi ambayo sikuwahi kuhisi hapo awali. Nilifungwa katika njozi ya utukufu wa Mungu, na ulionekana kama vile ulikuwa ukipanda juu zaidi na zaidi kutoka duniani, na nilioneshwa kitu fulani kuhusu safari za watu wa Marejeo kwenda katika Mji Mtakatifu, kama ilivyosimuliwa hapa chini. {EW 13.2}

## Sura ya 1

## Njozi Yangu ya Kwanza

[Mtazamo huu ulitolewa mara tu baada Kukatishwa Tamaa Kukuu kwa Marejeo mnamo 1844, na ulichapishwa kwa mara ya kwanza mnamo mwaka

1846. Ni matukio machache tu ya siku zijazo yalionekana wakati huo. Maoni ya baadaye yamekuwa kamili zaidi. [Angalia pia kiambatisho.] Kama Mungu alivyonionesha safari za watu wa Marejeo kwenda katika Mji Mtakatifu na thawabu kubwa watakazopewa wale wanaosubiri kurudi kwa Bwana wao kutoka kwenye arusi, inaweza kuwa wajibu wangu kuwapa mfano mfupi wa kile ambacho Mungu amenifunulia. Watakatifu wapendwa wana majaribio mengi watakayopaswa kuyapitia. Lakini dhiki yetu nyepesi, iliyo ya muda wa kitambo tu, yatufanyia utukufu wa milele uzidio kuwa mwingi sana - wakati hatuangalii vitu vinavyoonekana, kwa maana vitu vinavyoonekana ni vya muda tu, lakini vitu visivyoonekana ni vya milele. Nimejaribu kuleta habari njema na zabibu chache kutoka Kanaani ya mbinguni, jambo ambalo lingefanya watu wengi kunipiga kwa mawe, kama vile kutano lilivyosema kwamba Kalebu na Yoshua wapigwe kwa mawe kwa sababu ya taarifa yao. (Hesabu 14:10). Lakini ninawaambia ninyi ndugu na dada zangu katika Bwana, hii ni nchi nzuri, nasi tunaweza kwenda na kuimiliki. {EW 13.3}

Nilipokuwa nikiomba kwenye madhabahu ya familia, Roho Mtakatifu alianguka juu yangu, na

nilionekana kama vile nilikuwa ninainuka juu zaidi na zaidi, juu zaidi ya ulimwengu wa giza. Niligeuka kuwatazama Wanamarejeo walioko duniani, lakini sikuweza kuwapata, ndipo sauti iliponiambia, "Angalia tena, na uangalie juu kidogo."Nami nikainua macho yangu, na nikaona njia iliyonyoka na nyembamba, imekwa juu ya ulimwengu. Katika njia hii watu wa Wanamarejeo walikuwa wakisafiri kwenda katika mji, ambao ulikuwa mwisho wa njia. Walikuwa na nuru angavu iliyowekwa nyuma yao mwanzoni mwa njia, ambayo malaika aliniambia kuwa ilikuwa ni kilio cha usiku wa manane. Nuru hii iliangaza kote katika njia na ikatoa nuru kwa ajili miguu yao ili wasijikwae. Ikiwa walikaza macho yao kwa Yesu, ambaye alikuwa mbele yao, ambaye alikuwa akiwaongoza kwenda mjini, basi, walikuwa salama. Lakini punde baadhi walichoka, na kusema kuwa mji ulikuwa mbali mno, nao walitarajia kuwa wangekwishauingia mapema. Ndipo Yesu angewatia moyo kwa kuuinua mkono Wake wa kulia wenye utukufu, na kutoka katika mkono Wake nuru ilikuja ambayo iliyotanda juu ya kundi la Waadventista, nao wakapiga kelele, “Haleluya!” Wengine bila subira waliikataa nuru ile iliyokuwa nyuma yao na kusema kuwa si Mungu aliyekuwa

amewaongoza hadi sasa. Nuru iliyokuwa nyuma yao ilizimika, ikiacha miguu yao katika giza kamili, nao walijikwaa na kupoteza alama za kuwaongoza njia na kumpoteza Yesu, na walianguka kutoka katika njia, na kwenda chini katika ulimwengu wa giza na ulio mwovu. Punde [angalia kiambatisho.] tulisikia sauti ya Mungu kama ya maji mengi, ambayo ilitupa siku na saa ya kuja kwa Yesu. Watakatifu walio hai, 144,000 kwa idadi, waliijua na kuifahamua sauti ile, wakati waovu walidhani kuwa ilikuwa ni ngurumo na tetemeko la ardhi. Mungu alipotamka muda, alimimina juu yetu Roho Mtakatifu, na nyuso zetu zilianza kuwaka na kung’aa kwa utukufu wa Mungu, kama Musa alivyokuwa aliposhuka kutoka katika Mlima Horebu. {EW 14.1}

Wale 144,000 wote walitiwa muhuri na kuwa na umoja mkamilifu. Kwenye vipaji vya nyuso zao kuliandikwa, Mungu, Yerusalemu Mpya, na nyota tukufu iliyo na Jina jipya la Yesu. Kwa ajili ya hali yetu takatifu ya furaha, waovu walikasirishwa, na wangekimbia kwa nguvu nyingi kuweka mikono yao juu yetu kutusukuma gerezani, ambapo tungenyosha mkono kwa Jina la Bwana, nao wangeanguka chini bila msaada. Hapo ndipo

ilikuwa kwamba sinagogi la Shetani lilijua kuwa Mungu alitupenda sisi ambao tungewaoshana miguu na kuwasalimu ndugu kwa busu takatifu, nao waliabudu miguuni petu. {**EW 15.1**}

Mara macho yetu yalivutwa kuelekea upande wa mashariki, kwa kuwa wingu dogo jeusi lilitokea, lenye ukubwa kama nusu ya mkono wa mwanadamu, ambalo sote tulijua kuwa ni ishara ya Mwana wa Adamu. Sisi sote kwa ukimya mzito tulilitazama lile wingu lilipokaribia na likazidi kuwa angavu zaidi, tukufu, na tukufu zaidi, hadi lilipokuwa wingu kubwa jeupe. Sehemu ya chini ilionekana kama moto, upinde wa mvua ulikuwa juu ya wingu lile, wakati ambapo kulizunguka walikuwa ni malaika elfu kumi, wakiimba wimbo mzuri mno; na juu yake aliketi Mwana wa Adamu. Nywele zake zilikuwa nyeupe na zenye mawimbi na kujilaza mabegani Mwake; na juu ya kichwa Chake kulikuwa na taji nyingi. Miguu yake ilikuwa na mwonekano wa moto, na katika mkono Wake wa kulia kulikuwa na mundu mkali, na katika mkono Wake wa kushoto kulikuwa na tarumbeta ya fedha. Macho Yake yalikuwa kama miali ya moto, ambayo yaliwachunguza kabisa watoto Wake kikamilifu. Kisha nyuso zote zikafifia rangi kwa hofu, na wale

ambao Mungu aliwakataa zikawa nyeusi. Ndipo sote tukapaza sauti, “Ni nani atakayeweza kusimama?  Je vazi langu halina doa?” Kisha malaika wakaacha kuimba, na kulikuwapo na wakati wa ukimya wa kutisha, wakati Yesu aliposema: "Wale walio na mikono safi na mioyo safi wataweza kusimama; Neema Yangu yawatosha.” Kwa maneno haya nyuso zetu ziliangaza, na furaha ilijaa kila moyo. Na malaika wakapaza sauti zaidi na kuimba tena, wakati wingu lile likiwa linazidi kuikaribia dunia. {**EW 15.1**}

Ndipo tarumbeta ile ya Yesu ya fedha ilitoa sauti, huku akishuka juu ya wingu, akiwa amezungukwa na moto. Kisha aliinua macho na mikono Yake kuelekea mbinguni, na kupaza sauti, “Amkeni! Amkeni! Amkeni! enyi mliolala katika mavumbi, na kuinuka.” Ndipo kulipokuwa na tetemeko kubwa la ardhi. Makaburi yalifunguka, na wafu walitoka wakiwa wamevikwa kutokufa. Wale 144, 000 walipiga kelele, “Haleluya!” walipowatambua marafiki zao waliokuwa wametengwa nao kwa mauti, na papo hapo tulibadilishwa na kunyakuliwa pamoja nao tupate kumlaki Bwana angani. {**EW 16.1**}

Na sote tuliingia ndani ya wingu lile, na kwa siku

saba tulikuwa tunapaa kuelekea katika bahari ya kioo, wakati Yesu alipozileta taji zile, na kuziweka juu ya vichwa vyetu kwa mkono Wake wa kuume. Alitupa vinubi vya dhahabu na mitende ya ushindi. Hapa kwenye bahari ya kioo wale 144,000 walisimama katika mraba kamili. Baadhi yao walikuwa na taji zenye kung'aa sana, zingine hazikung'aa sana. Baadhi ya taji zilionekana kuwa nzito kwa kujaa nyota, wakati zingine zilikuwa na nyota chache tu. Wote waliridhika kabisa na taji zao. Na wote walikuwa wamevikwa joho jeupe la utukufu, kuanzia mabegani hadi miguuni. Malaika walituzunguka sote tulipokuwa tukitembea juu ya bahari ya kioo kuelekea kwenye lango la mji. Yesu aliuinua mkono Wake wenye nguvu na ulio mtukufu, akalishika lango la lulu, akalizungusha kwenye bawaba zake na kulifungua, na kutuambia, "Mmeyafua mavazi yenu katika damu Yangu, mlisimama imara kwa ajili ya Ukweli Wangu, ingieni ndani." Sote tulitembea kuingia ndani na tulijisikia kwamba tulikuwa na haki kamili katika mji. {EW 16.2}

Hapa tuliuona mti wa uzima na kiti cha enzi cha Mungu. Kutoka katika kiti cha enzi ulitokea mto safi wa maji, na kila upande wa mto huu kulikuwapo mti

wa uzima. Upande mmoja wa mto kulikuwako na shina la mti, na shina upande wa pili wa mto, yote mawili yakiwa ni ya dhahabu halisi, angavu. Mwanzoni nilidhani kuwa niliona miti miwili. Niliangalia tena, na nikaona kwamba ilikuwa imeungana kwa juu na kuwa mti mmoja. Hivyo kulikuwa na mti wa uzima katika kila upande wa mto ule. Matawi yake yaliinama na kufika mahali tulipokuwa tumesimama, na matunda yalikuwa matukufu; yalionekana kama dhahabu iliyochanganywa na fedha. {**EW 17.1**}

Sisi sote tulikwenda chini ya mti ule na kuketi chini kutazama utukufu wa mahali hapo, wakati Ndugu Fitch na Stockman, [tazama kiambatisho.] ambao walikuwa wameihubiri injili ya ufalme, na ambao Mungu alikuwa amewaweka kaburini ili apate kuwaokoa, walitujia na kutuuliza kuhusu yale tuliyoyapitia wakati walipokuwa wamelala. Tulijaribu kukumbuka majaribio yetu yaliyokuwa makubwa kabisa, lakini yalionekana kuwa madogo sana yakilinganishwa na uzito wa utukufu wa milele uzidio kuwa mwingi sana, ambao ulituzunguka kiasi kwamba hatukuweza kutamka kwa sauti, na sote tulipaza sauti, "Haleluya, **Hakuna gharama kubwa, kufika mbinguni!"** nasi tuligusa vinubi vyetu

vitukufu, na kuyafanya matao ya mbinguni kurindima. {**EW 17.2**}

Yesu akituongoza sisi sote tulishuka kutoka katika mji ule, kuja katika dunia hii, juu ya mlima mkubwa na wenye nguvu, ambao haukuweza kumbeba Yesu. Nao ulipasuka vipande vipande, kukawa na uwanda mkubwa sana. Ndipo tulipoangalia juu, na kuuona, mji ule mkubwa, wenye misingi kumi na miwili, na milango kumi na miwili, na kila upande milango mitatu, na malaika yu katika kila mlango. Sisi sote tulipaza sauti zetu na kusema: "Mji, mji Mkubwa, unakuja; unashuka kutoka kwa Mungu mbinguni;" na ukaja na kutua na kukaa mahali pale ambapo tulikuwa tumesimama. Kisha tukaanza kuangalia vitu vitukufu vilivyokuwa nje ya mji. Huko nikaona nyumba za fahari mno, ambazo zilikuwa na mwonekano wa fedha, zikitegemezwa na nguzo nne zilizopakwa kwa lulu za kupendeza mno kutazama. Hizi zilikuwa zikaliwe na watakatifu. Ndani ya kila moja kulikuwamo na rafu ya dhahabu. Niliwaona watakatifu wengi wakiingia ndani ya nyumba hizi, wakivua taji zao

zinazometameta na kuziweka juu ya rafu, kisha wakatoka kwenda katika uwanja nje ya nyumba zao kufanya kitu fulani na ardhi; si kama tunavyopaswa kufanya na ardhi hapa; la hasha (aina ya kilimo yumkini). Nuru tukufu iliangaza kuzunguka vichwani mwao, na daima walikuwa wakipiga kelele na kutoa sifa kwa Mungu. {**EW 17.3**}

Niliona uwanja mwingine uliojaa maua ya kila aina, na nilipokuwa nikiyang'oa, nilipaza sauti, "Hayatafifia kamwe." Kilichofuata niliona shamba la nyasi ndefu, za kupendeza sana kutazama; zilikuwa za kijani kibichi na za mfano wa fedha na dhahabu, wakati zikipeperuka kwa fahari kwa ajili ya utukufu wa Mfalme Yesu. Kisha tukaingia katika mbuga ya malisho iliojaa kila aina ya wanyama- simba, mwana-kondoo, chui, na mbwa mwitu, wote wakiwa wameungana kwa umoja kamili. Tulipita katikati yao, nao walitufuata kwa amani. Kisha tukaingia kwenye msitu, si kama misitu yenye giza tuliyo nayo hapa duniani; la, hasha; bali ni myepesi, na yote yenye fahari; matawi ya miti yaliyumba-yumba, na sote tukapaza sauti, "Tutakaa salama nyikani na kulala msituni." Tulipita msituni, kwa maana tulikuwa njiani kuelekea katika Mlima Sayuni.{**EW 18.1**}

Tulipokuwa tukisafiri, tulikutana na watu ambao pia walikuwa wakiangalia utukufu wa mahali pale. Niliona rangi nyekundu kama kingo katika mavazi yao; taji zao ziling'aa; mavazi yao yalikuwa meupe safi. Tulipowasalimu, nilimwuliza Yesu hawa ni akina nani. Alisema walikuwa ni wafia dini ambao walikuwa wameuawa kwa ajili Yake. Pamoja nao kulikuwa na kundi lisilohesabika la watoto; wao pia walikuwa na pindo jekundu katika mavazi yao. Mlima Sayuni ulikuwa mbele yetu, na juu ya mlima kulikuwa na hekalu tukufu, na kuuzunguka kulikuwa na milima mingine saba, ambayo ilimea maua ya waridi na yungiyungi. Nami niliwaona watoto wadogo wakipanda, au, ikiwa walichagua, walitumia mabawa yao madogo na kuruka, hadi juu ya milima na kung'oa maua yale yasiyonyauka kamwe. Kulikuwa na miti ya kila aina kuzunguka hekalu kwa ajili ya kupapamba mahali hapo: mteashuri, mtidhari, mberoshi, mbono, mhadasi, mkomamanga, na mtini ulioinamishwa kwa uzito wa tini zake zilizokuja kwa wakati ufaao-hizi zilipafanya mahali hapo pote kuwa na utukufu. Tulipokuwa tunakaribia kuingia katika hekalu takatifu, Yesu aliinua sauti yake nzuri na kusema, “Ni wale 144,000 tu, ndiyo watakaoingia mahali hapa,” na tulipaza sauti,

“Haleluya.” {EW 18.2}

Hekalu hili lilitegemezwa kwa nguzo saba, zote za dhahabu angavu, iliyopambwa kwa lulu ya kupendeza mno. Mambo ya ajabu niliyoyaona pale siwezi kuyaelezea. Laiti ningeweza kuzungumza kwa lugha ya Kanaani, ndipo ningeweza kuelezea kidogo kuhusu utukufu wa ulimwengu ule ulio bora zaidi. Niliona pale mbao za mawe ambamo ndani yake majina ya hao 144,000 yaliandikwa kwa herufi za dhahabu. Baada ya kuuona utukufu wa Hekalu, tulitoka nje, na Yesu akatuacha na kwenda mjini. Punde tulisikia tena sauti  Yake nzuri, ikisema, “Njoni, watu Wangu, mmetoka katika dhiki kubwa, mmeyafanya mapenzi Yangu; mmeteseka kwa ajili Yangu; ingieni kula chakula cha jioni, kwa maana nitajifunga, na kuwahudumia.” Tulipaza sauti, “Haleluya! Utukufu! Na kuingia mjini. Kisha nikaona meza ya fedha safi; ilikuwa na urefu wa maili nyingi, lakini macho yetu yaliweza kuiona yote. Niliona matunda ya mti wa uzima, mana, lozi, tini, komamanga, zabibu, na aina nyingine nyingi za matunda. Nilimwomba Yesu aniruhusu nile hayo matunda. Yeye Alisema, “Si kwa sasa. Wale wanaokula matunda ya nchi hii hawarudi tena duniani. Lakini baada ya muda kitambo, kama

mtakuwa waaminifu, mtakula matunda ya mti wa uzima na kunywa maji kutoka katika chemchemi." Naye alisema: "Mnapaswa kurudi tena duniani na kusimulia wengine kile nilichodhihirisha kwenu." Kisha malaika akanibeba kwa upole hadi kwenye ulimwengu huu wa giza. Wakati mwingine nadhani kuwa siwezi kukaa hapa tena; vitu vyote vya dunia vinaonekana kuwa ni vya kutia huzuni. Ninajisikia mpweke sana hapa, kwa sababu nimeiona nchi iliyo nzuri zaidi. Laiti ningelikuwa na mabawa kama njiwa, basi ningeruka na kwenda kupumzika! {**EW 19.1**}

*****

Baada ya kutoka katika njozi, kila kitu kilionekana kuwa kimebadilika; utusitusi ulitanda juu ya yote niliyoyaona. Lo, ni jinsi gani ulimwengu huu ulivyoonekana kuwa giza kwangu. Nilitoa machozi nilipojikuta niko hapa, na kujisikia kutamani sana kuwa nyumbani (homesick). Nilikuwa nimeuona ulimwengu ulio bora, nao ulikuwa umeuvuruga na kuuhafifisha ulimwengu huu tunaoishi, katika mawazo yangu. Niliwasimulia kundi letu dogo huko Portland mandhari ile, ambao wakati huo waliamini kabisa kuwa [njozi ile] ilitoka kwa Mungu. Ule ulikuwa ni wakati wenye nguvu.

Uzito wa umilele ulitulia juu yetu. Karibu wiki moja baada ya hii njozi, Bwana alinipa mandhari nyingine na kunionesha majaribu ambayo ilibidi niyapitie, na kwamba ni lazima niende na kuwasimulia wengine kile Alichonifunulia, na kwamba nitapaswa kukabiliana na upinzani mkubwa na kuteseka kwa uchungu wa roho kwa kwenda. Lakini malaika yule alisema, “Neema ya Mungu yakutosha; Yeye atakushikilia.” {**EW 20.1**}

Baada ya kutoka katika njozi hii, nilitaabika sana. Afya yangu ilikuwa hafifu sana, na nilikuwa na umri wa miaka kumi na saba tu. Nilijua kuwa wengi walikuwa wameanguka kwa kujiinua, na nilijua kuwa ikiwa kwa njia yoyote ningelijiinua, Mungu angeniacha, na hakika ningepotea. Nilimwendea Bwana katika maombi na kumwomba aweke mzigo huu kwa mtu mwingine. Ilionekana kwangu kwamba nisingeweza kuubeba. Nililala kifudifudi kwa muda mrefu, na nuru yote niliyoweza kupata ilikuwa, "Wajulishe wengine kile nilichokufunulia." {**EW 20.2**}

Katika njozi yangu iliyofuata nilimwomba Bwana kwa bidii, kwamba, ikiwa ni lazima niende kuyasimulia yale aliyonionesha, basi Yeye Mwenyewe anizuie nisipate kujiinua. Kisha

alinionesha kuwa ombi langu lilijibiwa, na ikiwa ningekuwa katika hatari ya kujiinua mkono Wake ungewekwa juu yangu, na ningeteseka kwa ugonjwa. Malaika yule alisema, "Ukiutoa ujumbe huu kwa uaminifu, na kuvumilia hadi mwisho, utakula matunda ya mti wa uzima na kunywa maji ya mto wa uzima." {**EW 21.1**}

Punde taarifa ilienezwa kote kwamba maono hayo yalikuwa matokeo ya kiinimacho (mesmerism), [tazama kiambatisho.] na Waadventista wengi walikuwa tayari kuamini na kusambaza taarifa hiyo. Tabibu ambaye alikuwa ni mtia kiinimacho maarufu aliniambia kwamba mandhari niliyoyaona yalikuwa ni kiinimacho, kwamba nilikuwa mtu rahisi sana kufanyiwa viinimacho, na kwamba angeweza kunitia kiinimacho na kunipa maono. Nilimwambia kwamba, Bwana alikuwa amenionesha katika njozi kwamba kiinimacho kilitoka kwa ibilisi, kutoka katika shimo lisilokuwa na mwisho, na kwamba muda si mrefu kingekwenda huko, pamoja na wale ambao waliendelea kukitumia. Ndipo nilipompa uhuru wa kunitia kiinimacho kama angeweza. Alijaribu kwa zaidi ya nusu saa, akitumia nguvu tofauti, na kisha alisalimu amri kwa kukata tamaa. Kwa imani kwa Mungu niliweza kupinga uwezo

wake, kiasi kwamba ‘ushirikina’ wake huo haukuniathiri hata kidogo. {EW 21.2}

Kama ningepata njozi katika mkutano, wengi wangesema kwamba ilikuwa ni msisimko na kwamba mtu fulani alikuwa amenitia kiinimacho (mesmerism). Kisha ningekwenda peke yangu msituni, ambako hakuna jicho wala sikio ila la Mungu lingeweza kuniona au kunisikia, na kumwomba, na wakati mwingine angenipa maono huko. Kisha nilifurahi, na nikawaambia kile ambacho Mungu alikuwa amenifunulia mimi nikiwa peke yangu, ambapo hakuna mwanadamu angeweza kunishawishi. Lakini niliambiwa na baadhi ya watu kuwa nilikuwa nimejitia kiinimacho mimi mwenyewe. Lo, niliwaza, je imefikia hapa kwamba wale ambao kwa uaminifu, wanakwenda kwa Mungu peke yao kuomba ahadi Zake na kudai wokovu Zake, wanashinikiziwa kwa nguvu kwamba wako chini ya uwezo mbaya na wenye kuharibu roho wa kiinimacho? Je, sisi tunamwomba Baba yetu mwema aliye mbinguni kwa ajili ya “mkate,” na kisha tunapokea tu “jiwe” au “nge”? Mambo haya yaliijeruhi roho yangu, na kuikamua-kamua/kuisongonyoa roho yangu kwa uchungu mkali, karibu ya kukata tamaa, wakati ambapo

wengi wangetaka kunifanya niamini kwamba hakukuwa na Roho Mtakatifu na kwamba uzoefu wote ambao watu watakatifu wa Mungu wameupitia ulikuwa ni kiinimacho tu au udanganyifu wa Shetani. {EW 21.3}

Kwa wakati huu kulikuwapo na ushupavu wa dini wa hali ya juu huko Maine. Wengine walijiepusha kabisa na kazi na kuwafuta ushirika wale wote ambao hawangeyakubali maoni yao kuhusu jambo hili, na vitu vingine ambavyo walivichukulia kuwa ni wajibu wa kidini. Mungu alinifunulia makosa haya katika njozi na kunituma kwa watoto Wake waliokuwa wanakosea; lakini wengi wao walikataa kabisa ujumbe huo, na kunishutumu kuwa nilikubaliana na ulimwengu. Kwa upande mwingine, Waadventista wale wa majina tu walinishutumu kuwa mshupavu, na muongo, na kwa baadhi nilionekana vibaya, kama kiongozi wa dini iliyopitiliza, shupavu wa kidini tabia ambayo kwa kweli nilikuwa nikijitahidi kuiondoa. Nyakati tofauti ziliwekwa mara kwa mara kuhusu kurudi kwa Bwana na zilihimizwa kwa ndugu; lakini Bwana alinionesha kwamba nyaka zote zingepita, kwa kuwa wakati wa taabu ni lazima uje kabla ya kuja kwa Kristo, na kwamba kila wakati ambao

uliwekwa na kupita ungedhoofisha tu imani ya watu wa Mungu. Kwa hili nilishutumiwa kuwa upande wa mtumishi mwovu ambaye alisema moyoni mwake, “Bwana wangu anachelewesha kuja Kwake” {**EW 22.1**}

Mambo haya yote yaliilemea sana roho yangu, na katika mkanganyiko huo wakati mwingine nilijaribiwa kutilia shaka uzoefu wangu mwenyewe. Wakati tulipokuwa katika maombi ya familia asubuhi moja, uweza wa Mungu ulianza kutulia juu yangu, na wazo lilipita kwa haraka akilini mwangu kwamba hilo lilikuwa ni kiinimacho, yaani nguvu za giza, nami nikawa naupinga uweza huo. Mara moja nikawa bubu na kwa muda kitambo nilipoteza fahamu juu ya kila kitu karibu nami. Kisha nikaona dhambi yangu katika kutilia shaka uweza wa Mungu, na kwamba kwa kufanya hivyo nilifanywa kuwa bubu, na kwamba ulimi wangu ungefunguliwa katika muda chini ya saa ishirini na nne. Kisha kadi ikawekwa mbele yangu, ambayo juu yake yaliandikwa mafungu (ya Biblia), hizi aya 50 za Maandiko, zilikuwa zimeandikwa kwa herufi za dhahabu. [Mafungu haya yametolewa mwishoni mwa makala haya]. Baada ya kutoka katika njozi hii, niliita niletewe sleti/ubao, na nikaandika juu yake

kwamba nilikuwa bubu, pia kile nilichoona, na kwamba nilitaka Biblia kubwa. Nilichukua Biblia na kwa haraka nikafungua mafungu yote ambayo nilikuwa nimeyaona kwenye kadi ile. Sikuweza kuongea siku nzima. Mapema asubuhi roho yangu ilijaa furaha, na ulimi wangu ulifunguliwa na ukapata kupaza sifa kuu za Mungu. Baada ya hapo sikuthubutu kuwa na shaka au hata kwa kitambo kidogo kuupinga uweza wa Mungu, hata kama watu wengine wangenifikiria vipi. {**EW 22.2**}

Mnamo mwaka 1846, nilipokuwa Fairhaven, Massachusetts, dada yangu (ambaye kwa kawaida aliandamana nami wakati huo), Dada A., Ndugu G., na mimi tulianza safiri kwa mashua ili kutembelea familia fulani kwenye Kisiwa cha Magharibi. Usiku ulikuwa unakaribia tulipoanza safari, Tulikuwa tumeenda umbali mfupi tu wakati dhoruba ilipotokea ghafla. Radi ilipiga na kimulimuli cha umeme wa radi kikaja, na mvua ilitunyeshea kwa mbubujiko mkubwa. Ilionekana wazi kuwa ilikuwa lazima tupotee, isipokuwa kama Mungu angetuokoa.{**EW 23.1**}

Nilipiga magoti ndani ya mashua na kuanza kumlilia Mungu apate kutuokoa. Na hapo juu ya mawimbi yaliyosukasuka, wakati maji yalipopita juu

ya mashua na kunyesha juu yetu, nilichukuliwa katika njozi na kuona kwamba punde kila tone la maji katika bahari lingekauka kabla hatujaangamia, kwa kuwa kazi yangu ndiyo tu ilikuwa imeanza. Baada ya kutoka katika njozi ile, hofu yangu yote iliondoka, nasi tukaimba na kumsifu Mungu; kisha mashua yetu ndogo ikawa kwetu Betheli inayoelea. Mhariri wa *The Advent Herald* amesema kwamba maono yangu yalifahamika kuwa ni "matokeo ya matendo ya kiinimacho." Lakini, ninauliza, kulikuwa na fursa gani kwa ajili ya utendaji wa kiinimacho katika wakati kama huo? Ndugu G. alikuwa na mengi zaidi ya aliyoweza kufanya ili kuiongoza mashua ile vizuri. Alijaribu kutia nanga, lakini nanga ikaburuzwa. Mashua yetu ndogo ilitupwa juu ya mawimbi na kusukumwa na upepo, huku kukiwa na giza kiasi kwamba hatukuweza kuona upande mmoja wa mashua kutoka upande mwingine. Mara nanga ilishika, na Ndugu G. Akaomba msaada. Kulikuwa na nyumba mbili katika kisiwa hicho, na ilithibitika kuwa tulikuwa karibu na moja ya nyumba hizo, lakini si ile ambayo tulitaka kwenda. Familia yote ilikuwa imekwisha kulala kupumzika isipokuwa mtoto mdogo mmoja, ambaye alisikia kwa majaliwa wito wa kuomba msaada juu ya maji. Muda si mrefu

baba yake alikuja kutupatia msaada, na, kwenye mashua ndogo, alitupeleka ufukweni. Tulitumia sehemu kubwa ya usiku huu tukimshukuru Mungu na kumsifu kwa ajili ya wema Wake wa ajabu kwetu.{**EW 23.2**}

* Mesmerism, hyponotism au viinimacho ni nguvu za giza -Sumaku ya wanyama, pia inajulikana kama mesmerism, ni nadharia iliyobuniwa na daktari wa Ujerumani Franz Mesmer katika karne ya 18. Inathibitisha kuwapo kwa nguvu ya asili isiyoonekana iliyo katika viumbe vyote vilivyo hai, ipo ndani wanadamu, wanyama, na mimea. Alidai kuwa nguvu hiyo inaweza kuwa na athari za kimwili, ikiwa ni pamoja na uponyaji.

***

## Maandiko Yaliyotajwa katika Ukurasa Uliotangulia

"Na tazama! Utakuwa bubu, usiweze kusema, mpaka siku ile yatakapotukia hayo, kwa sababu hukuyasadiki Maneno Yangu; nayo yatatimizwa kwa wakati wake." Luka 1:20. **{EW 24.1}**

"Na yote aliyo nayo Baba ni Yangu; kwa hiyo nalisema ya kwamba atatwaa katika yaliyo Yangu, na kuwapasheni habari." Yohana 16:15.**{EW 24.2}**

"Wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowajalia kutamka." Matendo ya Mitume 2:4. **{EW 24.3}**

"Basi sasa, Bwana, yaangalie matisho yao;

ukawajalie watumwa wako kunena Neno Lako kwa ujasiri wote, ukinyosha mkono Wako kuponya; ishara na maajabu vifanyike kwa Jina la Mtumishi Wako mtakatifu Yesu. Hata walipokwisha kumwomba Mungu, mahali pale walipokusanyika pakatikiswa, wote wakajaa Roho Mtakatifu, wakanena Neno la Mungu kwa ujasiri.” Matendo ya Mitume 4:29-31. **{EW 24.4}**

“Msiwape mbwa kilicho kitakatifu, wala msitupe lulu zenu mbele ya nguruwe, wasije wakazikanyaga chini ya miguu yao, wakageuka na kuwararua. Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtaona; bisheni, nanyi mtafunguliwa; kwa maana kila aombaye hupokea; naye atafutaye huona; naye abishaye atafunguliwa. Au kuna mtu yupi kwenu, ambaye, mwanawe akimwomba mkate, atampa jiwe? Au akiomba samaki, atampa nyoka? Basi ikiwa ninyi, mlio waovu, mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! Si zaidi sana Baba yenu aliye mbinguni atawapa mema wao wamwombao? Basi yoyote myatakayo mtendewe na watu, nanyi watendeeni vivyo hivyo; maana hiyo ndiyo torati na manabii. Jihadharini na manabii wa uongo, watu wanaowajia wamevaa mavazi ya kondoo, walakini kwa ndani ni mbwa-mwitu wakali.” Mathayo 7:6-12, 15. **{EW 24.5}**

“Kwa maana watatokea makristo wa uongo, na manabii wa uongo, nao watatoa ishara kubwa na maajabu; wapate kuwapoteza, kama yamkini, hata walio wateule.” Mathayo 24:24.**{EW 25.1}**

“Basi kama mlivyompokea Kristo Yesu, Bwana, enendeni vivyo hivyo katika Yeye; wenye shina na wenye kujengwa katika Yeye; mmefanywa imara kwa imani, kama mlivyofundishwa; mkizidi kutoa shukrani. Angalieni mtu asiwafanye mateka kwa elimu yake ya bure na madanganyo matupu, kwa jinsi ya mapokeo ya wanadamu, kwa jinsi ya mafundisho ya awali ya ulimwengu, wala si kwa jinsi ya Kristo.” Wakolosai 2: 6-8. **{EW 25.2}**

“Basi msiutupe ujasiri wenu, kwa maana una thawabu kuu. Maana mnahitaji saburi, ili kwamba mkiisha kuyafanya mapenzi ya Mungu mpate ile ahadi. Kwa kuwa bado kitambo kidogo sana, Yeye ajaye atakuja, wala hatakawia. Lakini mwenye haki Wangu ataishi kwa imani; Naye akisita-sita, Roho Yangu haina furaha naye. Lakini sisi hatumo miongoni mwao wasitao na kupotea, bali tumo miongoni mwa hao walio na imani ya kutuokoa roho zetu.” Waebrania 10:35-39. **{EW 25.3}**

“Kwa maana yeye aliyeingia katika raha yake

amestarehe mwenyewe katika kazi yake, kama vile Mungu alivyostarehe katika kazi zake. Basi, na tufanye bidii kuingia katika raha ile, ili kwamba mtu ye yote asije akaanguka kwa mfano uo huo wa kuasi. Maana Neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo." Waebrania 4:10-12.**{EW 25.4}**

"Nami niliaminilo ndilo hili, ya kwamba Yeye aliyeanza kazi njema mioyoni mwenu ataimaliza hata siku ya Kristo Yesu ... Lakini mwenendo wenu na uwe kama inavyoipasa Injili ya Kristo, ili, nikija na kuwaona ninyi, au nisipokuwapo, niyasikie mambo yenu, kama mnasimama imara katika roho moja, kwa moyo mmoja mkiishindania imani ya Injili; wala hamwaogopi adui zenu, katika neno lolote; kwao hao ni ishara mathubuti ya kupotea, bali kwenu ninyi ni ishara ya wokovu, huo utokao kwa Mungu. Maana mmepewa kwa ajili ya Kristo, si kumwamini tu, ila na kuteswa kwa ajili yake." Wafilipi 1:6, 27-29.**{EW 26.1}**

"Kwa maana Ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa

kulitimiza kusudi Lake jema. Yatendeni mambo yote pasipo manung'uniko wala mashindano, mpate kuwa wana wa Mungu wasio na lawama, wala udanganyifu, wasio na hila kati ya kizazi chenye ukaidi, kilichopotoka; ambao kati ya hao mnaonekana kuwa kama mianga katika ulimwengu.” Wafilipi 2:13-15. **{EW 26.2}**

“Hatimaye, mzidi kuwa hodari katika Bwana na katika uweza wa nguvu Zake. Vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kuzipinga hila za Shetani. Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho. Kwa sababu hiyo twaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kushindana siku ya uovu, na mkiisha kuyatimiza yote, kusimama. Basi simameni, hali mmejifunga kweli viunoni, na kuvaa dirii ya haki kifuani, na kufungiwa miguu utayari tupatao kwa Injili ya amani; zaidi ya yote mkiitwaa ngao ya imani, ambayo kwa hiyo mtaweza kuizima mishale yote yenye moto ya yule mwovu. Tena ipokeeni chapeo ya wokovu, na upanga wa Roho ambao ni Neno la Mungu; kwa sala zote na maombi mkisali kila wakati katika Roho, mkikesha kwa jambo hilo na kudumu katika

kuwaombea watakatifu wote.” Waefeso 6:10-18.**{EW 26.3}**

“Tena iweni wafadhili ninyi kwa ninyi, wenye huruma, mkasameheane kama na Mungu katika Kristo alivyowasamehe ninyi.” Waefeso 4:32.**{EW 26.4}**

“Mkiisha kujitakasa roho zenu kwa kuitii kweli, hata kuufikilia upendano wa ndugu usio na unafiki, basi jitahidini kupendana kwa moyo.” 1 Petro 1:22. **{EW 27.1}**

“Amri mpya nawapa, Mpendane. Kama vile nilivyowapenda ninyi, nanyi mpendane vivyo hivyo. Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi Wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi.” Yohana 13:34,35.**{EW 27.2}**

“ Jijaribuni wenyewe kwamba mmekuwa katika imani; jithibitisheni wenyewe. Au hamjijui wenyewe, kwamba Yesu Kristo  Yu ndani yenu? Isipokuwa mmekataliwa.” 2 Wakorintho 13:5.**{EW 27.3}**

“Kwa kadiri ya neema ya Mungu niliyopewa, mimi, kama mkuu wa wajenzi mwenye hekima, naliuweka msingi, na mtu mwingine anajenga juu yake. Lakini kila mtu na aangalie jinsi anavyojenga juu yake. Maana msingi mwingine hakuna mtu

awezaye kuuweka, isipokuwa ni ule uliokwisha kuwekwa, yaani, Yesu Kristo. Lakini kama mtu akijenga juu ya msingi huo, dhahabu au fedha au mawe ya thamani, au miti au majani au manyasi, kazi ya kila mtu itakuwa dhahiri. Maana siku ile itaidhihirisha, kwa kuwa yafunuliwa katika moto; na ule moto wenyewe utaijaribu kazi ya kila mtu, ni ya namna gani.” 1 Wakorintho 3:10-13.**{EW 27.4}**

“ Jitunzeni nafsi zenu, na lile kundi lote nalo, ambalo Roho Mtakatifu amewaweka ninyi kuwa waangalizi ndani yake, mpate kulilisha kanisa Lake Mungu, alilolinunua kwa damu Yake Mwenyewe. Najua mimi ya kuwa baada ya kuondoka kwangu mbwa-mwitu wakali wataingia kwenu, wasilihurumie kundi; tena katika ninyi wenyewe watainuka watu wakisema mapotovu, wawavute hao wanafunzi wawaandamie wao.” Matendo ya Mitume 20:28-30.**{EW 27.5}**

Nastaajabu kwa kuwa mnamwacha upesi hivi Yeye aliyewaita katika neema ya Kristo, na kugeukia injili ya namna nyingine. Wala si nyingine; lakini wapo watu wawataabishao na kutaka kuigeuza injili ya Kristo. Lakini ijapokuwa sisi au malaika wa mbinguni atawahubiri ninyi injili yoyote isipokuwa hiyo tuliyowahubiri, na alaaniwe. Kama

tulivyotangulia kusema, na sasa, nasema tena, mtu awaye yote akiwahubiri ninyi injili yoyote isipokuwa hiyo mliyoipokea, na alaaniwe. Wagalatia 1:6-9.**{EW 27.6}**

Basi, yoyote mliyosema gizani yatasikiwa mwangani; na mliyonena sikioni mwa mtu katika vyumba vya ndani, yatahubiriwa juu ya dari. Nami nawaambia ninyi rafiki Zangu, msiwaogope hao wauuao mwili, kisha baada ya hayo hawana wawezalo kutenda zaidi. Lakini nitawaonya mtakayemwogopa; mwogopeni yule ambaye akiisha kumwua mtu ana uweza wa kumtupa katika Jehanum; naam, nawaambia, Mwogopeni huyo. Je! Mashomoro watano hawauzwi kwa senti mbili? Wala hasahauliwi hata mmojawapo mbele za Mungu. Lakini hata nywele za vichwa vyenu zimehesabiwa zote. Msiogope basi, bora ninyi kuliko mashomoro wengi.Luka 12:3-7 **{EW 28.1}**

Kwa maana imeandikwa, Atakuagizia malaika zake wakulinde; na ya kwamba, mikononi mwao watakuchukua, Usije ukajikwaa mguu wako katika jiwe.. Luka 4:10, 11.**{EW 28.2}**

Kwa kuwa Mungu, aliyesema, Nuru itang'aa toka gizani, Ndiye aliyeng'aa mioyoni mwetu, atupe

nuru ya elimu ya utukufu wa Mungu katika uso wa Yesu Kristo. Lakini tuna hazina hii katika vyombo vya udongo, ili adhama kuu ya uwezo iwe ya Mungu, wala si kutoka kwetu. Pande zote twadhikika, bali hatusongwi; twaona shaka, bali hatukati tamaa; twaudhiwa, bali hatuachwi; twatupwa chini, bali hatuangamizwi. 2 Wakorintho 4:6-9.**{EW 28.3}**

Maana dhiki yetu nyepesi, iliyo ya muda wa kitambo tu, yatufanyia utukufu wa milele uzidio kuwa mwingi sana; tusiviangalie vinavyoonekana, bali visivyoonekana. Kwa maana vinavyoonekana ni vya muda tu; bali visivyoonekana ni vya milele. 2 Wakorintho 4:17-18. **{EW 28.4}**

Nanyi mnalindwa na nguvu za Mungu kwa njia ya imani hata mpate wokovu ulio tayari kufunuliwa wakati wa mwisho. Mnafurahi sana wakati huo, ijapokuwa sasa kwa kitambo kidogo, ikiwa ni lazima, mmehuzunishwa kwa majaribu ya namna mbalimbali; ili kwamba kujaribiwa kwa imani yenu, ambayo ina thamani kuu kuliko dhahabu ipoteayo, ijapokuwa hiyo hujaribiwa kwa moto, kuonekane kuwa kwenye sifa na utukufu na heshima, katika kufunuliwa Kwake Yesu Kristo. 1 Petro 1:5-7.**{EW 28.5}**

Kwa kuwa sasa twaishi, ikiwa ninyi mnasimama imara katika Bwana. 1 Wathesalonike 3:8. **{EW 28.6}**

Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa Jina Langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya; watashika nyoka; hata wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya. Marko 16:17,18.**{EW 29.1}**

Wazazi wake wakawajibu, wakasema, Tunajua ya kuwa huyu ndiye mwana wetu, tena ya kuwa alizaliwa kipofu; lakini jinsi aonavyo sasa hatujui; wala hatujui ni nani aliyemfumbua macho. Mwulizeni yeye mwenyewe; yeye ni mtu mzima; atajisemea mwenyewe. Wazazi wake waliyasema hayo kwa sababu waliwaogopa Wayahudi; kwa maana Wayahudi walikuwa wamekwisha kuafikiana kwamba mtu akimkiri kuwa ni Kristo, atatengwa na sinagogi. Ndiyo sababu wale wazazi wake walisema, Ni mtu mzima, mwulizeni yeye. Basi mara ya pili wakamwita yule mtu aliyekuwa kipofu, wakamwambia, Mpe Mungu utukufu. Sisi tunajua ya kuwa mtu huyo ni mwenye dhambi. Basi yule mtu akajibu, Kwamba Yeye ni Mwenye dhambi sijui. Najua neno moja, kuwa mimi nalikuwa kipofu na sasa naona. Basi wakamwambia, Alikutendea nini?

Alikufumbua macho jinsi gani? Akawajibu, Nimekwisha kuwaambia, wala hamkusikia; mbona mnataka kusikia tena? Ninyi nanyi mnataka kuwa wanafunzi Wake? Yohana 9:20-27.**{EW 29.2}**

Nanyi mkiomba lolote kwa Jina Langu, hilo nitalifanya, ili Baba atukuzwe ndani ya Mwana. Mkiniomba neno lo lote kwa Jina Langu, nitalifanya. Mkinipenda, mtazishika amri

Zangu. Yohana 14:13-15.**{EW 29.3}**

Ninyi mkikaa ndani Yangu, na Maneno Yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa. Hivyo hutukuzwa Baba Yangu, kwa vile mzaavyo sana; nanyi mtakuwa wanafunzi Wangu. Yohana 15:7,8. **{EW 29.4}**

Na mara palikuwapo ndani ya sinagogi lao mtu mwenye pepo mchafu; akapaza sauti, akisema, Tuna nini nawe, Yesu wa Nazareti? Je! Umekuja kutuangamiza? Nakutambua U nani, Mtakatifu wa Mungu. Yesu akamkemea, akisema, Fumba kinywa, umtoke. Marko 1:23-25. **{EW 29.5}**

Kwa maana nimekwisha kujua hakika ya kwamba, wala mauti, wala uzima, wala malaika, wala wenye mamlaka, wala yaliyopo, wala yatakayokuwapo, wala wenye uwezo, wala yaliyo

juu, wala yaliyo chini, wala kiumbe kinginecho chote hakitaweza kututenga na upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu Bwana wetu. Warumi 8:38, 39.**{EW 30.1}**

Na kwa malaika wa kanisa lililoko Filadelfia andika; Haya ndiyo anenayo Yeye aliye mtakatifu, aliye wa Kweli, aliye na ufunguo wa Daudi, yeye mwenye kufungua wala hapana afungaye, naye afunga wala hapana afunguaye. Nayajua matendo yako. Tazama, nimekupa mlango uliofunguliwa mbele yako, ambao hapana awezaye kuufunga, kwa kuwa unazo nguvu kidogo, nawe umelitunza Neno Langu, wala hukulikana Jina Langu. Tazama, nakupa walio wa sinagogi la Shetani, wasemao kwamba ni Wayahudi, nao sio, bali wasema uongo. Tazama, nitawafanya waje kusujudu mbele ya miguu yako, na kujua ya kuwa nimekupenda. Kwa kuwa umelishika Neno la subira Yangu, Mimi Nami nitakulinda, utoke katika saa ya kuharibiwa iliyo tayari kuujilia ulimwengu wote, kuwajaribu wakaao juu ya nchi. Naja upesi. Shika sana ulicho nacho, asije mtu akaitwaa taji yako. Yeye ashindaye, nitamfanya kuwa nguzo katika hekalu la Mungu Wangu, wala hatatoka humo tena kabisa, Nami nitaandika juu yake Jina la Mungu Wangu, na jina la

mji wa Mungu Wangu, huo Yerusalemu mpya, ushukao kutoka mbinguni kwa Mungu Wangu, na Jina Langu Mwenyewe, lile jipya. Yeye aliye na sikio, na alisikie Neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa. Ufunuo 3:7-13. **{EW 30.2}**

Hawa ndio wasiotiwa unajisi pamoja na wanawake, kwa maana ni bikira. Hawa ndio wamfuatao Mwana-Kondoo kila aendako. Hawa wamenunuliwa katika wanadamu, malimbuko kwa Mungu na kwa Mwana-Kondoo. Na katika vinywa vyao haukuonekana uongo. Maana hawana mawaa. Ufunuo 14:4, 5. **{EW 30.3}**

Kwa maana sisi, wenyeji wetu uko mbinguni; kutoka huko tena tunamtazamia Mwokozi, Bwana Yesu Kristo. Wafilipi 3:20.**{EW 30.4}**

Kwa hiyo ndugu, vumilieni, hata kuja Kwake Bwana. Tazama, mkulima hungoja mazao ya nchi yaliyo ya thamani, huvumilia kwa ajili yake hata yatakapopata mvua ya kwanza na ya mwisho. Nanyi vumilieni, mthibitishe mioyo yenu, kwa maana kuja Kwake Bwana kunakaribia. Yakobo 5:7-8. **{EW 30.5}**

Atakayeubadili mwili wetu wa unyonge, upate kufanana na mwili Wake wa utukufu, kwa uweza ule

ambao kwa huo aweza hata kuvitiisha vitu vyote viwe chini Yake. Wafilipi 3:21. **{EW 31.1}**

Kisha nikaona, na tazama, wingu jeupe, na juu ya wingu hilo ameketi mmoja, mfano wa Mwanadamu, mwenye taji ya dhahabu juu ya kichwa Chake, na katika mkono Wake mundu mkali. Na malaika mwingine akatoka katika hekalu, akimlilia kwa sauti kuu Yeye aliyekuwa ameketi juu ya lile wingu, Tia mundu wako, ukavune; kwa kuwa saa ya kuvuna imekuja; kwa kuwa mavuno ya nchi yamekomaa. Na Yeye aliyeketi juu ya wingu akautupa mundu Wake juu ya nchi, nchi ikavunwa. Kisha malaika mwingine akatoka katika lile hekalu lililoko mbinguni, Yeye Naye ana mundu mkali. Ufunuo 14:14-17. **{EW 31.2}**

Basi, imesalia raha yaSabato kwa watu wa Mungu. Waebrania 4:9.**{EW 31.3}**

Nami nikauona mji ule mtakatifu, Yerusalemu mpya, ukishuka kutoka mbinguni kwa Mungu, umewekwa tayari, kama bibi-arusi aliyekwisha kupambwa kwa mumewe. Ufunuo 21:2.**{EW 31.4}**

Kisha nikaona, na tazama, huyo Mwana-Kondoo amesimama juu ya mlima Sayuni, na watu mia na arobaini na nne elfu pamoja Naye, wenye

Jina Lake na Jina la Baba Yake limeandikwa katika vipaji vya nyuso zao. Ufunuo 14:1. **{EW 31.5}**

Kisha akanionyesha mto wa maji ya uzima, wenye kung'aa kama bilauri, ukitoka katika kiti cha enzi cha Mungu, na cha Mwana-Kondoo, katikati ya njia kuu yake. Na upande huu na upande huu wa ule mto, ulikuwapo mti wa uzima, uzaao matunda, aina kumi na mbili, wenye kutoa matunda yake kila mwezi; na majani ya mti huo ni ya kuwaponya mataifa. Wala hapatakuwa na laana yoyote tena. Na kiti cha enzi cha Mungu na cha Mwana-Kondoo kitakuwamo ndani yake. Na watumwa Wake watamtumikia; nao watamwona uso Wake, na Jina Lake litakuwa katika vipaji vya nyuso zao. Wala hapatakuwa na usiku tena; wala hawana haja ya taa wala ya nuru ya jua; kwa kuwa Bwana Mungu huwatia nuru, nao watatawala hata milele na milele. Ufunuo 22:1-5.**{EW 31.6}**

## Sura ya 2: Maono Yaliyofuata

Bwana alinipa mandhari ifuatayo katika mwaka wa 1847, wakati ndugu walipokuwa wamekusanyika siku ya Sabato, huko Topsham, Maine.**{EW 32.1}**

Tulihisi roho isiyo ya kawaida ya maombi. Na

tulipokuwa tunaomba, Roho Mtakatifu alikuja juu yetu. Tulikuwa na furaha sana. Punde nilipotea kwa mambo ya kidunia na nilikuwa nimefungwa katika maono ya utukufu wa Mungu. Nilimwona malaika akiruka haraka kuja kwangu. Alinichukua haraka kutoka duniani hadi kwenye Mji Mtakatifu. Katika mji huu niliona hekalu ambalo niliingia ndani yake. Nilipita kwenye mlango kabla sijafika kwenye pazia la kwanza. Pazia hili liliinuliwa, nami nikapita kwenda mahali Patakatifu. Hapa niliona madhabahu ya kufukizia uvumba, kinara cha taa, na taa saba, na meza ambayo mikate ya wonyesho ilikuwa juu yake. Baada ya kutazama utukufu wa Patakatifu, Yesu aliinua pazia la pili na nikaingia katika Patakatifu pa Patakatifu.**{EW 32.2}**

Katika Patakatifu pa Patakatifu niliona Sanduku la Agano; juu yake na ubavuni mwake ilikuwa ni dhahabu safi. Kila mwisho wa Sanduku la Agano kulikuwa na kerubi mwenye kupendeza, na mabawa yake yalikuwa yametandazwa juu yake. Nyuso zao zilielekeana, nao waliangalia chini. Kati ya malaika hao kulikuwapo na chetezo cha dhahabu. Juu ya Sanduku la Agano, pale waliposimama malaika wale, palikuwa na utukufu ung'aao sana,

ulioonekana kama kiti cha enzi alipokaa Mungu. Yesu alisimama kando ya Sanduku lile la Agano, na pale sala za watakatifu zilipomjia, uvumba ndani ya chetezo ulitoa moshi, na Yeye angetoa sala zao pamoja na moshi ule wa uvumba kwa Baba Yake. Ndani ya Sanduku la Agano mlikuwamo na sufuria la dhahabu lenye mana, fimbo ya Haruni iliyochipuka, na Mbao za Mawe zilizokunjwa pamoja kama kitabu. Yesu alizifungua, nami niliona Amri Kumi zimeandikwa juu yake kwa kidole cha Mungu. Juu ya ubao mmoja zilikuwapo nne, na juu ya mwingine sita. Lakini ile ya nne, yaani amri ya Sabato, iling'aa kuliko zingine zote; kwa kuwa Sabato iliwekwa wakfu ili ipate kutunzwa kwa ajili ya Jina takatifu la Mungu. Sabato takatifu ilionekana tukufu - duara ya utukufu ilikuwa imeizunguka pande zote (halo). Niliona kwamba amri ya Sabato haikuwa imegongomelewa msalabani. Kama ingelikuwa hivyo, basi hata zile amri nyingine tisa nazo ziligongomelewa; na hivyo sasa sisi tuko huru kuzivunja Amri zote kumi, ikiwemo na kuivunja ile ya nne. Niliona kwamba Mungu hakuwa ameibadilisha Sabato, kwa sababu Yeye habadiliki kamwe. Lakini Papa aliibadilisha kutoka katika siku ya saba hadi kuwa siku ya

kwanza ya juma; kwa kuwa alipaswa kubadili nyakati na sheria.**{EW 32.3}**

Nami niliona kuwa kama Mungu angeibadilisha Sabato kutoka katika siku ya saba hadi katika siku ya kwanza, angeweza kubadilisha maandishi ya amri ya Sabato, yaliyoandikwa kwenye mbao zile za mawe, ambazo kwa sasa ziko ndani ya Sanduku la Agano katika mahali Patakatifu pa Patakatifu katika hekalu lililoko mbinguni; nayo ingesomeka hivi: “Siku ya kwanza ndiyo Sabato ya Bwana Mungu wako.” Lakini niliona kwamba ilisomeka sawa na pale ilipoandikwa juu ya mbao za mawe kwa kidole cha Mungu, na kutolewa kwa Musa juu ya Mlima Sinai. “Lakini siku ya saba ni Sabato ya Bwana, Mungu wako.” Niliona kwamba Sabato takatifu ndiyo ukuta, na itakuwa, ukuta unaotenganisha kati ya Israeli wa kweli wa Mungu na wasioamini; na kwamba Sabato ndiyo hoja kubwa ya kuunganisha mioyo ya watakatifu wapendwa wa Mungu, wanaosubiri. **{EW 33.1}**

Niliona kuwa Mungu alikuwa na watoto ambao hawaioni na kuitunza Sabato. Hawajaikataa nuru iliyo juu Yake. Na mwanzoni mwa wakati wa taabu, tulijazwa na Roho Mtakatifu tuliposonga mbele na kuitangaza Sabato kwa ukamilifu zaidi. [Angalia

ukurasa wa 85.] Hili liliwakasirisha makanisa na Waadventista wa majina, [angalia pia kiambatisho.], kwa kuwa hawakuweza kuukanusha ukweli wa Sabato (kuuthibitisha kuwa ni uwongo). Na wakati huu wateule wa Mungu wote waliona wazi kwamba tulikuwa na Ukweli, nao walijitokeza na kuyavumilia mateso pamoja nasi. Nami niliona upanga, njaa, na tauni, na ghasia kubwa katika nchi. Waovu walidhani kwamba tulileta hukumu juu yao, nao waliinuka na kufanya shauri la kutuondoa duniani, wakidhani kwamba hapo ndipo uovu utakapokomeshwa. **{EW 33.2}**

Katika wakati wa taabu sisi sote tulikimbia kutoka katika miji na vijiji, lakini tulifuatiliwa na waovu, ambao waliingia katika nyumba za watakatifu wakiwa na upanga. Waliinua upanga ili kutuua, lakini ulivunjika, na kuanguka chini bila nguvu kama bua. Ndipo sote tulipolia mchana na usiku kwa ajili ya ukombozi, na kilio hiki kilipanda juu kwa Mungu. Jua lilichomoza, na mwezi ukasimama kimya. Mito ilikoma kutiririka. Mawingu meusi, mazito yalitokea na kugongana. Lakini, palikuwa na mahali fulani dhahiri, penye utukufu tulivu, ambapo kutoka huko sauti ya Mungu ilisikika kama maji mengi, ambayo ilitikisa mbingu na nchi.

Mbingu zilifunguka na kufungwa na zilikuwa katika vurugu. Milima ilitikisika kama mwanzi katika upepo, na kurusha mawe yaliyochongoka kote kote. Bahari ilichemka kama maji ya moto kwenye chungu na kurusha mawe juu ya nchi. Na pale Mungu alipotamka siku na saa ya kuja kwa Yesu na kulitoa agano la milele kwa watu Wake, Alisema sentensi moja, na kisha alitua kwa muda, wakati Maneno yale yalipokuwa yanapita juu ya nchi. Waisraeli wa Mungu walisimama macho yao yakiwa yamekazwa kuelekea juu, huku wakisikiliza Maneno hayo yakitoka kwenye kinywa cha Yehova, na kupita juu ya nchi kama ngurumo za radi yenye sauti kubwa mno. Kulikuwapo na umakini wa kuogofya. Na katika kila mwisho wa sentesi watakatifu walipaza sauti na kusema, “Utukufu! Haleluya!” Nyuso zao ziliangazwa na utukufu wa Mungu; nazo ziling'aa kwa utukufu, kama uso wa Musa aliposhuka kutoka Sinai. Waovu hawakuweza kuwaangalia kwa sababu ya utukufu. Na pale baraka isiyo na kikomo ilipotamkwa kwa wale ambao walikuwa wamemheshimu Mungu kwa kuitunza Sabato Yake kuwa takatifu, kulikuwapo na kelele kubwa ya ushindi juu ya mnyama na juu ya sanamu yake. **{EW 34.1}**

Ndipo ilipoanza jubilii, wakati ambapo nchi ilipaswa kupumzika. Nilimwona mtumwa mcha Mungu akiinuka kwa shangwe na ushindi na kuitikisa minyororo iliyomfunga, wakati bwana wake mwovu alikuwa amechanganyikiwa na hakujua la kufanya; kwa kuwa waovu hawakuweza kuyaelewa Maneno ya sauti ya Mungu. Mara lilionekana lile wingu kubwa jeupe. Lilionekana kuwa zuri sana kuliko lilivyowahi kuwa wakati uliopita. Juu yake aliketi Mwana wa Adamu. Mwanzoni hatukumwona Yesu juu ya wingu lile, lakini lilipokaribia dunia, tuliweza kuiona nafsi Yake ya kupendeza. Wingu hili, pale lilipoonekana kwa mara ya kwanza, lilikuwa ishara ya Mwana wa Adamu akiwa mbinguni. Sauti ya Mwana wa Mungu iliwaita watakatifu waliolala, wakiwa wamevikwa hali ya kutokufa yenye utukufu. Watakatifu walio hai walibadilishwa kwa kufumba na kfumbua na kunyakuliwa pamoja nao kwenye gari la wingu. Lilionekana kuwa na utukufu kote wakati lilipokuwa likizunguka juu. Katika kila upande wa gari kulikuwa na mabawa, na chini yake magurudumu. Na gari lilipokuwa linakwenda juu, magurudumu yalilia, "Mtakatifu," na mabawa, yaliposonga, yalilia, "Mtakatifu," na msafara wa malaika watakatifu waliolizunguka wingu lile

walipaza sauti, "Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Mungu Mwenyezi!" Watakatifu waliokuwa katika wingu lile walipaza sauti, "Utukufu! Haleluya!” Na gari likapita kwenda juu katika Mji Mtakatifu. Yesu alifungua wazi milango ya mji wa dhahabu na kutuongoza kuingia ndani yake. Hapa tulikaribishwa, kwa kuwa tulikuwa tumezishika “amri za Mungu,” na kuwa na “amri kuuendea huo mti wa uzima.” **{EW 35.1}**

## Sura ya 3: Kutiwa Muhuri

Katika mwanzo wa Sabato takatifu, Januari 5, 1849, tulishiriki katika maombi pamoja na familia ya Ndugu Belden huko Rocky Hill, Connecticut, na Roho Mtakatifu akatua juu yetu. Nilichukuliwa katika njozi hadi mahali Patakatifu paPatakatifu, ambapo nilimwona Yesu bado akiwaombea Israeli. Chini ya vazi lake kulikuwa na kengele na komamanga. Kisha nikaona kwamba Yesu asingetoka Patakatifu pa Patakatifu hadi kila jambo litakapokuwa limeamuliwa ama kwa wokovu au kwa uharibifu, na kwamba ghadhabu ya Mungu isingekuja hadi pale Yesu atakapomaliza kazi Yake katika Patakatifu pa Patakatifu, na kuvua mavazi

Yake ya kikuhani, na kujivika mavazi ya kisasi. Ndipo Yesu atatoka kuwa kati ya Baba na mwanadamu, na Mungu hatanyamaza kimya tena, lakini atamimina ghadhabu Yake juu ya wale ambao wameukataa Ukweli Wake. Niliona kuwa hasira ya mataifa, ghadhabu ya Mungu, na wakati wa kuwahukumu wafu vilikuwa vimetengana na dhahiri, tukio moja likifuata jingine, pia kwamba Mikaeli alikuwa hajasimama, na kwamba wakati wa taabu, kama ambavyo haujawahi kamwe kuwapo, ulikuwa bado haujaanza. Mataifa sasa yanakasirika, lakini Kuhani Mkuu wetu atakapomaliza kazi yake katika patakatifu, atasimama, atavaa mavazi ya kisasi, na kisha mapigo saba ya mwisho yatamiminwa.**{EW 36.1}**

Niliona kwamba malaika wale wanne wangeshikilia pepo nne mpaka pale kazi ya Yesu katika patakatifu itakapokamilika, na kisha yatakuja mapigo saba ya mwisho. Mapigo haya yaliwakasirisha waovu dhidi ya wenye haki; walidhani kwamba tumeileta hukumu za Mungu juu yao, na kwamba ikiwa wangeweza kutuondoa katika dunia, basi,  mapigo yangekomeshwa. Amri ilitolewa ya kuwaua watakatifu, ambayo iliwafanya kulia mchana na usiku kwa ajili ya ukombozi. Huu

ndio ulikuwa wakati wa taabu ya Yakobo. Ndipo watakatifu wote wakalia kwa uchungu wa roho, na waliokolewa kwa sauti ya Mungu. Wale 144,000 walishinda. Nyuso zao ziliangazwa kwa utukufu wa Mungu. Kisha nilioneshwa kundi lililokuwa likiomboleza kwa uchungu mkuu. Juu ya mavazi yao, maandishi haya yaliandikwa kwa herufi kubwa, "Umepimwa katika mizani, nawe umeonekana kuwa umepungua." Niliuliza kundi hili ni la akina nani. Malaika akasema: “Watu hawa ndio wale ambao walikuwa wakiitunza Sabato nao wameiacha.” Niliwasikia wakilia kwa sauti kuu, "Tuliamini kuhusu kuja Kwako, na kufundisha juu yake kwa nguvu." Na walipokuwa wakizungumza, macho yao yalianguka juu ya nguo zao, na kuyaona maandishi yale, na ndipo wangeomboleza kwa sauti kubwa. Niliona kwamba walikuwa wamekunywa maji kutoka katika vilindi virefu, na kuyachafua mabaki yake kwa miguu yao, na kuyafanya yanuke—waliikanyaga Sabato chini ya miguu yao—na hii ndiyo sababu walipimwa katika mizani na kuonekana kuwa wamepungua.**{EW 36.2}**

Kisha malaika aliyefuatana nami akanielekeza tena kwenye mji, ambako niliona malaika wanne wakiruka kwa mabawa yao kuelekea kwenye lango

la mji. Walikuwa tu ndipo wanampa kadi ya dhahabu malaika yule aliyekuwa langoni nilipoona malaika mwingine akiruka kwa kasi kutoka upande wa utukufu bora mno, na akipaza sauti kubwa kwa malaika wale wengine, na kupunga kitu juu na chini mkononi mwake. Nilimuuliza malaika yule aliyefuatana nami maelezo ya kile nilichokiona. Aliniambia kuwa nisingeweza kuona zaidi kwa wakati ule, lakini baada ya muda mfupi angenionesha mambo hayo ambayo niliyaona, kwamba yalimaanisha nini. **{EW 37.1}**

Siku ya Sabato alasiri, mmoja kati yetu alikuwa mgonjwa, aliomba aombewe apate kupona. Sote tuliungana katika kuomba kwa Tabibu ambaye kamwe hashindwi na ugonjwa, na wakati nguvu ya uponyaji iliposhuka chini, na mgonjwa huyu kuponywa, Roho alishuka juu yangu, na nikachukuliwa katika njozi.**{EW 37.2}**

Niliwaona malaika wanne ambao walikuwa na kazi ya kufanya duniani, nao walikuwa njiani kwenda kuitimiliza. Yesu alikuwa amevaa mavazi ya kikuhani. Aliwatazama kwa huruma juu ya wale waliosalia, kisha akainua mikono yake, na kwa sauti kubwa ya huruma alipaza sauti, "*Damu Yangu, Baba, damu Yangu, damu Yangu, damu Yangu!*" Ndipo

nilipoona nuru angavu mno ikitoka kwa Mungu, aliyeketi juu ya kiti kikubwa cheupe cha enzi, nayo ikaangazwa kote kumzunguka Yesu. Kisha nilimwona malaika mwenye agizo kutoka kwa Yesu, akiruka kwa haraka kwenda kwa wale malaika wanne waliokuwa na kazi ya kufanya duniani, na akipunga kitu juu na chini mkononi mwake, na kupiga kelele kwa sauti kubwa, "Shikilia! Shikilia! Shikilia! Shikilia! Hadi watumishi wa Mungu watakapokuwa wametiwa muhuri kwenye vipaji vya nyuso zao."**{EW 38.1}**

Nilimuuliza malaika aliyefuatana nami maana ya kile nilichokisikia, na kile ambacho wale malaika wanne walikuwa karibu kukifanya. Akaniambia, Mungu Ndiye aliyezizuia zile pepo nne, tena Ndiye aliyewaagiza malaika Zake waende juu ya nchi, ya kuwa wale malaika wanne walikuwa na mamlaka kutoka kwa Mungu juu ya pepo nne, na ya kuwa walikuwa karibu kuzifungulia; lakini mikono yao ilipokuwa inalegezwa ili kuachia zile pepo nne ambazo karibu zilikuwa karibu kuvuma; jicho la Yesu lenye rehema liliwaona wale masalia, ambao walikuwa hawajatiwa muhuri; naye akamwinulia Baba mikono Yake na kumsihi ya kwamba alikuwa amemwaga damu Yake kwa ajili yao. Ndipo malaika

mwingine alipoagizwa kuruka kwa haraka kwenda kwa wale malaika wanne na kuwaambia washikilie, mpaka pale watumishi wa Mungu watakapokuwa wametiwa muhuri kwa muhuri wa Mungu aliye hai katika vipaji vya nyuso zao.**{EW 38.2}**

## Sura ya 4: Upendo wa Mungu kwa Watu Wake

Nimeona upendo Mungu alionao kwa watu Wake, nao ni mkubwa sana. Niliwaona malaika wakiwa juu ya watakatifu na mabawa yao yakiwa yametandazwa kuwazunguka. Kila mtakatifu alikuwa na malaika aliyeambatana naye. Ikiwa watakatifu wangelia kwa kukata tamaa, au walikuwa hatarini, malaika ambao daima wanaambatana nao wangeruka juu kwa haraka kupeleka habari, na malaika katika mji wangeacha kuimba. Kisha Yesu angeamuru malaika mwingine ashuke kuwatia moyo, kuwaangalia, na kujaribu kuwazuia wasitoke nje ya njia nyembamba; lakini ikiwa hawangezingatia utunzaji wa makini wa malaika hawa, na hawangefarijiwa nao, na kuendelea kupotoka, malaika wangepata huzuni na kulia. Wangelipeleka habari hiyo juu, na malaika wote walioko katika mji wangelia, na kisha kwa

sauti kuu wangesema, "Amina!" Lakini ikiwa watakatifu wangelikaza macho yao katika thawabu iliyokuwa mbele yao na kumtukuza Mungu kwa kumsifu, basi malaika wangebeba habari njema za furaha kwenda katika mji, na malaika katika mji wangegusa vinubi vyao vya dhahabu na kuimba kwa sauti kubwa, "Haleluya!" na matao ya mbinguni yangelivuma kwa nyimbo zao tamu.**{EW 39.1}**

Kuna utaratibu kamili na maelewano katika Mji Mtakatifu. Malaika wote walioagizwa kutembelea duniani wanashikilia kadi ya dhahabu, ambayo wanaionesha kwa malaika kwenye malango ya mji kila wanapoingia na kutoka. Mbinguni ni mahali pazuri. Ninatamani sana kuwa pale na kumwona Yesu wangu mpendwa, na mwema, ambaye aliyatoa maisha Yake kwa ajili yangu, na kubadilishwa kufanana na sura Yake tukufu. Lo, laiti ningekuwa na lugha  ya kuelezea utukufu wa ulimwengu angavu ujao! Ninaona kiu kwa ajili ya vijito vilivyo hai vinavyoufurahisha mji wa Mungu wetu. **{EW 39.2}**

Bwana amenipa kuona mandhari ya malimwengu mengine. Nilipewa mabawa, na malaika alifuatana nami kutoka mjini hadi mahali palipokuwa na mwangaza na utukufu. Nyasi za

mahali hapo zilikuwa za kijani kibichi hai, na ndege wa pale waliimba wimbo laini na mtamu ambao ulikuwa una sehemu tofauti zinazofuatana. Wakazi wa mahali pale walikuwa ni wa kila kimo; walikuwa ni waadilifu, wenye fahari, na wenye kupendeza. Walibeba mfano halisi wa Yesu, na nyuso zao zilichangamka kwa furaha takatifu, ikielezea uhuru na furaha ya mahali hapo. Nilimuuliza mmoja wao kwa nini walikuwa wazuri kiasi kile zaidi ya wale walioko juu ya dunia. Jibu lilikuwa: “Sisi tumeishi kwa utii kamili kwa amri za Mungu, wala hatujaanguka katika kutokutii, kama wale walioko duniani.” Kisha niliona miti miwili, mmoja ulionekana kufanana sana na mti ule wa uzima ulioko katika mji. Matunda ya miti yote miwili yalionekana kuwa mazuri, lakini ya mti mmoja hawakuweza kula. Walikuwa na uwezo wa kula matunda ya miti yote miwili, lakini walikatazwa kula ya mti mmoja. Kisha malaika aliyefuatana nami aliniambia, "Hakuna mtu yeyote katika mahali hapa ambaye ameonja tunda la mti uliokatazwa; lakini kama wangekula, wangeanguka." Kisha nilichukuliwa kwenda katika nchi iliyokuwa na miezi saba (seven moons). Pale nilimwona mzee mwema Henoko, ambaye alikuwa amepaishwa mbinguni.

Na kwenye mkono wake wa kulia, alikuwa amebeba mtende mtukufu, na katika kila jani kuliandikwa “Ushindi.” Kuzunguka kichwa chake kulikuwa na shada jeupe linalong’aa, na majani katika shada hilo, na katikati ya kila jani kwenye shada hilo, liliandikwa "Usafi," na kulizunguka shada hilo kulikuwa na mawe ya rangi mbalimbali, ambayo yaliangaza kwa mng’aro unaozidi wa nyota, na uliorudisha nuru juu ya herufi hizo na kuzikuza. Kwenye sehemu ya nyuma ya kichwa chake kulikuwa na upinde uliolifungia shada hilo, na juu ya upinde huo kuliandikwa "Utakatifu." Juu ya shada kulikuwa na taji ya kupendeza ambayo iling'aa kuliko jua. Nilimuuliza kama hapa ndipo mahali alipoletwa kutoka duniani. Alisema, “ Hapa siyo; nyumbani kwangu ni katika mji, nami nimekuja kupatembelea mahali hapa.” Alizunguka zunguka katika eneo hilo kana kwamba yuko nyumbani kabisa. Nilimwomba malaika aliyefuatana nami aniruhusu kubaki mahali hapo. Sikuweza kuvumilia wazo la kurudi tena kwenye ulimwengu huu wa giza. Ndipo malaika yule aliposema, “Ni lazima urudi, na ikiwa wewe ni mwaminifu, wewe, pamoja na wale 144,000, mtakuwa na fursa ya kutembelea malimwengu yote na kutazama kazi za mikono ya Mungu.” **{EW 39.3}**

## Sura ya 5: Kutikiswa kwa Nguvu za Mbingu

Desemba 16, 1848, Bwana alinipa mandhari ya kutikiswa kwa nguvu za mbingu. Niliona kwamba Bwana aliposema “mbingu,” katika kutoa ishara zilizoandikwa na Mathayo, Marko, na Luka, Alimaanisha mbingu, na Aliposema “dunia” Alimaanisha dunia. Nguvu za mbingu ni jua, mwezi, na nyota. Hizi zinatawala mbinguni. Nguvu za dunia ni zile zinazotawala duniani. Nguvu za mbinguni zitatikiswa kwa sauti ya Mungu. Hapo ndipo, jua, mwezi, na nyota zitakapoondolewa kutoka katika mahali pake. Hazitatoweka, lakini zitatikiswa kwa sauti ya Mungu. **{EW 41.1}**

Mawingu meusi, mazito yalitokea na kugongana. Angahewa liligawanyika na kurudi nyuma; kisha tungeweza kuona juu kupitia katika nafasi ya wazi katika nyota ya Orioni, ambapo huko sauti ya Mungu ilitoka. Mji Mtakatifu utashuka kupitia nafasi hiyo ya wazi. Niliona kwamba nguvu za dunia sasa zinatikiswa na kwamba matukio yanakuja kwa utaratibu. Vita, na tetesi za vita, upanga, njaa, na tauni, kwanza vitazitikisa nguvu za dunia, ndipo

sauti ya Mungu itatikisa jua, na mwezi, na nyota, na nchi hii pia. Niliona kwamba kutikiswa kwa mamlaka huko Ulaya, kama wengine wanavyofundisha, siyo kutikiswa kwa nguvu za mbinguni, bali ni kutikiswa kwa mataifa yenye hasira. **{EW 41.2}**

## Sura ya 6:Mlango Uliofunguliwa na Mlango Uliofungwa

Sabato, Machi 24, 1849, tulikuwa na mkutano mzuri na wa kuvutia sana pamoja na ndugu huko Topsham, Maine. Roho Mtakatifu alimiminwa juu yetu, nami nikachukuliwa katika Roho kwenda hadi katika mji wa Mungu aliye hai. Kisha nilioneshwa kwamba amri za Mungu na ushuhuda wa Yesu Kristo unaohusiana na mlango uliofungwa visingeweza kutenganishwa, na kwamba wakati wa amri za Mungu kung'aa kwa umuhimu wake wote, na wa watu wa Mungu kujaribiwa kuhusiana na Ukweli wa Sabato, ulikuwa ni wakati ule ambapo mlango ulifunguliwa katika mahali Patakatifu pa Patakatifu katika hekalu la mbinguni, ambapo Sanduku la Agano lipo, ambalo ndani yake zimo zile amri kumi. Mlango huu haukufunguliwa mpaka pale

upatanisho wa Yesu ulipomalizika katika Patakatifu pa hekalu mnamo mwaka 1844. Kisha Yesu alisimama na kuufunga mlango wa mahali Patakatifu, na kufungua mlango unaoingia ndani wa Patakatifu pa Patakatifu, na kupita ndani ya pazia la pili, ambapo sasa anasimama, kando ya Sanduku la Agano, na ambapo imani ya Israeli sasa inafikia. **{EW 42.1}**

Niliona kwamba Yesu aliufunga mlango wa mahali Patakatifu, na hakuna mtu anayeweza kuufungua; na kwamba alikuwa ameufungua mlango wa kuingia ndani ya Patakatifu pa Patakatifu, na hakuna mtu anayeweza kuufunga (Ufunuo 3:7, 8); [angalia ukurasa wa 86]. Kwa kuwa Yesu amefungua mlango wa kuingia Patakatifu pa Patakatifu, palipo na Sanduku la Agano, amri zimekuwa zikiwaangazia watu wa Mungu, nao wanapimwa juu ya suala la Sabato. **{EW 42.2}**

Niliona kwamba jaribio la sasa juu ya Sabato lisingeweza kuja mpaka upatanisho wa Yesu katika Patakatifu umemalizika Naye amepita na kuingia ndani ya pazia la pili; kwa hiyo Wakristo ambao walilala kabla ya mlango kufunguliwa wa kuingia katika Patakatifu pa Patakatifu, wakati kilio cha usiku wa manane kilipomalizika, katika mwezi wa

saba, 1844, na ambao walikuwa hawajaishika Sabato ya Kweli, sasa wanapumzika katika tumaini; kwa kuwa  hawakuwa na nuru na mtihani/jaribio kuhusu Sabato ambalo sasa tunalo tangu mlango huo ulipofunguliwa. Niliona kwamba Shetani alikuwa akiwajaribu baadhi ya watu wa Mungu kuhusiana na suala hili. Kwa sababu Wakristo wengi wema wamelala kwa ushindi wakiwa katika, imani na hawakuwa wameitunza Sabato ya Kweli, walikuwa na shaka juu ya kuwa kwake jaribio kwetu sasa.**{EW 42.2}**

Maadui wa Ukweli wa sasa wamekuwa wakijaribu kuufungua mlango wa mahali patakatifu, ambao Yesu ameufunga, na kuufunga mlango wa Patakatifu pa Patakatifu, ambao aliufungua mnamo 1844, mahali ambapo Sanduku la Agano lipo, likiwa na mbao mbili za mawe ambazo juu yake zimeandikwa amri kumi kwa kidole cha Yehova.**{EW 43.1}**

Shetani sasa anatumia kila mbinu katika wakati huu wa kutiwa muhuri ili kuzuia akili za watu wa Mungu kutoka katika Ukweli wa sasa na kuwasababisha kuyumbayumba. Niliona mfuniko au kinga ambayo Mungu alikuwa akiiweka karibu juu ya watu Wake kuwalinda katika wakati wa taabu;

na kila roho ambayo ilikuwa thabiti juu ya Ukweli huu na ilikuwa safi moyoni ilipaswa kufunikwa na kinga ya Mwenyezi Mungu. **{EW 43.2}**

Shetani alilijua hili, na alikuwa kazini kwa nguvu kubwa kuweka akili za watu wengi kadiri ambavyo angeweza kuyumbayumba na kutokutulia katika Ukweli. Niliona kwamba ubishaji hodi kimuujiza huko New York na maeneo mengine ilikuwa ni nguvu ya Shetani, na kwamba mambo hayo yangekuwa ya kawaida zaidi na zaidi, yakiwa yamevikwa vazi la kidini ili kuwaliwaza waliodanganywa kuwa kuna usalama mkubwa na kuvuta akili za watu wa Mungu, ikiwezekana, kwa mambo hayo na kuwafanya wawe na mashaka juu ya mafundisho na uweza wa Roho Mtakatifu. (Angalia ukurasa wa 86. Angalia pia kiambatisho.] **{EW 43.3}**

Niliona kwamba Shetani alikuwa akifanya kazi kupitia kwa mawakala kwa njia kadhaa. Alikuwa kazini kupitia kwa wachungaji ambao wameukataa Ukweli na kujiachilia katika udanganyifu wenye nguvu wa kuamini uwongo kwamba wangeweza kuhukumiwa. Walipokuwa wanahubiri au kuomba, baadhi wangeanguka kifudifudi na bila kujiweza, si kwa nguvu ya Roho Mtakatifu, bali kwa nguvu ya

Shetani iliyovuviwa juu ya mawakala hawa, na kupitia kwao kwenda kwa watu. Wakati wa kuhubiri, kuomba, au kuzungumza, baadhi ya waliokiri kuwa Waadventista ambao walikuwa wameukataa Ukweli wa sasa walitumia kiinimacho (mesmerism) ili kupata wafuasi, na watu wangefurahi katika ushawishi huu, kwa maana walidhani kuwa ni Roho Mtakatifu. Wengine walioitumia hichi kiinimacho, walikuwa mbali sana katika giza na udanganyifu wa ibilisi kiasi kwamba walidhani kuwa ulikuwa ni uweza wa Mungu, waliopewa ili wapate kuutumia. Walikuwa wamemfanya Mungu kwa ujumla kuwa mtu kama wao wenyewe na waliukadiria uweza Wake kama kitu cha bure. **{EW 43.3}**

Baadhi ya mawakala hawa wa Shetani walikuwa wakiathiri miili ya baadhi ya watakatifu—wale ambao hawakuweza kuwadanganya na kuwavuta mbali na Ukweli kwa uwezo wa Kishetani. Lo, laiti wote wangeweza kuiona mandhari yake kama vile Mungu alivyoidhihirisha kwangu, ili wapate kujua zaidi hila za Shetani na kujihadhari kwa kuwa kwenye kituo chao cha ulinzi! Niliona kwamba Shetani alikuwa kazini kwa njia hizi ili apate kuwavuruga, kuwadanganya, na kuwavuta watu wa Mungu, sasa

hivi katika wakati huu wa kutiwa muhuri. Niliwaona wengine ambao hawakuwa wamesimama imara kwa ajili ya Ukweli wa sasa. Magoti yao yalikuwa yakitetemeka, na miguu yao ikiteleza, kwa sababu haikusimamishwa kwa uthabiti katika Ukweli, na kinga ya Mwenyezi Mungu isingeweza kuwekwa juu yao wakati walikuwa wakitetemeka hivyo (Hawakuweza kufunikwa na mbawa za Mwenyezi Mungu).**{EW 44.1}**

Shetani alikuwa akijaribu kwa kila mbinu yake kuwashikilia mahali pale walipokuwa, hadi pale uwekaji muhuri ulipopita, hadi kinga ilipokuwa imewekwa juu ya watu wa Mungu, nao waliachwa bila kimbilio kutokana na ghadhabu inayowaka ya Mungu, katika mapigo saba ya mwisho. Mungu ameanza kuiweka kinga hii juu ya watu Wake, na hivi karibuni itaiweka juu ya wote ambao watapata kimbilio katika siku ile ya mauaji makuu. Mungu atatenda kwa uweza kwa ajili ya watu Wake; na Shetani ataruhusiwa kufanya kazi pia.**{EW 44.2}**

Niliona kwamba ishara na maajabu ya kimiujiza pamoja na matengenezo bandia vingeongezeka na kuenea. Matengenezo ambayo yalioneshwa kwangu hayakuwa matengenezo ya kutoka katika makosa na kuingia katika Ukweli. Malaika

aliyeandamana nami aliniambia nitafute utungu wa roho kwa wenye dhambi kama ilivyozoeleka kuwa hapo zamani. Nilitazama, lakini sikuweza kuiona; kwa maana wakati wa wokovu wao umepita. [Mwandishi wa maneno haya hakuyaelewa kama fundisho kwamba wakati wa wokovu wa wenye dhambi wote ulikuwa umepita. Wakati ule hasa mambo hayo yalipoandikwa yeye mwenyewe alikuwa akifanya kazi kwa bidii kwa ajili ya wokovu wa wenye dhambi, kama alivyokuwa akifanya tangu wakati ule.**{EW 45.1}**

Ufahamu wake juu ya jambo hili kama lilivyowasilishwa kwake umetolewa katika ibara zifuatazo, na ya kwanza ilichapishwa mwaka wa 1854, na ya pili mwaka wa 1888: **{EW 45.2}**

"'Matengenezo bandia' yaliyorejelewa hapa bado hayajaonekana kwa ukamilifu zaidi. Maoni haya yanahusiana zaidi na wale ambao wamesikia na kuikataa nuru ya fundisho la marejeo. Yanatolewa kwa ajili ya udanganyifu mkubwa. Watu kama hao hawatakuwa na "uchungu wa roho kwa ajili ya wenye dhambi kama ilivyokuwa katika siku zilizopita. Wakiwa wameikataa marejeo, na kutolewa kwa udanganyifu wa Shetani, 'wakati wa wokovu wao umepita.' Hii, hata hivyo, haihusiani na

wale ambao hawajasikia na kulikataa fundisho la ujio wa pili.” **{EW 45.3}**

“Ni jambo la kuogofya kuchukulia kwa wepesi Ukweli ambao umesadikisha uelewa wetu na kugusa mioyo yetu. Hatuwezi kuyakataa maonyo ambayo Mungu kwa huruma anayatuma kwetu bila kuangamia. Ujumbe ulitumwa kutoka mbinguni kwa ulimwengu katika siku za Nuhu, na wokovu wa watu ulitegemea jinsi walivyoushughulikia ujumbe huo. Kwa sababu walilikataa onyo hilo, Roho wa Mungu aliondolewa kutoka katika jamii yenye dhambi, nao waliangamia katika maji ya Gharika. Wakati wa Ibrahimu, rehema ilikoma kuwasihi wenyeji wa Sodoma wenye hatia na wote isipokuwa Lutu na mkewe na binti zake wawili waliteketezwa kwa moto ulioshuka kutoka mbinguni. Hivyo katika siku za Kristo. Mwana wa Mungu alitangaza kwa Wayahudi wasioamini wa kizazi kile: ‘Nyumba yenu mmeachiwa hali ya ukiwa.’ Akitazama hata siku za mwisho, Yule Mwenye mamlaka iyo hiyo isiyo na kikomo anatangaza, kuhusu wale ambao ‘hawakukubali kuipenda ile Kweli, wapate kuokolewa,’ ‘Kwa hiyo Mungu awaletea nguvu ya upotevu, wauamini uongo: ili wahukumiwe ambao hawakuiamini Kweli, bali walikuwa wakijifurahisha

katika udhalimu.’ Kadiri wanavyoyakataa mafundisho ya Neno Lake, Mungu huondoa Roho Wake na kuwaacha kwenye udanganyifu wanaoupenda.]**{EW 45.4}**

## Sura ya 7: Kujaribiwa kwa Imani Yetu

Katika wakati huu wa taabu, tunahitaji kutiana moyo na kufarijiana sisi kwa sisi. Majaribu ya Shetani ni makubwa sasa kuliko yalivyowahi kuwa hapo awali, kwa kuwa anajua kwamba muda wake ni mfupi na kwamba hivi karibuni sana kila kesi itakuwa imeamuliwa, ama kwa maisha au kwa mauti. Sasa si wakati wa kuzama chini na kuachana na kuvunjika moyo na majaribio; ni lazima tuyavumilie mateso yetu yote na tumtumaini kabisa Mwenyezi Mungu wa Yakobo. Bwana amenionesha kwamba neema Yake inatosheleza kwa majaribu yetu yote; na ingawa ni makubwa kuliko hapo awali, lakini bado ikiwa tunamtumaini kabisa Mungu, tunaweza kushinda kila jaribu na kwa neema Yake kufanikiwa kuwa washindi.**{EW 46.1}**

Ikiwa tutayashinda majaribio yetu na kupata ushindi dhidi ya majaribu ya Shetani, basi

tunavumilia kujaribiwa kwa imani yetu, ambayo ni ya thamani kubwa kuliko dhahabu, na tunakuwa na nguvu na kujiandaa vizuri zaidi kukabiliana na yale yanayofuata. Lakini ikiwa tutazama chini na kusalimu amri kwa majaribu ya Shetani, tutakuwa dhaifu zaidi na hatutapata thawabu kwa ajili ya jaribu hilo na hatutakuwa tumejiandaa vyema kwa linalofuata. Kwa namna hii, tutazidi kuwa dhaifu na dhaifu zaidi, hadi tutakapoongozwa kuwa mateka na Shetani kama apendavyo. Ni lazima tuwe na silaha zote za Mungu na tuwe tayari wakati wowote kwa ajili ya kupambana na nguvu za giza (Waefeso 6). Pale mitihani na majaribu yanapotujia kwa haraka, hebu twendeni kwa Mungu na kumlilia kwa kuumia moyoni katika maombi. Yeye hatatuRudisha bila chochote, bali atatupa neema na nguvu za kushinda, na za kuzivunja nguvu za adui. Lo, laiti wote wangeweza kuona mambo haya katika nuru yake halisi na kuyavumilia magumu kama askari wema wa Yesu! Ndipo Israeli wangeweza kusonga mbele, wakiwa na nguvu katika Mungu, na katika uweza wa nguvu Yake. **{EW 46.2}**

Mungu alinionesha kwamba aliwapa watu wake kikombe kichungu wapate kukinywea, ili apate kuwasafisha na kuwatakasa. Ni funda chungu na

lafanana na sumu, na wanaweza kulifanya kuwa chungu zaidi kwa kunung'unika, kulalamika, na kuwa na uchungu moyoni. Bali wale wanaokipokea kwa jinsi hiyo ni lazima watapata funda lingine, kwa kuwa lile la kwanza halijawa na athari yake iliyokusudiwa moyoni. Na kama lile la pili halitekelezi kazi iliyotarajiwa, basi lazima wapate na lingine, na lingine, mpaka litekeleze kazi yake iliyokusudiwa, au wataachwa wakiwa najisi, wachafu moyoni. Niliona kwamba kikombe hiki kichungu kinaweza kutiwa utamu kwa subira, uvumilivu, na maombi, na kwamba kitakuwa na matokeo yake yaliyokusudiwa juu ya mioyo ya wale wanaokipokea, na Mungu ataheshimiwa na kutukuzwa. Si jambo dogo kuwa Mkristo na kumilikiwa na kukubaliwa na Mungu. Bwana amenionesha wengine wanaoukiri Ukweli wa sasa, ambao maisha yao hayalingani na kile wanachokikiri. Wana kiwango cha uchaji Mungu kwa ujumla cha chini sana, na wamepungua sana katika utakatifu wa Biblia. Wengine hujihusisha na mazungumzo ya ovyo na yasiyofaa, na wengine husalimu amri kwa kujiinua nafsi zao. Hatupaswi kutarajia kujifurahisha wenyewe, kuishi na kutenda kama ulimwengu, kuwa na anasa zake, na kufurahia

ushirika wa wale ambao ni wa ulimwengu, na halafu kutawala pamoja na Kristo katika utukufu.**{EW 47.1}**

Ni lazima tuwe washirika wa mateso ya Kristo hapa ikiwa tutashiriki katika utukufu Wake baadaye. Kama tunatafuta masilahi yetu wenyewe, jinsi tunavyoweza kujifurahisha wenyewe, badala ya kutafuta kumpendeza Mungu na kuendeleza kusudi Lake lenye thamani kubwa, lenye mateso, tutamfedhehesha na kumkosea adabu Mungu na kazi Yake takatifu tunayokiri kuipenda. Tunao muda mfupi tu wa kumfanyia kazi Mungu. Hakuna kitu kinachopaswa kupendwa mpaka kufika hatua ya kutoweza kutolewa kafara kwa ajili ya wokovu wa kundi la Yesu lililotawanyika na kupasuka. Wale wanaofanya agano na Mungu kwa kafara sasa hivi punde watakusanywa nyumbani ili wapate kushiriki thawabu kubwa na kumiliki ufalme mpya milele na milele.**{EW 47.2}**

Lo, hebu na tuishi kikamilifu kwa ajili ya Bwana na kuonesha kwa maisha yenye utaratibu mzuri na mazungumzo ya kumcha Mungu kwamba tumekuwa na Yesu na sisi ni wafuasi Wake wapole na wanyenyekevu. Imetupasa kuifanya kazi maadam ni mchana, kwa sababu usiku wa giza wa taabu na uchungu utakapokuja, tutakuwa

tumechelewa sana kufanya kazi kwa ajili ya Mungu. Yesu Yuko katika hekalu Lake takatifu na sasa atakubali dhabihu zetu, maombi yetu, na maungamo yetu juu ya makosa na dhambi na atasamehe makosa yote ya Israeli, ili yapate kufutwa kabla hajaondoka katika Patakatifu. Wakati Yesu atakapotoka katika Patakatifu, basi wale ambao ni watakatifu na wenye haki watazidi kuwa watakatifu na wenye haki; kwa kuwa dhambi zao zote zitafutwa, nao watatiwa muhuri, kwa muhuri wa Mungu aliye hai. Lakini wale walio wadhalimu na wachafu watazidi kudhulumu na kuwa wachafu; kwa kuwa wakati huo hatakuwapo Kuhani wa kutoa dhabihu zao, katika Patakatifu, kwa maungamo yao, na maombi yao mbele ya kiti cha enzi cha Baba. Kwa hiyo kile kinachofanywa kwa ajili ya kuokoa roho kutokana na dhoruba ijayo ya ghadhabu ni lazima kifanyike kabla ya Yesu kuondoka katika Patakatifu pa Patakatifu pa mbinguni.**{EW 48.1}**

****

## Sura ya 8-Kwa "Kundi Dogo"

Ndugu Wapendwa: Bwana alinionesha, Januari 26, 1850, kile nitakachosimulia. Niliona kwamba

baadhi ya watu wa Mungu ni wajinga na wamebweteka nao hawajaamka kikamilifu; hawautambui wakati tunaoishi sasa, na kwamba mtu yule aliye na “ufagio wa kuondoa uchafu” umeingia, [angalia “ndoto ya William Miller,” ukurasa wa 81.] na kwamba baadhi wako katika hatari ya kufagiliwa mbali. Nilimsihi Yesu apate kuwaokoa, kuwahurumia kwa kitambo zaidi, na kuwaruhusu kuona hatari yao ya kuogofya, ili wapate kujiandaa kabla hawajachelewa sana milele. Malaika akajibu, “Uharibifu unakuja kama upepo wa kisulisuli wenye nguvu.” Nilimsihi malaika yule awahurumie na kuwaokoa wale waliuopenda ulimwengu huu, ambao walikuwa wameshikamana na mali zao na hawakuwa tayari kujitenga na kuwa huru kutokana nazo na kutoa kafara kwa ajili ya kuwaharakisha wajumbe katika njia yao kwenda kuwalisha kondoo wenye njaa ambao walikuwa wanaangamia kwa kukosa chakula cha kiroho.**{EW 48.2}**

Nilipoziona roho maskini zikifa kwa kukosa ukweli wa sasa, na wengine waliokiri kuuamini ukweli walikuwa wakiwaacha wafe kwa kuzuia mali zilizofaa kuendeleza kazi ya Mungu, mandhari ile ilikuwa ni ya kuhuzunisha sana, nami nilimwomba

malaika yule aiondoe kutoka kwangu. Niliona kwamba wakati kazi ya Mungu ilihitaji kutoka kwa baadhi mali zao, kama kijana yule aliyekuja kwa Yesu (Mathayo 19:16-22) waliondoka wakiwa na huzuni, na kwamba punde baa linalofurika litapita na kuzoa mali zao zote, na ndipo itakuwa imechelewa mno kutoa sadaka ya mali ya kidunia, na kujiwekea hazina mbinguni.

Kishanikamwona Mkombozi mtukufu, mzuri na wa kupendeza; kwamba aliacha ufalme wa utukufu na kuja katika ulimwengu huu wa giza na upweke kutoa maisha yake ya thamani na kufa, mwenye haki kwa ajili yao wasio haki. Alibeba dhihaka na mijeledi ya kikatili, alivaa taji ya miiba iliyosokotwa, na kutokwa matone makubwa jasho ya damu kwenye bustani, wakati mzigo wa dhambi za ulimwengu wote ulipokuwa juu Yake. Malaika akamuuliza: "Kwa ajili ya nini?" Nikaona na kajua kuwa ilikuwa ni kwa ajili yetu, kwa ajili ya dhambi zetu aliteswa, ili kwa damu yake ya thamani apate kutukomboa kwa ajili ya Mungu.**{EW 49.1}**

Kisha tena wakawekwa mbele yangu wale ambao hawakuwa tayari kutoa mali za ulimwengu huu kwa ajili ya kuokoa roho zinazoangamia kwa kuwatumia ukweli wakati Yesu amesimama mbele

ya Baba akiwatetea kwa ajili ya damu Yake, mateso Yake, na kifo Chake kwa ajili yao; na wakati wajumbe wa Mungu wanangojea, tayari kuwapelekea ukweli unaookoa ili waweze kutiwa muhuri kwa muhuri wa Mungu aliye hai. Ni ngumu kwa baadhi ya wale wanaokiri kuuamini ukweli wa sasa kufanya hata kidogo sana kama vile kuwapa wajumbe pesa za Mungu ambazo amewakopesha wapate kuwa mawakili juu Yake.**{EW 49.2}**

Yesu atesekaye, upendo Wake wa kina kiasi cha kumwongoza kutoa maisha Yake kwa ajili ya mwanadamu, aliwekwa tena mbele yangu; pia maisha ya wale waliodai kuwa ni wafuasi wake, ambao walikuwa na mali ya ulimwengu huu, lakini waliona kuwa ni jambo kubwa mno kusaidia kazi ya wokovu. Malaika yule aliuliza, “ Je watua kama hao wataweza kuingia mbinguni?” Malaika mwingine akajibu, "Hasha, kamwe, kamwe, kamwe. Wale ambao hawana shauku na kazi ya Mungu duniani hawawezi kamwe kuuimba wimbo wa upendo unaokomboa huko juu.” Niliona kwamba kazi ya haraka ambayo Mungu alikuwa akiifanya duniani punde ingefupishwa katika haki na kwamba wajumbe ni lazima waende mbio kwa kasi katika njia yao kwenda kulitafuta kundi lililotawanyika.

Malaika mmoja aliuliza, “ Je wote ni wajumbe?” Mwingine alijibu, “Hapana, hapana; wajumbe wa Mungu wana ujumbe.” **{EW 50.1}**

Niliona kuwa kusudi la Mungu lilikuwa limekawilishwa na kudharauliwa na baadhi ya waliokuwa wanasafiri ambao hawakuwa na ujumbe kutoka kwa Mungu. [angalia kiambatisho.] Watu kama hao watalazimika kutoa hesabu kwa Mungu kwa kila shilingi ambayo wametumia katika kusafiri kwenda mahali ambapo haikuwa wajibu wao kwenda, kwa sababu fedhaa hiyo ingeweza kusaidia katika kaziya Mungu; na kwa ajili ya ukosefu wa chakula cha kiroho ambacho kingeweza kutolewa kwao na wajumbe walioitwa na kuteuliwa na Mungu, kama wangelikuwa na fedha, roho zimekosa chakula na kufa kwa njaa. Niliona kwamba wale ambao wana nguvu ya kufanya kazi kwa mikono yao na kusaidia kuendeleza kazi walikuwa wanawajibika kwa ajili ya nguvu zao kama vile wengine walivyowajibika kwa mali zao.**{EW 50.2}**

Mtikiso wenye nguvu umeanza na utaendelea, na wote watatikiswa na kutolewa nje wale ambao hawako tayari kuchukua msimamo thabiti na usiokubali kushindwa kwa ajili ya ukweli na kujitoa kwa ajili ya Mungu na kaziYake. Malaika aliuliza,

“Mnadhani kwamba yeyote atalazimishwa kutoa kafara?” Hapana, hapana, Ni lazima iwe sadaka ya hiari. Itahitaji yote kwa ajili ya kununua shamba." Nilimlilia Mungu apate kuwahurumia watu Wake, ambao baadhi yao walikuwa wanazimia na kufa. Ndipo nilipoona kuwa hukumu za Mwenyezi zilikuwa zinakuja kwa haraka, nami nilimwomba malaika yule aseme na watu kwa lugha yake. Alisema, "Ngurumo zote na radi za Mlima Sinai zisingeweza kuwagusa wale ambao hawataguswa na ukweli dhahiri wa Neno la Mungu, wala ujumbe wa malaika hautaweza kuwaamsha."**{EW 50.3}**

Kisha nikaona uzuri na kupendeza kwa Yesu. Joho Lake lilikuwa jeupe sana. Hakuna lugha inaweza kuelezea utukufu wake na uzuri uliotukuka. Wote, wote wanaozitunza amri za Mungu, wataingia ndani ya mji kupitia katika milango yake na watakuwa na amri ya kuuendea huo mti wa uzima na milele kuwa mbele ya Yesu mpendwa, ambaye uso Wake unang'aa kuliko jua wakati wa adhuhuri. **{EW 51.1}**

Nilioneshwa Adamu na Hawa wakiwa Edeni. Walikula matunda ya ule mti uliokatazwa, nao walifukuzwa kutoka Bustanini, na upanga wa moto uliwekwa kuuzunguka mti wa uzima, wasije wakala

matunda yake na kuwa wenye dhambi wasiokufa. Mti wa uzima ulikuwa ni wa kudumisha kutokufa. Nilimsikia malaika akiuliza, "Ni nani katika familia ya Adamu aliyeupita upanga wa moto na kula kutoka katika mti wa uzima?" Nilisikia malaika mwingine akijibu, "Hakuna hata mmoja wa familia ya Adamu aliyepita upanga huo wa moto na kula kutoka katika mti huo; kwa hiyo hakuna mwenye dhambi asiyekufa. Nafsi itendayo dhambi itakufa kifo cha milele - kifo ambacho kitadumu milele, ambacho kutoka katika hicho hakutakuwa na tumaini la ufufuo; na ndipo ghadhabu ya Mungu itakapotulizwa.**{EW 51.2}**

“Watakatifu watapumzika katika Mji Mtakatifu na kutawala kama wafalme na makuhani kwa miaka elfu moja; kisha Yesu atashuka pamoja na watakatifu juu ya Mlima wa Mizeituni, na mlima huo utapasuka vipande na kuwa uwanda mkubwa sana kwa ajili ya Paradiso ya Mungu kutulia juu yake. Na sehemu ya nchi iliyobaki haitatakaswa hata mwisho wa miaka ile elfu moja, wakati ambapo wafu waovu wanafufuliwa, na kukusanyika kuuzunguka mji. Miguu ya waovu kamwe haitainajisi dunia iliyoumbwa upya tena. Moto utashuka kutoka kwa Mungu kutoka mbinguni na kuwala—kuwateketeza

kabisa shina na matawi. Shetani ndiye shina, na watoto wake ndio matawi. Moto ule ule utakaowala waovu ndio utakaoitaksa dunia.**{EW 51.3}**

****

## Sura ya 9-Mapigo ya Mwisho na Hukumu

Katika mkutano mkuu Kanisa la Wasabato duniani, unaojulikana kama General conference of Seventh Day Adventist Church, kwa wale waliouamini Ukweli wa sasa, uliofanyika Sutton, Vermont, Septemba, 1850, nilioneshwa kuwa mapigo saba ya mwisho yatamwagwa baada ya Yesu kutoka katika Patakatifu. Malaika alisema, “Ni ghadhabu ya Mungu na ya Mwanakondoo inayosababisha uharibifu au mauti ya waovu. Kwa sauti ya Mungu watakatifu watakuwa wenye nguvu na wa kuogofya kama jeshi lenye bendera, lakini hawataitekeleza hukumu iliyoandikwa kwa wakati ule. Utekelezaji wa hukumu hiyo utakuwa mwishoni mwa miaka ile elfu moja.” **{EW 52.1}**

Baada ya watakatifu kubadilishwa na kuvaa kutokufa na kunyakuliwa pamoja na Yesu, baada ya kupokea vinubi vyao, mavazi yao, na taji zao, na kuingia katika  Jiji, Yesu na watakatifu wanakaa katika hukumu. Vitabu vinafunguliwa—kitabu cha

uzima na kitabu cha mauti. Kitabu cha uzima kina matendo mema ya watakatifu; na kitabu ch mauti kina matendo mabaya ya waovu. Vitabu hivi vinalinganishwa na kitabu cha sheria, Biblia, na kulingana na hilo watu wanahukumiwa. Watakatifu, kwa pamoja na Yesu, wanapitisha hukumu yao juu ya wafu waovu. “Tazameni,” malaika alisema, “watakatifu, kwa kupatana na Yesu, wameketi katika hukumu, na kuwahukumu waovu kulingana na matendo yaliyofanywa katika mwili, na kile ambacho ni lazima wakipokee wakati wa utekelezaji wa hukumu kimewekwa mbele ya majina yao.” Hii, Niliiona, ilikuwa ndio kazi ya watakatifu pamoja na Yesu katika kipindi cha miaka elfu moja katika Mji Mtakatifu kabla haujashuka duniani. Kisha, mwisho wa ile miaka elfu moja, Yesu, pamoja na malaika na watakatifu wote, wanatoka katika Mji Mtakatifu, na wakati anaposhuka kuja duniani pamoja nao, wafu waovu watafufuliwa; na ndipo watu wale hasa “waliomchoma” wakiwa wamefufuliwa, watamwona kwa mbali katika utukufu Wake wote, malaika pamoja na watakatifu wakiwa pamoja Naye, nao wataomboleza kwa ajili Yake. Wataona alama za misumari katika mikono Yake na katika miguu Yake, na mahali walipopachoma kwa mkuki ubavuni

Mwake. Alama za misumari na mkuki wakati ule zitakuwa ni utukufu Wake. Ni mwishoni mwa miaka elfu moja ndipo Yesu anasimama juu ya Mlima wa Mizeituni, na mlima unagawanyika vipande vipande na kuwa uwanda mkubwa. Wale wanaokimbia wakati ule ni waovu, ambao mara tu ndio wamefufuliwa. Kisha Mji Mtakatifu unashuka chini na kutulia juu ya uwanda ule. Ndipo Shetani anapowajaza waovu kwa roho yake. Kuwatia moyo kwa matumaini ya madanganyo/uongo kwamba jeshi lililoko mjini ni dogo, na kwamba jeshi lake ni kubwa, na kwamba wanaweza kuwashinda watakatifu na kuuchukua mji ule. **{EW 52.2}**

Wakati Shetani alipokuwa akilikusanya jeshi lake, watakatifu walikuwa katika mji, wakiuona uzuri na utukufu wa Paradiso ya Mungu. Yesu alikuwa Ndiye mkuu wao, akiwaongoza. Ghafla Mwokozi mpendwa alikuwa ameondoka katika kundi letu; lakini punde tulisikia sauti Yake ya kupendeza, ikisema, “Njooni, mliobarikiwa na Baba Yangu, urithini ufalme mliowekewa tayari tangu kuumbwa ulimwengu.” Tulikusanyika kumzunguka Yesu, na mara tu alipofunga malango ya mji, laana ilitamkwa juu ya waovu. Milango ilikuwa imefungwa. Ndipo watakatifu walitumia mabawa yao na kupaa hadi

juu ya ukuta wa mji. Yesu pia alikuwa pamoja nao; taji Yake ilionekana iking'aa na yenye utukufu. Ilikuwa ni taji ndani ya taji, saba kwa idadi. Taji za watakatifu yalikuwa ni ya dhahabu safi kabisa, iliyopambwa na nyota. Nyuso zao ziliangaza kwa utukufu, kwa sababu walikuwa katika mfano halisi wa Yesu; na pale walipoinuka na kusogea wote kwa pamoja hadi juu ya mji, nilipendezwa mno na mandhari ile. **{EW 53.1}**

Ndipo wale waovu walipoona kile walichokuwa wamekipoteza; na moto ulipumuliwa kutoka kwa Mungu na kuwateketeza kabisa. Huu ndio ulikuwa *utekelezaji wa hukumu*. Waovu basi walipokea kama ambavyo watakatifu, kwa kushirikiana na Yesu, walikuwa wamehukumiwa wakati wa miaka ile elfu moja. Moto ule ule kutoka kwa Mungu uliowateketeza waovu uliitakasa dunia yote. Milima iliyovunjika, yenye mawe yaliyochongoka iliyeyuka kwa joto kali, anga pia, na makapi yote yaliteketezwa. Ndipo urithi wetu ulipofunguliwa mbele yetu, wenye utukufu na mzuri, nasi tuliurithi ulimwengu wote na uliofanywa upya. Sisi sote tulipiga kelele kwa sauti kuu, "Utukufu; Haleluya!"**{EW 54.1}**

*****

## Sura ya 10-Mwisho wa Zile Siku 2300

Niliona kiti cha enzi na juu yake ameketi Baba na Mwana. Niliuona uso wa Yesu na kupendezwa na nafsi Yake ya kupendeza. Nafsi ya Baba sikuweza kuiona, kwa kuwa wingu la nuru yenye utukufu lilimfunika. Nilimuuliza Yesu ikiwa Baba Yake alikuwa na umbo kama Lake. Alisema Alikuwa nalo, lakini sikuweza kuuona, kwa maana Alisema, "Kama ungeona mara moja utukufu wa nafsi yake, ungekoma kuwepo-ungekufa.” Mbele ya kiti cha enzi niliwaona wana Marejeo—kanisa na ulimwengu. Niliona makundi mawili, moja likiwa limesujudu mbele ya kiti cha enzi, likivutiwa sana, wakati lingine limesimama pasipo shauku, na bila kujali. Wale ambao walikuwa wamesujudu mbele ya kiti cha enzi walitoa maombi yao na kumtazama Yesu; kisha Yeye angemtazama Baba Yake, na kuonekana akimsihi. Nuru ingetoka kwa Baba kwenda kwa Mwana na kutoka kwa Mwana kwenda kwa kundi linaloomba. Kisha nikaona nuru angavu mno ikitoka kwa Baba kwenda kwa Mwana, na kutoka kwa Mwana ilitanda juu ya watu wale waliokuwa mbele ya kiti cha enzi. Lakini ni wachache tu waliipokea nuru hii kubwa. Wengi walitoka chini yake na mara moja wakaipinga; wengine walikuwa wazembe na

hawakuithamini nuru ile, nayo iliondoka kwao. Baadhi waliithamini, nao wakaenda na kusujudu pamoja na lile kundi dogo lililokuwa linaomba. Kundi hili lote lilipokea nuru ile na kuifurahia, na nyuso zao ziliangaza kwa utukufu Wake. **{EW 54.2}**

Nilimwona Baba akiinuka kutoka katika kiti cha enzi, [angalia ukurasa wa 92.] na katika gari la moto aliingia katika Patakatifu pa Patakatifu ndani ya pazia, na kuketi. Kisha Yesu aliinuka kutoka kwenye kiti cha enzi, na wengi wa wale waliokuwa wamesujudu, walisimama pamoja na Yeye. Sikuona hata mwale mmoja wa nuru ukipita kutoka kwa Yesu kwenda kwa umati ule usiojali baada ya Yeye kuinuka, nao waliachwa katika giza kamili. Wale ambao waliinuka wakati Yesu alipofanya hivyo, walimkazia macho wakati alipokuwa anaondoka kwenye kiti cha enzi na kuwaongoza nje kidogo. Kisha aliuinua mkono Wake wa kuume, nasi tulisikia sauti Yake nzuri ikisema, "Subirini hapa; ninakwenda kwa Baba Yangu kuupokea ufalme; tunzeni mavazi yenu yasiwe na doa, na baada ya muda mfupi nitarudi kutoka kwenye arusi na kuwakaribisha Kwangu." Ndipo gari lenye mawingu, lenye magurudumu kama moto uwakao, lililozungukwa na malaika, lilikuja mahali

alipokuwapo Yesu. Yeye Aliingia ndani ya gari na kuchukuliwa hadi Patakatifu pa Patakatifu, ambapo Baba alikuwa ameketi. Pale nilimwona Yesu, Kuhani Mkuu adhimu amesimama mbele ya Baba. Juu ya upindo wa vazi Lake kulikuwa na kengele na komamanga, kengele na komamanga. Wale walioinuka pamoja na Yesu wangeiinua imani yao Kwake, wakati akiwa katika Patakatifu pa Patakatifu, na kuomba, "Baba yangu, tupe Roho Wako." Kisha Yesu angewavuvia Roho Mtakatifu kwa pumzi Yake. Katika pumzi hiyo kulikuwa na nuru, nguvu, na upendo mwingi, furaha, na amani. **{EW 55.1}**

Niligeuka kulitazama kundi lile ambalo bado lilikuwa limesujudu mbele ya kiti cha enzi; nao hawakujua ya kuwa Yesu ameliacha. Shetani alionekana kuwa kando ya kiti cha enzi, akijaribu kuendelea na kazi ya Mungu. Niliwaona wakiangalia juu katika kiti cha enzi na kuomba, "Baba, tupe Roho Wako." Shetani wakati huo angevuvia juu yao uwezo usio mtakatifu; ndani yake kulikuwa na nuru na nguvu nyingi, lakini upendo mtamu ulikosekana, furaha, na amani. Lengo la Shetani lilikuwa ni kuwadumisha katika udanganyifu na kuwavuta nyuma na kuwadanganya watoto wa Mungu.

***** {EW 56.1}

## Sura ya 11-Wajibu kwa Kuzingatia Wakati wa Taabu

Bwana amenionesha mara kwa mara kwamba ni kinyume na Biblia kufanya maandalizi kwa ajili ya mahitaji yetu ya kidunia wakati wa taabu. Niliona kwamba ikiwa watakatifu walikuwa na chakula walichokiweka akiba au kilichoko shambani wakati wa taabu, wakati ambapo upanga, njaa, na tauni ziko katika nchi, kingechukuliwa kutoka kwao kwa mikono yenye nguvu na wageni wangeyavuna mashamba yao. Ndipo itakuwa wakati wetu wa kumtumainia Mungu kabisa, Naye atatuhimili. Niliona kwamba mkate wetu na maji vitakuwa vya hakika wakati huo, na kwamba hatutakosa au kuteseka kwa njaa; kwa maana Mungu anaweza kutandika meza jangwani kwa ajili yetu. Kama ni lazima angeweza kutuma kunguru kutulisha, kama alivyofanya kumlisha Eliya, au kunyesha mana kutoka mbinguni, kama alivyofanya kwa Waisraeli.**{EW 56.2}**

Nyumba na ardhi hazitawafaa watakatifu katika

wakati wa taabu, kwa kuwa wakati huo watalazimika kukimbia mbele ya makundi ya watu wenye hasira, na wakati huo mali zao haziwezi kutolewa kwa ajili ya kuendeleza kazi ya ukweli wa sasa. Nilioneshwa kwamba ni mapenzi ya Mungu kwamba watakatifu wajiweke huru kutokana na kila mzigo kabla ya wakati wa taabu kuja, na kufanya agano na Mungu kwa njia ya kutoa kafara. Ikiwa wana mali yao juu ya madhabahu na kumwomba Mungu kwa bidii kwa ajili ya wajibu, atawafundisha ni wakati gani wa kuviondoa vitu hivi. Ndipo watakapokuwa huru wakati wa taabu, na kutokuwa na kizuizi chochote cha kuwalemea. **{EW 56.3}**

Niliona kwamba ikiwa mtu yeyote angeshikilia mali yake na kuacha kumuuliza Bwana kuhusu wajibu wake, Asingefanya wajibu ujulikane, na wangeruhusiwa kuhifadhi mali yao, na katika wakati wa taabu ingekuja mbele yao kama mlima kuwaponda, nao wangejaribu kuitupilia mbali, lakini wasingeweza. Niliwasikia baadhi yao wakiomboleza hivi: “Kaziilikuwa ikidhoofika, watu wa Mungu walikuwa wanakufa kwa njaa ya ukweli, na hatukufanya juhudi yoyote kutoa ili kuziba upungufu huo; sasa mali yetu haina maana yoyote.

Laiti tungeiachilia, na kuweka hazina mbinguni!" Niliona kwamba kafara haikuongezeka, bali ilipungua na kuteketea. Pia niliona kwamba Mungu hakuwahitaji watu wake wote kuachia mali zao kwa wakati mmoja; lakini kama wangetaka kufundishwa, Angewafundisha, wakati wa uhitaji, wakati gani wa kuuza na kiasi gani cha kuuza. Baadhi walitakiwa kutoa mali zao katika nyakati zilizopita ili kuendeleza kazi ya Marejeo, wakati ambapo wengine wameruhusiwa kuzitunza mali zao hadi wakati wa uhitaji. Ndipo, kama kaziitakavyohitaji, wajibu wao ni kuiuza. **{EW 57.1}**

Niliona kwamba ujumbe, "Uzeni mlicho nacho, na kutoa sadaka," haujatolewa, na baadhi, katika nuru yake dhahiri, na lengo la maneno ya Mwokozi wetu halijawasilishwa kwa uwazi. Lengo la kuuza si kutoa kwa wale ambao wanaweza kufanya kazi na kujikimu wenyewe, bali ni kueneza ukweli. Ni dhambi kuwasaidia na kuwaendekeza katika uvivu wale ambao wana uwezo wa kufanya kazi. Baadhi wamekuwa na bidii ya kuhudhuria mikutano yote, si kwa ajili ya kumtukuza Mungu, bali kwa ajili ya "mikate na samaki." Walio kama hao ingelikuwa bora zaidi kwao kuwa nyumbani wakifanya kazi kwa

mikono yao, "jambo ambalo ni jema," ili kutoa mahitaji ya familia zao na kuwa na kitu cha kutoa ili kutegemeza kazi ya thamani kuu ya ukweli wa sasa. Sasa ndio wakati wa kuweka hazina mbinguni na kuweka mioyo yetu sawa, tayari kwa wakati wa taabu. Ni wale tu ambao wana mikono safi na mioyo safi ndio watakaosimama katika wakati huo wa jaribu. Sasa ndio wakati wa sheria ya Mungu kuwa katika akili zetu, vipaji vya nyuso, na kuandikwa katika mioyo yetu. **{EW 57.2}**

Bwana amenionesha hatari ya kuruhusu akili zetu kujazwa na mawazo na masumbufu ya kidunia. Niliona kwamba akili zingine zinaongozwa mbali na ukweli wa sasa na upendo wa Biblia Takatifu kwa kusoma vitabu vingine vya kusisimua; wengine wamejawa na wasiwasi na masumbufu kuhusu kile watakachokula, kunywa, na kuvaa. Wengine wanaangalia mbali sana kwa ajili ya kuja kwa Bwana. Muda umeendelea kwa miaka michache zaidi kuliko walivyotarajia; kwa hiyo wanafikiri kuwa inaweza kuendelea miaka michache zaidi, na kwa njia hii akili zao zinaongozwa kutoka katika ukweli wa sasa, kwenda nje kuutafuta ulimwengu. Katika mambo haya niliona hatari kubwa; maana akili ikiwa imejazwa na vitu vingine, ukweli wa sasa

unafungiwa nje, na hakuna nafasi katika vipaji vya nyuso zetu kwa ajili ya muhuri wa Mungu aliye hai. Niliona kuwa muda wa Yesu kuwa katika patakatifu pa patakatifu ulikuwa umekaribia kwisha na muda huo unaweza kudumu kwa kitambo kidogo tu. Wakati wowote wa mapumziko tulio nao tunapaswa kuutumia katika kuichunguza Biblia, ambayo ndiyo itatuhukumu katika siku ya mwisho. **{EW 58.1}**

Ndugu na dada zangu wapendwa, hebu amri za Mungu na ushuhuda wa Yesu Kristo viwe katika akili zenu daima na hebu vizuie mawazo na masumbufu ya dunia. Mnapolala na mnapoamka, hebu na viwe tafakuri yenu. Ishi na kutenda kabisa kwa kupatana na kuja kwa Mwana wa Adamu. Muda wa kutia muhuri ni mfupi sana, nao utaisha hivi karibuni. Sasa ndio muda, wakati malaika wanne wanashikilia pepo nne, kufanya wito wetu na uchaguzi kuwa wa uhakika. **{EW 58.2}**

## Sura ya 12- Kugongagonga kwa kushangaza, kwa mafumbo-UMIZIMU-(Mysterious Rapping)* Angalia mwisho wa hii sura.

Agosti 24, 1850, niliona kwamba “umizimu-mysterious rapping” ulikuwa ni nguvu ya Shetani; baadhi ya huo ulitoka kwake moja kwa moja, na mwingine kupitia kwa mawakala wake, lakini wote ulitoka kwa Shetani. Hii ilikuwa ni kazi yake ambayo alitimiliza kwa njia mbalimbali; lakini bado watu wengi katika makanisa na ulimwengu walikuwa wamefunikwa na giza kuu kiasi kwamba walidhani na kushikilia kwamba ilikuwa ni nguvu ya Mungu. Malaika yule alisema, “ Je, haiwapasi watu kutafuta habari kwa Mungu wao? Je, waende kwa watu waliokufa kwa ajili ya watu walio hai?” Je walio hai wawaendee wafu kutafuta maarifa? Wafu hawajui lolote. Je, kwa ajili ya Mungu aliye hai mnakwenda kwa wafu? Wamemwacha Mungu aliye hai ili wapate kuzungumza na wafu ambao hawajui lolote. (Angalia Isaya 8:19, 20.) **{EW 59.1}**

Niliona kwamba punde ingechukuliwa kuwa ni kufuru kuzungumza dhidi ya umizimu ule (spirit rapping), na kwamba ungeenea zaidi na zaidi, kwamba nguvu za Shetani zingeongezeka zaidi na baadhi ya wafuasi wake waaminifu wangekuwa na uwezo wa kufanya miujiza na hata kuleta moto kutoka mbinguni mbele ya macho ya watu.

Nilioneshwa kwamba kwa umizimu na kiinimacho wachawi hawa wa kisasa bado wangeelezea miujiza yote iliyofanywa na Bwana wetu Yesu Kristo, na kwamba wengi wangeamini kwamba kazi zote za nguvu za Mwana wa Mungu wakati alipokuwapo duniani zilitimilizwa kwa nguvu hii hii (spirit rapping and mesmerism). [Mtazamo huu ulipotolewa, umizimu ulikuwa ndio tu umeinuka na bado ulikuwa mdogo; kulikuwa na watu wachache tu wenye kuwasiliana na mizimu. Tangu wakati huo umeenea duniani kote na wafuasi wake wanahesabika kwa mamilioni. Kama jambo la kawaida, watu wanaowasiliana na mizimu wameikataa Biblia na kuudharau Ukristo. Watu binafsi, kwa nyakati tofauti, walililaani jambo hili na kulipinga, lakini walikuwa wachache sana kiasi kwamba hakuna tahadhari iliyochukuliwa dhidi yao. Sasa watu wanaoamini kuwasiliana na mizimu wanabadilisha mbinu zao, na wengi hujiita "Wakristo wanaowasiliana na roho za wafu." Wakitangaza kwamba haitaridhisha kupuuza dini, na kuthibitisha kwamba wana imani ya kweli ya Kikristo. Kwa kuzingatia, pia, kwamba makasisi wengi maarufu wanakubaliana na umizimu, sasa tunaona njia iliyo wazi kwa utimilifu kamili wa utabiri huu, uliotolewa mnamo mwaka

1850. Soma pia maoni ya mwandishi katika ukurasa wa 86.] Nilielekezwa nyuma wakati wa Musa na kuona ishara na maajabu ambayo Mungu aliyafanya kupitia kwake mbele ya Farao, ambayo mengi yaliigizwa na waganga wa Misri; na kwamba mara tu kabla ya ukombozi wa mwisho wa watakatifu, Mungu angefanya kazi kwa nguvu kwa ajili ya watu Wake, na wachawi hawa wa kisasa wangeruhusiwa kuiga kazi ya Mungu.**{EW 59.2}**

Wakati huo utakuja hivi karibuni, nasi tutalazimika kuushikilia mkono wenye nguvu wa Yehova; kwa maana ishara hizi kuu zote na maajabu makubwa ya Ibilisi yamekusudiwa kuwadanganya watu wa Mungu na kuwaangusha chini-kuwashinda. Akili zetu zinapaswa kuwekwa kwa Mungu, na hatupaswi kuogopa hofu ya waovu, yaani, kuogopa kile wanachokiogopa, na kuheshimu kile wanachokiheshimu, bali tuwe jasiri na hodari kwa ajili ya Ukweli. Kama macho yetu yangefunguliwa, tungeliona aina za malaika waovu walio karibu nasi, wakijaribu kubuni njia mpya ya kutusumbua na kutuangamiza. Na tungelipaswa pia kuwaona malaika wa Mungu wakitulinda kutokana na nguvu zao; kwa kuwa jicho la Mungu linaloangalia daima liko juu ya Israeli kwa ajili ya

mema, na atawalinda na kuwaokoa watu Wake, ikiwa wataweka matumaini yao Kwake. Adui atakapokuja kama mafuriko, Roho wa Bwana atainua bendera dhidi yake.**{EW 60.1}**

Malaika yule akasema, “Kumbuka uko katika ardhi iliyorogwa.” Niliona kwamba ni lazima tukeshe na kuvaa silaha zote na kuchukua ngao ya imani, na hapo ndipo tutakapoweza kusimama, na mishale ya moto ya yule mwovu haitaweza kutudhuru. **{EW 60.2}**

*Spirit rapping is a practice that involves mediums using knocking and tapping to communicate with spirits during séances, which is linked to the spiritualism movement. The Fox sisters are known for their role in the rise of spiritualism in the 19th century after they began hearing mysterious rapping sounds in their home:

Kugongagonga  kusikojulikana kulikohusu waaguzi kutumia  ili kuwasiliana na mizimu wakati wa mikutano ya harakati ya umizimu. Akina dada Fox wanajulikana kwa sehemu yao waliyofanya katika kuongezeka kwa imani ya mizimu katika karne ya 19 baada ya kuanza kusikia sauti za ajabu zikigongagonga na kubishabisha, nyumbani mwao:.

## Sura 13-Wajumbe

[Angalia Kiambatisho.]

Bwana amenionesha mara nyingi, hali na mahitaji ya vito vya thamani waliotawanyika ambao bado hawajapata nuru ya Ukweli wa sasa, na ameonesha kwamba wajumbe wanapaswa kuharakisha kwenda kwao haraka iwezekanavyo, kuwapa ile nuru. Wengi kote kutuzunguka wanahitaji tu kuondolewa chuki na ubaguzi wao na ushahidi wa msimamo wetu wa sasa kuenea mbele yao kutoka katika Neno, nao wataupokea Ukweli wa sasa kwa furaha. Wajumbe wanapaswa kuziangalia roho kama wale ambao ni lazima watatoa hesabu. Maisha yao yanapaswa kuwa ni maisha ya kazi ngumu na maumivu makali ya roho, wakati ule ambapo uzito wa kazi ya thamani ya Kristo lakini iliyojeruhiwa mara nyingi iko juu yao. Watalazimika kuweka kando masilahi na starehe, faraja za ulimwengu na kuifanya kazi hii kuwa jambo la kwanza kufanya yote yaliyo katika uwezo wao ili kuuendeleza Ukweli wa sasa na kuokoa roho zinazoangamia. **{EW 61.1}**

Pia watapata thawabu nyingi. Katika taji zao za furaha wale waliosaidiwa kuponyoka makucha ya shetani nao na hatimaye kuokolewa watang'aa kama nyota milele na milele. Na kwa umilele wote watafurahia kuridhika moyoni ya kuwa wamefanya kile walichoweza katika kuuwasilisha Ukweli katika

usafi na uzuri wake, kiasi kwamba roho ziliupenda, zilitakaswa kupitia kwa huo, na kujinufaisha kwa fursa isiyokadirika ya kufanywa tajiri, na kuoshwa kwa damu ya Mwana-Kondoo na kukombolewa kwa ajili ya Mungu.**{EW 61.2}**

Niliona kwamba wachungaji wanapaswa kushauriana na wale ambao kwao wana sababu ya kuwaamini, wale ambao wamekuwa katika ujumbe wote, na wako imara katika Ukweli wote wa sasa, kabla ya kutetea mambo mapya muhimu, ambayo wanaweza kufikiria kuwa Biblia inakubaliana na kuidumisha. Ndipo wachungaji watakapokuwa wameungana kikamilifu na muungano wa wachungaji utahisiwa na kanisa. Mwendo kama huo niliona ungezuia migawanyiko isiyo na furaha, na kisha kusingekuwapo na hatari ya kundi la thamani kugawanywa, na kondoo kutawanyika bila mchungaji.**{EW 61.3}**

Pia niliona kwamba Mungu alikuwa na wajumbe ambao angewatumia katika kusudi Lake, lakini hawakuwa tayari. Walikuwa wapuuzi mno na waiso na umakini, kiasi kwamba hawakuweza kutoa mvuto mzuri kwa kundi na hawakuhisi uzito wa kazi na thamani ya roho kama vile ambavyo wajumbe wa Mungu wanapaswa kuhisi kwa ajili ya kuleta

matokeo mema. Malaika alisema, "*Iweni safi ninyi mnaochukua vyombo vya Bwana. Iweni safi ninyi mnaochukua vyombo vya Bwana*." Wanaweza kutimiliza mema kidogo tu isipokuwa wamejitoa kabisa kwa Mungu na kuhisi umuhimu na uzito wa ujumbe wa mwisho wa rehema ambao sasa unatolewa kwa kundi lililotawanyika. Baadhi ambao Mungu hajawaita wako tayari sana kuambatana na ujumbe huu. Lakini kama wangeuhisi uzito wa kazi hii na majukumu ya cheo kama hicho, wangehisi kurudi nyuma na kusema pamoja na Mtume, "Naye ni nani atoshaye kwa mambo hayo?" Sababu moja kwa nini wako tayari sana kwenda ni kwamba Mungu hajaweka uzito wa kazi hii juu yao. Si wote waliotangaza ujumbe wa malaika wa kwanza na wa pili wanapaswa kuutoa ule wa tatu, hata baada ya kuukubali kikamilifu, kwa maana baadhi wamekuwa katika makosa mengi na udanganyifu kiasi kwamba wanaweza tu kuokoa nafsi zao wenyewe, na kama watajitolea kuwaongoza wengine, watakuwa tu njia ya kuwaangusha. Lakini niliona kwamba baadhi ambao hapo awali waliingia kwa kina katika ushupavu wa dini, yaani kupitiliza, wangekuwa wa kwanza sasa kukimbia kabla Mungu hajawatuma, kabla hawajatakaswa kutokana na makosa yao ya

awali; wakiwa na uongo uliochanganywa na Ukweli, wangelisha kundi la Mungu kwa huo, na kama wangeliruhusiwa kuendelea, kundi lingedhoofika, na mashaka na mauti vingefuata. Niliona kwamba ingebidi wapepetwe na kupepetwa, hadi wameondolewa makosa yao yote, vinginevyo wasingeweza kamwe kuingia katika ufalme. Wajumbe hawakuweza kuwa na ujasiri katika kuwahukumu na kuwatambua wale ambao wamekuwa katika makosa na ushabiki kidini unaopitiliza, kama ule ambao wangekuwa nao kwa wale ambao wamekuwa katika Ukweli na si katika makosa ya kupindukia. Wengi, pia, ni wepesi mno kuwasukumiza kuingia shambani baadhi ambao ndio tu wameukiri Ukweli wa sasa, ambao wana mengi ya kujifunza na mengi ya kufanya kabla hawajaweza kuwa sawa mbele za Mungu wao wenyewe, sembuse kuonesha njia kwa wengine.**{EW 62.1}**

Niliona umuhimu wa wajumbe, hasa, kuangalia na kuzuia ushupavu wote wa kidini popote wanapoweza kuuona ukiinuka. Shetani anasonga kila upande, na tusipokesha kwa ajili ya kumpinga, na macho yetu yakafunguliwa kwa hila na mitego yake, na kuwa na silaha zote za Mungu, mishale ya

moto ya mwovu itatupiga. Kuna Kweli nyingi za thamani sana zilizo katika Neno la Mungu, lakini ni "U*kweli wa sasa*" ambao kundi linauhitaji sasa. Nimeona hatari ya wajumbe kukimbia kutoka katika hoja muhimu za Ukweli wa sasa, kuelezea sana mada ambazo hazijakusudiwa kuunganisha kundi na kutakasa roho. Shetani hapa atatumia kwa manufaa kila njia inayowezekana kuijeruhi kazi ya Mungu.**{EW 63.1}**

Lakini mada kama vile patakatifu, kwa kuhusiana na siku 2300, amri za Mungu na imani ya Yesu, zimekusudiwa kikamilifu kuelezea vuguvugu la Marejeo lililopita na kuonesha msimamo wetu wa sasa ni nini, kuimarisha imani za wenye mashaka, na kutoa uhakika kwa mustakabali wenye utukufu. Hizi, nimeziona mara nyingi, zilikuwa ndizo mada kuu ambazo wajumbe wanapaswa kuzielezea sana.**{EW 63.2}**

Ikiwa wajumbe wateule wa Bwana wangesubiri kila kikwazo kuondolewa katika njia yao, wengi kamwe wasingekwenda kuwatafuta kondoo waliotawanyika. Shetani ataweka vizuizi vingi sana ili kuwazuia wasifanye kazi. Lakini watalazimika kwenda kwa imani, wakimtumainia Yeye aliyewaita katika kazi Yake, na Yeye atafungua njia mbele yao,

kwa kadiri itakavyokuwa ni kwa faida yao na utukufu Wake. Yesu, mwalimu na Kielelezo Kikuu (Mfano Mkuu), hakuwa na mahali pa kuweka kichwa chake. Maisha Yake yalikuwa ni ya kazi ya taabu, huzuni, na mateso; hatimaye alijitoa mwenyewe kwa ajili yetu. Wale ambao, wanazisihi roho zipate kupatanishwa na Mungu, badala ya Kristo, na ambao wanatarajia kutawala pamoja na Kristo katika utukufu, ni lazima watarajie kushiriki mateso Yake hapa. “Wapandao kwa machozi Watavuna kwa kelele za furaha. Ingawa mtu anakwenda zake akilia, Azichukuapo mbegu za kupanda. Hakika atarudi kwa kelele za furaha, Aichukuapo miganda yake." Zaburi 126:5, 6. **{EW 63.3}**

*****

## Sura ya 14-Chapa ya Mnyama

Katika mandhari iliyooneshwa Juni 27, 1850, malaika aliyeandamana nami alisema, “Muda unakaribia kwisha. Je, unaakisi taswira ya kupendeza ya Yesu kama mlivyopaswa?” Kisha nilielekezwa duniani na nikaona kwamba

kungepaswa kuwapo na kujiweka tayari miongoni mwa wale ambao hivi karibuni wameukubali ujumbe wa malaika wa tatu. Malaika alisema, “ Jiandae, jiandae, jiandae.” (Get Ready, Get Ready, Get Ready) Mtapaswa kufa kifo kikubwa zaidi kwa ulimwengu kuliko ambavyo mmewahi kufa.” Niliona kwamba kulikuwa na kazi kubwa ya kufanywa kwa ajili yao bali muda mchache tu wa kuifanya.**{EW 64.1}**

Kisha niliona kwamba mapigo saba ya mwisho yangemiminwa juu ya wale ambao hawana mahali pa kimbilio, lakini ulimwengu haukuyajali kama vile matone mengi ya maji yaliyokuwa karibu kuanguka. Kisha niliwezeshwa kuvumilia kuona mandhari ya kutisha ya mapigo saba ya mwisho, ghadhabu ya Mungu. Niliona kwamba hasira Yake ilikuwa ya kuogofya na ya kutisha, na kama angeunyosha mkono Wake, au kuuinua kwa hasira, wakazi wa ulimwengu wangekuwa kana kwamba hawajawahi kuwapo, au wangepatwa na madonda yasiyotibika na mapigo yanayonyausha ambayo yangekuja juu yao, na wasingepata ukombozi wowote, bali wangeangamizwa nayo. Hofu kuu ilinishika, nami nilianguka kifudifudi mbele ya malaika yule na kumwomba aiondoe mandhari ile, aifiche kwangu,

kwa maana ilikuwa ya kuogofya sana. Kisha nilitambua, kama ambavyo sikuwahi kamwe hapo kabla, umuhimu wa kulichunguza Neno la Mungu kwa makini, ili kujua jinsi ya kuyaepuka mapigo ambayo Neno hilo linayatangaza kuwa yatakuja juu ya wote wasiomcha Mungu ambao watamwabudu mnyama na sanamu yake na kupokea chapa yake katika vipaji vya nyuso zao au katika mikono yao. Ilikuwa ni ajabu kubwa kwangu kwamba mtu yeyote angeweza kukiuka sheria ya Mungu na kuikanyaga Sabato Yake takatifu, wakati ambapo vitisho na shutuma za kuogofya kiasi hicho vilikuwa dhidi yao.**{EW 64.2}**

Papa ameibadilisha siku ya mapumziko kutoka siku ya saba kwenda katika siku ya kwanza. Amefikiria kubadilisha ile amri aliyopewa ya kumfanya mwanadamu amkumbuke Muumba wake. Amefikiria kubadilisha amri kubwa kabisa katika Amri kumi za Mungu na hivyo kujifanya kuwa sawa na Mungu, au hata kujiinua juu zaidi ya Mungu. Bwana habadiliki, kwa hivyo sheria yake haibadiliki; lakini papa amejiinua juu ya Mungu, katika kujitahidi kubadilisha maagizo Yake yasiyobadilika ya utakatifu, haki, na wema. Ameikanyaga chini ya mguu siku ya Mungu iliyotakaswa, na, kwa

mamlaka yake mwenyewe, kuweka katika nafasi yake moja ya zile siku sita za kazi. Taifa lote limemfuata huyo mnyama, na kila juma wanamwibia Mungu muda Wake mtakatifu. Papa amefanya ufa katika sheria takatifu ya Mungu, lakini niliona kwamba muda ulikuwa umefika kwa ukamilifu wa palipobomoka kutengenezwa na watu wa Mungu na mahali palipokuwa ukiwa kujengwa.**{EW 65.1}**

Nilimwomba Mungu mbele ya yule malaika apate kuwaokoa watu Wake ambao walikuwa wamepotea, awaokoe kwa sababu ya rehema zake. Mapigo yanapoanza kuanguka, wale wanaoendelea kuivunja Sabato takatifu hawatafungua vinywa vyao kutoa kusihi na udhuru ambao kwa sasa wanatoa kama sababu ya kuacha kuitunza. Vinywa vyao vitafungwa wakati yale mapigo yanapoanguka, na Mtoa sheria mkuu anahitaji haki kwa wale ambao wameichukulia sheria Yake takatifu kwa dhihaka na wameiita "laana kwa mwanadamu," "huzuni," na "dhaifu na kwamba zitavunjika muda wowote." Wakati watu hao wanahisi uwezo wa kushika kwa nguvu wa sheria hii ukiwashikilia, Maneno haya yataonekana mbele yao katika herufi zilizo hai, nao watatambua dhambi ya kuichukulia kwa dhihaka

sheria ile ambayo Neno la Mungu linaiita "*takatifu*, ya *haki*, na *nzuri*.**{EW 65.2}**"

Kisha nilielekezwa katika utukufu wa mbinguni, katika hazina iliyowekwa pale kwa ajili ya waaminifu. Kila kitu kilikuwa kizuri na kitukufu. Malaika wangeimba wimbo mzuri, kisha wangeacha kuimba na kuchukua taji zao kutoka kwenye vichwa vyao na kuzitupa zikimetameta miguuni pa Yesu aliye mzuri sana, na kwa sauti nzuri walipaza sauti, "Utukufu, Haleluya!" Nilijiunga nao katika nyimbo zao za sifa na heshima kwa Mwanakondoo, na kila wakati nilipofungua kinywa changu kumsifu, nilijisikia kuwa na hisia ya utukufu usioweza kuelezeka ambao ulinizunguka. Ulikuwa ni utukufu wa milele uzidio kuwa mwingi sana. Malaika alisema, “Waliosalia wachache wanaompenda Mungu na kuzishika amri Zake na kuwa waaminifu mpaka mwisho, wataufurahia utukufu huu na milele watakuwa mbele ya Yesu na kuimba pamoja na malaika watakatifu.”**{EW 66.1}**

Kisha macho yangu yalichukuliwa kutoka katika utukufu huo, nami nilielekezwa kwa masalio walioko duniani. Malaika aliwaambia, “ Je mtayaepuka mapigo saba ya mwisho? Mtaenda kutoka utukufu hadi utukufu na kuyafurahia yote

ambayo Mungu ameyaandaa kwa ajili ya wote wampendao na wako tayari kuteseka kwa ajili Yake? Kama ndivyo ilivyo, itawabidi kufa ili mpate kuishi. Kaeni tayari, Iweni tayari, kaeni tayari. Mnapaswa kuwa na maandalizi makubwa kuliko mliyonayo kwa sasa, kwa kuwa siku ya Bwana inakuja, katili kwa ghadhabu na hasira kali, ili kuifanya nchi kuwa ukiwa na kuwaangamiza wenye dhambi kutoka ndani yake  Toeni vyote kafara kwa Mungu.  Wekeni yote juu ya madhabahu Yake (dhabihuni yote)—nafsi, mali, na yote, kuwa dhabihu iliyo hai. Itahitaji kutoa yote ili mpate kuingia katika utukufu. Jiwekeeni hazina mbinguni, ambapo mwivi hawezi kupakaribia wala kutu kuharibu. Ni lazima mwe washirika wa mateso ya Kristo hapa kama mtakuwa washirika pamoja naye katika utukufu Wake utakaokuja baadaye." **{EW 66.2}**

Mbingu itakuwa rahisi sana kuingia (heaven is cheap enough!), ikiwa tutaipata kupitia katika mateso. Ni lazima tujikane nafsi njiani kote, tuifie nafsi kila siku, na kumruhusu Yesu peke yake aonekane, na kuufanya utukufu wake kuonekana daima. Niliona kwamba wale ambao wameukubali Ukweli kwa siku za karibuni wangelazimika kujua maana ya kuteseka kwa ajili ya Kristo, kwamba

wangekuwa na majaribu ya kupitia ambayo yangekuwa makali na yenye kuumiza, ili wapate kutakaswa na kuandaliwa kupitia mateso kupokea muhuri wa Mungu aliye hai, kupita katika wakati wa taabu, kumwona Mfalme katika uzuri Wake, na kuishi katika uwepo wa Mungu na wa malaika watakatifu.**{EW 67.1}**

Nilipoona kile tunachopaswa kuwa ili tupate kuurithi utukufu, na kisha kuona jinsi Yesu alivyoteseka ili kupata urithi mwingi kiasi kile kwa ajili yetu, niliomba kwamba tupate kubatizwa katika mateso ya Kristo, ili tusiyaepuke majaribu, wala kujikunja, bali tuyavumilie kwa uvumilivu na furaha, tukijua yale ambayo Yesu aliyapitia ili sisi kwa umaskini na mateso Yake tupate kutajirika. Malaika Alisema, “jikane nafsi, ni lazima upige hatua kwa haraka.” Baadhi yetu tumekuwa na muda wa kupata ukweli na kuendelea hatua kwa hatua, na kila hatua ambayo tumeipiga imetupa nguvu ya kupiga hatua inayofuata. Lakini sasa muda umekaribia kwisha, na kile ambacho tumekuwa tukijifunza kwa miaka, watu watalazimika kujifunza katika miezi michache. Pia kutakuwa na mengi ya kuondoa mawazoni na mengi zaidi ya kujifunza. Wale ambao hawatakubali kuipokea chapa ya mnyama na sanamu yake wakati

amri itakapotolewa, ni lazima wawe na uamuzi *sasa* wa kusema, *Hapana*, sisi hatutaiheshimu taasisi ya mnyama.**{EW 67.2}**

## Sura ya 15-Kipofu Kumwongoza Kipofu

Nimeona jinsi ambavyo viongozi vipofu walivyokuwa wakifanya kazi kwa bidii kufanya roho ziwe vipofu kama wao wenyewe, bila kutambua ni nini kinachowajia. Wanajiinua wenyewe dhidi ya Ukweli, na kadiri Ukweli unavyoshinda, wengi ambao waliwatazama walimu hawa kama watu wa Mungu na kutegemea kutoka kwao kupata nuru, wanafadhaika. Wanawauliza viongozi hawa kuhusiana na Sabato, na wao, kwa lengo la kuiondoa amri ya nne, watawajibu kuhusiana na hiyo. Niliona kwamba uaminifu halisi haukuzingatiwa katika kuchukua misimamo mingi ambayo ilichukuliwa dhidi ya Sabato. Lengo kuu ni kuizunguka Sabato ya Bwana, na kuiacha, na kisha kutunza siku nyingine ambayo si ile iliyotakaswa na kutukuzwa na Yehova. Ikiwa wanasukumwa kutoka katika msimamo mmoja, wanachukua msimamo

ulio kinyume, hata msimamo ule ambao walikuwa nao muda mfupi tu ulioopita ambao waliushutumu kama ulio na mapungufu-na usio na hekima. **{EW 68.1}**

Watu wa Mungu wanaingia katika umoja wa imani. Wale wanaoitunza Sabato ya Biblia wameungana katika maoni yao juu ya Ukweli wa Biblia. Lakini wale wanaoipinga Sabato miongoni mwa watu wa Marejeo wamefarakana na kutengana kwa namna ya kushangaza. Mmoja anajitokeza kwa upinzani dhidi ya Sabato na kuitangaza kuwa hivi na vile, na katika hitimisho anaiita iliyo thabiti. Lakini kadri juhudi yake isivyolipumzisha suala hilo katika Ukweli, na kadri kusudi la Sabato linavyoendelea na watoto wa Bwana bado wanaikubali, mwingine anajitokeza ili apate kuiangusha. Lakini katika kuwasilisha maoni yake ili kuikataa Sabato, anabomoa kabisa hoja za yule aliyefanya jitihada za kwanza dhidi ya Ukweli, na kuwasilisha nadharia iliyo kinyume chake kama ilivyo kwetu. Vivyo hivyo, kwa wa tatu na wa nne; lakini hakuna hata mmoja wao atakayeipatia kama ilivyo katika Neno la Mungu: "Siku ya saba ni Sabato ya Bwana, Mungu wako."**{EW 68.2}**

Watu kama hao, niliona, wana mawazo ya

kimwili, kwa hiyo hawaitii sheria takatifu ya Mungu. Hawakubaliani miongoni mwao wenyewe, lakini bado wanafanya kazi kwa bidii kwa mawazo yao kupotosha maana ya Maandiko ili kufanya ufa katika Sheria ya Mungu, kubadilisha, kukomesha, au kufanya chochote na amri ya nne badala ya kuitunza. Wanataka kulinyamazisha kundi la Mungu juu ya suala hili; kwa hiyo wanapata kitu kwa matumaini kwamba kitawatuliza na kwamba wengi wa wafuasi wao watazichunguza Biblia zao kidogo sana kiasi kwamba viongozi wao wanaweza kwa urahisi kufanya makosa kuonekana kama ndiyo Ukweli, na wanaipokea hivyo, bila kutazama juu kuliko viongozi wao.**{EW 69.1}**

**** *

## Sura ya 16-Maandalizi kwa Ajili ya Mwisho

Huko Oswego, New York, mnamo Septemba 7, 1850, Bwana alinionesha kwamba kazi kubwa inapaswa kufanywa kwa ajili ya watu Wake kabla hawajaweza kusimama vitani katika siku ya Bwana. Nilielekezwa kwa wale wanaokiri kuwa Waadventista, lakini wanaukataa Ukweli wa sasa, na kuona kwamba walikuwa wakigawanyika na

kwamba mkono wa Bwana ulikuwa katikati yao kuwagawanya na kuwatawanya sasa katika wakati wa kukusanya, ili kwamba vyombo vya thamani miongoni mwao, ambao hapo awali walidanganywa, wafunguliwe macho yao wapate kuona hali yao ya kweli. Na sasa Ukweli unapowasilishwa kwao na wajumbe wa Bwana, wako tayari kuusikiliza, na kuona uzuri na upatanifu wake, na kuwaacha washirika na makosa yao ya zamani, kuupokea kwa moyo Ukweli wa thamani na kusimama mahali ambapo wanaweza kuufasili msimamo wao.**{EW 69.2}**

Niliona kwamba wale wanaoipinga Sabato ya Bwana wasingeweza kuchukua Biblia na kuonesha kwamba msimamo wetu sio sahihi; kwa hiyo wangewakashifu wale wanaoamini na kufundisha Ukweli na wangeshambulia tabia zao. Wengi ambao hapo awali walikuwa waangalifu na walimpenda Mungu na Neno Lake wamekuwa wagumu sana kwa kukataa nuru ya Ukweli kiasi kwamba hawasiti kuwasilisha vibaya na kuwashutumu kwa uwongo wale wanaoipenda Sabato takatifu, ikiwa kwa kufanya hivyo wanaweza kujeruhi mvuto wa wale wanaotangaza Ukweli bila woga. Lakini mambo haya hayatazuia kazi ya Mungu. Kiuhalisia, njia hii

inayofuatwa na wale wanaouchukia Ukweli itakuwa ndiyo njia hasa ya kufungua macho ya wengine. Kila kito cha thamani kitasababishwa kuonekana na kukusanywa, kwa kuwa mkono wa Bwana umewekwa karibu kuwarejesha waliosalia wa watu Wake, naye ataikamilisha kazi hiyo kwa utukufu. **{EW 69.3}**

Sisi tunaoiamini ile Kweli tunapaswa kuwa waangalifu sana kutokutoa fursa kwa ajili ya mema yetu kuzungumziwa vibaya. Tunapaswa kufahamu kwamba kila hatua tunayoichukua ni kufuatana na Biblia; kwa sababu wale wanaozichukia amri za Mungu watashinda kutokana na hatua mbaya na makosa yetu, kama waovu walivyofanya mnamo mwaka 1843.**{EW 70.1}**

Mei 14, 1851, niliona uzuri na kupendeza kwa Yesu. Nilipoona utukufu Wake, wazo halikunijia kwamba ningeweza kutengwa kutoka katika uwepo Wake. Niliona nuru ikitoka katika utukufu ule uliomzunguka Baba, na ilipokuwa inajongea karibu na mimi, mwili wangu ulitetemeka na kutikisika kama jani. Nilidhani kwamba kama ingenikaribia ningekoma kuwepo/ningekufa, lakini nuru ile ilinipita. Ndipo ningeweza kuwa na hisia fulani ya Mungu mkuu na wa kuogofya ambaye tunapaswa

kutenda pamoja naye. Niliona wakati ule ni maoni hafifu kiasi gani walionayo baadhi juu ya utakatifu wa Mungu, na ni kiasi gani wanalitaja bure Jina Lake lililo takatifu na la kuheshimiwa sana, bila kutambua kwamba ni Mungu, Mungu mkuu na wa kuogofya, ambaye Ndiye wanazungumza juu yake. Wakati wa kuomba, wengi hutumia maneno ya kizembe na yasiyo na heshima, yanayomhuzunisha Roho mwema wa Bwana na kusababisha maombi yao kufungiwa nje ya mbingu.**{EW 70.2}**

Niliona pia kwamba wengi hawajui kile wanacholazimika kuwa ili waweze kuishi mbele za macho ya Bwana pasipo kuwa na kuhani mkuu katika patakatifu wakati wa taabu. Wale wanaopokea muhuri wa Mungu aliye hai na kulindwa katika wakati wa taabu ni lazima waakisi sura ya Yesu kikamilifu.**{EW 71.1}**

Niliona kwamba wengi walikuwa wakipuuza maandalizi ambayo yalikuwa yanahitajika sana na walikuwa wakitazamia wakati wa "kuburudishwa" na "mvua ya masika" kuwaandaa kuwa tayari kusimama katika siku ya Bwana na kuishi machoni pake. Lo, ni wangapi niliwaona katika wakati wa taabu wakiwa bila kinga! Walikuwa wamepuuza maandalizi yaliyohitajika; kwa hiyo hawakuweza

kupata kuburudishwa ambako wote lazima wawe nako ili kuwaandaa kuishi machoni pa Mungu mtakatifu. Wale wanaokataa kuchongwa* na manabii na kushindwa kusafisha roho zao kwa kuitii Kweli yote, na ambao wako tayari kuamini kwamba hali yao ni bora zaidi kuliko ilivyo hasa, watafikia wakati wa kuanguka kwa mapigo, na kisha kuona kwamba walihitajika kuchongwa na kusawazishwa kwa ajili ya jengo. Lakini wakati ule hakutakuwa na muda wa kufanya hivyo na hakuna Mtetezi wa kutetea kesi yao mbele ya Baba. Kabla ya wakati huu tamko lenye uzito wa kuogofya litakuwa limetolewa, "Mwenye kudhulumu na azidi kudhulumu; na mwenye uchafu na azidi kuwa mchafu; na mwenye haki na azidi kufanya haki; na mtakatifu na azidi kutakaswa." Niliona kwamba hakuna mtu angeweza kushiriki "kuburudishwa" kule isipokuwa kama watakuwa wamepata ushindi juu ya kila hatari, juu ya kiburi, ubinafsi, kuupenda ulimwengu, na juu ya kila neno na tendo baya. Tunapaswa, kwa hiyo, kuwa tunajongea karibu na Bwana zaidi na zaidi, na kwa dhati na bidii kujitahidi kuyafanya maandalizi yale ambayo ni muhimu katika kutuwezesha kusimama katika vita katika siku ile ya Bwana. Hebu wote wakumbuke kwamba

Mungu ni mtakatifu na kwamba hakuna kiumbe hata mmoja isipokuwa wale walio watakatifu wanaweza kukaa mbele ya uso Wake *(Kuchonga kama mawe ili kuondoa ncha kali na kuwa laini).**{EW 71.2}**

## Sura ya 17-Maombi na Imani

Nimeona mara kwa mara kwamba watoto wa Bwana hupuuza mno maombi, hasa maombi ya faragha, kwa kiasi kikubwa mno, kiasi kwamba wengi hawaitumii imani ile ambayo ni haki na wajibu wao kutumia, mara nyingi wakingojea hisia ile ambayo imani peke yake inaweza kuileta. Hisia si imani; haya mawili ni tofauti. Imani ni kwa ajili yetu kutumia, na kuizoeza, lakini hisia za furaha na baraka ni za Mungu kutoa. Neema ya Mungu huja katika nafsi kupitia njia ya imani iliyo hai, na imani hiyo iko katika uwezo wetu kuitumia.**{EW 72.1}**

Imani ya kweli hushikilia na kudai baraka iliyoahidiwa kabla haijapatikana na kuhisiwa. Ni lazima tupeleke maombi yetu kwa imani ndani ya pazia la pili na kuruhusu imani yetu kuishikilia baraka iliyoahidiwa na kudai kuwa ni yetu. Ndipo hapo tunapaswa kuamini kwamba tunaipokea

baraka hiyo, kwa sababu imani yetu imeishikilia, na kulingana na Neno ni yetu. "Yoyote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu." Marko 11:24. Hii ndiyo imani, imani ya wazi, kuamini kwamba tunapokea baraka, hata kabla ya kuipata. Baraka iliyoahidiwa inapopatikana na kufurahiwa, imani inamezwa. Lakini wengi hudhani kuwa wana imani kubwa wakati wanapokuwa naRoho Mtakatifu kwa wingi na kwamba hawawezi kuwa na imani isipokuwa wanahisi nguvu ya Roho. Watu kama hao wanachanganya imani na baraka ambayo huja kupitia imani. Wakati hasa wa kutumia imani ni pale tunapohisi kutokuwa kabisa na Roho. Wakati ambapo mawingu mazito ya giza yanaonekana kutanda juu ya akili, huo ndio wakati wa kuruhusu imani iliyo hai kulitoboa giza hilo na kuyatawanya mawingu. Imani ya Kweli huegemea juu ya ahadi zilizo katika Neno la Mungu, na wale tu ambao wanalitii Neno hilo wanaweza kuzidai ahadi zake tukufu. “Mkikaa ndani Yangu na Maneno Yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa.” Yohana 15:7. “na lolote tuombalo, twalipokea Kwake, kwa kuwa twazishika amri Zake, na kuyatenda yapendezayo machoni Pake.” 1

Yohana 3:22.**{EW 72.2}**

Tunapaswa sana kuwa katika maombi ya faragha. Kristo ndiye mzabibu, ninyi ni matawi. Na ikiwa tungepaswa kukua na kusitawi, ni lazima tuendelee daima kupata ute wa mti wenye lishe kutoka kwa Mzabibu ulio Hai; kwa kuwa tukiwa tumetengwa na Mzabibu tunakosa nguvu.**{EW 73.1}**

Nilimuuliza malaika kwa nini hakukuwa na imani na nguvu tena katika Israeli. Alisema, "Mnauachilia mkono wa Bwana mapema mno. Sukumeni maombi yenu kwenda katika kiti cha enzi, na kushikilia kwa imani thabiti. Ahadi ni za hakika. Aminini kwamba mnapokea vitu vile mnavyoviomba, nanyi mtavipata." Kisha nilielekezwa kwa Eliya. Alikuwa chini ya hisia kali sawa na sisi, naye aliomba kwa bidii. Imani yake ililivumilia mitihani/jaribu Aliomba mara saba mbele za Bwana, na mwishowe wingu lilionekana. Niliona kwamba tulikuwa na shaka na ahadi za hakika, na kumjeruhi Mwokozi kwa kukosa kwetu imani. Malaika alisema, " Jifunge silaha, na juu ya yote chukua ngao ya imani; kwa kuwa hiyo itaulinda moyo, uhai hasa, kutokana na mishale ya moto ya yule mwovu." Ikiwa adui ataweza kuwaongoza wale waliokata tamaa katika kuondoa macho yao kutoka kwa Yesu, na

kujitazama wao wenyewe, na kufikiri sana juu ya kutokustahili kwao, badala ya kuwaza sana juu ya ustahili wa Yesu, upendo Wake, sifa Zake, na rehema Yake kuu, ataiondolea mbali ngao yao ya imani na kupata lengo lake; watakuwa wazi kwa majaribu yake makali. Kwa hivyo wanyonge wanapaswa kumtazama Yesu, na kumwamini Yeye; hapo ndipo wanapoonesha imani.**{EW 73.2}**

## Sura ya 18-Wakati wa Kukusanya

Septemba 23, Bwana alinionesha kwamba alikuwa amenyosha mkono Wake mara ya pili ili kuwarejesha masalia/waliosalia miongoni mwa watu Wake, [angalia ukurasa wa 86.] na kwamba jitihada lazima ziongezwe tena maradufu katika wakati huu wa kukusanya. Wakati wa kutawanywa, Israeli ilipigwa na kuraruliwa, lakini sasa wakati wa kukusanya Mungu atawaponya na kuwafunga watu Wake. Wakati wa kutawanywa, juhudi zilizofanywa kueneza Ukweli zilikuwa na matokeo madogo tu, zikikamilisha kidogo tu au kutokukamilisha chochote; lakini wakati wa kukusanya, wakati Mungu ameweka mkono Wake kuwakusanya watu

Wake, juhudi za kueneza Ukweli zitakuwa na matokeo yake yaliyokusudiwa. Wote wanapaswa kuwa wamoja na wenye bidii katika kazi. Niliona kuwa ilikuwa makosa kwa yeyote kurejelea kutawanywa kama mifano ya kutuongoza sasa katika kukusanya; kwa kuwa kama Mungu hatatufanyia zaidi ya yale aliyofanya wakati huo, Israeli isingekusanywa kamwe. Nimeona kwamba chati ile ya 1843 iliongozwa na mkono wa Bwana, na kwamba haipaswi kubadilishwa; kwamba takwimu zilikuwa kama Yeye alivyozitaka ziwe; kwamba mkono Wake ulikuwa juu yake na kuficha makosa katika baadhi ya takwimu, ili yasiweze kuonekana na mtu yeyote, mpaka pale mkono Wake utakapoondolewa. [Hii inadokeza kuhusu chati ile iliyotumiwa wakati wa vuguvugu la 1843, na inarejelea kwa namna ya pekee katika hesabu ya vipindi vya unabii kama vilivyoonekana kwenye chati hiyo. Sentensi inayofuata inaeleza kwamba kulikuwa na kukosa usahihi ambako katika majaliwa ya Mungu kuliruhusiwa kuwepo. Lakini hii haizuii uchapishaji wa chati baadaye, kitu ambacho kingeweza kusahihisha kosa hilo, baada ya vuguvugu la 1843 kupita, na hesabu kama ilivyokuwa imefanywa hapo awali kumaliza kusudi

Lake.] **{EW 74.1}**

Kisha nikaona kuhusiana na "ya daima" (Danieli 8:12) kwamba neno "sadaka" lilitolewa na hekima ya mwanadamu, na halistahili kuwa katika fungu hilo, na kwamba Bwana alitoa mtazamo sahihi juu yake kwa wale waliotoa kilio cha saa ya hukumu. Wakati umoja ulipokuwepo, kabla ya 1844, karibu wote walikuwa wamoja juu ya maoni sahihi ya "daima au kila siku"; lakini katika mchafuko tangu 1844, maoni mengine yamepokelewa kwa moyo, na giza na mchafuko vimefuatia. Muda haujawahi kuwa kipimo tangu 1844, na kamwe hautakuwa tena kipimo.**{EW 74.2}**

Bwana amenionesha kwamba ujumbe wa malaika wa tatu lazima uende, na kutangazwa kwa watoto wa Bwana waliotawanyika, lakini haupaswi kutegemea wakati. Niliona kwamba baadhi walikuwa wanapata msisimko wa bandia, kutokana na wakati wa kuhubiri; lakini ujumbe wa malaika wa tatu ni wenye nguvu kuliko wakati unavyoweza kuwa. Niliona kwamba ujumbe huu unaweza kusimama juu ya msingi wake wenyewe na hauhitaji wakati kwa ajili ya kuuimarisha; na kwamba utakwenda kwa uwezo wenye nguvu nyingi, na kutenda kazi yake, na utafupishwa katika

haki.**{EW 75.1}**

Kisha nilielekezwa kwa baadhi ambao wako katika kosa kubwa la kuamini kwamba ni jukumu lao kwenda katika Yerusalemu ya Kale, [angalia kiambatisho.] na kufikiri kwamba wana kazi ya kufanya huko kabla Bwana hajaja. Mtazamo kama huo umekusudiwa kuchukua akili na shauku kutoka katika kazi ya sasa ya Bwana, chini ya ujumbe wa malaika wa tatu; kwa kuwa wale wanaodhani kwamba bado wanapaswa kwenda Yerusalemu wataweka  akili zao huko, na fedha zao zitazuiliwa kwenda katika kazi ya Ukweli wa sasa ili zipate kuwafikisha wao wenyewe pamoja na wengine wengine mahali pale. Niliona kwamba utume kama huo haungetimiza mema halisi, kwamba ungechukua muda mrefu sana kuwafanya Wayahudi wachache sana kuamini hata katika ujio wa kwanza wa Kristo, sembuse kuamini katika ujio Wake wa pili. Niliona kwamba Shetani alikuwa amewadanganya sana baadhi ya watu katika jambo hili na kwamba roho zilizowazunguka kote katika nchi hii zingeweza kusaidiwa na wao na kuongozwa katika kuzishika amri za Mungu, lakini walikuwa wakiwaacha waangamie. Niliona pia kwamba Yerusalemu ya Kale isingeweza kujengwa tena

kamwe; na kwamba Shetani alikuwa akifanya kila awezalo kuziongoza akili za watoto wa Bwana katika mambo haya sasa, katika wakati wa kukusanya, ili kuwazuia wasiweke shauku yao yote katika kazi ya Bwana ya sasa, na kuwafanya wapuuze maandalizi muhimu kwa ajili ya siku ya Bwana. **{EW 75.2}**

*****

**Msomaji Mpendwa:** Utambuzi wa wajibu kwa ndugu na dada zangu na shauku kwamba damu ya roho isije ikapatikana kwenye nguo zangu, zimeniongoza katika kuandika kazi hii ndogo. Ninajua kutokuamini ambako kuko katika akili za watu wengi kuhusiana na maono, pia kwamba wengi wanaokiri kuwa wanamtafuta Kristo na kufundisha kwamba tuko katika "siku za mwisho" wanayaita yote kuwa ni ya Shetani. Natarajia upinzani mkubwa kutoka kwa watu kama hao, na kama nisingehisi kwamba Bwana analihitaji hilo kutoka kwangu, nisingeyaweka maoni yangu hadharani kiasi hicho, kwa kuwa, pengine yataibua chuki na dharau kutoka kwa baadhi. Lakini ninamtii Mungu kuliko mwanadamu.**{EW 76.1}**

Wakati Bwana aliponipa maagizo mbalimbali

kwa mara ya kwanza ya kuwasilisha kwa watu Wake, ilikuwa ni vigumu kwangu kuyatangaza, na mara nyingi niliyalainisha na kuyafanya yawe laini kadiri ilivyowezekana kwa kuogopa kuwahuzunisha wengine. Ilikuwa ni jaribu kubwa kutangaza Jumbe/maagizo kama Bwana alivyoyatoa kwangu. Sikutambua kuwa sikuwa mwaminifu mno na sikuona dhambi na hatari ya mwelekeo kama huo hadi nilipochukuliwa katika maono mbele ya Yesu. Aliniangalia kwa uso uliokunjwa na kugeuza uso Wake kutoka kwangu. Haiwezekani kuelezea hofu na uchungu niliohisi wakati ule. Nilianguka kifudifudi mbele Yake, lakini sikuwa na uwezo wa kusema neno lolote. Lo, nilitamani kiasi gani kufunikwa na kufichwa kutoka katika uso ule uliokunjwa ndita kwa namna ya kutisha! Kisha niliweza kutambua, kwa kiasi fulani, hisia za waliopotea zitakavyokuwa pale watakapolia, "Milima na miamba, tuangukieni, tusitirini, mbele za uso Wake Yeye aketiye juu ya kiti cha enzi, na hasira ya Mwana-Kondoo." **{EW 76.2}**

Wakati huu malaika aliniambia niinuke, na mandhari yaliyokutana na macho yangu hayawezi kuelezeka. Kundi moja lilikuwa likiwasilishwa mbele yangu ambalo nywele na mavazi yake yalivurugika

na ambao nyuso zao zilikuwa taswira hasa ya kukata tamaa na hofu kuu. Walikuja karibu nami na kuchukua mavazi yao na kuyasugua juu ya mavazi yangu. Niliyatazama mavazi yangu na kuona kwamba yalikuwa na madoa ya damu, na kwamba damu ile ilikuwa ikitoboa matundu ndani yake. Tena nilianguka chini ya miguu ya yule malaika aliyeandamana nami. Sikuweza kutoa udhuru hata mmoja. Ulimi wangu ulikataa matamshi yote, nami nilitamani kuwa mbali na mahali Patakatifu kama hapo. Tena malaika yule alinisimamisha kwa miguu yangu na kusema, "Hii si hali yako sasa, lakini tukio hili limepita mbele yako kukujulisha hali yako inavyokuwa ikiwa utapuuza kuwatangazia wengine kile ambacho Bwana amekuonesha. Lakini ikiwa utakuwa mwaminifu hata mwisho, utakula matunda ya mti wa uzima na kunywa maji kutoka katika mto wa maji ya uzima. Itakupasa kupitia mateso mengi, lakini neema ya Mungu yatosha." Ndipo nilipojisikia kuwa tayari kutenda yote ambayo Bwana angetaka niyatende ili niweze kupata ukubali Wake na wala siyo chuki Yake yenye uso uliokunjwa ndita kwa kuogofya sana.**{EW 76.3}**

Mara nyingi nimeshtakiwa kwa uongo kwamba ninafundisha maoni yanayohusiana na Umizimu.

Lakini kabla mhariri wa *Day-Star* [angalia kiambatisho.] hajaingia katika udanganyifu huo, Bwana alinipa mandhari ya athari ya kusikitisha na ya kutia ukiwa ambayo ingeletwa juu ya kundi na yeye [mhariri] na wengine katika kufundisha mitazamo ya umizimu. Mara nyingi nimemwona Yesu Mwenye kupendeza, kwamba Yeye ni nafsi. Nilimuuliza kama Baba Yake alikuwa ni nafsi na alikuwa na umbo kama Lake. Yesu alisema, "Mimi Niko katika mfano halisi wa nafsi ya Baba Yangu." **{EW 77.1}**

Mara nyingi nimeona kwamba mtazamo wa umizimu uliondoa utukufu wote wa mbinguni, na kwamba katika akili nyingi, kiti cha enzi cha Daudi na nafsi ya Yesu Mwenye kupendeza vimechomwa katika moto wa Umizimu. Nimeona kwamba baadhi ambao wamedanganywa na kuongozwa katika kosa hili wataletwa kwenye nuru ya Ukweli, lakini itakuwa vigumu mno kwao kuondokana kabisa na nguvu za udanganyifu za Umizimu. Watu kama hao wanapaswa kufanya kazi kamili katika kukiri makosa yao na kuyaacha milele.**{EW 77.2}**

Ninapendekeza kwako, msomaji mpendwa, Neno la Mungu kama kanuni ya imani na desturi yako. Kwa Neno hilo tutapaswa kuhukumiwa.

Mungu, katika Neno hilo, ameahidi kutoa njozi katika “*siku za mwisho*”; si kwa ajili ya kuwa kanuni mpya ya imani, bali kuwa faraja ya watu Wake, na kuwasahihisha wale wanaokosea kutoka katika Ukweli wa Biblia. Hivyo ndivyo Mungu alivyoshughulika na Petro pale alipokuwa karibu kumtuma kuhubiri kwa watu wa Mataifa. (Matendo 10.)**{EW 78.1}**

Kwa wale ambao wanaweza kuisambaza kazi hii ndogo, Ningesema kwamba imekusudiwa kwa ajili ya wale tu walio wanyofu au dhati pekee yao, na si kwa wale ambao wangedhihaki mambo ya Roho wa Mungu.**{EW 78.2}**

*****

## Sura ya 19-Ndoto za Mama White

[*Imerejelewa katika Ukurasa wa 12*]

Niliota kuhusu kuona hekalu ambalo watu wengi walikuwa wakikusanyika. Ni wale tu ambao walilikimbilia hekalu hilo kupata usalama, ndio wangeokolewa mwisho wa kufungwa kwa wakati. Wale wote ambao walibaki nje wangepotea milele.

Umati wa watu uliokuwa nje, ambao walikuwa wakienda njia zao mbalimbali, walikuwa wakiwadhihaki na kuwafanyia mizaha wale ambao walikuwa wakiingia hekaluni, na kuwaambia kwamba mpango huu wa usalama ulikuwa udanganyifu wa kijanja, kwamba, kwa kweli, hakukuwa na hatari yoyote ya kuepuka. Hata waliwashikilia baadhi ili kuwazuia wasiharakishe ndani ya kuta.**{EW 78.3}**

Kwa kuogopa kuchekwa na kudhihakiwa, nilifikiri kuwa ingekuwa bora kusubiri hadi umati umetawanyika, au hadi pale ambapo ningeweza kuingia bila wao kuniona. Lakini idadi iliongezeka badala ya kupungua, na kwa kuogopa kuchelewa sana, niliondoka haraka nyumbani kwangu na kujipenyeza kupitia katika umati ule. Katika shauku yangu ya kufika hekaluni sikuangalia au kujali umati ulionizunguka. Nilipoingia katika jengo hilo, niliona kwamba hekalu hili kubwa lilitegemezwa na nguzo moja kubwa, na katika hili alikuwa amefungwa Mwana-Kondoo aliyeraruliwa-raruliwa vibaya na kutokwa na damu. Sisi tuliokuwapo tulionekana kujua kwamba Mwanakondoo Huyu alikuwa ameraruliwa na kuchubuliwa kwa sababu yetu. Wote walioingia hekaluni ni lazima waje mbele Yake

na kukiri dhambi zao.**{EW 78.4}**

Mara tu mbele ya Mwana-Kondoo huyu kulikuwa na viti vilivyoinuliwa ambavyo juu yake waliketi kundi la watu waliokuwa wakionekana kuwa wenye furaha sana. Nuru ya mbinguni ilionekana kuangaza juu ya nyuso zao, nao walimsifu Mungu na kuimba nyimbo za shukrani za furaha ambazo zilionekana kuwa kama muziki wa malaika. Hawa ndio wale waliokuja mbele ya Mwanakondoo, wakakiri dhambi zao, wakasamehewa, na sasa walikuwa wakingojea kwa matarajio yenye furaha tukio fulani la furaha.**{EW 79.1}**

Hata baada ya kuingia katika jengo hili hofu ilinijia na hisia ya aibu kwamba ni lazima nijinyenyekeshe mbele ya watu hawa. Lakini nilionekana kulazimika kusonga mbele, na polepole nilikuwa nikiizunguka nguzo kwa ajili ya kumkabili Mwanakondoo, wakati tarumbeta ilipolia, hekalu lilitetemeka, kelele za ushindi ziliinuka kutoka kwa watakatifu waliokusanyika, nuru ya kutisha ililiangazia jengo hilo, kisha kukawa na giza nene. Watu wote wale wenye furaha walikuwa wametoweka pamoja na mwangaza, na niliachwa peke yangu katika hofu kuu ya kimya ya usiku.**{EW**

**79.2}**

Niliamka kwa uchungu wa akili na sikuweza kujiridhisha kwamba nilikuwa nikiota ndoto. Ilionekana kwangu kwamba hukumu yangu ilikuwa imeamuliwa, kwamba Roho wa Bwana alikuwa ameniacha, na kamwe asingerudi tena. Hali yangu ya kukata tamaa ilizidi kuwa nzito, kama hilo lingetokea.**{EW 79.3}**

Punde baada ya hii nilipata ndoto nyingine. Nilionekana kuwa nimekaa katika hali ya kukata tamaa kwa unyonge kabisa, na uso wangu ukiwa mikononi mwangu, nikitafakari hivi: Kama Yesu angekuwa duniani, ningekwenda Kwake, nikajitupe miguuni Pake, na kumwambia mateso yangu yote. Yeye Asingeweza kuniacha, angenihurumia, nami ningempenda na kumtumikia daima. Mara tu wakati huo mlango ulifunguliwa, na mtu mwenye umbo na sura nzuri aliingia. Aliniangalia kwa huruma na kusema: “ Je, unataka kumwona Yesu? Yupo hapa na unweza kumwona ukiwa unatamani kufanya hivyo. Chukua kila kitu ulicho nacho na unifuate.”**{EW 79.4}**

Masikio yangu yalilisikia hili kwa furaha isiyoelezeka, na kwa furaha nilikusanya mali yangu

ndogo, kila kipambo kidogo kizuri cha thamani ndogo kilichothaminiwa, na kumfuata mwongozaji wangu. Aliniongoza kwenye ngazi zilizoinuka sana na zilizoonekana kuwa si imara. Nilipoanza kupanda ngazi ile, alinitahadharisha kukaza macho yangu kuangalia juu, nisije nikapata kizunguzungu na kuanguka. Wengine wengi ambao walikuwa wakiupanda mwinuko ule wa wima walianguka kabla ya kufika kileleni.**{EW 80.1}**

Hatimaye tulifikia hatua ya mwisho na kusimama mbele ya mlango. Hapa mwongozaji wangu alinielekeza kuacha vitu vyote ambavyo nilikuwa nimekuja navyo. Kwa furaha niliweka chini; kisha alifungua mlango na kuniambia niingie. Baada ya muda mfupi nilisimama mbele ya Yesu. Ule uso mzuri ulikuwa dhahiri wa nisingeweza kuukosea. Sura angavu ya ukarimu na ukuu kama ile isingeweza kuwa ya mtu mwingine yeyote. Kadiri macho Yake yalivyonitazama, nilijua mara moja kuwa alikuwa anajua kila hali ya maisha yangu na mawazo yangu yote ya ndani na hisia.**{EW 80.2}**

Nilijaribu kujikinga na macho Yake, nikihisi kutoweza kuvumilia macho Yake yachunguzayo, lakini alinikaribia kwa tabasamu, na, huku akiweka mkono Wake juu ya kichwa changu, alisema:

“Usiogope.” Kusikika kwa sauti Yake tamu kulisisimua moyo wangu kwa furaha ambayo nilikuwa sijawahi kuipata hapo awali. Nilikuwa na furaha mno kuweza kutamka neno, lakini, nikiwa nimezidiwa na furaha isiyoelezeka, nilishuka kifudifudi miguuni Pake. Nilipokuwa nimelala pale pasipo kujiweza, mandhari mazuri na za utukufu zilipita mbele yangu, na nilionekana kuwa nimefika katika usalama na amani ya mbinguni. Hatimaye nguvu zangu zilirudi, nami niliinuka. Macho ya upendo ya Yesu bado yalikuwa juu yangu, na tabasamu Lake lilijaza roho yangu kwa furaha. Uwepo Wake ulinijaza kwa kicho takatifu na upendo usioelezeka.**{EW 80.3}**

Mwongozaji wangu sasa alifungua mlango nasi sote tulitoka nje. Aliniambia nichukue tena vitu vile nilivyoviacha nje. Hili likiwa limetendeka, alinikabidhi kamba ya kijani iliyoviringishwa kwa karibu. Hii alinielekeza niiweka karibu na moyo wangu, na nilipotaka kumwona Yesu, niichukue kutoka kifuani mwangu na kuinyosha hadi mwisho. Alinionya nisije nikaiacha kubaki ikiwa imeviringishwa kwa muda wowote, isije ikajifunga mafundo na kisha ikawa vigumu kuinyosha. Niliiweka kamba ile karibu na moyo wangu na kwa

furaha nikashuka katika ngazi ile nyembamba, huku nikimsifu Bwana na kwa furaha nikawaambia wote niliokutana nao mahali ambapo wangeweza kumpata Yesu. Ndoto hii ilinipa matumaini. Kamba ya kijani iliwakilisha imani akilini mwangu, na uzuri na usahili wa kumtegemea Mungu ulianza kupambazuka katika nafsi yangu iliyokuwa imeingiwa giza.**{EW 81.1}**

*****

## Sura ya 20 -Ndoto ya William Miller

[*Iliyotajwa kwenye Ukurasa wa 48*]

Niliota kwamba Mungu, kwa mkono usioonekana, alinitumia kibweta kilichofanyizwa kwa namna ya pekee kilichokuwa na urefu wa takriban inchi kumi kwa **sita mraba,** kilichotengenezwa kwa mpingo na kupambwa kwa lulu kwa namna ya pekee. Kwenye kibweta kulikuwa na ufunguo ulioshikizwa. Mara moja niliuchukua ufunguo ule na kukifungua kibweta kile, ambapo, kwa mshangao na mshituko wangu, nilikuta kimejaa vito vya kila aina na ukubwa, almasi, mawe

ya thamani, na sarafu za dhahabu na za fedha zenye kila kipimo na thamani, vikiwa vimepangwa vizuri katika sehemu zake kadhaa ndani ya kibweta hiki; na kwa kupangwa hivyo viliakisi nuru na utukufu unaolingana na jua peke yake. **{EW 81.2}**

Nilifikiri kuwa haikuwa jukumu langu kufurahia mwonekano huu mzuri peke yangu, ingawa moyo wangu ulifurahi kupita kiasi kwa mng'aro, uzuri, na thamani ya vilivyokuwa ndani yake. Kwa hivyo nililiweka kwenye meza katika chumba changu na kutangaza neno ili wote ambao wangekuwa na shauku waweze kuja na kuona mandhari yenye utukufu na mng'aro ambayo haijawahi kuonekana kwa macho ya mwanadamu katika maisha haya.**{EW 81.1}**

Watu walianza kuingia ndani, mwanzoni wakiwa wachache kwa idadi, lakini wakaongezeka na kuwa umati. Walipoangalia ndani ya kibweta kile kwa mara ya kwanza, walishangaa na kupiga kelele kwa furaha. Lakini watazamaji walipoongezeka, kila mtu alianza kuvisumbua vito vile, wakivitoa kwenye kibweta na kuvitawanya juu ya meza.**{EW 82.1}**

Nilianza kuwaza kwamba mmiliki angelihitaji kibweta na vito tena kutoka mkononi mwangu; na

kama ningeruhusu vitawanyike, nisingeweza kamwe kuviweka tena katika nafasi yake kwenye kibweta kama hapo awali; na nilihisi kuwa nisingeweza kutimiza uwajibikaji wake, kwani ungekuwa ni mkubwa sana. Kisha nikaanza kuwasihi watu wasiviguse, wala kuvitoa kwenye kibweta kile; lakini kadiri nilivyozidi kuwasihi, ndivyo walivyovitawanya zaidi; na sasa walionekana kuvitawanya kwenye chumba chote, sakafuni na kwenye kila samani chumbani.**{EW 82.2}**

Kisha niliona kwamba miongoni mwa vito na sarafu halisi walivyokuwa wamevitawanya kulikuwa na idadi isiyohesabika ya vito visivyo halisi na sarafu bandia. Nilikasirishwa sana na mwenendo wao mbaya na kukosa shukrani, nami niliwalaumu na kuwashutumu kwa hilo, lakini kadri nilivyoshutumu, ndivyo walivyotawanya vito visivyo halisi na sarafu bandia miongoni mwa vile halisi.**{EW 82.3}**

Kisha nilichukizwa katika nafsi yangu ya kimwili na nikaanza kutumia nguvu ya kimwili kuwasukuma nje ya chumba kile; lakini nilipokuwa nikimsukuma mmoja kutoka nje, watatu zaidi wangeingia na kuleta uchafu na takataka za mbao na mchanga na kila aina ya takataka, hadi zikafunika kila kimoja cha

vito vya kweli, almasi, na sarafu, ambavyo vyote viliondolewa machoni visionekane. Pia walikipasua vipande vipande kile kibweta changu na kukitawanya miongoni mwa takataka. Nilidhani kuwa hakuna mtu aliyejali huzuni yangu au hasira yangu. Nilikata tamaa kabisa na kuvunjika moyo, nami niliketi chini na kulia.**{EW 82.4}**

Nilipokuwa nikilia hivyo na kuomboleza kwa hasara yangu kubwa na uwajibikaji, nilimkumbuka Mungu, na kumwomba kwa bidii kwamba aniletee msaada.**{EW 83.1}**

Papo hapo mlango ulifunguka, na mtu akaingia chumbani, na watu wote wakaondoka; na Yeye, akiwa na brashi ya kusafishia uchafu mkononi mwake, alifungua madirisha, na kuanza kufagia uchafu na takataka kutoka chumbani mle.**{EW 83.2}**

Nilimpazia sauti aache, kwa maana kulikuwa na vito vya thamani vilivyotawanyika miongoni mwa takataka. Aliniambia "usiogope" kwa maana angeviangalia. **{EW 83.3}**

Ndipo, alipokuwa anafagia uchafu na takataka, vito vya uwongo na sarafu bandia, vyote viliinuka na kutoka nje ya dirisha kama wingu, na upepo ulivibeba na kuvipeleka mbali. Katika pilikapilika hii

nilifumba macho yangu kwa kitambo; nilipoyafungua, takataka zote zilikuwa zimetoweka. Vito vya thamani, almasi, sarafu za dhahabu na fedha, vilikuwa vimetulia huku vimetawanyika kwa wingi kote chumbani.**{EW 83.5}**

Kisha akakiweka kibweta kile juu ya meza, kikiwa kikubwa na kizuri zaidi ya kile cha zamani, naye alikusanya vito, almasi, sarafu, kwa mkono, na kuvitia ndani ya kibweta, hadi hakuna hata kimoja kilichoachwa, ingawa baadhi ya almasi hazikuwa kubwa kuliko ncha ya pini.**{EW 83.6}**

Kisha aliniita “njoo uone.” **{EW 83.7}**

Niliangalia ndani ya kibweta kile, lakini macho yangu yalitiwa kiwi na mandhari ile. Viling’aa kwa utukufu ulio mara kumi zaidi ya ule wa zamani. Nilidhani kuwa vilikuwa vimesuguliwa mchangani kwa miguu ya watu wale waovu ambao walikuwa wamevitawanya na kuvikanyaga mavumbini. Vilipangwa kwa mpangilio mzuri kwenye kibweta kile, kila kimoja mahali pake, bila jitihada yoyote iliyoonekana kwa Mtu yule aliyekuwa anavitupia ndani. Nilipiga kelele kwa furaha sana, na kelele ile iliniamsha.**{EW 83.8}**

SEHEMU YA PILI

## Nyongeza

### Ufafanuzi

**Wapendwa Marafiki Wakristo**: Kama ambavyo nimetoa muhtasari mfupi wa uzoefu na maoni yangu, yaliyochapishwa mnamo 1851, inaonekana kuwa ni wajibu wangu kuangalia mambo kadhaa katika kazi hiyo ndogo, na pia kutoa maoni zaidi ya hivi karibuni.**{EW 85.1}**

1. Katika ukurasa 33 yametolewa yafuatayo: "Niliona kwamba Sabato takatifu ni, na itakuwa, ukuta unaotenganisha kati ya Israeli wa Kweli wa Mungu na wasioamini; na kwamba Sabato ni suala kubwa la kuunganisha mioyo ya watakatifu wapendwa wa Mungu, wanaosubiri. Niliona kwamba Mungu ana watoto wasioiona na kuitunza Sabato. Hawajaikataa nuru inayoihusu. Na katika mwanzo wa wakati wa taabu, tulijazwa na Roho Mtakatifu kadiri tulivyosonga mbele na kuitangaza Sabato kwa ukamilifu zaidi."**{EW 85.2}**

Mtazamo huu ulitolewa mnamo mwaka 1847 wakati ambapo kulikuwa na ndugu wachache sana wa Marejeo waliokuwa wakiitunza Sabato, na katika hawa ni wachache tu walidhani kwamba utunzaji

wake ulikuwa na umuhimu wa kutosha, kuchora mstari ili kutenganisha kati ya watu wa Mungu na wasioamini. Sasa utimilizaji wa mtazamo ule unaanza kuonekana. “Kuanza kwa wakati ule wa taabu,” uliotajwa hapa hakurejelei wakati ambapo mapigo yataanza kumwagwa, bali kipindi kile kifupi mara tu kabla hayajamwagwa, wakati Kristo Yuko katika Patakatifu. Wakati huo, pale kazi ya wokovu inapofungwa, taabu itakuwa ikija duniani, na mataifa yatakasirika, lakini yatazuiwa ili yasizuie kazi ya malaika wa tatu. Wakati huo “mvua ya masika,” au kuburudishwa kutokana na uwepo wa Bwana, kutakuja, ili kuipa nguvu sauti ile kuu ya malaika wa tatu, na kuwaandaa watakatifu kusimama katika kipindi kile ambapo mapigo saba ya mwisho yatamwagwa.**{EW 85.3}**

2. Mtazamo wa "Mlango uliofunguliwa na Mlango Uliofungwa", katika ukurasa wa 42-45, ulitolewa mnamo mwaka 1849. Matumizi ya Ufunuo 3:7, 8, kuhusiana na Patakatifu pa mbinguni na huduma ya Kristo ilikuwa *mpya* kabisa kwangu. Nilikuwa sijawahi kusikia wazo hilo likitolewa na mtu yeyote yule. Sasa kadiri ambavyo mada ya Patakatifu inavyoeleweka wazi, matumizi yale yanaonekana katika nguvu na uzuri wake.**{EW 86.1}**

3. Mtazamo kwamba Bwana "alikuwa ameunyosha mkono Wake kwa mara ya pili kwa ajili ya kuwarejesha waliosalia wa watu wake," kwenye ukurasa wa 74, unarejelea tu muungano na nguvu ambazo ziliwahi kuwepo kati ya wale wanaomtafuta Kristo, na Ukweli kwamba alikuwa ameanza kuwaunganisha na kuwainua watu Wake tena. **{EW 86.2}**

4. *Udhihirisho wa Roho*. [angalia kiambatisho.] katika ukurasa 43 inasomeka kama ifuatavyo: “Niliona kwamba umizimu huko New York na maeneo mengine ulikuwa ni nguvu ya Shetani, na kwamba mambo hayo yangekuwa ya kawaida zaidi na zaidi, yakiwa yamevikwa vazi la kidini ili kuwatuliza waliodanganywa kuhusu uwepo wa usalama mkubwa na kuziteka akili za watu wa Mungu, ikiwezekana, kwa mambo hayo na kuwafanya wawe na mashaka juu ya mafundisho na nguvu za Roho Mtakatifu. Mtazamo huu ulitolewa mwaka wa 1849, karibu miaka mitano tangu wakati ule. Kisha udhihirisho wa roho uliwekwa mipaka kwenye mji wa Rochester, uliojulikana kama "Umizimu wa Rochester uliofanywa kwa ishara za kugongagonga au kubishabisha-mysterious rappings." Tangu wakati

ule uzushi umeenea zaidi ya matarajio ya mtu yeyote.**{EW 86.3}**

Mengi ya maoni kwenye ukurasa wa 59, yaliyopewa kichwa cha "Umizimu" yaliyotolewa Agosti 1850, yametimizwa, na sasa yanatimizwa. Hapa kuna sehemu yake: “Niliona kwamba punde ingechukuliwa kuwa ni kufuru kuzungumza dhidi ya umizimu, na kwamba ingeenea zaidi na zaidi, kiasi kwamba nguvu za Shetani zingeongezeka na baadhi ya wafuasi wake waliojitoa wangekuwa na uwezo wa kufanya miujiza na hata kushusha moto kutoka mbinguni mbele ya macho ya watu. Nilioneshwa kwamba kutokana na umizimu na kiinimacho waganga hawa wa kisasa bado wangeelezea kuwa sababu ya miujiza yote iliyofanywa na Bwana wetu Yesu Kristo, na kwamba wengi wangeamini kwamba kazi zote za nguvu za Mwana wa Mungu wakati akiwapo duniani zilitimizwa kwa nguvu hii hii.” (rappings and mesmerism) **{EW 86.4}**

Niliona udanganyifu wa umizimu—maendeleo ambayo ulikuwa ukifanya, na kwamba kama ingewezekana ungewadanganya wateule hasa. Shetani atakuwa na uwezo wa kuleta mbele yetu kuonekana kwa maumbo yanayodaiwa kuwa ni

jamaa zetu au marafiki ambao kwa sasa wamelala katika Yesu. Itafanywa ionekane kana kwamba marafiki hawa walikuwepo; maneno ambayo waliyatamka wakiwa hapa, ambayo tuliyazoea, yatasemwa, na toni ya sauti ile ile waliyokuwa nayo walipokuwa hai itaanguka kwenye sikio la wanadamu. Yote haya ni kwa ajili ya kuwadanganya watakatifu na kuwanasa katika kuuamini udanganyifu huu.**{EW 87.1}**

Niliona kwamba watakatifu ni lazima wapate uelewa kamili wa Ukweli wa sasa, ambao watalazimika kuudumisha kutoka katika Maandiko. Ni lazima wafahamu hali ya wafu; kwani roho za mashetani bado zitawatokea, zikidai kuwa ni marafiki zao wapendwa na jamaa, ambao watawatangazia kwamba Sabato imebadilishwa, na pia mafundisho mengine yasiyotokana na Maandiko. Watafanya yote yaliyo katika uwezo wao kuchochea huruma na watafanya miujiza mbele yao ili kuthibitisha kile wanachokitangaza. Watu wa Mungu ni lazima wawe tayari kuzipinga nguvu hizi na kusimama imara na Ukweli wa Biblia kwamba wafu hawajui neno lolote, na kwamba wao wanaoonekana kwao ni roho za mashetani. Akili zetu hazipaswi kuchukuliwa na vitu

vinavyotuzunguka, bali ni lazima zijazwe na Ukweli wa sasa na maandalizi ya kutoa sababu ya tumaini letu kwa upole na hofu. Ni lazima tutafute hekima kutoka juu ili tuweze kusimama katika siku hii ya makosa na udanganyifu.**{EW 87.2}**

Lazima tuchunguze vizuri msingi wa tumaini letu, kwa kuwa itabidi tutoe sababu kuhusu hilo kutoka katika Maandiko. Udanganyifu huu utaenea, na tutalazimika kupambana nao uso kwa uso; na isipokuwa tumejiandaa kwa hilo, tutanaswa na kushindwa. Lakini ikiwa tunafanya kile tunachoweze kwa upande wetu ili kuwa tayari kwa vita ambavyo viko mbele yetu, Mungu atafanya sehemu Yake, na mkono Wake wenye nguvu zote utatulinda. Angetuma mapema sana kila malaika kutoka katika utukufu kwa ajili ya kuwasaidia roho waaminifu, kuwazingira kwa boma, badala ya kuwaruhusu wadanganywe na kuongozwa kwenda mbali na maajabu ya uongo ya Shetani. **{EW 88.1}**

Niliona wepesi ambao kwa huo udanganyifu huu ulikuwa ukienea. Msururu wa mabehewa ya treni ulioneshwa kwangu, ukienda kwa kasi ya umeme. Malaika yule aliniambia niangalie kwa makini. Nilikaza macho yangu kwenye msafara huu. Ilionekana kwamba dunia yote ilikuwa ndani yake,

kwamba isingewezekana kuwapo hata mtu mmoja aliyebaki. Malaika alisema: “Wanafunga katika mafungu tayari kwa kuteketeza.” Kisha alinionesha mwongozaji, ambaye alionekana kuwa mtu adhimu, mwenye haki, ambaye abiria wote walimwangalia na kumheshimu sana. Nilishangazwa na kumuuliza malaika aliyeambatana nami huyu alikuwa ni nani. Alisema, “Huyu ni Shetani. Yeye ndiye kiongozi (kondakta) katika umbo la malaika mwenye nuru. Ameichukua dunia mateka. Wamekabidhiwa kwa udanganyifu wenye nguvu, kuamini uwongo, ili wapate kuangamia. Wakala huyu, anayemfuata kwa ukuu, ni mhandisi, na wengine katika mawakala wake wamewekwa kutumika katika madaraka mbalimbali kama ambavyo atawahitaji, na wote wanakwenda kwa mwendo wa umeme kufikia kuangamia kabisa.” **{EW 88.2}**

Nilimuuliza malaika kama hakuwepo mtu hata mmoja aliyebaki. Aliniambia niangalie upande mwingine, na nikaona kundi dogo wakisafiri katika njia nyembamba. Wote walionekana kuwa na umoja imara, wamefungwa pamoja kwa Ukweli, katika mafungu, au makundi. Malaika akasema, “Malaika wa tatu anawafunga, au kuwatia muhuri, kwa ajili ya kuwekwa ghalani mbinguni.” Kundi hili dogo

walionekana kuwa wamechoka kwa taabu, kana kwamba walikuwa wamepitia majaribu, migogoro na mapambano makali sana. Na ilionekana kana kwamba jua lilikuwa ndio tu limechomoza kutoka nyuma ya wingu na kuangaza nyuso zao, na kuwafanya waonekane kuwa washindi, kana kwamba ushindi wao ulikuwa karibu kupatikana.**{EW 88.3}**

Niliona kwamba Bwana ameupa ulimwengu fursa ya kuugundua mtego ule. Jambo hili moja ni ushahidi wa kutosha kwa Mkristo, kama hakukuwa na mwingine; yaani, kwamba hakuna tofauti inayowekwa kati ya vyenye thamani na visivyo na thamani. Thomas Paine, ambaye mwili wake sasa umefinyangwa kuwa mavumbi na ambaye ataitwa mwishoni mwa ile miaka elfu moja, katika ufufuo wa pili, kwa ajili ya kupokea thawabu yake na kupata mauti ya pili, anawakilishwa na Shetani kuwa yuko mbinguni, na kuinuliwa sana huko. Shetani alimtumia duniani kwa kadiri alivyoweza, na sasa anaendelea na kazi ile ile kupitia kujifanya kuwa na Thomas Paine aliyeinuliwa sana na kuheshimiwa mbinguni; kama alivyokuwa akifundisha hapa, Shetani angefanya ionekane kwamba anafundisha mbinguni. Wapo baadhi

ambao waliyatazama maisha na kifo chake kwa hofu kuu, na mafundisho yake yaliyopotoka wakati alipokuwa akiishi, lakini ambao sasa wanakubali kufundishwa naye, mmoja wa watu waovu kabisa na waliopotoka mno, ambaye alimdharau Mungu na sheria Yake. [Ili kufahamu nguvu ya maneno haya msomaji anahitajika kuelewa kwamba kazi ilichapishwa kwa kupitia njia ya “Padri C. Hammond,” iliyoitwa Hija ya Thomas Paine katika Ulimwengu wa Roho-*Pilgrimage of Thomas Paine in the Spirit World*, ambayo kwayo Paine anawakilishwa kama roho iliyotukuka katika *mbingu ya saba*. Na katika “Darasa la Uchunguzi huko New York,” ilisemekana kwamba Kristo mwenyewe alikuwa amezungumza na muaguzi na kufunua kwamba alikuwa katika *mbingu ya sita*. Tofauti itaeleweka wakati itapokumbukwa kwamba zinawakilisha roho kama zinazoendelea katika ulimwengu wa roho, na kwamba Kristo, baada ya miaka zaidi ya 1800 ya maendeleo, amefikia mbingu ya sita, wakati Paine, katika miaka 100, amefikia ya saba! Maelezo zaidi ya haya yanaweza kupatikana katika taarifa ya daktari Hare, kwamba dada yake ambaye ni roho alisema kuwa maendeleo yake yalikuwa yamepunguzwa na imani yake juu ya

upatanisho wa Kristo. Hivyo ndivyo umizimu unavyowainua makafiri na ukafiri.  Angalia pia kiambatanisho.] **{EW 89.1}**

Yeye ambaye ni baba wa uongo, anaupofusha na kuudanganya ulimwengu, kwa kuwatuma malaika zake kusema kwa niaba ya mitume, na kufanya ionekane kwamba wanapingana na yale waliyoyaandika  wakiongozwa na Roho Mtakatifu walipokuwa duniani. Malaika hawa wa uongo huwafanya mitume kupotosha mafundisho yao wenyewe na kuyatangaza kuwa yamepotoshwa. Kwa kufanya hivyo Shetani hufurahia kuwatupa wanaodai kuwa Wakristo na ulimwengu wote katika mashaka juu ya Neno la Mungu. Kitabu hicho kitakatifu kinapinga moja kwa moja njia yake na kuzuia mipango yake; kwa hiyo anawaongoza kutilia mashaka asili yake ya Kiungu. Kisha anamweka kafiri, Thomas Paine, kana kwamba aliiongozwa kuingia mbinguni wakati alipokufa, na sasa, akiungana na mitume watakatifu ambao aliwachukia duniani, walikuwa wakijihusisha katika kuufundisha ulimwengu.**{EW 90.1}**

Shetani anampa kila mmoja wa malaika wake sehemu ya kutenda. Anawaamuru wote kuwa wenye hila, stadi, na werevu. Anawaagiza baadhi

yao kuigiza nafasi ya mitume na kuzungumza kwa niaba yao, wakati ambapo wengine watapaswa kuigiza nafasi ya makafiri na watu waovu ambao walikufa wakimlaani Mungu, lakini sasa wanaonekana kuwa watu wa kidini sana. Hakuna tofauti inayowekwa kati ya mitume watakatifu mno na makafiri waovu kabisa. Wote wawili wanaoneshwa kufundisha kitu kile kile. Haidhuru ni nani Shetani anamfanya azungumze, maadam lengo lake linatimizwa. Alikuwa ameunganishwa kwa karibu sana na Paine duniani, akimsaidia katika kazi yake, kiasi kwamba ni jambo rahisi kwake kuyajua maneno yale hasa Paine aliyoyatumia na mwandiko hasa wa yule aliyemtumikia kwa uaminifu  na kutimiza makusudi yake vizuri. Shetani aliamuru mengi ya yale aliyoyaandika Paine, na ni jambo rahisi kwake kuamuru hisia kupitia kwa malaika zake sasa na kufanya ionekane kwamba yanatoka kwa Thomas Paine, ambaye, wakati alipokuwa hai, alikuwa mtumishi aliyejitoa, wa yule mwovu. Hii ndio kazi bora ya Shetani. Fundisho hili lote, linalodaiwa kuwa linatoka kwa mitume na watakatifu na watu waovu ambao wamekufa, huja moja kwa moja kutoka katika enzi yake ya kishetani.**{EW 90.2}**

Ukweli kwamba Shetani anadai kwamba yule ambaye yeye alimpenda sana, na huyo ambaye alimchukia Mungu kikamilifu, sasa yuko pamoja na mitume watakatifu na malaika katika utukufu, unapaswa kutosha kuondoa pazia kutoka katika akili zote na kuwafunulia kazi za giza, za fumbo za Shetani. Kwa kweli anauambia ulimwengu na makafiri, “Haidhuru wewe ni mwovu kiasi gani, haidhuru kama unamwamini au unamkataa Mungu au Biblia, ishi unavyopenda, mbinguni ni nyumbani kwenu; kwa kuwa wote wanajua kwamba kama Thomas Paine yuko mbinguni, na ameinuliwa kiasi kile, hakika watafika huko.” Kosa hili ni dhahiri kiasi kwamba wote wanaweza kuliona kama wanataka. Shetani sasa anatenda kupitia kwa watu kama Thomas Paine kile ambacho amekuwa akijaribu kukifanya tangu anguko lake. Yeye, kupitia katika uwezo wake na maajabu yake ya uongo, anararua msingi wa tumaini la Mkristo na kuliondoa jua lile ambalo linapaswa kuiangazia njia nyembamba ya kwenda mbinguni. Anaufanya ulimwengu uamini kwamba Biblia haijavuviwa, kwamba haina chochote zaidi ya kitabu chochote cha hadithi, huku akishikilia kitu fulani cha kuchukua nafasi yake; yaani, *udhihirisho wa umizimu!* **{EW 91.1}**

Hii ni njia iliyotengwa kabisa kwa ajili yake mwenyewe na kuwa chini ya udhibiti wake, na anaweza kuifanya dunia kuamini chochote atakacho. Kitabu kile ambacho kitamhukumu yeye pamoja na wafuasi wake anakisogeza nyuma kwenye giza au kivuli, mahali pale hasa anapotaka kiwepo. Mwokozi wa ulimwengu anamfanya kuwa si zaidi ya mtu wa kawaida; na kama walinzi wa Kirumi walioolilinda kaburi la Yesu walivyoeneza habari ya uwongo ambayo makuhani wakuu na wazee walizitia vinywani mwao, ndivyo wafuasi maskini, waliodanganywa wa udhihirisho huu wa umizimu wa kidanganyifu watarudia na kujaribu kuifanya ionekane kwamba hakuna chochote cha kimuujiza kuhusu kuzaliwa, kufa, na kufufuka kwa Mwokozi wetu. Baada ya kumweka Yesu huko nyuma, wanavuta usikivu wa ulimwengu kwao wenyewe na kwa miujiza yao na maajabu ya uongo, ambayo, wanatangaza, kuwa ni ya utukufu zaidi sana kuliko kazi za Kristo. Hivyo ulimwengu unachukuliwa katika mtego na kutulizwa kujisikia kuwa katika usalama, pasipo kugundua udanganyifu wao mbaya hadi pale mapigo saba ya mwisho yanopomiminwa. Shetani anacheka anapoona mpango wake unafanikiwa vizuri sana na

ulimwengu wote ukiwa umekamatwa kwa hila zake.**{EW 91.2}**

5. Katika ukurasa wa 55, nilieleza kwamba wingu lenye nuru tukufu lilimfunika Baba na kwamba nafsi Yake isingeweza kuonekana. Nilisema pia kwamba nilimwona Baba akiinuka kutoka kwenye kiti cha enzi. Baba alikuwa amefunikwa na mwili wa nuru na utukufu, ili kwamba nafsi Yake isiweze kuonekana; lakini bado nilijua kwamba alikuwa ni Baba na kwamba kutoka katika nafsi Yake kulitoka nuru na utukufu huu. Nilipouona mwili huu wa nuru na utukufu ukiinuka kutoka katika kiti cha enzi, nilijua ni kwa sababu Baba alikuwa amesogea, kwa hiyo nikasema, nilimwona Baba akiinuka. Utukufu, au uzuri, wa umbo Lake sikuwahi kuuona kamwe; hakuna mtu aliyeweza kuuona na kuishi; lakini bado mwili wa nuru na utukufu ulioifunika nafsi Yake ungeweza kuonekana.**{EW 92.1}**

Pia nilieleza kwamba “Shetani alionekana kuwa karibu na kiti cha enzi, akijaribu kuendelea na kazi ya Mungu.” Nitatoa sentensi nyingine kutoka ukurasa huo huo: "Niligeuka kuangalia kundi la wale ambao bado walikuwa wamesujudu mbele ya kiti cha enzi." Sasa kundi hili linalaoomba lilikuwa katika hali hii ya kufa, duniani, lakini bado

liliwakilishwa kwangu kama vile limesujudu mbele ya kiti cha enzi. Kamwe sikuwa na wazo kwamba watu hawa kwa kweli walikuwa katika Yerusalemu Mpya. Wala kamwe kufikiri kwamba mwanadamu yeyote angeweza kudhani kwamba niliamini kwamba Shetani kwa kweli alikuwa katika Yerusalemu Mpya. Lakini je, Yohana hakumwona joka mkubwa jekundu mbinguni? Hakika. "Ikaonekana ishara nyingine mbinguni; na tazama, joka kubwa jekundu, alikuwa na vichwa saba na pembe kumi." Ufunuo 12:3. Jitu la kutisha kiasi gani kuwepo mbinguni! Hapa inaonekana kuwapo nafasi nzuri ya dhihaka kama ilivyo katika tafsiri ambayo wengine wameweka juu ya kauli zangu.**{EW 92.2}**

6. Katika ukurasa wa 48-52 kuna maoni yaliyotolewa Januari, 1850. Sehemu ya maoni hayo ambayo inahusiana na fedha kuzuiwa kwa ajili ya wajumbe, ilihusika hasa na wakati ule. Tangu wakati huo, marafiki wa kazi ya Ukweli wa sasa wameinuliwa, ambao wameusubiri wakati wa kufaa kufanya mema kwa fedha zao. Wengine wametoa kwa ukarimu mno, kwa madhara ya wapokeaji. Kwa takriban miaka miwili nimeoneshwa mengi zaidi kuhusiana na matumizi ya ovyo na huru ya pesa za Bwana, kuliko kukosekana kwake (ubaradhifu

unaharibu mambo kuliko umasikini).**{EW 93.1}**

Ifuatayo ni kutoka katika maono yaliyotolewa huko Jackson, Michigan, Juni 2, 1853. Ilihusiana sana na ndugu walioko pale: “Niliona kwamba ndugu walianza kutoa sadaka mali yao na kuitoa bila kuwa na lengo la kweli lililowekwa mbele yao-kazi inayoumia -nao waliitoa kwa uhuru sana, kiasi kingi mno, na mara nyingi mno. Niliona kwamba walimu walipaswa kusimama mahali pa kusahihisha kosa hili na kuweka mvuto mzuri kanisani. Fedha imefanywa kuwa isiyo na/au umuhimu kidogo, ya kutolewa mapema iwezekanavyo. Mfano mbaya umewekwa na baadhi katika kukubali michango mikubwa bila kutoa onyo hata kidogo kwa wale ambao wana fedha kutokuitumia kwa uhuru na bila hadhari. Kwa kukubali fedha nyingi kiasi hicho, bila kuhoji kama Mungu alikuwa amelifanya kuwa wajibu wa ndugu huyo kutoa kiasi kikubwa hivyo, utoaji wa fedha nyingi sana umeruhusiwa.**{EW 93.2}**

“Wale ambao walitoa pia walikosea, kwa kukosa kuwa na uangalifu wa kuhoji juu ya mahitaji ya jambo hilo, ikiwa kulikuwa na haja halisi au la. Wale waliokuwa na fedha walitupwa katika mkanganyiko mkubwa. Ndugu mmoja aliumia sana kwa sababu

ya fedha nyingi kuwekwa mikononi mwake. Hakujifunza matumizi yenye kupunguza gharama, lakini aliishi kwa ubadhirifu, na katika safari zake aliweka fedha hapa na pale bila faida yoyote. Alieneza mvuto mbaya kwa kufanya matumizi huru ya namana hiyo ya fedha za Bwana, na angesema moyoni mwake, na kwa wengine, 'Kuna fedha za kutosha katika J—, nyingi zaidi ya zinazoweza kutumika kabla Bwana hajaja.' baadhi walidhurika sana na mwelekeo kama huo na wakaingia katika Ukweli wakiwa na maoni yasiyo sahihi, bila kutambua kwamba ilikuwa ni fedha ya Bwana waliyokuwa wakiitumia bila kuhisi thamani yake. Wale roho maskini ambao ndio tu wameukubali ujumbe wa malaika wa tatu na kuwa na mfano kama huo ukiwekwa mbele yao watakuwa na mengi ya kujifunza kuhusu kujikana nafsi na kuteseka kwa ajili ya Kristo. Watalazimika kujifunza kuachana na raha, na maisha bwerere, kuacha kujishughulisha na hali inayofaa na starehe yao, na kuzingatia thamani ya roho. Wale ambao wanahisi "ole" juu yao hawatajitoa kwa ajili ya kufanya maandalizi mazuri ya kusafiri kwa raha na starehe. Baadhi ambao hawana wito wametiwa moyo kuingia shambani. Wengine wameathiriwa na mambo haya

na hawajahisi haja ya matumizi ya kupunguza gharama, ya kujikana nafsi, na kuweka katika hazina ya Bwana. Wangehisi na kusema, 'Kuna wengine ambao wana fedha ya kutosha; watatoa kwa ajili ya makala. Sihitajiki kufanya chochote. Makala hii itafadhiliwa bila msaada wangu." **{EW 93.3}**

Haijawa jaribio dogo kwangu kuona kwamba baadhi wamechukua sehemu hiyo ya maoni yangu ambayo ilihusiana na kutoa sadaka mali ili kutegemeza kazi na kufanya matumizi mabaya ya hiyo; wanatumia fedha kwa ubadhirifu, huku wakipuuza kutekeleza kanuni za sehemu zingine. Katika ukurasa wa 50, soma yafuatayo: "Niliona kwamba kazi ya Mungu ilikuwa imezuiliwa na kufedheheshwa na baadhi waliokuwa wanasafiri ambao hawakuwa na ujumbe kutoka kwa Mungu. Watu kama hao watalazimika kutoa hesabu kwa Mungu kwa kila dola ambayo wameitumia katika kusafiri mahali ambapo haikuwa wajibu wao kwenda, kwa sababu fedha hizo zingeweza kusaidia katika kazi ya Mungu." Pia, ukurasa 50: "Niliona kwamba wale ambao wana nguvu ya kufanya kazi kwa mikono yao na kusaidia kutegemeza kazi hii, waliwajibika kwa nguvu zao kama wengine

walivyowajibika kwa mali zao."**{EW 94.1}**

Napenda kuvuta usikivu hapa wa pakee kuhusiana na mtazamo wa mada hii inayotolewa katika ukurasa wa 57. Hapa kuna dondoo fupi: "Lengo la maneno ya Mwokozi wetu [katika Luka 12:33] halijawasilishwa wazi-wazi." Niliona kwamba "lengo la kuuza si kuwapa wale ambao wanaweza kufanya kazi na kujikimu wenyewe, bali ni kueneza Ukweli. Ni dhambi kuwasaidia na hivyo kuwaingiza katika uvivu wale ambao wanaweza kufanya kazi. Baadhi wamekuwa na bidii kuhudhuria mikutano yote, si kwa ajili ya kumtukuza Mungu, bali ni kwaajili ya "mikate na samaki." Watu kama hao ingekuwa bora zaidi kama wangekuwa nyumbani wakifanya kazi kwa mikono yao, "jambo ambalo ni jema," wakitoa mahitaji ya familia zao na kuwa na kitu cha kutoa ili kutegemeza kazi ile ya thamani." Imekuwa ni mpango wa Shetani katika nyakati zilizopita kuwasukuma baadhi kwa roho ya haraka kutumia fedha kwa uhuru, na kuwashawishi ndugu kutoa fedha zao kwa pupa, ili kwamba kupitia katika wingi wa fedha zinazotupwa bila tahadhari, kizembe na kwa haraka, roho zipate kudhurika na kupotea, na kwamba sasa, wakati ambapo Ukweli unapaswa kuenezwa sana, uhitaji uweze kuonekana. Kusudi

Lake, kwa kiwango fulani, limetimizwa. **{EW 95.1}**

Bwana ameonesha makosa ya wengi katika kuwaangalia wale tu ambao wana mali ili kusaidia uchapishaji wa makala na vijitabu. Wote wanapaswa kutimiza wajibu wao. Wale ambao wana nguvu ya kufanya kazi kwa mikono yao, na kupata fedha za kusaidia kuendeleza kazi hii, wanawajibika kwa hilo kama wengine wanavyowajibika kwa mali zao. Kila mtoto wa Mungu anayekiri kuuamini Ukweli wa sasa, anapaswa kuwa na ari ya kutenda sehemu yake katika kusudi hili.**{EW 95.2}**

Mnamo Julai, 1853, niliona kwamba haikuwa kama ilivyopaswa kuwa kwamba gazeti, linalomilikiwa na kuidhinishwa na Mungu, lingetoka kwa nadra kiasi hicho. Kusudi, katika wakati huu ambao tunaishi, linahitaji gazeti hili kila juma, [*Review and Herald* kabla ya wakati huu lilikuwa likichapishwa pasipo utaratibu kabisa na sasa lilikuwa likitolewa mara moja kwa miezi miwili.] Na uchapishaji wa vijitabu vingi zaidi za kufunua makosa yanayoongezeka ya wakati huu; lakini kazi hii inakawilishwa kwa kukosa fedha. Niliona kwamba Ukweli ni lazima uende na kwamba hatupaswi kuwa na hofu sana, kwamba vijitabu na

gazeti ni bora viende kwa watatu ambapo havihitajiki kuliko kuwa na mtu mmoja aliyenyimwa ambaye anazithamini na angeweza kufaidika nazo. Niliona kwamba ishara za siku za mwisho zinapaswa kuwekwa wazi, kwa kuwa maonesho ya Shetani yanaongezeka. Machapisho ya Shetani na mawakala wake yanaongezeka, na nguvu zake zinakua, na kile tunachokifanya ili kufikisha Ukweli kwa watu wengine inabidi kifanyike kwa haraka.**{EW 95.3}**

Nilioneshwa kwamba Ukweli ukisha kuchapishwa sasa, utasimama, kwa kuwa ni Ukweli wa siku za mwisho; utaishi, na machache tu yanapaswa kusemwa kuhusiana na siku za baadaye. Maneno mengi yasiyo na idadi hayahitajiki kuwekwa katika makala hii kuhalalisha kile kinachojieleza chenyewe na kuangaza kwa uwazi wake. Ukweli ni mnyofu, rahisi, dhahiri, nao unajitokeza kwa ujasiri na kujitetea wenyewe; lakini makosa hayako hivyo. Huwa yanapinda na kujisokota kiasi kwamba inahitajika maneno mengi kuweza kulielezea katika umbo lake hilo la kupindapinda. Niliona kwamba nuru yote waliyokuwa wameipokea katika maeneo fulani ilikuwa imetoka kwenye gazeti lile; kwamba roho

zilipokea Ukweli kwa njia hii, na kisha kuuzungumza kwa wengine; na kwamba sasa katika maeneo yale ambapo kuna watu kadhaa, hao waliinuliwa na mjumbe huyu wa kimya. Ndiye peke yake aliyekuwa mhubiri wao. Kazi ya kupeleka Ukweli haipaswi kuzuiwa katika maendeleo yake ya kusonga mbele kwa sababu ya ukosefu wa fedha.**{EW 96.1}**

## Sura ya 21 ---Utaratibu wa Injili (Gospel Order)-Waliogopa kuwa Taasisi

Bwana ameonesha kwamba utaratibu wa injili umeogopwa na kupuuzwa mno. [Waadventista walikuwa ni wa makanisa yote, na mwanzoni hawakuwa na wazo la kuunda kanisa lingine. Baada ya 1844 kulikuwa na machafuko makubwa, na walio wengi walipinga kwa nguvu kuunda taasisi ya kidini na mfumo wowote, wakishikilia kwamba mfumo wowote ulikuwa ni kinyume na uhuru kamili wa injili. Ushuhuda na kazi za Ellen White daima zimekuwa kinyume na ushupavu wa kidini, na katika maagizo yaliyotolewa kupitia kwake, mfumo kwa namna fulani ulisisitizwa mapema, kuwa muhimu, katika kuzuia machafuko.] Urasimu unapaswa kuepukwa; lakini, katika kufanya hivyo, utaratibu haupaswi

kupuuzwa. Kuna utaratibu mbinguni. Kulikuwa na utaratibu katika kanisa Kristo alipokuwapo duniani, na baada ya kuondoka Kwake utaratibu huo ulizingatiwa kabisa miongoni mwa mitume Wake. Na sasa katika siku hizi za mwisho, wakati Mungu anapowaleta watoto wake katika umoja wa imani, kuna haja kubwa ya utaratibu kuliko ilivyowahi kuwa hapo awali; kwa maana, wakati Mungu anapowaunganisha watoto Wake, Shetani na malaika zake waovu wanashughulika sana kuuzuia umoja huu na kuuharibu. Kwa hivyo watu wanaharakisha kwenda shambani mwa Bwana, ambao hawana hekima na busara, huenda wasiotawala vyema nyumba zao wenyewe, na wasiokuwa na utaratibu au utawala kwa wachache wale ambao Mungu amewapa wajibu juu yao nyumbani; lakini bado wanahisi kuwa wana uwezo wa kulisimamia kundi. Wanapiga hatua nyingi zisizo sahihi, na wale wasioifahamu imani yetu wanawahukumu wajumbe wote kuwa kama watu hawa waliojituma wenyewe. Hivyo kazi ya Mungu inashutumiwa, na Ukweli kuepukwa na wengi wasioamini ambao vinginevyo wangekuwa wanyofu na kuuliza kwa shauku, je, mambo haya ndivyo yalivyo?**{EW 97.1}**

Watu ambao maisha yao si matakatifu na ambao hawana sifa za kufundisha Ukweli wa sasa wanaingia shambani bila kuthibitishwa na kanisa au ndugu kwa ujumla, na machafuko na mfarakano ndio matokeo. Baadhi wana nadharia fulani kuhusu Ukweli, na wanaweza kuwasilisha hoja, lakini hawana hali ya kiroho, busara, na uzoefu; wanashindwa katika mambo mengi ambayo ni muhimu sana kwao kuyaelewa kabla ya kufundisha Ukweli. Wengine hawana uwezo huo wa kutoa hoja, lakini kwa sababu ndugu wachache huwasikia wakiomba vizuri na kutoa ushauri wa kufurahisha mara kwa mara, wanashinikizwa kwenda shambani, kujihusisha katika kazi ambayo Mungu hajawapa uwezo na ambayo kwayo hawana uzoefu na busara ya kutosha. Kiburi cha kiroho huja, wanajiinua, na kutenda chini ya udanganyifu wa kufikiri kuwa wao ni watenda kazi. Hawajitambui wenyewe. Hawana busara na fikira za subira, wanazungumza kwa majivuno juu yao wenyewe, na wanasema mambo mengi ambayo hawawezi kuyathibitisha kutoka katika Neno. Mungu analijua hili; kwa hiyo hawaiti watu kama hao kufanya kazi katika nyakati hizi za hatari, na ndugu wanapaswa kuwa waangalifu wasiwasukume kwenda shambani wale ambao

Yeye hajawaita.**{EW 97.2}**

Wale watu ambao hawajaitwa na Mungu kwa ujumla ndio wale hasa ambao wanajiamini mno kwamba wameitwa hivyo na kwamba kazi zao ni muhimu sana. Wanakwenda shambani na kwa ujumla hawaweki mvuto mzuri; lakini bado katika maeneo mengine wana kipimo fulani cha mafanikio, na hii huwaongoza wao na wengine kufikiri kwamba hakika wameitwa na Mungu. Si ushahidi wa hakika kwamba wanadamu wameitwa na Mungu kwa sababu wana mafanikio fulani; kwa kuwa malaika wa Mungu sasa wanagusa mioyo ya watoto Wake waaminifu ili kuelimisha ufahamu wao kwa Ukweli wa sasa, ili wapate kuushikilia na kuishi. Na hata kama watu wanaojituma wenyewe watajiweka mahali ambapo Mungu hajawaweka, na kukiri kuwa ni walimu, na roho kupokea Ukweli kwa kuwasikia wakiuzungmzia, huu si ushahidi kwamba wameitwa na Mungu. Roho zinazopokea Ukweli kutoka kwao huupokea ili zipate kuletwa katika majaribu na utumwa, na baadaye wanapogundua kwamba watu hawa hawakuwa wamesimama katika shauri la Mungu. Hata wale watu waovu wanapozungumza Ukweli, baadhi ya watu wanaweza kuupokea; lakini hauwaletei wale ambao waliuzungumza katika

namna yoyote ya kuungwa mkono zaidi na Mungu. Watu waovu bado ni waovu tu, na kulingana na udanganyifu walioutenda juu ya wale ambao walikuwa ni wapendwa wa Mungu, na kulingana na machafuko yaliyoletwa kanisani, ndivyo adhabu yao itakavyokuwa; dhambi zao hazidumu zimefunikwa, bali zitafichuliwa katika siku ile ya hasira kali ya Mungu.**{EW 98.1}**

Hawa wajumbe waliojituma wenyewe ni laana katika kazi. Roho aminifu huweka tumaini kwao, wakidhani kwamba wanatembea katika ushauri wa Mungu na kwamba wako katika muungano na kanisa, na hivyo huwaruhusu kusimamia ibada, na, kadri wajibu unavyowekwa wazi kwamba lazima wafanye kazi zao za kwanza, huwaruhusu kubatizwa nao. Lakini nuru inapokuja, kama itakavyokuwa hakika, na wanajua kwamba watu hawa hawako vile walivyowaelewa kuwa , wajumbe wa Mungu walioitwa na wateule, wanatupwa katika majaribu na mashaka juu ya Ukweli ambao wamepokea na kuhisi kwamba lazima wajifunze tena; wanasumbuliwa na kufadhaishwa na adui kuhusu uzoefu wao wote, kama Mungu amewaongoza au la, na hawaridhiki hadi watakapobatizwa tena na kuanza upya.  Roho za

wajumbe wa Mungu zinachoshwa zaidi sana kwenda mahali ambapo wale ambao wametumia mvuto huu mbaya kuliko kuingia katika nyanja mpya. Watumishi wa Mungu wanapaswa kushughulika kwa wazi, kutenda wazi, na kutoficha makosa; kwa kuwa wamesimama kati ya walio hai na wafu na hivyo ni lazima watoe hesabu ya uaminifu wao, utume wao, na mvuto wanaotoa kwa kundi ambalo Bwana amewafanya kuwa waangalizi.**{EW 99.1}**

Wale wanaoupokea Ukweli na kuletwa katika majaribu kama hayo bado wangeweza kuupata ukweli kama watu hawa wangekaa mbali na kujaza nafasi za chini ambazo Bwana aliwapangia. Jicho la Mungu lilikuwa juu ya vito Vyake vya thamani, na Yeye angewaelekeza kwenda kwao wajumbe Wake walioitwa na kuteuliwa—watu ambao wangesonga mbele kwa ufahamu. Nuru ya Ukweli ingewaonesha na kuwafunulia roho hizi nafasi yao halisi, nao wangeupokea Ukweli kwa ufahamu na kuridhishwa na uzuri na uwazi wake. Na kadiri walivyohisi matokeo yake yenye nguvu, wangeweza kuwa na nguvu na kueneza mvuto mtakatifu.**{EW 99.2}**

Tena, nilionyeshwa hatari ya wale wanaosafiri ambao Mungu hakuwaita. Ikiwa wana mafanikio

fulani, sifa ambazo zinapungua zitaonekana. Hatua ambazo si za busara zitafanywa, na kwa ukosefu wa hekima roho zingine za thamani zinaweza kuendeshwa kwenda mahali ambapo hazitaweza kufikiwa kamwe. Niliona kwamba kanisa linapaswa kuhisi wajibu wake na linapaswa kuangalia kwa makini na kwa shauku katika maisha, sifa, na mwenendo wa jumla wa wale wanaokiri kuwa walimu. Ikiwa ushahidi usio na shaka hautolewi kwamba Mungu amewaita, na kwamba "ole" itakuwa juu yao ikiwa hawatautii wito huu, ni wajibu wa kanisa kutenda na kufanya ijulikane kwamba watu hawa hawatambuliwi kama walimu na kanisa. Huu ndiyo mwelekeo pekee ambao kanisa linaweza kuchukua ili kuwa wazi katika suala hili, kwa kuwa mzigo uko juu yao.**{EW 100.1}**

Niliona kwamba mlango huu ambao adui anautumia kungia kulifadhaisha na kulisumbua kundi, unaweza kufungwa. Nilimuuliza malaika jinsi gani ungeweza kufungwa. Alisema, “Kanisa lazima likimbilie katika Neno la Mungu na kuwa imara, kwa kusimikwa katika utaratibu wa injili, ambao umeachwa bila kutiliwa maanani na kupuuzwa.” Hii ina umuhimu wa lazima ili kulileta kanisa katika umoja wa imani. Niliona kwamba katika siku za

mitume kanisa lilikuwa katika hatari ya kudanganywa na kulazimishwa na walimu wa uongo. Kwa hiyo ndugu walichagua watu ambao walikuwa wametoa ushahidi mzuri kwamba walikuwa na uwezo wa kutawala vizuri nyumba zao na kuhifadhi utaratibu katika familia zao wenyewe, na ambao wangeweza kuwaelimisha wale waliokuwa gizani. Mungu aliulizwa kuhusu hawa, na kisha, kulingana na mawazo ya kanisa na Roho Mtakatifu, walitengwa kwa kuwekewa mikono. Wakiwa wamepokea utume wao kutoka kwa Mungu na kuwa na idhini ya kanisa, walisonga mbele wakibatiza kwa Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, na kusimamia ibada za nyumba ya Bwana, mara nyingi wakiwahudumia watakatifu kwa kuwapa ishara za mwili uliovunjwa na damu iliyomwagwa ya Mwokozi aliyesulubiwa, ili kudumisha kuwa na upya katika kumbukumbu ya watoto wapendwa wa Mungu mateso na kifo Chake.**{EW 100.2}**

Niliona kwamba sasa hatuko salama zaidi kutokana na walimu wa uongo kuliko walivyokuwa wakati wa mitume; na, ikiwa hatufanyi zaidi, tunapaswa kuchukua hatua maalum kama walivyofanya ili kupata amani, upatanifu, na umoja

wa kundi. Tunao mfano wao, na tunapaswa kuufuata.  Ndugu wenye uzoefu na wenye akili timamu wanapaswa kukusanyika, na kwa kufuata Neno la Mungu na kibali cha Roho Mtakatifu, wanapaswa, kwa maombi ya bidii, kuweka mikono juu ya wale ambao wametoa uthibitisho kamili kwamba wamepokea agizo lao kutoka kwa Mungu, na kuwatenga kando, ili wapate kujitoa kabisa kwa kazi Yake. Tendo hili lingeonesha kibali cha kanisa kwa ajili ya kusonga kwao mbele kama wajumbe kubeba ujumbe makini kabisa uliowahi kutolewa kwa wanadamu.**{EW 100.2}**

Mungu hatakabidhi utunzaji wa kundi Lake la thamani kwa watu ambao akili na utambuzi vimedhoofishwa kwa makosa ya zamani ambayo wameyahifadhi kwa upendo na kuyathamini, kama kile kinachoitwa nadharia ya ukamilifu (perfectiniosim) [angalia kiambatisho.] na Umizimu, na ambao, kwa mwelekeo wao wakati wakiwa katika makosa haya, wamejidhalilisha na kuleta lawama juu ya kazi ya  ukweli. Ingawa kwa sasa wanaweza kujisikia huru kutokana na makosa na kuwa na uwezo wa kusonga mbele na kufundisha ujumbe huu wa mwisho, Mungu hatawakubali. Yeye Hatazikabidhi roho za thamani katika uangalizi wao;

kwa maana hukumu yao ilipotoshwa wakati walipokuwa katika makosa, na sasa imedhoofika. Yeye aliye mkuu na mtakatifu ni Mungu Mwenye wivu, Naye atawakubali watu watakatifu kuubeba Ukweli Wake. Sheria takatifu iliyonenwa na Mungu kutoka Sinai ni sehemu Yake Yeye mwenyewe, na watu watakatifu ambao wanaitunza hasa peke yao ndio watakaomheshimu kwa kuifundisha kwa wengine.**{EW 101.1}**

Watumishi wa Mungu ambao wanafundisha Ukweli wanapaswa kuwa watu wenye busara. Wanapaswa kuwa watu ambao wanaweza kuvumilia upinzani na wala hawasisimki (mihemko isipitilize); kwa kuwa wale wanaoupinga Ukweli watawaonea wale wanaoufundisha, na kila kipingamizi kinachoweza kutolewa, kitaletwa katika namna yake iliyo mbaya mno dhidi ya Ukweli. Watumishi wa Mungu wanaoubeba ujumbe ni lazima wawe tayari kuviondoa vipingamizi hivi, kwa utulivu na upole, kwa nuru ya Ukweli. Mara nyingi wapinzani huzungumza na wahudumu wa Mungu kwa namna ya kukasirisha, ili kutaka kutoka kwao kitu kama hicho hicho, ili waweze kukitumia kwa kadiri iwezekanavyo na kuwatangazia wengine kwamba walimu wa amri wana roho ya ukali na ni

wakatili, kama ambavyo imeripotiwa. Niliona kwamba ni lazima tujiandae kwa vipingamizi, na kwa uvumilivu, busara, na upole, hebu viwe na uzito unaozistahili, si kuvitupilia mbali au kuviondoa kwa madai dhahiri, na hivyo kumlemea anayepinga, na kudhihirisha roho ngumu kwake; bali vipe vipingamizi uzito wake, kisha ulete nuru na nguvu ya Ukweli, na iache iwe na uzito zaidi na kuyaondoa makosa. Hivyo mawazo mazuri yatatengenezwa, na wapinzani waaminifu watakiri kwamba walikuwa wamedanganywa na kwamba watunzaji wa amri si vile ambavyo wamewasilishwa kuwa.**{EW 102.1}**

Wale wanaokiri kuwa watumishi wa Mungu aliye hai ni lazima wawe tayari kuwa watumishi wa wote, badala ya kuinuliwa juu ya ndugu, na ni lazima wawe na roho ya ukarimu na ya heshima. Ikiwa watakosea, wanapaswa kuwa tayari kukiri na kuungama kabisa. Uaminifu wa dhamira hauwezi kusimama kama udhuru wa kutokukiri makosa. Ungamo hauwezi kupunguza imani ya kanisa kwa mjumbe, na angeweza kuweka mfano mzuri; roho ya kuungama inapaswa kutiwa moyo kanisani, na muungano mtamu ungekuwa ndio matokeo yake. Wale wanaodai kuwa walimu wanapaswa kuwa mifano ya uchaji Mungu, upole, na unyenyekevu,

wenye roho ya ukarimu, ili kuvuta roho kwa Yesu na Ukweli wa Biblia. Mhudumu wa Kristo anapaswa kuwa safi katika mazungumzo na katika matendo. Anapaswa kukumbuka daima kwamba anashughulikia Maneno ya uvuvio, Maneno ya Mungu mtakatifu. Ni lazima pia akumbuke kwamba kundi limekabidhiwa kwa ajili ya uangalizi wake, na kwamba anapaswa kupeleka kesi zao kwa Yesu, na kusihi kama Yesu anavyotuombea kwa Baba. Nilielekezwa nyuma kwa wana wa Israeli zamani na kuona jinsi wahudumu wa Patakatifu walivyokuwa wasafi na watakatifu, kwa sababu waliletwa na kazi yao katika uhusiano wa karibu na Mungu. Wale wanaohudumu ni lazima wawe watakatifu, wasafi, na wasio na waa, ama sivyo Mungu atawaangamiza. Mungu hajabadilika. Yeye ni mtakatifu na msafi, na ni mahsusi (anabainisha), kama alivyokuwa daima. Wale wanaodai kuwa wahudumu wa Yesu wanapaswa kuwa watu wenye uzoefu na uchaji Mungu wa kina, na ndipo nyakati zote na mahali popote wanaweza kutoa mvuto mtakatifu.**{EW 102.2}**

Nimeona kuwa sasa ni wakati wa wajumbe kuondoka katika makao yao wakati wowote panapo nafasi, na kwamba Mungu atawatangulia na

kufungua mioyo ya wengine kusikia. Sehemu mpya lazima ziingiwe, na, popote hili linapofanywa, itakuwa vizuri, ikiwa ni sawa, kwenda watu wawili wawili, ili kuinuana mikono kila mtu na mwenzake. Mpango kama huu uliwasilishwa: Ingekuwa vizuri kwa ndugu wawili kuanza pamoja na kusafiri pamoja kwenda katika sehemu zenye giza mno, ambapo kuna upinzani mwingi na ambapo kazi kubwa kabisa inahitajika, na kwa juhudi za pamoja na imani thabiti kuweka Ukweli mbele ya wale walio gizani. Na ndipo, kama wangeweza kutimiza zaidi kwa kutembelea maeneo mengi, waende kila mtu peke yake, lakini wakutane mara kwa mara, wanapokuwa katika ziara hiyo, ili wapate kutiana moyo kwa imani yao, na kwa jinsi hiyo kuimarishana na kuinuana mikono kila mmoja na mwenzake. Pia, hebu na wazungumze juu ya maeneo yaliyofunguliwa kwa ajili yao, na waamue ni karama gani kati ya karama walizo nazo itahitajika zaidi, na ni kwa njia gani wanaweza kufanikiwa zaidi katika kufikia moyo. Kisha wanapotengana tena ujasiri na nguvu zao zitafanywa upya kuweza kukabiliana na upinzani na giza, na kufanya kazi kwa mioyo inayohisi upendo, ili kuokoa roho zinazoangamia.**{EW 103.1}**

Niliona kwamba watumishi wa Mungu hawapaswi kwenda katika eneo lile lile tena na tena kufanya kazi, bali wanapaswa kutafuta roho katika maeneo mapya. Wale ambao tayari wamekwisha kuimarika katika Ukweli hawapaswi kuhitaji sana kazi yao; kwa kuwa wanapaswa kuwa na uwezo wa kusimama peke yao, na kuwaimarisha wengine wanaowazunguka, wakati wajumbe wa Mungu wakitembelea maeneo ya giza na ya upweke, wakiweka Ukweli mbele ya wale ambao kwa sasa hawajaelimishwa kuhusu Ukweli wa sasa.**{EW 104.1}**

*****

## Sura ya 22-Matatizo ya Kanisa

[Kutoka katika *Review and Herald*, Agosti 11, 1853].

**Wapendwa Kaka na Dada**: Kadiri makosa yanavyoendelea kwa haraka, tunapaswa kujitahidi kuwa macho katika kazi ya Mungu, na kuutambua wakati tunaoishi. Giza litaifunika dunia, na giza nene mno juu ya watu. Na inapokuwa kwamba

karibu wote wanaotuzunguka wanafunikwa katika giza nene la makosa na udanganyifu, itafaa kwetu sisi kuondoa ujinga na kuishi karibu na Mungu, ambapo tutaweza kuakisi miale ya Kiungu ya nuru na utukufu kutoka usoni pa Yesu. Kadiri giza linavyozidi kuwa nene na makosa kuongezeka, tunapaswa kupata ujuzi mkamilifu zaidi wa Ukweli na kuwa tayari kudumisha msimamo wetu kutoka katika Maandiko.**{EW 104.2}**

Ni lazima tutakaswe kupitia katika Kweli, tujiweke wakfu kabisa kwa Mungu, na hivyo kuishi kulingana na ungamo letu takatifu ili Bwana aweze kutoa nuru inayoongezeka juu yetu, na ili tuweze kuona nuru katika nuru Yake, na kuimarishwa na nguvu Zake. Kila wakati tusiokuwa macho tunakuwa katika uwezekano wa kuzingirwa na kushambuliwa na adui na tunakuwa katika hatari kubwa ya kushindwa na nguvu za giza. Shetani anawaagiza malaika zake kuwa macho na kuwaangusha wote wanaoweza kuwaangusha; kujua ukaidi na dhambi zinazowazinga wale wanaoukiri Ukweli, na kutupa giza kuwazunguka, ili wapate kukoma kuwa waangalifu, wachukue mwelekeo ambao utaifedhehesha kazi wanayodai kuipenda, na kuleta huzuni kwa kanisa. Roho za hawa waliopotoka,

wasiokesha zinakua na giza zaidi, na nuru ya mbinguni inafifia kutoka kwao. Hawawezi kuzigundua dhambi zile zinazowazinga, na Shetani anazungusha wavu wake kuwazunguka, nao wananaswa katika mtego wake.**{EW 105.1}**

Mungu Ndiye nguvu yetu. Ni lazima tumtazame kwa ajili ya hekima, mwongozo na uongozi, na kuuzingatia utukufu Wake, mema ya kanisa, na wokovu wa roho zetu wenyewe, lazima tuzishinde dhambi zile zinazotuzinga. Tunapaswa kila mtu binafsi kujitahidi kupata ushindi mpya kila siku. Ni lazima tujifunze kusimama kila mtu peke yake na kumtegemea Mungu kabisa. Ni bora kwetu kujifunza hili mapema iwezekanavyo. Hebu kila mtu na atambue mahali pale anaposhindwa, kisha kwa uaminifu aangalie kwamba dhambi zake hazitamwangusha, bali atapata ushindi juu yake. Hapo ndipo tunaweza kuwa na ujasiri kwa Mungu, na kanisa litaokolewa kutoka katika matatizo makubwa.**{EW 105.2}**

Wajumbe wa Mungu, wanapotoka nyumbani kwao kwa ajili ya kufanya kazi kwa ajili ya wokovu wa roho, wanatumia muda wao mwingi sana katika kufanya kazi kwa ajili ya wale ambao wamekuwa katika Ukweli kwa miaka mingi, lakini ambao bado

ni dhaifu, kwa sababu wanalegeza hatamu pasipo lazima, wanaacha kujilinda wenyewe, na, wakati mwingine nadhani, wanamjaribu adui ili apate kuwajaribu. Wanaingia katika shida fulani ndogo na jaribu, na muda wa watumishi wa Bwana unatumika katika kuwatembelea. Wanashikiliwa kwa saa nyingi na hata kwa siku kadhaa, na roho zao zinahuzunika na kujeruhiwa kwa kusikia shida ndogo ndogo na majaribu yakizungumzwa, kila mmoja akikuza malalamiko yake mwenyewe ili kuyafanya yaonekane kuwa mazito kadiri iwezekanavyo, kwa hofu kwamba watumishi wa Mungu watayafikiria kuwa madogo mno kuweza kuonekana. Badala ya kuwategemea watumishi wa Bwana kuwasaidia kutoka katika majaribu haya, wanapaswa kuanguka mbele za Mungu na kufunga na kuomba hadi majaribu hayo yameondolewa.**{EW 105.3}**

Wengine wanaonekana kufikiria kwamba kazi pekee ambayo Mungu amewaita wajumbe kuingia shambani, ni kuwaendea pale wananapoagiza kuwabeba mikononi mwao; na kwamba sehemu muhimu zaidi ya kazi yao ni kutatua majaribu na shida ndogo ndogo ambazo wamejiletea wao wenyewe kwa kuchukua hatua ambazo si za busara, na kwa kumpa adui njia, na kuendekeza roho

isiyokubali kushindwa, yenye kutafuta makosa kwa wale wanaowazunguka. Lakini yuko wapi kondoo mwenye njaa wakati huu? Anakuwa mwenye njaa kali kwaajili ya mkate wa uzima. Wale ambao wanaujua Ukweli nao wamethibitishwa ndani yake, lakini hawautii—ikiwa wangeutii, wangeokolewa katika majaribu haya mengi—yanayowashikilia wajumbe, na kusudi hasa la Mungu kuwaita shambani halijatimizwa. Watumishi wa Mungu wanahuzunishwa na ujasiri wao kuchukuliwa kutoka kanisani na mambo kama hayo, wakati ambapo yote walipaswa kujitahidi kufanya ni kutokuongeza hata uzito wa unyoya katika mzigo wao, bali kwa maneno ya kutia matumaini, na maombi ya imani, wanapaswa kuwasaidia. Je, wangekuwa huru zaidi kiasi gani ikiwa wote wanaoukiri Ukweli wangetazama kuwazunguka na kujaribu kuwasaidia wengine, badala ya kudai msaada mwingi kwao wenyewe. Kama ilivyo, watumishi wa Mungu wanapoingia mahali pa giza, ambapo Ukweli bado haujatangazwa, wanakuwa na roho iliyojeruhiwa iliyosababishwa na majaribu yasiyo ya lazima ya ndugu zao. Zaidi ya haya yote, ni lazima wakutane na kutokuamini na chuki ya wapinzani na kukanyagwa na baadhi yao.**{EW 106.1}**

Ingekuwa rahisi kiasi gani kuathiri moyo na ni kiasi gani Mungu angetukuzwa ikiwa watumishi Wake wangekuwa huru kutokana na kuvunjika moyo na jaribu, ili waweze kwa roho iliyo huru kuwasilisha Ukweli katika uzuri wake. Wale ambao wamekuwa na hatia ya kuhitaji sana utendaji kazi wa watumishi wa Mungu na kuwalemea kwa majaribu na matatizo ambayo ni wao wenyewe walipaswa kuyashughulikia, watalazimika kutoa hesabu kwa Mungu kwa ajili ya muda wote na fedha ambazo zimetumika katika kujifurahisha wao wenyewe, na hivyo kumridhisha adui. Walipaswa kuwa katika hali ya kuwasaidia ndugu zao. Hawakupaswa kamwe kukubali kushindwa na majaribio na shida zao ili kulemea mkutano mzima, au kungojea hadi baadhi ya wajumbe wamekuja ili kuyasuluhisha; bali wanapaswa kuwa sawa mbele za Mungu wao wenyewe, wafanye majaribu yao kuondolewa kabisa, na kuwa tayari pale wafanyakazi wanapokuja kuinua mikono yao badala ya kuwadhoofisha.**{EW 107.1}**

****

## Sura ya 23-Tumaini la Kanisa

[Kutoka katika *Review and Herald*, Juni 10, 1852.]

Kama nilivyotazama hivi karibuni ili kupata wafuasi wanyenyekevu wa Yesu mpole na mnyenyekevu, akili yangu imeshugulishwa sana. Wengi wanaodai kuwa wanatazamia ujio wa haraka wa Kristo wanapatana na ulimwengu huu na kutafuta kwa bidii kusifiwa  na kupigiwa makofi, na wale wanaowazunguka kuliko kukubaliwa na Mungu. Wao ni baridi na wanapenda urasmi, wana Ukristo wa desturi, usio na jotojoto, kama tu yale makanisa ya majina ambayo wao walikuwa washiriki wake muda mfupi  uliopita. Maneno yaliyoelekezwa kwa kanisa la Laodikia yanaelezea hali yao ya sasa kikamilifu. (Angalia Ufunuo 3:14-20.) “Si baridi wala si moto,” lakini “vuguvugu.” Na wasiposikiliza ushauri wa "Shahidi mwaminifu na wa Kweli," na kutubu kwa bidii na kupata "dhahabu iliyojaribiwa motoni," "mavazi meupe," na "macho," Yeye atawatema kutoka kinywani Mwake.**{EW 107.2}**

Wakati umefika ambapo sehemu kubwa ya wale ambao hapo awali walifurahi na kupiga kelele kwa furaha kwa sababu ya kuja kwa Bwana kunakokaribia, wako chini ya makanisa na ulimwengu ambao hapo awali waliwadhihaki na kuwadharau kwa kuamini kwamba Yesu anakuja, na kueneza kila aina ya uongo ili kuongeza chuki dhidi yao na kuharibu mvuto wao. Sasa, ikiwa

yeyote anamtamani Mungu aliye hai, akiwa na njaa na kiu ya haki, na Mungu anampa kuhisi nguvu Zake, na kuiridhisha nafsi yao inayotamani kwa kumwaga nje upendo Wake moyoni mwake, na ikiwa anamtukuza Mungu kwa kumsifu, Yeye, kwa hawa wanaodai kuwa waumini katika kuja kwa Bwana hivi karibuni, mara nyingi huchukuliwa kuwa wamedanganywa, na kushambuliwa kwamba wamepata viini macho (mesmerized) au wameteswa na pepo waovu/wachafu.**{EW 108.1}**

Wengi wa hawa wanaodai kuwa Wakristo huvaa, huongea, na kutenda kama walimwengu, na kitu pekee ambacho wanaweza kujulikana kuwa ni Wakristo, ni maneno yao ya mdomoni tu, yaani husema kwamba wao ni Wakristo. Ingawa wanadai kuwa wanamtafuta Kristo, mazungumzo yao hayako mbinguni, bali katika mambo ya kidunia. "Ni watu wa tabia gani" wanapaswa kuwa "katika mwenendo mtakatifu na utauwa," wale wanaodai kuwa "wanaitazamia na kuiharakisha ile siku ya Mungu." 2 Petro 3:11, 12. "Na kila mwenye matumaini haya katika Yeye, hujitakasa kama Yeye alivyo mtakatifu.". 1 Yohana 3:3. Lakini ni dhahiri kwamba wengi wanaobeba  Jina la Waadventista hujifunza zaidi kupamba miili yao na kuonekana vizuri machoni pa ulimwengu kuliko wanavyojifunza kutoka kwa Neno la Mungu jinsi wanavyoweza kukubaliwa Naye.**{EW 108.2}**

Je! Ingekuwaje, kama Yesu wetu mpendwa, na Mfano wetu, angefanya kuonekana Kwake kati yao na wale

wanaokiri dini kwa ujumla,wakati ule wa ujio Wake wa kwanza? Yeye alizaliwa kwenye hori la wanyama. Hebu mfuate Yeye kupitia maisha Yake na huduma Yake. Alikuwa mtu wa huzuni na ajuaye sikitiko. Hawa watu wanaodai kuwa Wakristo wangeona aibu usoni pale watakapomwona Mwokozi mpole na mnyenyekevu ambaye alivaa nguo ya kawaida, lisilo na mshono au mapambo, Naye hakuwa na mahali pa kulaza kichwa Chake. Maisha Yake yasiyo na doa, ya kujikana yangewahukumu; taadhima Yake takatifu ingekuwa kizuizi kichungu juu ya kuchukulia kwao mambo kwa wepesi  na kicheko visivyo na maana; mazungumzo Yake yasiyo na hila yangekagua mazungumzo yao ya kidunia na ya tamaa mbaya; kutangaza Kwake Ukweli usiotiwa chumvi, unaokata, kungeonesha tabia yao halisi, na wangetamani kupata mfano wa upole, Yesu Mwenye kupendeza, atoke mbele yao kwa haraka iwezekanavyo. Wangekuwa miongoni mwa watu wa kwanza kujaribu kumkamata kwa Maneno Yake, na kupaza sauti, "Msulubishe! Msulubishe!**{EW 108.2}**

Hebu na tumfuate Yesu alipokuwa akienda Yerusalemu kwa upole, wakati "umati wote wa wanafunzi walipoanza kufurahi na kumsifu Mungu kwa sauti kuu, ... wakisema, Na ahimidiwe Mfalme ajaye kwa  Jina la Bwana. Amani mbinguni, na utukufu huko juu. Baadhi ya Mafarisayo waliokuwako katika lile kundi la watu, walimwambia Yesu, "Mwalimu, wanyamazishe wanafunzi Wako!" Yesu akawajibu, "Nawaambieni, kama hawa

wakinyamaza, hakika hayo mawe yatapaza sauti." Sehemu kubwa leo, ya wale wanaodai kumtazamia Kristo kama mafarisayo wa awali, wangetaka wanafunzi wanyamazishwe, na bila shaka wangepaza sauti, “Huu ni ushupavu! Ni kiini macho! Kiini macho!" Na wanafunzi, wangetandaza mavazi yao na matawi ya mitende njiani, wangefikiriwa kuwa ni watu wabadhirifu na wasiostaarabika, na wanaoleta fujo. Lakini Mwenyezi Mungu angependa watu Wake hapa duniani wasiwe kama wafu na kuwa na ubaridi, bali wamsifu na kumtukuza Yeye.  Mungu Atapokea utukufu kutoka kwa baadhi ya watu, na ikiwa wale wa chaguo Lake, wale wanaozishika amri Zake, wangenyamaza, basi mawe yale yangepiga kelele. **{EW 109.1}**

Yesu anakuja, lakini sio kama wakati wa ujio Wake wa kwanza, mtoto mchanga huko Bethlehemu; sio kama alivyopanda Punda kwenda Yerusalemu, wakati wanafunzi walimsifu Mungu kwa sauti kubwa na kupiga kelele, "Hosana"; lakini kwa utukufu wa Baba na kwa msafara wote wa malaika watakatifu kumsindikiza njiani kwenda duniani. Mbingu yote haitabaki na malaika hata mmoja, wakati watakatifu wakimngojea na kutazama mbinguni, kama vile watu wa Galilaya walivyomtazama wakati alipopaa juu, kutoka Mlima wa Mizeituni. Na ndipo wale watakatifu, wale waliofuata kikamilifu kielelezo chema, watapaza sauti kwa shangwe, wakimtazama, wakisema, Tazama, huyu Ndiye Mungu wetu; tuliyemngojea, Naye atatuokoa sisi. Nao watabadilishwa

“kwa nukta moja, kufumba na kufumbua, wakati wa parapanda ya mwisho”—parapanda hiyo ambayo huwaamsha watakatifu waliolala, na kuwaita kutoka vitandani mwao mavumbini, wakiwa wamevaa hali ya kutokufa kwa utukufu, na kupaza sauti, “Ushindi! Ushindi! dhidi ya kifo na kaburi!” Watakatifu waliobadilishwa, watanyakuliwa pamoja na malaika kukutana na Bwana hewani, kamwe wasitenganishwe tena na kusudi la upendo wao (Bwana).**{EW 110.1}**

Tukiwa na matarajio kama haya mbele yetu, tumaini tukufu kama hili, ukombozi kama huu ambao Kristo ameununua kwa ajili yetu kwa damu Yake Mwenyewe, tutanyamazaje basi? Je, hatutamsifu Mungu hata kwa kupaza sauti, kama walivyofanya wanafunzi wakati Yesu alipopanda kwenda Yerusalemu? Je, matarajio yetu si matukufu zaidi kuliko yalivyokuwa yao? Ni nani basi awezaye kuthubutu kutukataza kumtukuza Mungu kwa sauti kuu, wakati tukiwa na tumaini kuu la namna hii, la kutokufa tena, na lililojaa utukufu? Tumekwisha kuonja nguvu za ulimwengu ujao, na tunatamani sana kupata zaidi. Nafsi yangu yote inamlilia Mungu aliye hai, nami sitaridhika mpaka nimejazwa na utimilifu Wake wote. **{EW 110.2}**

## Sura ya 24-Maandalizi kwa Ajili ya Ujio wa Kristo

[Kutoka katika *Review and Herald*, Februari 17, 1853.]

**Kaka na Dada wapendwa**: Je, tunaamini kwa moyo wote kwamba Kristo Yuaja upesi na kwamba sasa tunaupata ujumbe wa mwisho wa rehema ambao utawahi kutolewa kwa ulimwengu wenye hatia? Je mfano wetu uko vile unavyopaswa kuwa? Je, sisi, kwa maisha yetu na mazungumzo matakatifu, tunawaonesha wale wanaotuzunguka kwamba tunatazamia kuonekana katika utukufu kwa Bwana na Mwokozi wetu Yesu Kristo, ambaye atabadilisha miili hii miovu na kuifanya iwe kama mwili Wake wa utukufu? Nina hofu kwamba hatuamini na kutambua mambo haya kama tunavyopaswa. Wale ambao wanaamini Ukweli muhimu ambao tunaukiri, wanapaswa kuonesha na kuishi imani yao kwa matendo. Kuna kutafuta sana burudani na mambo yanayovuta usikivu katika ulimwengu huu; akili inaachwa kushughulika sana juu ya mavazi, na ulimi unajishughulisha mara nyingi katika mazungumzo mepesi na hafifu, yaletayo uongo katika ungamo letu, kwa kuwa mazungumzo yetu hayako mbinguni, ambako kutoka huko tunamtarajia Mwokozi.**{EW 111.1}**

Malaika wanatutunza na kutulinda; mara nyingi sisi tunawahuzunisha malaika hawa kwa kujiingiza katika mazungumzo hafifu, mzaha, na utani, na pia

kwa kuzama katika hali ya uzembe, kutojali na ujinga. Ingawa tunaweza hapa na pale, kufanya juhudi kwa ajili ya ushindi na kuupata, ila ikiwa hatutautunza, bali tukazama katika hali ile ile ya uzembe, na kutojali, isiyoweza kuvumilia majaribu na kumpinga adui, basi hatuvumilii majaribu ya imani yetu ambayo ni ya thamani zaidi kuliko dhahabu. Hatuteseki kwa ajili ya Kristo, na kuona fahari katika dhiki.**{EW 111.2}**

Kuna ukosefu mkubwa wa ustahimilivu wa Kikristo na kumtumikia Mungu kutokana na kanuni. Hatupaswi kujitahidi kuipendeza na kuifurahisha nafsi, bali kumheshimu na kumtukuza Mungu, na katika yote tunayoyatenda na kusema kuelekeza jicho letu kukita katika utukufu Wake tu. Kama tungeliruhusu mioyo yetu kuvutiwa na maneno muhimu yafuatayo, na kuyazingatia daima, tusingeanguka katika majaribu kwa urahisi kiasi hicho na maneno yetu yangekuwa machache na yaliyochaguliwa vyema: “Yeye alijeruhiwa kwa makosa yetu, Alichubuliwa kwa maovu yetu; Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake, Na kwa kupigwa Kwake sisi tumepona.” "Kila neno lisilo maana, watakalolinena wanadamu, watatoa hesabu ya neno hilo siku ya hukumu." “U Mungu uonaye.”

au (Wewe Mungu unaniona mimi) **{EW 111.2}**

Hatuwezi kuyafikiria maneno haya muhimu, na kukumbuka mateso ya Yesu ili kwamba sisi wenye dhambi maskini tupate msamaha na kukombolewa kwa Mungu kwa damu Yake ya thamani zaidi, bila kuhisi kizuizi kitakatifu juu yetu na shauku ya dhati ya kuteseka kwa ajili Yake ambaye aliteseka na kuvumilia mengi kwa ajili yetu. Ikiwa tunatafakari mambo haya, nafsi yetu pendwa, na hadhi yake, itanyenyekezwa, na nafasi yake, itamilikiwa na usahili na unyenyekevu kama wa mtoto, ambao utakubali karipio kutoka kwa wengine na hautakasirika kwa urahisi. Roho ya ukaidi, na ubinafsi wa kufanya mtu anachopenda tu, haitaingia kuitawala nafsi.**{EW 112.1}**

Furaha za kweli za Mkristo na faraja ni lazima viwe mbinguni, na hakika vitakuwa mbinguni. Roho zenye matamanio makubwa sana, ambazo zimeonja nguvu za ulimwengu ujao na kushiriki katika karamu ya furaha ya mbinguni, hazitaridhika na mambo ya dunia. Watu kama hao watapata mambo mengi ya kufanya katika nyakati zao za kubarizi. Roho zao zitavutwa kumtafuta Mungu. Pale hazina yao ilipo, ndipo moyo wao utakapokuwapo, wakishikilia ushirika mtamu na

Mungu wanayempenda na kumwabudu. Burudani yao itakuwa katika kuitafakari hazina yao—Mji Mtakatifu, dunia iliyofanywa upya, makao yao ya milele. Na wanapoyatafakari sana mambo hayo ambayo ni ya fahari sana, utukufu, safi, na matakatifu, mbingu italetwa karibu, nao watahisi nguvu ya Roho Mtakatifu, na hii itaelekea kuyafanya mawazo kuaachana zaidi na zaidi na ulimwengu na kusababisha faraja yao na furaha yao kuu kuwa katika vitu vya mbinguni, makao yao mazuri na ya kupendeza. Nguvu ya mvuto kwa Mungu na mbingu wakati huo itakuwa kubwa sana kiasi kwamba hakuna kitu kitakachoweza kuvuta akili zao kutoka katika lengo kuu la kupata wokovu wa roho na kumheshimu na kumtukuza Mungu.**{EW 112.2}**

Ninapotambua ni kiasi gani kimefanywa kwa ajili yetu kutudumisha kuwa wema, na katika njia sahihi, ninaongozwa kushangaa, na kupaza sauti "Lo, ni upendo mkuu ulioje, upendo wa ajabu kiasi gani, alio nao Mwana wa Mungu kwa ajili yetu wenye dhambi maskini! Je, Tunapaswa kuwa wajinga na wazembe wakati kila kitu ambacho kinaweza kufanyika, kinafanywa kwa ajili ya wokovu wetu? Mbingu yote inavutiwa na sisi. Tunapaswa kuwa hai na kuamka ili kumheshimu, kumtukuza, na

kumwabudu Yeye aliye juu na Mwenye utukufu na fahari kuu sana. Mioyo yetu ingepaswa kububujika kwa upendo na shukrani Kwake Yeye ambaye amekuwa Mwenye upendo mwingi na huruma kwetu kwa kiasi hicho. Kwa maisha yetu tunapaswa kumheshimu Yeye, na kwa mazungumzo safi na matakatifu tuonyeshe kwamba sisi tumezaliwa kutoka juu, kwamba dunia hii siyo nyumbani kwetu, bali kwamba sisi ni wasafiri na wageni hapa, tukisafiri  na kwenda kwenye nchi iliyo bora zaidi.**{EW 113.1}**

Wengi wanaolikiri  Jina la Kristo na kudai kuwa wanautarajia ujio Wake wa haraka, hawajui ni nini maana ya kuteseka kwa ajili ya Kristo. Mioyo yao bado haijatiishwa na neema, na hawajaifia nafsi, kama ambavyo mara nyingi huoneshwa kwa njia tofauti-tofauti. Wakati huo huo wanazungumza juu ya kuwa na majaribu. Lakini sababu kuu ya majaribu yao ni moyo usiotiishwa, ambao unaifanya nafsi iwe nyepesi kuudhika, kiasi kwamba mara nyingi hujaribiwa. Kama watu kama hao wangeweza kutambua maana ya kuwa wafuasi wanyenyekevu wa Kristo, na Mkristo wa kweli, wangeanza kufanya kazi kwa dhati na bidii na kuanza kwa usahihi. Wangeweza kwanza kuifia

nafsi, kisha kufanya haraka kusali wakati wowote, na kuzuia kila hisia kali ya moyo. Salimisheni kujiamini, ujasiri wenu na kujitosheleza nafsi, ndugu, na kumfuata Yeye aliye Mfano wa upole. Daima mwekeni Yesu katika akili zenu kiasi kwamba Yeye ni mfano wenu na lazima mkanyage katika nyayo Zake. Mtazameni Yesu, mwenye kuanzisha na Mwenye kutimiza imani yetu; Yeye ambaye kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele Yake aliustahimili msalaba, akiidharau aibu. Yeye Alivumilia upinzani wa wenye dhambi dhidi Yake Mwenyewe. Yeye kwa sababu ya upendo Wake kwetu, alikuwa Mwana-Kondoo Yule mpole, aliyechinjwa, aliyejeruhiwa, aliyechubuliwa, aliyepigwa, na kuteswa. **{EW 113.2}**

Hebu, basi, na tuvumilie kitu fulani kwa uchangamfu kwa ajili ya Yesu, tuisulubishe nafsi kila siku, na kuwa washirika wa mateso ya Kristo hapa, ili tupate kufanywa kuwa washirika pamoja Naye wa utukufu Wake, na kuvikwa taji ya utukufu, heshima, kutokufa, na uzima wa milele.**{EW 114.1}**

****

## Sura ya 25-Uaminifu katika Mikutano ya Kijamii

Bwana amenionesha kwamba kunapaswa kuwa

na shauku kubwa miongoni mwa watunzaji wa Sabato katika kuendeleza mikutano yao na kuifanya iwe ya kuvutia. Kuna haja kubwa ya kuonyesha matamanio na nishati katika mwelekeo huu. Wote wanapaswa kuwa na kitu cha kusema kwa ajili ya Bwana, kwa kuwa kwa kufanya hivyo watabarikiwa. *Kitabu cha Kumbukumbu* kinaandikwa kwa ajili ya wale ambao hawaachi kukusanyika wenyewe pamoja, bali huzungumza mara kwa mara kila mtu na mwenzake. Waliosalia watashinda kwa damu ya Mwanakondoo na neno la ushuhuda wao. Wengine wanatarajia kushinda kwa damu ya Mwanakondoo peke yake, bila kufanya juhudi yoyote maalum ya kwao binafsi. Niliona kwamba Mungu amekuwa ni Mwenye rehema kwa kutujalia uwezo wa kuzungumza. Ametupa ulimi, na tunawajibika Kwake kwa ajili ya matumizi yake. Tunapaswa kumtukuza Mungu kwa kinywa chetu, tukizungumza kwa heshima juu ya Ukweli na juu ya rehema Zake zisizo na mpaka, na kushinda kwa neno la ushuhuda wetu kupitia katika damu ya Mwana-Kondoo.**{EW 114.2}**

Hatupaswi kukusanyika ili kukaa kimya; wale tu wanakumbukwa na Bwana ambao wanakusanyika ili kuzungumza juu ya heshima na utukufu Wake na

kusema juu ya uweza Wake; juu ya watu kama hao baraka za Mungu zitatulia, na wataburudishwa. Ikiwa wote wangekwenda kama wanavyopaswa, hakuna muda wa thamani ungepotea bure bila kutumika, na hakuna karipio ambalo lingehitajika kutolewa kwa sababu ya sala ndefu na kusihi kwingi; muda wote ungetawaliwa na shuhuda fupi-fupi za wazi na maombi.  Omba, amini, na upokee. Kuna kumdhihaki Bwana kwingi sana, kuomba kwingi sana ambako si kuomba na ambako huwachosha malaika na kumchukiza Mungu, maombi mengi mno ya bure, yasiyo na maana. Kwanza tunapaswa kujisikia kuwa tu wahitaji, na kisha kumwomba Mungu vitu tunavyovihitaji, tukiamini kwamba Yeye anatupatia, hata wakati ule tunapoomba; na kisha imani yetu itakua, wote watajengwa, walio dhaifu wataimarishwa, na waliovunjika moyo na kukata tamaa watafanywa watazame juu na kuamini kwamba Mungu ni mtoaji wa thawabu kwa wale wote wanaomtafuta kwa bidii. **{EW 115.1}**

Wengine wanasita kuhudhuria katika mkutano kwa sababu hawana kitu kipya cha kusema na kwamba watalazimika kurudia kisa kile kile ikiwa watazungumza. Niliona kwamba chini ya hili

kulikuwa na kiburi, kwamba Mungu na malaika walishuhudia shuhuda za watakatifu na walipendezwa sana na kutukuzwa kwa kurudiwa kila wiki. Bwana anapenda usahili na unyenyekevu, bali huchukizwa, na malaika wanahuzunishwa wakati wale warithi bayana wa Mungu na warithi pamoja na Yesu wanaporuhusu muda wa thamani kubwa uwe ukipotea bila kutumika katika mikutano yao.**{EW 115.2}**

Ikiwa ndugu wangekuwa mahali ambapo wangepaswa kuwa (ushirika), wasingekuwa na hasara ya kukosa kitu cha kusema kwa ajili ya heshima ya Yesu, ambaye alining'inia juu ya msalaba wa Kalvari kwa ajili ya dhambi zao. Kama wangelithamini zaidi hisia ya kutambua kule kujishusha kwa Mungu kwa kumtoa Mwanawe mpendwa wa pekee kufa kama dhabihu kwa ajili ya dhambi na makosa yetu, na mateso na maumivu makali ya Yesu kwa ajili ya kufanya njia ya kuokoka kwa mtu mwenye hatia, ili aweze kupokea msamaha na kuishi, basi, wangekuwa tayari zaidi kumtukuza na kumwadhimisha Yesu. Wasingeweza kukaa kimya, bali kwa kushukuru na kupendezwa wangezungumza juu ya utukufu Wake na kusema juu ya uweza Wake. Na kwa kufanya hivyo baraka

za Mungu zingetulia juu yao. Hata kama kisa kile kile kingelirudiwa, bado Mungu angetukuzwa. Malaika yule alinionesha wale ambao hawakomi mchana wala usiku kupaza sauti wakisema Mtakatifu, Mtakatifu Mungu Mwenyezi." "Marudio haya endelevu ya malaika" yule malaika yule aliongeza, "na bado Mungu anatukuzwa kwa hayo." Hata kama tutaweza kusimulia kisa kile kile tena na tena, kisa hicho kitamheshimu Mungu, na kuonesha kuwa sisi tunajali wema na rehema Zake kwetu (sisi hatupuuzii wema na rehema Zake). **{EW 115.3}**

Niliona kwamba makanisa yasiyo ya kweli, yale ya majina tu, yameanguka; kwamba ubaridi na kifo vinatawala miongoni mwao. Kama wangelifuata Neno la Mungu, basi lingeliwanyenyekesha. Lakini wanakuwa juu kuliko kazi ya Bwana. Ni fedheha sana kwao kurudia kisa kile kile sahili cha wema wa Mungu wanapokutana pamoja, nao wanasoma ili kupata kitu fulani kipya, kitu kikubwa, na kufanya maneno yao kuwa sahihi kwa sikio na ya kupendeza kwa mwanadamu, na Roho wa Mungu huwaacha. Tunapofuata njia ya unyenyekevu ya Biblia, tutapata miguso ya Roho wa Mungu. Sote tutakuwa katika upatanifu mzuri ikiwa tutafuata mkondo wa unyenyekevu wa Ukweli, tukimtegemea Mungu

kabisa, na hakutakuwa na hatari ya kuathiriwa na malaika waovu. Ni wakati ule nafsi zinapokuwa juu kuliko Roho wa Mungu, na kwenda kwa nguvu zao wenyewe, ndipo malaika huacha kuwalinda, na wanaachwa katika mapigo ya Shetani. **{EW 116.1}**

Wajibu umewekwa katika Neno la Mungu, ambao utendaji wake utawafanya watu wa Mungu kuwa wanyenyekevu na waliojitenga na ulimwengu, na kuwazuia kurudi nyuma, kama makanisa yale yasiyo ya kweli, na ya majina tu. Kuosha miguu na kushiriki meaza ya Bwana kunapaswa kufanyika mara nyingi zaidi. Yesu alituwekea mfano huo, na alituambia tufanye kama alivyofanya. Niliona kwamba mfano Wake unapaswa kufuatwa kikamilifu kwa kadiri inavyowezekana; lakini bado kaka na dada hawaendi kwa busara kama ilivyopaswa kuwa katika kuoshana miguu, na machafuko yamesababishwa. Inapaswa kuletwa katika maeneo mapya kwa uangalifu na hekima, hasa pale ambapo watu hawajajulishwa kuhusiana na mfano huu na mafundisho ya Bwana wetu juu ya jambo hili, na pale ambapo wana chuki dhidi yake. Roho nyingi aminifu, kupitia katika ushawishi wa walimu wa zamani ambao walikuwa na imani kwao, wanachukia au kuwa na ubaguzi sana, dhidi ya

wajibu huu dhahiri, na mada hii inapaswa kuletwa kwao kwa wakati na namna inayofaa. **{EW 116.2}**

Hakuna mfano uliotolewa katika Neno kwa kaka kuosha miguu ya dada; [angalia kiambatisho.] lakini kuna mfano kwa madada kuosha miguu ya akina kaka. Mariamu aliosha miguu ya Yesu kwa machozi yake, na kuipangusa kwa nywele za kichwa chake. (Angalia pia 1 Timotheo 5:10.) Niliona kwamba Bwana alikuwa amewasukuma akina dada kuosha miguu ya akina kaka na kwamba hii ilikuwa ni kulingana na utaratibu wa injili. Wote wanapaswa kwenda kwa uelewa na si wasifanye huku kuoshana miguu kuwa kaida au utaratibu wa kuchosha (tedious ceremony). **{EW 117.1}**

Salamu takatifu iliyotajwa katika injili ya Yesu Kristo na mtume Paulo inapaswa kuzingatiwa katika sifa yake ya halisi. *Ni busu takatifu*. [tazama kiambatisho.] Inapaswa kuzingatiwa kama ishara ya ushirika kwa marafiki Wakristo wakati wa kutengana, na wakati wa kukutana tena baada ya kutengana kwa majuma au miezi. Katika 1 Wathesalonike 5:26 Paulo anasema: “Wasalimuni ndugu wote kwa busu takatifu.” Katika sura hiyo hiyo anasema: " Jitengeni na ubaya wa kila namna." Hakuwezi kuwa na mwonekano wa uovu wakati

busu takatifu limetolewa kwa wakati na mahali sahihi.**{EW 117.2}**

Niliona kwamba mkono wenye nguvu wa adui umewekwa dhidi ya kazi ya Mungu, na msaada na nguvu ya kila mtu anayelipenda kusudi la ile Kweli anapaswa kujiorodhesha katika kusaidia hii kazi; shauku kubwa inapaswa kudhihirishwa na hao ili kuinua juu mikono ya wale wanaoitetea ile Kweli, ili kwa kukesha na ulinzi thabiti, waweze kumfungia nje adui. Wote wanapaswa kusimama kama mtu mmoja, wenye umoja katika kazi. Kila nguvu ya roho inapaswa kuwa macho, kwani kile kinachofanyika ni lazima kifanyike haraka kabisa. **{EW 117.3}**

Kisha nikamwona malaika wa tatu. Malaika aliyeandamana nami akasema, “Kazi yake huyu malaika ni ya kuogofya. Utume wake ni wa kutisha. Yeye ni malaika ambaye atabainisha ngano kutoka kutoka katika magugu, na kutia muhuri, au kufunga matita ya ngano kwa ajili ya ghala ya mbinguni. Mambo haya yanapaswa kushughulisha akili yote, na usikivu wote."**{EW 118.1}**

## Sura ya 26-Kwa Wasio na Uzoefu

Wengine, niwaliona, hawana hisia ya kutambua

umuhimu wa Ukweli au matokeo yake, na wakitenda kwa msukumo wa wakati wakati huo au kutokana na msisimko, mara nyingi hufuata hisia zao na kupuuza utaratibu wa kanisa. Watu kama hao wanaonekana kufikiri kwamba dini hutegemea sana kupiga kelele tu. [Angalia kiambatisho.] Baadhi ambao ndio tu wameupokea Ukweli wa ujumbe wa malaika wa tatu, na wako tayari kuwakemea na kuwafundisha wale ambao wamethibitishwa katika Ukweli kwa miaka mingi, na ambao wameteseka kwa ajili yake na kuhisi nguvu yake ya kutakasa. Wale wanaotiwa kiburi kiasi hicho na adui watapaswa kuhisi mvuto utakasao wa Ukweli na kupata utambuzi wa jinsi ulivyowapata wakiwa - "wanyonge, na wenye taabu, na maskini, na kipofu, na uchi." Wakati Ukweli unapoanza kuwatakasa na kusafisha toka kwao takataka na bati, kama ambavyo kwa hakika itakuwa pale itakapopokelewa kwa upendo, yule ambaye kazi hii kubwa imefanywa kwake hatahisi kuwa yeye ni tajiri na ameongezeka katika mali na hana haja ya kitu chochote.**{EW 118.2}**

Wale wanaoukiri Ukweli na kufikiri kuwa wanaujua wote kabla hawajajifunza kanuni zake za kwanza, na ambao wana haraka ya kuchukua nafasi

ya walimu na kuwakaripia wale ambao kwa miaka wamesimama kwa ushupavu kuutetea Ukweli, wanaonesha wazi kwamba hawana ufahamu wa ile Kweli, na wala hawajui hata moja ya matokeo yake; kwa kuwa kama wangejua nguvu yoyote ya utakaso, wangepaswa kuzaa matunda ya amani ya haki na kunyenyekeshwa chini ya uwezo wake mzuri na wenye nguvu. Wangezaa matunda kwa ajili ya utukufu wa Mungu, na kuelewa kile ambacho Ukweli umewafanyia, na kuwachukulia wengine kuwa bora kuliko wao wenyewe.**{EW 118.3}**

Niliona kuwa wale waliosalia hawakuwa tayari kwa ajili ya kile kitakachokuja juu ya dunia. Ujinga, kama uchovu, ulionekana kuning'inia juu ya akili za wengi wa wale wanaokiri kuamini kwamba tunao ujumbe wa mwisho. Malaika yule aliyeandamana nami alipaza sauti kwa umakini wa kuogofya, " Jiandae! Jiandae! Jiandae! kwa maana hasira kali ya Bwana iko karibu kuja. Ghadhabu Yake itamiminwa, pasipo kuchanganywa na rehema, nanyi bado hamjawa tayari. Rarueni mioyo, wala si mavazi. Kazi kubwa ni lazima ifanyike kwa ajili ya masalia. Wengi wao wanafikiria sana juu ya majaribu madogo-madogo." Malaika yule akasema, "Vikosi vya malaika waovu wamewazunguka, nao

wanajaribu kugandamiza giza lao la kutisha, ili mpate kunaswa na kuchukuliwa. Mnaruhusu akili zenu kupotoshwa kwa urahisi mno kutoka katika kazi ya kujiandaa na katika Ukweli muhimu kabisa kwa ajili ya siku hizi za mwisho. Nanyi mnafikiria sana juu ya majaribu madogo-madogo. Na mnaingia katika maelezo ya kina ya matatizo madogo madogo ili kuyaelezea kwa kumridhisha huyu au yule." Mazungumzo yamerefushwa kati ya pande zinazohusika, na si tu kwamba muda wao umepotea, bali watumishi wa Mungu wanashikiliwa ili kuwasikiliza, wakati ambapo mioyo ya pande zote mbili haijatiishwa kwa neema. Kama kiburi na ubinafsi vingewekwa kando, dakika tano zingeondoa matatizo mengi. Malaika wamehuzunishwa, na Mungu kuchukizwa na saa nyingi ambazo zimetumika katika kujihesabia haki. Niliona kwamba Mungu hatainama chini na kusikiliza maelezo marefu ya kujihesabia haki (kujikosha), na wala hataki watumishi Wake kufanya hivyo, na hivyo muda wa thamani upotezwe ambao ungetumika katika kuwaonesha wakosaji makosa ya njia zao na kuzinyang'ua haraka roho, kutoka motoni.**{EW 119.1}**

Niliona kwamba watu wa Mungu wamebweteka

katika uwanja uliorogwa (uwanja wenye uchovu wa kiroho), na kwamba wengine wamepoteza karibu hisia zote za ufupi wa muda na thamani ya roho. Kiburi kimeingia miongoni mwa watunza Sabato—kiburi cha mavazi na mwonekano. Malaika alisema, "Watunza Sabato watalazimika kufia nafsi, kufia kiburi na kupenda kukubalika."**{EW 120.1}**

Ukweli, ukweli unaookoa, ni lazima utolewe kwa watu wenye njaa ambao wako gizani. Niliona kuwa wengi walimwomba Mungu apate kuwanyenyekesha; lakini kama Mungu angejibu maombi yao, ingekuwa ni kwa mambo ya kuogofya katika haki. Ilikuwa ni wajibu wao kujinyenyekesha wenyewe. Niliona kuwa ikiwa kujikweza kungeruhisiwa kuja, bila shaka kungeipotosha roho, na kama kusingeshindwa basi kungehakikisha kuangamia kwao. Mtu anapoanza kujiinua machoni pake mwenyewe na kufikiri kwamba anaweza kufanya kitu, Roho wa Mungu anaondolewa, na anaendelea kwa nguvu zake mwenyewe mpaka anapoangushwa. Niliona kwamba mtakatifu mmoja, kama alikuwa sahihi, angeweza kuusogeza mkono wa Mungu; lakini umati wa watu wengi pamoja, ikiwa ungekosea, ungekuwa dhaifu na usingeweza kutekeleza chochote. **{EW 120.2}**

Wengi wana mioyo isiyotiishwa, isiyo na unyenyekevu, na hufikiria zaidi juu ya malalamiko na majaribio yao madogo-madogo kuliko juu ya roho za wenye dhambi. Kama wangekuwa wanauona utukufu wa Mungu, wangekuwa na hisia kwa ajili ya roho zinazoangamia kuwazunguka; na pale wanapotambua hali yao ya hatari, wangeshikilia kwa nguvu, wakitumia imani kwa Mungu, na kuinua juu mikono ya watumishi Wake, ili kwa ujasiri, lakini bado kwa upendo, watangaze Ukweli na kuzionya roho zipate kuushikilia kabla sauti tamu ya rehema haijafifia. Malaika alisema, "Wale wanaolikiri  Jina Lake, hawako tayari." Niliona kwamba mapigo saba ya mwisho yalikuwa yanakuja juu ya vichwa visivyo na kinga vya waovu; na kisha wale waliowazuia watasikia lawama kali za wenye dhambi, na mioyo yao itazimia ndani yao.**{EW 120.3}**

Malaika alisema, "Mmekuwa mkiokota mabua (au majani makavu tu)—mkitafakari sana juu ya majaribu madogo madogo—na wenye dhambi ni lazima wapotee kama matokeo yake." Mungu Yuko tayari kufanya kazi kwa ajili yetu katika mikutano yetu, na ni furaha Yake kufanya kazi. Lakini Shetani

anasema, "Nitaizuia kazi hiyo." Mawakala wake wanasema, “Amina.” Wale wanaodai kuiamini Kweli wanatafakari sana juu ya majaribu na shida zao ndogo-ndogo ambazo Shetani amezikuza mbele yao. Muda unapotea ambao hauwezi kurudishwa. Maadui wa Ukweli wameona udhaifu wetu, Mungu amehuzunishwa, Kristo kujeruhiwa. Lengo la Shetani linatimizwa, mipango yake imefanikiwa, na anashangilia**{EW 121.1}**

.

*****

## Sura ya 27-Kujikana Nafsi

Niliona kwamba kulikuwa na hatari ya watakatifu kufanya maandalizi makubwa sana kwa ajili ya mikutano; kiasi kwamba wengine walilemewa kwa kuwahudumia sana watu kwa chakula; hamu ya kula lazima ipingwe/ikataliwe. Kuna hatari ya wengine kuhudhuria katika mikutano hii kwa ajili ya mikate na samaki. Niliona kwamba wale wote ambao wanaiendekeza nafsi kwa kutumia tumbaku iliyo najisi, wanapaswa kuiweka kando na kuweka fedha zao katika matumizi yaliyo bora. Hao wanaotoa kafara wanaojinyima anasa fulani na kuchukua fedha walizozitumia hapo awali kukidhi

hamu ya chakula na kuziweka katika hazina ya Bwana. Kama sarafu mbili za mjane, zawadi kama hizo zitatambuliwa na Mungu. Kiasi kinaweza kuwa ni kidogo tu; lakini ikiwa wote watafanya hivyo, zitakuwa na nguvu katika hazina. Kama wote wangejifunza wanauchumi kwa kupunguza gharama katika makorokoro yao ya mavazi, wakijinyima baadhi ya vitu ambavyo si vya lazima hasa na kuviweka kando kabisa vitu visivyofaa na vyenye madhara kama vile chai nyeusi ya China na kahawa (inayolimwa Mufindi au Kericho), wakitoa kwa ajili ya kazi ya Mungu kiasi kile ambacho wangetumia katika kununua vitu hivi, basi wangepokea baraka zaidi hapa na thawabu mbinguni. Wengi wanafikiri kwamba kwa sababu Mungu amewapa fedha, basi wanaweza kuishi bila uhitaji, kwamba wanaweza kuwa na chakula cha fahari ambacho si cha lazima, na kujivika kwa wingi, na wanafikiri kwamba si vyema kwao kujikana nafsi wakati wana mali ya nyingi au ya kutosha. Watu kama hao hawatoi kafara. Kama wangeishi kwa kimaskini kidogo na kutoa kwa ajili ya kazi ya Mungu ili kusaidia kuuendeleza Ukweli, wangekuwa wametoa kafara kwa upande wao, na wakati ule Mungu atakapomlipa kila mtu kulingana na

matendo yake, Yeye Mungu, atakumbuka.**{EW 121.2}**

## Sura ya 28-Kukosa Kicho

Niliona kwamba Jina takatifu la Mungu linapaswa kutumiwa kwa heshima na hofu. Maneno Mungu Mwenyezi yanaunganishwa pamoja na kutumiwa na baadhi katika maombi kwa namna ya kizembe, kipumbavu, ambayo inamchukiza Yeye. Watu kama hawa hawana hisia ya utambuzi wa Mungu au Ukweli, ama sivyo wasingezungumza bila heshima kiasi hicho juu ya Mungu mkuu na wa kuogofya, ambaye hivi karibuni atawahukumu katika siku ya mwisho. Malaika alisema, "Usiyaunganishe pamoja, Kwa kuwa Jina Lake ni la kuogofya." Wale ambao wanatambua ukuu na uadhama wa Mungu, watalitaja Jina Lake vinywani mwao kwa hofu takatifu. Yeye Anakaa katika nuru isiyofikika; hakuna mwanadamu anayeweza kumwona na kuishi. Niliona kwamba mambo haya yatapaswa kueleweka na kurekebishwa kabla ya kanisa kubarikiwa.**{EW 122.1}**

## Sura ya 29-Wachungaji wa Uongo

Nimeoneshwa kwamba wachungaji wa uongo walikuwa wamelewa, lakini si kwa divai (Kwa mafundisho ya uongo); hupepesuka, lakini si kwa kinywaji kikali. Ukweli wa Mungu umefungwa kabisa kwao, hawawezi kuusoma. Wanapohojiwa kuhusu Sabato ya siku ya saba ni nini, kama ndio au siyo Sabato ya Kweli ya Biblia, wanaelekeza akili za watu kwenye hekaya za kubuni. Niliona kwamba manabii hawa walikuwa kama mbweha wa jangwani. Hawakupanda kwenda mahali palipobomolewa au penye ufa, wala hawakutengeneza boma, ili watu wa Mungu wapate kusimama vitani katika siku ya Bwana. Wakati akili za mtu yeyote zinapoamka, na kuanza kuwauliza wachungaji hawa wa uongo kuhusu Ukweli, wanatumia njia rahisi na bora zaidi ya kutimiza lengo lao na kutuliza akili za wale wanaouliza, hata kubadilisha msimamo wao wenyewe ili kufanya hivyo. Nuru imewaangazia wengi kati ya wachungaji hawa, lakini hawakuikubali nao wamebadilisha misimamo yao mara kadhaa ili kuukwepa Ukweli na kutoroka kutoka katika mahitimisho ambayo ni lazima wangeyafikia ikiwa wangeendelea katika msimamo wao wa awali. Nguvu ya Ukweli ilibomoa msingi wao, lakini badala ya kujisalimisha kwenye

huo Ukweli, wao wangepanda juu ya jukwaa lingine ambalo hawakuridhika nalo hata wao wenyewe.**{EW 123.1}**

Niliona kwamba wengi wa wachungaji hawa walikuwa wameyakataa mafundisho ya zamani ya Mungu ya awali; walikuwa wameukataa na kuukana Ikweli mtakatifu ambao waliwahi kuutetea kwa bidii nao wakajifunika na kiinimacho na kila aina ya udanganyifu. Niliona kwamba walikuwa wamelewa kwa makosa na walikuwa wanaliongoza kundi lao kuelekea katika mauti. Wengi wa wapinzani wa Kweli ya Mungu hubuni uharibifu vichwani mwao katika vitanda vyao, na kukipambazuka asubuhi, wanatekeleza hila zao mbaya wapate kuidharau Kweli na kupata kitu kingine kipya cha kuwapendeza watu na kugeuza akili zao kutoka kwa ile Kweli ya thamani, iliyo muhimu kabisa.**{EW 123.2}**

Niliona kwamba makuhani ambao wanawashawishi makundi yao kwenda mautini punde watakamatwa katika kazi yao ya kuogofya. Mapigo ya Mungu yanakuja, lakini hayatatosha kwa wachungaji hawa wa uongo kuteswa na pigo moja au mawili kati ya haya. Mkono wa Mungu wakati huo bado utakuwa umenyoshwa kwa ghadhabu na haki na hautarudishwa Kwake tena hadi makusudi

Yake yametimizwa kikamilifu, na makuhani hawa mamluki wameongozwa kwenda kuabudu miguuni pa watakatifu, na kukiri kwamba Mungu amewapenda kwa sababu walishikilia kabisa Ukweli na kutunza amri za Mungu, hadi waovu wote watakapoangamizwa kutoka duniani.**{EW 124.1}**

Makundi mbalimbali ya waumini wanaodai kuamini kuhusu Marejeo kila kimoja kina Ukweli kidogo, lakini Mungu ametoa Ukweli huu wote kwa watoto Wake ambao wanaandaliwa kwa ajili ya siku ya Mungu. Amewapa pia Ukweli ambao hakuna hata kimoja kati ya vikundi hivi anayeujua, wala hawatauelewa. Mambo ambayo yamefungwa kabisa kwao, ila Mungu ameyafungua kwa wale ambao wataona na wako tayari kuelewa. Kama Mungu ana nuru yoyote mpya ya kuwasilisha, Yeye atawaruhusu wateule Wake wapendwa kuifahamu, pasipo kwenda kwao kufanya akili zao kuelimishwa kwa kuwasikia wale ambao wako katika giza na makosa. **{EW 124.2}**

Nilioneshwa umuhimu wa wale wanaoamini kwamba tunao ujumbe wa mwisho wa rehema, kutengana na wale ambao kila siku wanafyonza maarifa yenye makosa mapya. Niliona kwamba si vijana wala wazee wanapaswa kuhudhuria

mikutano yao; kwa kuwa ni vibaya kwa jinsi hiyo kuwatia moyo wakati wanapofundisha *makosa* ambayo ni sumu ya kufisha kwa roho na kufundisha kama mafundisho amri za wanadamu. Mvuto wa mikusanyiko kama hiyo si mzuri. Kama Mungu ametuokoa kutoka katika giza na makosa ya jinsi hiyo, tunapaswa kusimama imara katika kufunguliwa ambao kwa ajili ya huo ametuweka huru na kufurahi katika Ukweli. Mungu anachukizwa na sisi tunapokwenda kusikiliza makosa, pasipo kulazimika kwenda; kwa kuwa, isipokuwa Yeye ametutuma kwenye mikutano hiyo ambapo makosa yanalazimishwa kufahamika kwa watu kwa nguvu ya dhamira, Yeye hatatulinda. Malaika wanaondoa ulinzi wao juu yetu, na tunaachwa kwa mapigo ya adui, ili kutiwa giza na kudhoofishwa naye na nguvu za malaika zake waovu; na nuru inayotuzunguka inaambukizwa na uchafuzi kwa giza hilo. **{EW 124.3}**

Niliona kwamba hatuna muda wa kupoteza bure katika kusikiliza hekaya za kubuni. Akili zetu hazipaswi kupotoshwa kwa namna hiyo, bali zinapaswa kushughulishwa na Ukweli wa sasa, na kutafuta hekima ili tuweze kupata maarifa kamili zaidi ya msimamo wetu, ili kwa upole tuweze kutoa sababu ya tumaini letu kutoka katika Maandiko.

Wakati ambapo mafundisho ya uongo na makosa ya hatari yanagandamizwa akilini, hayawezi kuelezea sana juu ya Ukweli ambao utaifaa na kuiandaa nyumba ya Israeli kusimama katika siku ya Bwana. **{EW 125.1}**

## Sura ya 30- Zawadi ya Mungu kwa Mwanadamu

Nimeoneshwa upendo mkuu na kujishusha kwa Mungu kwa kumtoa Mwanawe afe ili mwanadamu apate msamaha na kuishi. Nilioneshwa Adamu na Hawa, ambao walibahatika kuona uzuri na kupendeza kwa bustani ya Edeni na kuruhusiwa kula matunda ya miti yote katika bustani isipokuwa mmoja. Lakini nyoka alimjaribu Hawa, naye alimjaribu mumewe, na wote wawili walikula matunda ya mti uliokatazwa. Walivunja amri ya Mungu na kuwa wenye dhambi. Habari zilienea mbinguni, na kila kinubi kilinyamazishwa. Malaika walihuzunika, na kuhofia Adamu na Hawa kunyosha mkono wao tena na kula matunda ya mti wa uzima na kuwa wenye dhambi milele. Lakini Mungu alisema kwamba angewafukuza wakosaji hao kutoka katika bustani, na kwa kuwatumia makerubi na upanga uwakao moto angeilinda njia ya

kuelekea katika mti wa uzima, ili mwanadamu asiweze kuukaribia na kula matunda yake, yanayodumisha hali ya kutokufa.**{EW 125.2}**

Huzuni iliijaza mbingu pale ilipotambuliwa kuwa mwanadamu alikuwa amepotea na kwamba ulimwengu ambao Mungu alikuwa ameuumba ulipaswa kujazwa na wanadamu wenye kufa waliojipeleka kwenye taabu, uharibifu magonjwa, na mauti, na kwamba hakukuwa na njia ya kuokoka kwa ajili ya mkosaji. Sasa familia yote ya Adamu ilipaswa kufa. Kisha nikamwona Yesu mwema na apendezaye na nikaona sura ya huruma na ya huzuni juu ya uso Wake. Mara nikamwona akiikaribia ile nuru angavu mno iliyomfunika Baba. Malaika aliyeambatana nami akasema, “Yupo katika mazungumzo ya faragha na Baba Yake.” Shauku ya malaika hawa ilionekana kuwa na nguvu sana wakati Yesu alipokuwa akizungumza na Baba Yake. Mara tatu alifungiwa ndani na nuru tukufu iliyomzunguka Baba, na mara ya tatu alipotoka kwa Baba tuliweza kuiona nafsi Yake. Uso Wake ulikuwa mtulivu, huru kutokana na mfadhaiko na masumbufu yote, na uling'aa kwa uzuri ambao maneno hayawezi kuelezea. Kisha aliwajulisha kwaya ya malaika kwamba njia ya kuokoka ilikuwa

imetengenezwa kwa ajili ya mwanadamu aliyepotea; kwamba alikuwa akimsihi Baba Yake, na alikuwa amepata ruhusa ya kuyatoa maisha Yake mwenyewe kama fidia kwa jamii hiyo, kubeba dhambi zao, na kuchukua hukumu ya kifo juu Yake Mwenyewe, na kwa jinsi hiyo kufungua njia ambayo wangeweza, kupitia kwa ustahili wa damu Yake, kupata msamaha wa makosa ya zamani, na kwa utii kurudishwa kwenye bustani ambayo kutoka humo walifukuzwa. Kisha wangeliweza tena kupata ruhusa ya kuyafikia matunda adhimu, yasiyoweza kufa ya mti wa uzima ambao kwa sasa walikuwa wamepoteza haki yote juu yake.**{EW 126.1}**

Kisha shangwe, shangwe isiyoelezeka, iliijaza mbingu, na kwaya ya mbinguni iliimba wimbo wa sifa na wa kuabudu. Waligusa vinubi vyao na kuimba noti ya juu kuliko waliyowahi kuimba hapo awali, kwa sababu ya rehema kuu na kujishusha kwa Mungu kwa kumtoa Mpendwa Wake apendwaye sana ili afe kwa ajili ya jamii ya waasi (Kujishusha na kuzaliwa kama mwanadamu). Kisha sifa na ibada vilimiminwa kwa ajili ya kujikana nafsi, kujinyima na dhabihu ya Yesu, kwa kukubali kuacha kifua cha Baba Yake, na kuchagua maisha ya mateso na maumivu makali, na kifo cha aibu, ili

aweze kuwapa uzima wengine. **{EW 126.2}**

Malaika alisema, “Unadhani Baba alimtoa Mwanawe mpendwa sana pasipo mapambano? La, hasha. Lilikuwa ni pambano hata kwa Mungu wa mbinguni, kama ni kumwacha mwanadamu mwenye hatia aangamie, au kumtoa Mwanawe mpendwa afe kwa ajili yake.” Malaika walikuwa na shauku sana kuhusu wokovu wa mwanadamu kiasi kwamba kungeweza kupatikana miongoni mwao wale ambao wangeweza kusalimisha utukufu wao na kutoa maisha yao kwa ajili ya mwanadamu anayeangamia. "Lakini," alisema malaika aliyeandamana nami, "hiyo isingesaidia kitu chochote." Uhalifu huo ulikuwa mkubwa mno kiasi kwamba uhai wa malaika usingeweza kulipa deni hilo. Hakuna chochote isipokuwa kifo na maombezi ya Mwana wa Mungu yangelipa deni, na kumwokoa mwanadamu aliyepotea kutoka katika huzuni na taabu isiyo na matumaini.**{EW 127.1}**

Lakini kazi ambayo walipewa malaika ilikuwa ni kupanda na kushuka wakiwa na faraja yenye kutia nguvu kutoka katika utukufu ili kumtuliza Mwana wa Mungu katika mateso Yake. Walimhudumia Yesu. Pia, kazi yao ilikuwa ni kuwalinda na kuwatunza raia wa neema kutokana na malaika

waovu na kutokana na giza ambalo lilikuwa likitupwa kuwazunguka kila wakati na Shetani. Niliona kwamba haingewezekana kwa Mungu kubadilisha sheria Yake ili kumwokoa mwanadamu mpotevu, anayeangamia; kwa hiyo alimruhusu Mwanawe mpendwa kufa kwa ajili ya dhambi za mwanadamu. **{EW 127.2}**

## SEHEMU YA TATU

## Karama za Roho, Gombo la 1

**(Maneno haya yalitolewa kwenye Kitabu cha Spiritual Gifts Gombo la 1 na Spirit of Prophecy 1 na yamewekwa kwa *muhtasari*, ambayo yanapatikana katika kitabu cha Pambano Kuu pia)**

## Utangulizi

Karama ya unabii ilidhihirishwa katika Kanisa wakati wa kipindi cha Wayahudi. Ikiwa ilitoweka

kwa karne chache, kwa sababu ya hali ya upotovu ya Kanisa kuelekea mwisho wa kipindi hicho, ilionekana tena mwishoni mwake kumkaribisha Masihi. Zakaria, baba wa Yohana mbatizaji, "Akajazwa na Roho Mtakatifu, akatabiri." Simeoni, mtu mwadilifu na mcha Mungu ambaye alikuwa “Akiitarajia faraja ya Israeli,” Alikuja kwa roho hekaluni, na kutabiri juu ya Yesu kama “Nuru ya kuwa mwangaza wa Mataifa, Na kuwa utukufu wa watu wako Israeli.” Na Anna, nabii mke, “Akamshukuru Mungu, na wote waliokuwa wakiutarajia ukombozi katika Yerusalemu akawatolea habari zake.” Na hakukuwa na nabii mkuu kuliko Yohana mbatizaji, ambaye alichaguliwa na Mungu kumtambulisha kwa Israeli "Mwana-Kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu." **{EW 133.1}**

Zama ya Kikristo ilianza na kumwagwa kwa roho, na karama nyingi mbalimbali za Roho zilidhihirishwa miongoni mwa waumini. Hizi zilikuwa nyingi mno kiasi kwamba Paulo angeweza kuliambia Kanisa la Korintho, “Lakini kila mmoja hupewa ufunuo wa Roho kwa kufaidiana.”—Kwa kila mmoja Kanisani, si kwa kila mmoja ulimwenguni, kama ambavyo wengi wameitumia.**{EW 133.2}**

Tangu uasi mkuu, karama hizi zimedhihirishwa kwa nadra; na hii huenda ndiyo sababu inayowafanya watu wanaodai kuwa Wakristo kwa ujumla kuamini kwamba zilikuwa ni kwa ajili ya kipindi cha Kanisa la Awali peke yake. Lakini je, si kwa sababu ya makosa na kutokuamini kwa Kanisa kwamba karama zimekoma? Na pale watu wa Mungu watakapofikia imani ya awali na matendo, kama watakavyokuwa kwa hakika kwa kutangaza amri za Mungu na imani ya Yesu, je, "Mvua ya masika" Haitakuza tena karama hizo? Kwa kufikiri kwa ulinganifu tunapaswa kutarajia hivyo. **{EW 133.3}**

Licha ya uasi mwingi wa zama za Kiyahudi, kilifunguliwa na kufungwa kwa udhihirisho maalum wa Roho ya Mungu. Na ni kukosa busara kudhani kwamba zama za Kikristo—nuru ambayo, ikilinganishwa na kipindi cha awali, ni kama nuru ya jua ikilinganishwa na mionzi dhaifu ya mwezi—ingepaswa kuanza kwa utukufu na kumalizia gizani. Na kwa kuwa kazi maalum ya Roho ilikuwa ni muhimu katika kuwaandaa watu kwa ajili ya ujio wa kwanza wa Kristo, ni kiasi gani zaidi kwa ajili ya ule wa pili; hasa kwa kuwa siku za mwisho zingekuwa ni za hatari kuliko siku zote

zilizopita, na manabii wa uongo walipaswa kuwa na uwezo wa kuonesha ishara kubwa na maajabu, wapate kuwadanganya, kama yamkini, hata hao wateule.**{EW 134.1}**

“Akawaambia, Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa. Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa Jina Langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya; watashika nyoka; hata wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya. Marko 16:15-18. **{EW 134.1}**

Tafsiri ya Campbell inasema, "Nguvu hizi za kustajaabisha (muujiza) zitaambatana na waumini." Karama hazikuwekewa mipaka kwa mitume, bali zilienea hadi kwa waumini. Ni nani atakayekuwa nazo? Wale wanaoamini. Kwa muda gani? Hakuna ukomo; ahadi hii inaenda sambamba na utume mkuu wa kuhubiri injili na kumfikia muumini wa mwisho.**{EW 134.2}**

Lakini inapingwa kwamba msaada huu uliahidiwa kwa mitume peke yao na wale walioamini kupitia kwa mahubiri yao; kwamba

waliutimiza utume huo, wakaanzisha injili, na kwamba karama hizo zilikoma na kizazi hicho. Hebu na tuone kama utume mkuu ulimalizika katika kizazi hicho. Mathayo 28:19-20 "Basi, enendeni, mkawawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa Jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi. siku zote, hata ukamilifu wa dahari." **{EW 134.3}**

Kwamba kuhubiriwa kwa injili chini ya utume huu hakukumalizika na Kanisa la awali ni dhahiri kutokana na ahadi, "Mimi Nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari." Haisemi, Mimi Nipo pamoja nanyi, mitume, kila mahali, hata mwisho wa dunia; bali Mimi Nipo pamoja nanyi siku zote, hata mwisho wa ulimwengu. Haitafaa kusema kuwa zama za Wayahudi inamaanishwa hapa, kwa kuwa hizo tayari zilikuwa zimemalizika katika msalaba. Kwa hivyo, ninahitimisha, kwamba kuhubiriwa na kuaminiwa kwa injili ya kale daima kutaanbatana na msaada ule ule wa kiroho. Utume wa mitume ulihusu zama za Kikristo, na kuijumuisha yote. Kwa hiyo karama zilipotezwa kwa sababu tu ya uasi, na zitahuishwa kwa uamsho wa imani na matendo ya

kale.**{EW 135.1}**

Katika 1 Wakorintho 12:28, tunafahamishwa kwamba Mungu ameweka, au ameteua, au amepanga, karama fulani za Roho katika kanisa. Kwa kukosekana kwa ushahidi wowote wa maandiko kwambaameziondoa au amezifuta, ni lazima tuhitimishe kwamba zilikusudiwa kuendelea kuwepo. Ushahidi uko wapi basi wa kuwa zimefutwa? Ni katika sura ile ile ambapo Sabato ya Kiyahudi imefutwa, na Sabato ya Kikristo kuanzishwa—sura iliyopo katika matendo ya ile siri ya kuasi na mtu wa kuasi. Lakini mpingaji anadai uthibitisho wa Biblia kwamba vipawa vilipaswa kukoma, vilivyomo katika aya zifuatazo: "Upendo haupungui neno wakati wowote; bali ukiwapo unabii utabatilika; zikiwapo lugha, zitakoma; yakiwapo maarifa, yatabatilika. Kwa maana tunafahamu kwa sehemu; na tunafanya unabii kwa sehemu; lakini ijapo ile iliyo kamili, iliyo kwa sehemu itabatilika. Nilipokuwa mtoto mchanga, nalisema kama mtoto mchanga, nalifahamu kama mtoto mchanga, nalifikiri kama mtoto mchanga; tokea hapo nilipokuwa mtu mzima, nimeyabatilisha mambo ya kitoto. Maana wakati wa sasa tunaona kwa kioo kwa jinsi ya fumbo; wakati ule tutaona uso kwa uso;

wakati wa sasa nafahamu kwa sehemu; wakati ule nitajua sana kama mimi nami ninavyojuliwa sana. Basi, sasa inadumu imani, tumaini, upendo, haya matatu; na katika hayo lililo kuu ni upendo.” 1 Wakorintho 13:8-13. **{EW 135.2}**

Aya hizi hazitabiri kukoma kwa karama za Roho, pia kukoma kwa imani na tumaini. Lakini ni lini zingepaswa kukoma? Bado tunatazamia wakati ambapo- **{EW 136.1}**

“Tumaini litakapobadilika na kuwa matunda ya furaha, imani kuwa kuona, na maombi kuwa sifa.”

Zinapaswa kukoma wakati kile kilicho kamili kitakapokuja, wakati hatutaona tena kupitia katika kioo kwa giza, bali uso kwa uso. Siku ile kamilifu, wakati wenye haki wanafanywa kuwa wakamilifu na kuona kama wanavyoonekana, bado ni katika siku zijazo. Ni kweli kwamba mtu wa kuasi, alipoufikia utu uzima, aliachana na “Mambo ya kitoto” kama unabii, lugha, na maarifa, na pia imani, tumaini, na upendo wa Wakristo wa awali. Lakini hakuna chochote katika Maandiko kuonesha kwamba Mungu alikusudia kuondoa karama ambazo alikuwa ameziweka katika Kanisa, mpaka ukamilisho wa imani na tumaini lake, mpaka utukufu uzidio wa hali

ya kutokufa umefunika udhihirisho mzuri kabisa wa nguvu ya kiroho na maarifa ambayo yamewahi kudhihirishwa katika hali hii ya kufa.**{EW 136.2}**

Pingamizi lililojengwa juu ya 2 Timotheo 3:16, ambalo wengine wamelitoa kwa umakini mzito, halistahili kutiliwa maanani, zaidi ya maneno ya kupitia tu. Ikiwa Paulo, kwa kusema kwamba maandiko yanapaswa kumfanya mtu wa Mungu kuwa mkamilifu, aliyekamilishwa apate kutenda kila tendo jema, alimaanisha kwamba hakuna kitu kingine chochote kinachopaswa kuandikwa kwa uvuvio, kwa nini yeyebasi wakati ule alipokuwa anaishi, alikuwa akiongeza Maandiko hayo? Angalau kwa nini hakuweka kalamu chini mara tu sentensi hiyo ilipoandikwa? Na kwa nini Yohana, miaka thelathini baadaye, aliandika kitabu cha Ufunuo? Kitabu hiki kina Aya zingine ambazo zinanukuliwa kuthibitisha kufutwa kwa karama za kiroho.**{EW 136.2}**

"Namshuhudia kila mtu ayasikiaye maneno ya unabii wa kitabu hiki, Mtu ye yote akiyaongeza, Mungu atamwongezea hayo mapigo yaliyoandikwa katika kitabu hiki. Na mtu yeyote akiondoa lo lote katika Maneno ya unabii wa kitabu hiki, Mungu atamwondolea sehemu yake katika ule mti wa

uzima, na katika ule mji mtakatifu, ambao habari zake zimeandikwa katika kitabu hiki.” Ufunuo 22:18, 19.**{EW 137.1}**

Kutokana na Aya hii inadaiwa kwamba Mungu, ambaye kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi, alizungumza zamani na baba zetu kwa njia ya manabii, na, katika mwanzo wa siku ya injili, kwa njia ya Yesu na mitume Wake, ameahidi kwa uaminifu kabisa kwamba kamwe hatawasilisha kitu chochote zaidi kwa mwanadamu kwa njia hiyo. Kwa hiyo unabii wote baada ya tarehe hii lazima uwe wa uongo. Hii, inasemekana, inafunga vitabu vinavyotambulika vya Biblia takatifu vilivyovuviwa Kama ndivyo ilivyo, kwa nini Yohana aliandika injili yake baada ya kurudi kutoka Patmo kwenda Efeso? Kwa kufanya hivyo, je, aliongeza kwenye maneno ya unabii wa kitabu kile kilichoandikwa katika kisiwa cha Patmo? Ni dhahiri, kutoka katika Aya hii, kwamba tahadhari dhidi ya kuongeza, au kupunguza hairejelei Biblia kama ilivyokusanywa, bali kitabu tofauti cha ufunuo, kama kilivyokuja kutoka katika mkono wa Mtume. Lakini bado hakuna mtu aliye na haki kuongeza au kutoa kutoka katika Kitabu chochote kilichoandikwa kwa uvuvio wa Mungu.  Je, Yohana, kwa kuandika kitabu cha

Ufunuo, aliongeza kitu chochote kwenye kitabu cha unabii wa Danieli? Hasha! Nabii hana haki ya kubadilisha Neno la Mungu. Lakini njozi za Yohana zinathibitisha, zile za Danieli na zinatoa mwanga zaidi juu ya mada zilizowasilishwa hapo. Basi, ninahitimisha kwamba, Bwana hajajifunga mwenyewe kukaa kimya, bali bado ana uhuru wa kusema. Iwe ni kwa lugha ya moyo wangu, nena, Ee Bwana, kupitia kwa umpendaye, mtumishi wako anasikia. **{EW 137.2}**

Hivyo jaribio la kuthibitisha kutoka katika Maandiko kufutwa kwa vipawa vya Roho, kumeonekana kushindwa kabisa. Na maadamu milango ya kuzimu haijalishinda Kanisa, bali Mungu bado ana watu duniani, tunaweza kutafuta uendelezwaji wa karama kuhusiana na ujumbe wa malaika wa tatu, ujumbe ambao utalirudisha Kanisa katika uwanja wa zama za mitume na kulifanya kuwa nuru Kweli—wala si giza—la ulimwengu. **{EW 137.3}**

Tena: Tunaonywa mapema kwamba kutakuwapo na manabii wa uongo katika siku za mwisho, na Biblia inatoa kipimo ambacho kwacho tutayapima mafundisho yao ili tuweze kutofautisha kati ya kilicho Kweli na cha uongo. Kipimo kikuu ni

sheria ya Mungu, ambacho kinatumika kwa unabii na kwa tabia ya kimaadili ya manabii. Kama kusingekuwa na unabii wa Kweli katika siku za mwisho, ingekuwa ni rahisi kiasi gani kusema Ukweli huo, na hivyo kuondoa nafasi zote za udanganyifu, kuliko kutoa kipimo ambacho kwacho ungejaribiwa, kana kwamba kungekuwapo na wa Kweli na pia wa uongo. **{EW 138.1}**

Katika Isaya 8:19, 20, ni unabii wa roho zinazojulikana za wakati wa sasa, na sheria imetolewa kama kipimo: "Na waende kwa sheria na ushuhuda; ikiwa hawasemi sawasawa na Neno hili, bila shaka kwa hao hapana asubuhi. " Kwa nini useme, “Ikiwa hawasemi,” ikiwa kusingekuwapo na udhihirisho wa Kweli wa kiroho au unabii kwa wakati mmoja? Yesu alisema, “ Jihadharini na manabii wa uongo.... "Mtawatambua kwa matunda yao." Mathayo 7:16. Hii ni sehemu ya mahubiri juu ya mlima wa Baraka, na wote wanaweza kuona kwamba hotuba hii ina matumizi ya jumla kwa kanisa katika zama za injili. Manabii wa uongo wanapaswa kujulikana kwa matunda yao; kwa maneno mengine, kwa tabia yao ya kimaadili. Kipimo pekee cha kuamua ikiwa matunda yao ni mema au mabaya ni sheria ya Mungu. Hivyo

tunaletwa kwa sheria na kwa ushuhuda. Manabii wa kweli hawatazungumza tu kulingana na neno hili, bali wataishi kulingana nalo. Mtu ambaye huzungumza na kuishi hivyo, Sithubutu kumhukumu.**{EW 138.2}**

Siku zote imekuwa ni tabia ya manabii wa uongo kwamba wanaona njozi za amani; nao watakuwa wakisema, Amani na usalama, wakati uharibifu wa ghafula utakapowajia. Wale wa kweli watakemea dhambi kwa ujasiri na kuonya juu ya ghadhabu inayokuja. **{EW 139.1}**

Unabii ambao unapingana na matamko ya wazi na ya hakika ya neno, unapaswa kukataliwa. Hivyo ndivyo Mwokozi wetu alivyowafundisha wanafunzi Wake alipowaonya kuhusu jinsi ya kuja Kwake mara ya pili. Baada ya Yesu kupaa mbinguni, mbele ya macho ya wanafunzi Wake, ilitangazwa waziwazi kabisa na malaika kwamba huyu Yesu angekuja kwa jinsi hiyo hiyo kama walivyomwona akienda mbinguni. Hivyo Yesu, katika kutabiri kazi ya manabii wa uongo wa siku za mwisho, anasema, “Basi wakiwaambia, Yuko jangwani, msitoke; yumo nyumbani, msisadiki.” Unabii wote wa kweli juu ya jambo hilo ni lazima utambue ujio Wake unaoonekana wazi kutoka mbinguni. Kwa nini Yesu

hakusema, kataeni unabii wote wa wakati huo; kwa kuwa hakutakuwepo na manabii wa Kweli wakati huo? **{EW 139.2}**

“Naye alitoa wengine kuwa mitume, na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wainjilisti na wengine kuwa wachungaji na waalimu; kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe; hata na sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani na kumfahamu sana Mwana wa Mungu, hata kuwa mtu mkamilifu, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo.” Waefeso 4:11-13. {**EW 139.3**}

Tunajifunza kutoka katika aya iliyopita kwamba Kristo alipopaa juu, aliwapa wanadamu karama. Miongoni mwa karama hizi wameorodheshwa mitume, manabii, wainjilisti, wachungaji, na walimu. Lengo la kupewa karama hizo lilikuwa ni kuwakamilisha watakatifu katika umoja na maarifa. Baadhi ambao wanakiri kuwa wachungaji na walimu katika siku hizi wanashikilia kwamba karama hizi zilitimiza lengo lao miaka elfu moja mia nane iliyopita, na kwa hiyo zikakoma. Kwa nini basi wasitupilie mbali majina yao ya wachungaji na walimu? Ikiwa ofisi ya nabii kwa mujibu wa maandiko iliwekewa mpaka kwa Kanisa la awali,

ndivyo ilivyo kwa ile ya mwinjilisti—na wengine wote; kwa maana hakuna tofauti iliyowekwa. **{EW 139.1}**

Sasa hebu tufikirie kidogo juu ya jambo hili. Karama hizi zote zilitolewa kwa ajili ya kuwakamilisha watakatifu katika umoja, maarifa, na roho. Chini ya mvuto wake, Kanisa la Awali kwa muda lilifurahia umoja huo: "Wote wakajaa Roho Mtakatifu, wakanena Neno la Mungu kwa ujasiri. Na jamii ya watu walioamini walikuwa na moyo mmoja na roho moja; wala hapana mmoja aliyesema ya kuwa kitu chochote alicho nacho ni mali yake mwenyewe; bali walikuwa na vitu vyote shirika. "Na mitume wakatoa ushuhuda wa kufufuka Kwake Yesu kwa nguvu nyingi, na neema nyingi ikawa juu yao wote." Matendo 4:31-33. Ni jinsi gani tungetamani hali kama hiyo leo! Lakini uasi pamoja na ushawishi wake wa kugawanya na kuangamiza uliharibu uzuri wa Kanisa Safi na kulivika vazi la magunia. Mgawanyiko na mchafuko vimekuwa ndio matokeo. Kamwe hakukuwa na tofauti kubwa kiasi hicho ya imani katika Jumuiya ya Wakristo kama ilivyo leo (kuna takribani ya madhehebu 48,000 ya Kikristo leo). Kama karama hizi zilikuwa muhimu katika kuhifadhi umoja wa Kanisa la awali, basi ni

zaidi sana kiasi gani, sisi tunahitaji karama hizi leo, katika kuurejesha umoja! Na kwamba ni kusudi la Mungu kurejesha umoja wa Kanisa katika siku za mwisho, ni dhahiri mno kutokana na unabii. Tunahakikishiwa kwamba walinzi wataona jicho kwa jicho, wakati Bwana atakapoirejesha Sayuni. Pia, kwamba wakati wa mwisho wenye hekima wataelewa. Hili litakapotimizwa kutakuwa na umoja wa imani na wote ambao Mungu anawahesabu kuwa wenye hekima; kwa kuwa wale ambao kwa kweli wanaelewa kwa usahihi, lazima wataelewe kwa namna sawa. Ni kitu gani basi, kitakachosababisha umoja huu isipokuwa karama zile ambazo zilitolewa kwa kusudi hili hasa? **{EW 140.1}**

Kutokana na fikira kama hizi, ni dhahiri kwamba hali kamilifu ya Kanisa lililotabiriwa hapa bado iko katika siku zijazo; kwa sababu hiyo, karama hizi bado hazijatimiza kusudi lake. Barua hii kwa Waefeso iliandikwa mnamo 64 B.K., takriban miaka miwili kabla Paulo hajamwambia Timotheo kwamba alikuwa tayari kumiminwa, na wakati wa kuondoka kwake ulikuwa umekaribia. Mbegu za uasi kwa sasa zilikuwa zikiota katika Kanisa, kwani Paulo alikuwa amesema miaka kumi kabla, katika barua yake ya

pili kwa Wathesalonike, “Siri ya kuasi hivi sasa inatenda kazi.” Mbwa mwitu wakali sasa walikuwa karibu kuingia ndani, wasiliachilie kundi.” Kanisa wakati huo lilikuwa haliinuki na kusonga mbele ili kuufikia ukamilifu huo katika umoja ambao umekusudiwa katika maandiko, bali lilikuwa karibu kuraruliwa na makundi na kuvurugwa na migawanyiko. Mtume alilifahamu hili; kwa hiyo ni lazima alitazama mbele zaidi ya uasi mkubwa, hadi katika kipindi cha kukusanywa kwa mabaki ya watu wa Mungu, pale aliposema, "Hata na sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani." Waefeso 4:11-13 Kwa hiyo karama ambazo ziliwekwa kanisani bado hazijamaliza muda wake. **{EW 140.2}**

“Msimzimishe Roho; msitweze unabii; jaribuni mambo yote; lishikeni lililo jema. 1 Wathesalonike 5:19-21. **{EW 141.1}**

Katika waraka huu mtume anawasilisha mada ya ujio wa pili wa Bwana. Kisha anaelezea hali ya ulimwengu usioamini wakati huo, ambao walikuwa wanasema, ni ya "Amani na usalama," wakati ambapo siku ya Bwana inakaribia kutokea kwa ghafla juu yao, na uharibifu wa ghafla unawajia kama mwizi usiku. Kisha analishauri Kanisa, kwa kuzingatia mambo haya, kuwa macho, kukesha na

kuwa na kiasi. Miongoni mwa mausia yanayofuata ni maneno ambayo tumeyanukuu, “Msimzimishe roho,” n.k. Wengine wanaweza kufikiri kwamba Aya hizi tatu zimejitenga kabisa kila moja kutoka kwa nyingine katika maana; lakini zina uhusiano wa asili katika utaratibu ambao zinasimama. Mtu anayemzimisha roho ataachwa kutweza unabii, ambao ni tunda halali la roho. “Nitamimina Roho Yangu juu ya wote wenye mwili; na wana wenu, waume kwa wake, watatabiri. Yoeli 2:28.**{EW 141.2}**

Msemo, " Jaribuni mambo yote," umewekewa mipaka katika mada ya hotuba, unabii, na tunapaswa kujaribu roho kwa vipimo ambavyo Mungu ametupa katika neno lake. Udanganyifu wa kiroho na unabii wa uongo umejaa wakati huu; na bila shaka maandishi haya yana matumizi maalum hapa. Lakini mtume hasemi, kataa kila kitu, bali jaribuni mambo yote; lishikeni lililo jema. **{EW 141.2}**

“Hata itakuwa, baada ya hayo, ya kwamba nitamimina roho yangu juu ya wote wenye mwili; na wana wenu, waume kwa wake, watatabiri, wazee wenu wataota ndoto, na vijana wenu wataona maono; tena juu ya watumishi wenu, wanaume kwa wanawake, katika siku zile, nitamimina Roho Yangu.

Nami nitaonyesha mambo ya ajabu katika mbingu na katika dunia, damu, na moto, na minara ya moshi. Jua litageuzwa kuwa giza, na mwezi kuwa damu, kabla haijaja hiyo siku ya Bwana iliyo kuu na itishayo. Na itakuwa ya kwamba mtu awaye yote atakayeliita Jina la Bwana ataokolewa; kwa kuwa katika mlima Sayuni na katika Yerusalemu watakuwako watu watakaookoka, kama Bwana alivyosema; na katika mabaki, hao awaitao Bwana." Yoeli 2:28-32.**{EW 142.1}**

Unabii huu wa Yoeli, unaozungumzia kumwagwa kwa Roho Mtakatifu katika siku za mwisho, haukutimizwa wote mwanzoni mwa kipindi cha injili. Hii ni dhahiri kutokana na maajabu katika mbingu na katika dunia, yaliyotambulishwa katika maandiko haya, ambayo yalipaswa kuwa ni utangulizi wa "hiyo *Siku ya Bwana* iliyo kuu na itishayo." Ingawa tumekuwa na ishara hizi, siku hiyo ya kutisha bado iko katika wakati ujao. Kipindi chote cha injili kinaweza kuitwa siku za mwisho, lakini kusema kwamba Siku za Mwisho ni miaka yote 1800 iliyopita, ni upuuzi. Hiz zinafika hadi katika siku ya Bwana na katika ukombozi wa waliosalia wa watu wa Mungu: "Kwa kuwa katika mlima Sayuni na katika Yerusalemu kutakuwako watu watakaookoka,

kama Bwana alivyosema, na katika mabaki, hao awaitao Bwana." **{EW 142.2}**

Mabaki hawa, wanaoishi katikati ya ishara na maajabu ambayo yanaongoza katika siku kuu na ya kutisha ya Bwana, bila shaka ndio wale waliosalia wa uzao wa mwanamke waliotajwa katika Ufunuo 12:17—Kizazi cha mwisho cha Kanisa duniani. “ Joka akamkasirikia yule mwanamke, akaenda zake afanye vita juu ya wazao wake waliosalia, wazishikao amri za Mungu, na kuwa na ushuhuda wa Yesu” **{EW 143.1}**

Waliosalia wa Kanisa la Injili watakuwa na karama hizo. Vita vitapiganwa dhidi yao kwa sababu wanazishika amri za Mungu na kuwa na ushuhuda wa Yesu Kristo. Ufunuo 12:17. Katika Ufunuo 19:10, ushuhuda wa Yesu unafafanuliwa kuwa ni roho ya unabii. Malaika alisema, “Mimi ni mjoli wako na wa ndugu zako walio na ushuhuda wa Yesu.” Katika Ufunuo 22:9, anarudia yale-yale katika kiini, kama ifuatavyo: "Mimi ni mjoli wako, na wa ndugu zako manabii." Kutoka katika ulinganishi huu tunaona nguvu ya Maneno, "Ushuhuda wa Yesu ndio roho ya unabii." Lakini ushuhuda wa Yesu unajumuisha karama zote za Roho huyo Mmoja. Paulo anasema: “Namshukuru Mungu siku zote kwa

ajili yenu, kwa sababu ya neema ya Mungu mliyopewa katika Kristo Yesu; kwa kuwa katika kila jambo mlitajirika katika Yeye, katika Maneno yote, na maarifa yote; kama ushuhuda wa Kristo ulivyothibitika kwenu; hata hamkupungukiwa na karama yoyote, mkikutazamia sana kufunuliwa Kwake Bwana wetu Yesu Kristo." 1 Wakorintho 1:4-7. Ushuhuda wa Kristo ulithibitishwa katika Kanisa la Korintho; na matokeo yake yalikuwa ni nini? Hawakuwa nyuma kwa karama yoyote; Je, sisi hatuhalalishiwi, basi, hatimaye kwamba wale waliosalia watakapothibitishwa kikamilifu katika ushuhuda wa Yesu, hawatakuwa nyuma katika kipawa chochote, huku wakisubiri ujio wa Bwana wetu Yesu Kristo? **{EW 143.2}**

Roswell F. Cottrell

## Sura ya 31-Kuanguka kwa Shetani

Shetani wakati fulani aliwahi kuwa malaika aliyeheshimiwa mbinguni, akimfuatia Kristo. Uso wake, kama wa wale malaika wengine, ulikuwa mpole na wenye kuonesha furaha. Paji la uso wake lilikuwa refu na pana likionesha akili nyingi. Umbo lake lilikuwa kamilifu; mwenendo wake mzuri na

mtukufu. Lakini Mungu alipomwambia Mwanawe, "Na tumfanye mtu kwa mfano wetu," Shetani alimwonea Yesu wivu. Alitamani kuombwa ushauri kuhusu kuumbwa kwa mwanadamu, na kwa sababu hakuombwa ushauri, alijawa na husuda, wivu, na chuki. Alitaka sana yeye ndiye awe mwenye kupokea heshima za juu kabisa mbinguni baada ya Mungu.**{EW 145.1}**

Hadi wakati huu mbingu yote ilikuwa katika utaratibu, upatanifu, na kutawaliwa kikamilifu na serikali ya Mungu. Ilikuwa ni dhambi ya juu kabisa kuasi dhidi ya utaratibu na mapenzi Yake. Mbingu yote ilionekana kuwa katika ghasia. Malaika walipangwa katika makundi, kila sehemu ikiwa na malaika kiongozi akiwaamrisha. Shetani, akiwa na tamaa ya makuu ya kutaka kujitukuza mwenyewe, na asitake kabisa kujiweka chini ya mamlaka ya Yesu, naye alikuwa akijipenyeza polepole na kwa hila dhidi ya serikali ya Mungu. Baadhi ya malaika walikubaliana na Shetani katika uasi wake na hata kumwonea huruma, na wengine walipambana sana kwa ajili ya heshima na hekima ya Mungu katika kumpa Mwanawe mamlaka. Kulikuwa na mashindano miongoni mwa malaika. Shetani na malaika waliokubaliana naye walikuwa

wanapambana kutaka kurekebisha serikali ya Mungu. Walitaka kuipeleleza hekima Yake isiyochunguzika, na kuhakikisha kusudi Lake katika kumtukuza Yesu na kumpa uweza na ukuu bila kikomo kiasi kile. Waliasi dhidi ya mamlaka ya Mwana. Jeshi lote la mbingu liliitwa kuonekana mbele ya Baba ili kila jambo liamuliwe. Pale iliamuliwa kwamba Shetani inabidi afukuzwe kutoka mbinguni, pamoja na malaika wote ambao waliungana naye katika uasi ule. Ndipo kulitokea vita mbinguni. Malaika walihusika katika vita hivyo; Shetani alitamani kumshinda Mwana wa Mungu pamoja na wale waliokuwa watiifu kwa mapenzi Yake. Lakini malaika wale wema na waaminifu walishinda, na Shetani, pamoja na wafuasi wake walifukuzwa kutoka mbinguni.**{EW 145.2}**

Baada ya Shetani na wale walioanguka pamoja naye kufungiwa nje ya mbingu, na kutambua kwamba alikuwa amepoteza milele usafi na utukufu wote wa mbingu, alitubu, na kutamani kurejeshwa katika nafasi yake mbinguni. Alikuwa tayari kuchukua nafasi yake sahihi, au nafasi yoyote ambayo angeweza kupewa. Lakini hapana, mbingu ni lazima isiwekwe katika hatari. Mbingu yote ingeweza kuharibiwa kama angerudishwa; kwa

kuwa dhambi ilianza kwake, ndiye aliyekuwa muasisi wa dhambi, na mbegu za uasi zilikuwa ndani yake. Yeye pamoja na wafuasi wake waliomboleza, na kusihi kurejeshwa katika kukubaliwa na Mungu. Lakini dhambi yao—chuki yao, husuda yao, na wivu wao—ilikuwa ni kubwa mno kiasi kwamba Mungu asingeweza kuifuta. Ni lazima idumu kuwapo ili ipate kupokea adhabu yake ya mwisho.**{EW 146.1}**

Shetani alipotambua kabisa kwamba hakukuwa na uwezekano kwake kukubaliwa tena na Mungu, uovu wake, uadui na chuki vilianza kudhihirika. Alishauriana na malaika zake, na mpango uliwekwa ili kuendelea kufanya kazi dhidi ya serikali ya Mungu. Pale Adamu na Hawa walipowekwa katika bustani ile nzuri, Shetani alikuwa akiweka mipango ya kuwaangamiza. Isingewezekana kwa vyovyote wenzi hawa wenye furaha kunyang'anywa furaha yao kama wangemtii Mungu. Shetani asingeweza kutumia uwezo wake juu yao isipokuwa kwanza wameacha kumtii Mungu na kupoteza fadhila Yake. Mpango kwa hiyo ni lazima utengenezwe wa kuwaongoza katika kutokutii ili waweze kupata kuchukiwa na Mungu na kufikishwa chini ya uwezo wa moja kwa moja wa Shetani Iliamuliwa kuwa

Shetani ni lazima achukue umbo lingine na kuonesha shauku kwa mwanadamu. Ni lazima apendekeze kwa hila dhidi ya Ukweli wa Mungu na kusababisha mashaka iwapo Mungu alimaanisha kile hasa alichokisema; kinachofuata, ni lazima achochee udadisi, na kuwaongoza katika kupeleleza mipango ya Mungu isiyochunguzika—dhambi ile hasa ambayo Shetani alikuwa na hatia nayo—na kuwaza kimantiki ni kwa sababu gani kuna masharti Yake kuhusiana na mti wa ujuzi wa mema na mabaya.**{EW 146.2}**

## Sura ya 32-Anguko la Mwanadamu

Malaika watakatifu mara nyingi walitembelea bustanini, na kutoa maelekezo kwa Adamu na Hawa kuhusu kazi yao na pia waliwafundisha kuhusu kuasi na kuanguka kwa Shetani. Malaika waliwaonya juu ya Shetani na kuwapa tahadhari wasitengane kila mmoja na mwenzake katika kazi yao, kwa kuwa wangeweza kukutanishwa na adui huyu aliyeanguka. Malaika pia waliwaamuru wafuate kwa karibu maelekezo ambayo Mungu alikuwa amewapa, kwa kuwa kwa utiifu kamili tu, ndiyo walikuwa salama. Ndipo adui huyu

aliyeanguka asingeweza kuwa na nguvu juu yao. **{EW 147.1}**

Shetani alianza kazi yake kwa Hawa, kumfanya asitii. Kwanza alifanya kosa kwa kutangatanga kutoka kwa mumewe, na kufuatiwa na kukaa karibu na ule mti uliokatazwa, kilichofuata kwa kusikia sauti ya yule mjaribu, na hata kuthubutu kutilia shaka kile alichokisema Mungu: "Kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika." Alifikiri kwamba huenda Bwana hakumaanisha hasa kile Alichokisema, na akithubutu, alinyosha mkono wake, akachukua tunda na kula. Lilikuwa linavutia machoni na kupendeza katika ladha. Kisha alikuwa na wivu kwamba Mungu alikuwa amewazuilia kile kilichokuwa chema kwao, naye alimpatia tunda mumewe, na hivyo kumjaribu. Alimsimulia Adamu yote ambayo nyoka huyo alikuwa amesema na akaonesha mshangao wake kwamba alikuwa na uwezo wa kusema.**{EW 147.2}**

Niliona huzuni ikija juu ya uso wa Adamu. Alionekana kuwa na hofu na kushtuka. Mapambano yalionekana yakiendelea katika fikra zake. Alihisi hakika kwamba huyu alikuwa ndiye adui yule ambaye walikuwa wameonywa dhidi yake, na kwamba mke wake lazima afe. Lazima

watenganishwe. Upendo wake kwa Hawa ulikuwa ni wenye nguvu, na kwa kukata tamaa kabisa aliamua kushiriki mauti yake (adhabu yake). Alilichukua tunda lile na kulila kwa haraka. Ndipo Shetani alishangilia. Alikuwa ameasi mbinguni, na kupata waliomuunga mkono ambao walimpenda na kumfuata katika uasi wake. Alianguka na kuwasababisha wengine kuanguka pamoja naye. Na sasa alikuwa amemjaribu mwanamke kutokumwamini Mungu, kuhoji hekima Yake, na kujitahidi kupenya katika mipango Yake yenye hekima isiyo na mpaka.  Shetani alijua kwamba mwanamke asingeanguka peke yake. Adamu, kupitia katika upendo wake kwa Hawa, aliacha kutii amri ya Mungu, na kuanguka pamoja naye.**{EW 148.1}**

Habari za kuanguka kwa mwanadamu zilienea katika mbingu yote (Sayari zote). Kila kinubi kilinyamazishwa. Malaika walitupa taji zao kutoka katika vichwa vyao kwa huzuni. Mbingu yote ilikuwa katika fadhaa. Baraza lilikaa ili kuamua ni kitu gani kifanyike kwa wenzi hawa wenye hatia. Malaika walihofu kwamba hawa wanandoa wangenyosha mkono, na kula matunda ya mti wa uzima, na kuwa wenye dhambi wasiokufa. Lakini Mungu alisema

kuwa angewafukuza watenda dhambi hawa kutoka katika bustani. Malaika mara moja waliagizwa kulinda njia ya kuelekea katika mti wa uzima. Ulikuwa ni mpango uliodhamiriwa wa Shetani kwamba Adamu na Hawa wasimtii Mungu, wachukiwe Naye, na kisha kula matunda ya mti wa uzima, ili wapate kuishi milele katika dhambi na kutokutii, na hivyo dhambi ipewe kutokufa. Lakini malaika watakatifu walitumwa kuwafukuza Adamu na Hawa kutoka bustanini, na kuzuia njia yao kuelekea katika mti wa uzima. Kila mmoja wa hawa malaika wenye nguvu, alikuwa nacho kitu katika mkono wake wa kulia, kilichoonekana kama panga linalometameta.**{EW 148.2}**

Ndipo Shetani aliposhangilia. Alikuwa amewafanya wengine kuteseka kwa kuanguka kwake. Alifungiwa nje ya mbingu, na wao nje ya Paradiso.**{EW 148.1}**

## Sura ya 33- Mpango wa Wokovu

Huzuni iliijaza mbingu, pale ilipotambuliwa kuwa mwanadamu alikuwa amepotea, na kwamba ulimwengu ambao Mungu alikuwa ameuumba ulipaswa kujazwa na wanadamu wenye kufa

walioandikiwa taabu, huzuni, magonjwa, na kifo, na kwamba hakukuwa na njia ya kuokoka kwa mkosaji. Familia yote ya Adamu lazima ife. Nilimwona Yesu Mwenye kupendeza na kuona sura ya huruma na huzuni juu ya uso Wake. Mara nikamwona akiikaribia ile nuru angavu mno iliyomfunika Baba. Malaika aliyeandamana nami akasema, Ana mazungumzo ya faragha na Baba Yake. Shauku ya malaika ilionekana kuwa kali wakati ule Yesu alipokuwa anazungumza na Baba Yake. Mara tatu alifungiwa ndani na nuru ile tukufu iliyomzunguka Baba, na mara ya tatu alipotoka kwa Baba, nafsi Yake iliweza kuonekana. Uso wake ulikuwa mtulivu, huru kutokana na mfadhaiko na mashaka yote, na uling'aa kwa ukarimu na uzuri, ambao maneno hayawezi kuelezea. Kisha akawajulisha jeshi la malaika kwamba njia ya kuokoka ilikuwa imefanywa kwa ajili ya mwanadamu aliyepotea. Aliwaambia kwamba alikuwa akimsihi Baba Yake, na alikuwa amejitolea kutoa maisha Yake kuwa fidia, kuchukua hukumu ya kifo juu Yake Mwenyewe, ili kupitia Kwake mwanadamu apate msamaha; ili kupitia kwa ustahili wa damu Yake, na utii kwa sheria ya Mungu, wangeweza kupata upendeleo na neema ya Mungu, na kuletwa tena katika bustani nzuri, na kula

matunda ya mti wa uzima. **{EW 149.2}**

Mwanzoni malaika hawakuweza kufurahi; kwani Kamanda wao hakuficha chochote kutoka kwao, bali alifungua mbele yao mpango wa wokovu. Yesu aliwaambia kwamba Yeye angesimama kati ya ghadhabu ya Baba Yake na mwanadamu mwenye hatia, kwamba angebeba uovu na dharau, na ni wachache tu wangempokea kama Mwana wa Mungu. Karibu wote wangemchukia na kumkataa. Angeacha utukufu Wake wote mbinguni, aonekane duniani kama mwanadamu, ajinyenyekeshe kama mwanadamu, apate kuyajua kupitia kwa uzoefu Wake mwenyewe majaribu mbalimbali ambayo kwayo mwanadamu angezongwa, ili aweze kujua jinsi ya kuwasaidia wale ambao wangejaribiwa; na kwamba hatimaye, baada ya utume Wake kama Mwalimu kukamilika, angetiwa mikononi mwa wanadamu, na kuvumilia karibu kila ukatili na mateso ambayo Shetani na malaika zake wangeweza kuwasukuma watu waovu kutenda; kwamba angekufa kifo cha ukatili mno, na kuning'nia kati ya mbingu na dunia kama mwenye dhambi mwenye hatia; kwamba angepitia saa nyingi za kuogofya za maumivu makali, ambayo hata malaika wasingeweza kuyatazama, bali

wangefunika nyuso zao wasiione mandhari ile. Si maumivu ya kimwili tu ambayo angeteseka nayo, bali maumivu ya kiakili, ambayo mateso ya kimwili yasingeweza kulinganishwa nayo. Uzito wa dhambi za ulimwengu wote ungekuwa juu Yake. Aliwaambia kwamba angekufa na kufufuka siku ya tatu, naye angepaa kwenda kwa Baba Yake kumwombea mwanadamu mkaidi, aliyepotoka, na mwenye hatia. **{EW 149.3}**

Malaika wakasujudu mbele Yake. Waliyatoa maisha yao. Yesu aliwaambia kwamba kwa kifo Chake angewaokoa wengi, kwamba uhai wa malaika usingeweza kulilipa deni lile. Maisha Yake peke yake yangekubaliwa na Baba Yake kama fidia kwa ajili ya mwanadamu. Yesu pia aliwaambia kwamba wangekuwa na sehemu ya kutenda, kuwa pamoja Naye na kwa nyakati tofautitofuti kumtia nguvu; kwamba angechukua asili iliyoanguka ya mwanadamu, na nguvu zake hata zisingekuwa sawa na zao (zingekuwa hafifu zaidi); kwamba wangekuwa mashahidi wa mateso na kudhalilishwa Kwake, na chuki za wanadamu Kwake, wangesisimshwa kwa hisia kali mno, na kupitia upendo wao Kwake wangetamani kumsaidia na kumwokoa kutoka kwa wauaji Wake; lakini kwamba

hawapaswi kuingilia kati kuzuia chochote wanachopaswa kukiona-kukishuhudia kwa macho yao; na kwamba wangefanya sehemu yao katika ufufuo Wake; kwamba mpango wa wokovu ulipangwa, na Baba Yake alikuwa ameukubali mpango huo.**{EW 150.1}**

Kwa huzuni takatifu Yesu aliwafariji na kuwatia tumaini malaika na kuwaambia kwamba baadaye wale atakaowakomboa watakuwa pamoja Naye, na kwamba kwa kifo Chake angelipa fidia ya kuwakomboa wengi na kumwangamiza yule aliyekuwa na nguvu ya kifo. Baba Yake wa mbinguni angempa Yeye ufalme, na mamlaka, ukuu wa ufalme chini ya mbingu zote, naye angeimiliki milele na milele. Shetani na wenye dhambi wangeangamizwa, wasiweze tena kamwe kuisumbua mbingu au dunia mpya iliyotakaswa. Yesu aliwaambia jeshi la mbinguni wapate kuridhika na mpango ambao Baba Yake alikuwa ameukubali na kufurahi kwamba kupitia kifo Chake mwanadamu aliyeanguka angeweza tena kuinuliwa ili apate kukubaliwa na Mungu na kuifurahia mbingu. **{EW 151.1}**

Ndipo furaha, furaha isiyoelezeka, iliijaza mbingu. Na jeshi la mbinguni waliimba wimbo wa sifa na

kuabudu. Waligusa vinubi vyao na kuimba noti ya juu zaidi kuliko walivyofanya hapo awali, kwa sababu ya rehema kuu na kujishusha kwa Mungu katika kumtoa Mpendwa Wake apendwaye sana ili afe kwa ajili ya jamii ya waasi. Sifa na ibada zilimiminwa kwa ajili ya kujinyima na dhabihu ya Yesu; kwamba angekubali kuacha kifua cha Baba yake, na kuchagua maisha ya mateso na maumivu makali, na kufa kifo cha aibu ili kuwapa uzima wengine.**{EW 151.2}**

Malaika alisema, “Unadhani Baba alimtoa Mwanawe mpendwa sana pasipo mapambano? La, hasha. Lilikuwa ni pambano hata kwa Mungu wa mbinguni, ama kumwacha mtu mwenye hatia aangamie, au kumtoa Mwanawe mpendwa afe kwa ajili yao. Malaika walikuwa na shauku sana kuhusu wokovu wa mwanadamu kiasi kwamba kungeweza kupatikana miongoni mwao wale ambao wangeweza kusalimisha utukufu wao na kutoa maisha yao kwa ajili ya mwanadamu anayeangamia. "Lakini," alisema malaika aliyeandamana nami, "hiyo isingesaidia kitu chochote." Uhalifu huo ulikuwa mkubwa mno kiasi kwamba uhai wa malaika usingeweza kulipa deni hilo. Hakuna chochote isipokuwa kifo na maombezi ya Mwana wa Mungu

yangelipa deni na kumwokoa mwanadamu aliyepotea kutoka katika huzuni na taabu isiyo na matumaini.**{EW 151.3}**

Lakini kazi ambayo walipewa malaika ilikuwa ni kupanda na kushuka wakiwa na faraja yenye kutia nguvu kutoka katika utukufu ili kumpa nafuu au kumtuliza Mwana wa Mungu katika mateso Yake. Walimtumikia Yesu. Pia, kazi yao ilikuwa ni kuwalinda na kuwatunza raia wa neema kutokana na malaika waovu na kutokana na giza ambalo lilikuwa likitupwa kuwazunguka kila wakati na Shetani. Niliona kwamba haingewezekana kwa Mungu kubadilisha sheria Yake ili kumwokoa mwanadamu mpotevu, anayeangamia; kwa hiyo alimruhusu Mwanawe mpendwa kufa kwa ajili ya dhambi za mwanadamu.**{EW 152.1}**

Shetani tena alifurahi pamoja na malaika zake kwamba angeweza, kwa kusababisha kuanguka kwa mwanadamu, kumvuta Mwana wa Mungu kutoka kwenye nafasi Yake ya juu. Aliwaambia malaika zake kwamba Yesu atakapolazimika kuchukua asili ya mwanadamu aliyeanguka, angeweza kumshinda na kuzuia kukamilishwa kwa mpango wa wokovu.**{EW 152.2}**

Nilioneshwa Shetani kama alivyokuwa hapo kwanza, malaika mwenye furaha aliyetukuka. Kisha nikaoneshwa jinsi alivyo sasa. Bado analo umbo la kifalme. Sura yake bado ni nzuri, kwa kuwa ni malaika aliyeanguka. Lakini sura ya uso wake imejaa wasiwasi, mashaka, kukosa furaha, hila, chuki, uharibifu, udanganyifu, na kila uovu. Uso ule ambao hapo awali ulikuwa nzuri sana, niliuangalia kwa namna ya pekee. Paji la uso wake lilianzia kwenye macho yake kurudi nyuma. Niliona kwamba kwa muda mrefu sana alikuwa amejielekeza kwenye uovu kiasi kwamba kila sifa njema ilishushwa hadhi, na kila sifa bainishi ya uovu kukuzwa. Macho yake yalikuwa ya hila, madanganyifu, yalionesha kuwa na akili nyingi. Mwili wake ulikuwa mkubwa ila nyama zilining'inia kuzunguka mikono na uso wake. Nilipokuwa namtazama, kidevu chake kilikuwa kikiegemea mkono wake wa kushoto. Naye alionekana kuwa katika mawazo mazito. Tabasamu lilikuwa juu ya uso wake, ambalo lilinifanya nitetemeke, lilikuwa limejaa uovu tele na udanganyifu wa kishetani. Tabasamu hili ni tabasamu lile anakuwa nalo mara tu kabla hajawa na uhakika wa kujipatia mhanga wake, na pale anapomfunga mhanga huyo katika

mtego wake tabasamu hili linageuka kuwa la kutisha.**{EW 152.3}**

## Sura ya 34 -Kuja kwa Kristo Mara ya Kwanza

Nilichukuliwa hadi wakati ambapo Yesu angechukua juu Yake mwenyewe asili ya mwanadamu, kujinyenyekesha kama mwanadamu, na kupitia majaribu ya Shetani.**{EW 153.1}**

Kuzaliwa Kwake hakukuwa na fahari yoyote ya kidunia. Alizaliwa katika zizi na kulazwa katika hori la ng'ombe; lakini bado kuzaliwa Kwake kuliheshimiwa zaidi mno kuliko wa mwana yeyote wa wanadamu. Malaika kutoka mbinguni waliwajulisha wachungaji juu ya ujio wa Yesu, na nuru na utukufu kutoka kwa Mungu viliandamana na ushuhuda wao. Jeshi la mbinguni liligusa vinubi vyao na kumtukuza Mungu. Walitangaza kwa shangwe ujio wa Mwana wa Mungu katika ulimwengu ulioanguka ili kukamilisha kazi ya ukombozi, na kwa kifo Chake kuleta amani, furaha, na uzima wa milele kwa mwanadamu. Mungu aliheshimu ujio wa Mwana Wake. Malaika walimwabudu.**{EW 153.2}**

Malaika wa Mungu walizungukazunguka juu ya

eneo la ubatizo Wake; Roho Mtakatifu alishuka katika mfano wa njiwa na kumulika juu yake, na watu waliposimama wakishangaa sana, na macho yao yakiwa yamekazwa Kwake, sauti ya Baba ilisikika kutoka mbinguni, ikisema, Huyu ni Mwanangu, mpendwa Wangu, ninayependezwa Naye.**{EW 153.3}**

Yohana hakuwa na hakika kwamba ni Mwokozi aliyekuja kubatizwa naye katika Yordani. Lakini Mungu alikuwa amemwahidi ishara ambayo kwayo angemjua Mwanakondoo wa Mungu. Ishara hiyo ilitolewa pale hua wa mbinguni alipotulia juu ya Yesu, na utukufu wa Mungu kung'aa kumzunguka. Ndipo Yohana akanyosha mkono wake, akielekeza kwa Yesu, na kusema, kwa sauti kuu, "Tazama, Mwana-Kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu!" **{EW 153.4}**

Yohana aliwajulisha wanafunzi wake kwamba Yesu Ndiye alikuwa Masihi aliyeahidiwa, Mwokozi wa ulimwengu. Kazi yake ilipokuwa inafungwa, aliwafundisha wanafunzi wake kumtazama Yesu, na kumfuata kama Mwalimu Mkuu. Maisha ya Yohana yalikuwa ya kusikitisha na ya kujinyima. Alitangaza ujio wa kwanza wa Kristo, lakini hakuruhusiwa kushuhudia miujiza Yake, na

kufurahia nguvu iliyodhihirishwa Naye. Wakati Yesu alipopaswa kujiweka kama mwalimu, Yohana alijua kwamba yeye mwenyewe ilikuwa ni lazima afe. Sauti yake ilisikika mara chache, isipokuwa jangwani. Maisha yake yalikuwa ni ya upweke. Hakushikamana na familia ya baba yake, ili kufurahia mfumo wa jamii yao, bali aliwaacha ili apate kutimiza wito wake. Umati wa watu uliondoka katika miji na vijiji vyenye shughuli nyingi na kumiminika jangwani ili wapate kuyasikia maneno ya nabii huyo wa ajabu. Yohana aliweka shoka kwenye shina la mti. Alikemea dhambi, bila kuhofia matokeo yake, na kuandaa njia kwa ajili ya Mwana-Kondoo wa Mungu.**{EW 154.1}**

Herode aliguswa aliposikia shuhuda za Yohana zenye nguvu, za wazi, na kwa shauku kubwa aliuliza ni nini angepaswa kufanya ili apate kuwa mwanafunzi wake. Yohana alijua Ukweli kwamba alikuwa anakaribia kumwoa mke wa kaka yake, wakati mumewe alikuwa bado anaishi, na kwa uaminifu alimwambia Herode kwamba hii haikuwa halali. Herode hakuwa radhi kutoa kafara yoyote. Alimwoa mke wa kaka yake, na kupitia ushawishi wa mke huyu, alimkamata Yohana na kumtia gerezani, akikusudia hata hivyo kumwachilia.

Alipokuwa huko amefungwa, Yohana alisikia kupitia kwa wanafunzi wake juu ya matendo makuu ya Yesu. Hakuweza kuyasikiliza Maneno Yake yenye neema, bali wanafunzi wale walimweleza na kumfariji kwa yale waliyokuwa wameyasikia. Punde Yohana alikatwa kichwa, kupitia kwa ushawishi wa mke wa Herode. Niliona kwamba wanafunzi wanyenyekevu kabisa ambao walimfuata Yesu, wakashuhudia miujiza Yake, na kusikia maneno ya kufariji ambayo yalianguka kutoka katika midomo Yake, walikuwa ni wakuu kuliko Yohana Mbatizaji; yaani, walikuwa wameinuliwa na kuheshimiwa zaidi, na walikuwa na starehe zaidi katika maisha yao.**{EW 154.2}**

Yohana alikuja katika roho na nguvu ya Eliya kutangaza ujio wa kwanza wa Yesu. Nilioneshwa kufikia siku za mwisho na kuona kwamba Yohana aliwawakilisha wale ambao watapaswa kusonga mbele kwa roho na nguvu ya Eliya, kutangaza siku ya ghadhabu na ujio wa pili wa Yesu.**{EW 155.1}**

Baada ya ubatizo wa Yesu katika Yordani, Yeye aliongozwa na Roho kwenda jangwani, apate kujaribiwa na ibilisi. Roho Mtakatifu alikuwa amemwandaa kwa ajili ya tukio hilo maalum la majaribu makali. Kwa muda wa siku arobaini

alijaribiwa na Shetani, na katika siku hizo hakula chochote. Kila kitu kumzunguka hakikuwa cha kupendeza, ambapo asili ya ubinadamu ingeongozwa kurudi nyuma. Alikuwa pamoja na wanyama wa porini na ibilisi, katika mahali pa ukiwa, penye upweke. Mwana wa Mungu alibadilika rangi ya uso na kupauka na kudhoofika, kwa sababu ya kufunga na mateso. Lakini njia Yake ilikuwa dhahiri, na ni lazima Atimize kazi ambayo Alikuja kuifanya.**{EW 155.2}**

Shetani alitumia fursa ya mateso ya Mwana wa Mungu kwa manufaa yake na kujiandaa kumzonga kwa majaribu ya namna nyingi, akitumaini kupata ushindi juu Yake, kwa sababu alikuwa amejinyenyekesha kama mwanadamu. Shetani alikuja na jaribu hili: “Ukiwa Ndiwe Mwana wa Mungu, amuru kwamba mawe haya yawe mikate.” Alimjaribu Yesu kujishusha ili kumpa uthibitisho wa kuwa Masihi, kwa kutumia uweza Wake wa Kiungu. Yesu alimjibu kwa upole, "Imeandikwa, Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila Neno litokalo katika kinywa cha Mungu." **{EW 155.3}**

Shetani alikuwa anatafuta mashindano na Yesu kuhusu kuwa Kwake Mwana wa Mungu. Alirejelea hali Yake dhaifu ya mateso na kwa kujigamba

alitamka kwa dhati kuwa yeye alikuwa na nguvu kuliko Yesu. Lakini Neno lililosemwa kutoka mbinguni, “Huyu ni Mwanangu, mpendwa Wangu, ninayependezwa Naye.” Lilitosha kumchukua Yesu katika mateso Yake yote. Niliona kwamba Kristo hakuwa na chochote cha kufanya katika kumshawishi Shetani juu ya uweza Wake au juu ya kuwa Kwake Mwokozi wa ulimwengu. Shetani alikuwa na ushahidi wa kutosha kuhusu nafasi adhimu na mamlaka ya Mwana wa Mungu. Kutokubali kwake kujisalimisha kwa mamlaka ya Kristo kulimfungia nje ya mbingu.**{EW 155.4}**

Ili apate kudhihirisha nguvu zake, Shetani alimchukua Yesu hadi Yerusalemu, na kumweka juu ya kilele cha hekalu, na huko akamjaribu apate kutoa ushahidi kwamba alikuwa Mwana wa Mungu, kwa kujitupa chini kutoka urefu huo wa kutia kizunguzungu. Shetani alikuja na maneno ya kutoka katika uvuvio wa Maandiko: “Maana imeandikwa, Atakuagizia malaika Zake; Na mikononi mwao watakuchukua; Usije ukajikwaa mguu wako katika jiwe." Yesu akijibu alimwambia, "Tena imeandikwa, Usimjaribu Bwana Mungu wako." Shetani alitaka kumfanya Yesu athubutu kutumia bila ruhusa rehema ya Baba Yake na kuhatarisha maisha Yake

kabla ya utimilizaji wa utume Wake. Alitumaini kwamba mpango wa wokovu ungeshindwa; lakini mpango uliwekwa kwa kina mno kiasi cha kutoweza kuangushwa au kuharibiwa na Shetani.**{EW 156.1}**

Kristo ni mfano kwa Wakristo wote. Pale wanapojaribiwa, au haki zao kubishaniwa, wanapaswa kuyachukulia hayo yote kwa uvumilivu. Hawapaswi kujisikia kwamba wana haki ya kumwita Bwana kuonesha uweza Wake ili waweze kupata ushindi dhidi ya adui zao, isipokuwa pale ambapo Mungu anaweza kuheshimiwa moja kwa moja na kutukuzwa kwa kufanya hivyo. Kama Yesu angejitupa kutoka kwenye kilele cha hekalu, asingemtukuza Baba Yake; kwa kuwa hakuna mtu ambaye angeshuhudia kitendo hicho isipokuwa Shetani na malaika wa Mungu. Na ingekuwa ni kumjaribu Bwana kuonesha uweza Wake kwa adui Yake mbaya kabisa. Ingekuwa ni kujishusha kwa yule ambaye Yesu alikuja kumshinda.**{EW 156.2}**

“Kisha Ibilisi akamchukua mpaka mlima mrefu mno, akamwonyesha milki zote za ulimwengu, na fahari yake, akamwambia, Haya yote nitakupa, ukianguka kunisujudia. Ndipo Yesu alipomwambia, Nenda zako, Shetani; kwa maana imeandikwa, Msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu Yeye

peke yake."**{EW 157.1}**

Shetani aliwasilisha mbele ya Yesu falme za ulimwengu katika nuru ya kuvutia mno. Kama pale Yesu angemwabudu, aliahidi kwamba angeachilia madai ya umiliki wa dunia. Ikiwa mpango wa wokovu ungepaswa kutekelezwa, na Yesu anapaswa kufa ili kumkomboa mwanadamu, Shetani alijua kwamba nguvu zake mwenyewe ni lazima ziwe na mipaka na hatimaye kuondolewa, na kwamba angeangamizwa. Kwa hiyo ulikuwa ni mpango wake uliodhamiriwa ili kuzuia, kama ingewezekana, ukamilishaji wa kazi ile kubwa ambayo ilikuwa imeanzishwa na Mwana wa Mungu. Kama mpango wa ukombozi wa mwanadamu ungeshindwa, Shetani angebaki na ufalme ambao wakati huo alidai kuwa ni wake. Na kama angefanikiwa, alijidanganya mwenyewe kwamba angetawala kwa kumpinga Mungu wa mbinguni. **{EW 157.2}**

Shetani alifurahi sana wakati Yesu alipoweka kando uweza na utukufu Wake na kuondoka mbinguni. Alidhani kuwa Mwana wa Mungu hapo alikuwa amewekwa chini ya uwezo wake. Jaribu lilifanyika kwa urahisi mno kwa wenzi wale watakatifu katika Edeni kiasi kwamba alitumaini

kwa nguvu zake za kishetani na hila kumwangusha hata Mwana wa Mungu, na hivyo kuokoa maisha yake mwenyewe na ufalme wake. Kama angeweza kumjaribu Yesu kuondoke katika mapenzi ya Baba Yake, lengo lake lingepatikana. Lakini Yesu alimkabili na mjaribu na kemeo, "Nenda nyuma yangu, Shetani." Alipaswa kumsujudia Baba Yake peke Yake. Shetani alidai ufalme wa dunia kuwa ni wake na akadokeza kwa Yesu kwamba mateso yake yote yangeweza kuachiliwa: kwamba si lazima afe ili kuupata ufalme wa ulimwengu huu; kama angemwabudu angeweza kuwa na mali yote ya dunia na utukufu wa kuwatawala. Lakini Yesu alikuwa thabiti. Alijua kwamba wakati ungekuja ambapo Angeweza kwa maisha Yake mwenyewe kuukomboa ufalme kutoka kwa Shetani, na kwamba, baada ya kipindi, wote mbinguni na duniani wangejiweka chini Yake. Yeye Alichagua maisha Yake ya mateso na kifo Chake cha kuogofya, kama njia iliyowekwa na Baba Yake ili aweze kuwa mrithi halali wa falme za dunia na kufanya zikabidhiwe mikononi Mwake kama milki ya milele. Shetani naye atakabidhiwa mikononi Mwake ili apate kuangamizwa kwa kifo, asiweze tena kamwe kumuudhi Yesu au watakatifu walio katika

utukufu.**{EW 157.3}**

## Sura ya 35-Huduma ya Kristo

Baada ya Shetani kumaliza majaribu yake, alimwacha Yesu kwa muda, na malaika wakamwandalia chakula jangwani, na kumtia nguvu, na baraka za Baba Yake zilitulia juu Yake. Shetani alikuwa ameshindwa katika majaribu yake makali kabisa; lakini bado alitazamia kipindi cha huduma ya Yesu, wakati ambapo kwa nyakati mbalimbali angejaribu werevu wake dhidi Yake. Bado alitarajia kumshinda kwa kuwachochea wale ambao hawangempokea Yesu, kumchukia na kujitahidi kumwangamiza. Shetani alifanya mkutano maalum pamoja na malaika zake. Walivunjika moyo na kukasirika kwamba hawakuweza chochote dhidi ya Mwana wa Mungu. Waliamua kwamba ni lazima wawe werevu kwa hila zaidi na kutumia uwezo wao kwa kiwango cha juu kabisa kuchochea kutokuamini katika akili za taifa Lake Mwenyewe kuhusu Yeye kuwa Mwokozi wa ulimwengu, na kwa njia hii kumkatisha Yesu tamaa katika utume Wake. Haidhuru Wayahudi watakuwa sahihi kiasi gani katika maadhimisho na kafara zao, kama

wangezuiwa kuutambua unabii na kufanywa kuamini kwamba Masihi alipaswa kutokea kama mfalme wa ulimwengu Mwenye nguvu, wangeweza kuongozwa kumdharau na kumkataa Yesu.**{EW 158.1}**

Nilioneshwa kwamba Shetani na malaika zake walikuwa na shughuli nyingi sana wakati wa huduma ya Kristo, wakiwatia watu moyo wa kutokuamini, chuki, na dharau. Mara nyingi Yesu alipotamka Ukweli unaochoma, akikemea dhambi zao, watu wangekasirika. Shetani na malaika zake waliwasukuma wapate kuyaondoa maisha ya Mwana wa Mungu. Zaidi ya mara moja walichukua mawe ili wapate kumponda, lakini malaika walimlinda na kumchukua kutoka katika umati wenye hasira hadi mahali penye usalama. Tena, Ukweli dhahiri ulipokuwa ukidondoka kutoka kwenye midomo Yake mitakatifu, umati wa watu walimshika na kumwongoza kwenye ukingo wa mteremko mkali wa mlima, wakikusudia kumtupa chini. Mashindano yakainuka miongoni mwao wenyewe kuhusu nini walipaswa kumtendea, wakati ambapo tena malaika walimficha asionekane na watu, Naye, akipita katikati yao, akaenda Zake.**{EW 159.1}**

Shetani bado alikuwa na tumaini kwamba mpango mkuu wa wokovu ungeshindwa. Alitumia nguvu zake zote kufanya mioyo ya watu kuwa migumu na hisia zao kuwa chungu dhidi ya Yesu. Alitumaini kwamba ni wachache sana wangempokea kama Mwana wa Mungu kiasi kwamba angeona kuwa mateso na kafara Yake ni kubwa mno kuweza kutolewa kwa ajili ya kundi dogo kiasi kile. Lakini niliona kwamba kama wangekuwepo watu wawili tu ambao wangemkubali Yesu kama Mwana wa Mungu na kumwamini kwa ajili ya kuokoa roho zao, Yeye angeutekeleza mpango huo.**{EW 159.2}**

Yesu alianza kazi Yake kwa kuvunja nguvu za Shetani juu ya mateso. Aliwarejesha wagonjwa katika afya, akawapa vipofu kuona, na kuwaponya vilema, na kuwafanya kurukaruka kwa furaha na kumtukuza Mungu. Aliwarejeshea afya wale waliokuwa dhaifu na waliofungwa na nguvu za kikatili za Shetani kwa miaka mingi. Kwa Maneno ya neema aliwafariji walio dhaifu, wanaotetemeka, na waliokata tamaa. Wale wanyonge, wanaoteseka ambao Shetani aliwashikilia kwa ushindi, Yesu aliwavuta kwa ghafla kutoka katika kuwashika kwake Shetani kwa nguvu, akiwaletea utimamu wa

mwili na shangwe kuu na furaha. Aliwafufua wafu kuwa wazima, nao walimtukuza Mungu kwa ajili ya udhihirisho mkuu wa uweza Wake. Alitenda kwa nguvu nyingi sana kwa ajili ya wote waliomwamini.**{EW 159.3}**

Maisha ya Kristo yalijaa Maneno na matendo ya ukarimu, huruma, na upendo. Alikuwa makini kila wakati kusikiliza na kupunguza shida za wale waliomjia. Watu wengi sana walibeba katika nafsi zao uthibitisho wa uweza Wake wa Kiungu. Lakini bado baada ya kazi hiyo kuwa imetimizwa, wengi walimwonea aibu Mwalimu mnyenyekevu lakini mwenye nguvu. Kwa sababu watawala hawakumwamini, watu hawakuwa tayari kumkubali Yesu. Alikuwa ni Mtu wa huzuni nyingi, ajuaye sikitiko. Hawakuweza kuvumilia kutawaliwa na maisha Yake ya kiasi, yna a kujikana nafsi. Walitaka kufurahia heshima ambayo ulimwengu uliitoa. Lakini bado wengi walimfuata Mwana wa Mungu na kuyasikiliza mafundisho Yake, wakila Maneno ambayo yalianguka kwa neema kubwa kutoka katika midomo Yake na kuyasherekea kama karamu. Maneno Yake yalijaa maana nzito, lakini yalikuwa wazi mno kiasi kwamba wale walio dhaifu kabisa waliweza kuyaelewa.**{EW 160.1}**

Shetani na malaika zake walipofusha macho na kutia giza ufahamu wa Wayahudi, na kuwachochea wakuu wa watu na watawala wapate kuyaondoa maisha ya Mwokozi. Wengine walitumwa wapate kumleta Yesu kwao; lakini walipokaribia mahali alipokuwa, walishangazwa sana. Walimwona akiwa amejawa na upole na huruma, pale alipoyashuhudia majonzi ya wanadamu. Walimsikia kwa upendo na upole akisema kwa kuwatia moyo wanyonge na wale waliokuwa katika mateso. Pia walimsikia kwa sauti yenye mamlaka, akiikemea nguvu ya Shetani na kuwaambia mateka wake kwenda wakiwa huru. Waliyasikia Naneno ya hekima ambayo yalitoka midomoni Mwake, nao walivutiwa na kutekewa nayo; hawakuweza kuweka mikono yao juu Yake. Walirudi kwa makuhani na wazee pasipo kuwa na Yesu. Walipoulizwa, “Kwa nini hamjamleta?” walisimulia kile walichokishuhudia katika miujiza Yake, na Maneno matakatifu ya hekima, upendo, na maarifa waliyoyasikia, na kuishia kwa kusema, "Hajanena kamwe mtu yeyote kama Huyu anavyonena." Makuhani wakuu waliwashutumu kwamba wao pia walikuwa wamedanganywa, na baadhi ya askari waliona aibu kwa sababu hawakuwa wamemchukua. Makuhani waliuliza kwa

namna ya dharau ikiwa kuna yeyote kati ya watawala aliyemwamini. Niliona kwamba wanasheria na wazee wengi walimwamini Yesu; lakini Shetani aliwazuia wasikiri hivyo; waliogopa shutuma za watu kuliko walivyomwogopa Mungu.**{EW 160.2}**

Kufikia hapo werevu na chuki ya Shetani havikuwa vimeuvunja mpango wa wokovu. Wakati wa kutimilizwa kwa kusudi ambalo kwalo Yesu alikuja ulimwenguni ulikuwa unakaribia. Shetani na malaika zake walishauriana pamoja na kuamua kulichochea taifa la Kristo Mwenyewe, kulilia kwa shauku damu Yake na kurundika juu Yake ukatili na dharau. Walitumaini kwamba Yesu angechukia kutendewa hivyo na kuacha kudumisha unyenyekevu na upole Wake.**{EW 161.1}**

Wakati Shetani alipokuwa akiweka mipango yake, Yesu alikuwa akiwafungulia wanafunzi Wake kwa uangalifu mateso ambayo ni lazima ayapitie—kwamba angesulubiwa na kwamba angefufuka siku ya tatu. Lakini ufahamu wao ulionekana kuwa mzito, na hawakuweza kuyaelewa yale aliyowaambia.**{EW 161.2}**

## Sura ya 36 -Kubadilika Sura (Mng’ao mlimani - Transfiguration)

Imani ya wanafunzi iliimarishwa sana wakati wa kubadilika sura kwa Yesu, waliporuhusiwa kuutazama utukufu wa Kristo na kusikia sauti kutoka mbinguni ikiishuhudia asili Yake ya Kiungu. Mungu alichagua kuwapa wafuasi wa Yesu uthibitisho thabiti kwamba alikuwa Ndiye Masihi aliyeahidiwa, kiasi kwamba katika huzuni yao kali na kukatishwa tamaa wakati wa kusulubiwa kwake, hawakuweza kuachilia kabisa ujasiri na imani yao. Wakati wa kubadilika sura Bwana alimtuma Musa na Eliya kuzungumza na Yesu kuhusu mateso na kifo Chake. Badala ya kuchagua malaika kuzungumza na Mwanawe, Mungu aliwachagua wale ambao wao wenyewe walikuwa wameyapata majaribu ya dunia.**{EW 162.1}**

Eliya alikuwa ametembea pamoja na Mungu. Kazi yake ilikuwa ni ya maumivu na yenye majaribu, kwa kuwa Bwana kwa kupitia kwake alizikemea dhambi za Israeli. Eliya alikuwa ni nabii wa Mungu; lakini alilazimika kukimbia kutoka mahali hadi mahali ili kuyaokoa maisha yake. Taifa lake mwenyewe lilimwinda kama mnyama wa mwitu ili wapate kumwangamiza. Lakini Mungu alimhamisha

Eliya mbinguni. Malaika walimchukua katika utukufu na ushindi kwenda mbinguni. **{EW 162.2}**

Musa alikuwa ni mkuu kuliko yeyote aliyewahi kuishi kabla yake. Aliheshimiwa sana na Mungu, akipewa upendeleo wa kuzungumza na Bwana uso kwa uso, kama mtu anavyozungumza na rafiki yake. Aliruhusiwa kuona nuru angavu na utukufu bora ambao ulimfunika Baba. Kupitia kwa Musa, Bwana aliwaokoa watoto wa Israeli kutoka katika utumwa wa Misri. Musa alikuwa ni mwombezi na mtetezi wa watu wake, ambaye mara nyingi alisimama kati yao na ghadhabu ya Mungu. Wakati hasira ya Bwana ilipowaka sana dhidi ya Israeli kwa sababu ya kutokuamini kwao, manung'uniko yao, na dhambi zao mbaya, upendo wa Musa kwao ulipimwa. Mungu alipendekeza apate kuwaangamiza na apate kutengeneza taifa lenye nguvu kupitia kwake. Musa alionesha upendo wake kwa Israeli kwa kusihi kwake kwa bidii kwa niaba yao. Katika dhiki yake alimwomba Mungu ageuke kutoka katika hasira Yake kali na awasamehe Israeli, au afute jina lake kutoka katika kitabu Chake. **{EW 162.3}**

Pale Waisraeli waliponung’unika dhidi ya Mungu na dhidi yake kwa sababu hawakuweza kupata maji, walimshutumu kwa kuwaongoza ili apate kuwaua

wao pamoja na watoto wao. Mungu aliyasikia manung'uniko yao na kumwambia Musa aseme na mwamba, ili watu wapate maji. Musa aliupiga mwamba kwa hasira na kujichukulia utukufu kwake mwenyewe. Ukaidi endelevu na manung'uniko ya wana wa Israeli yalimsababishia huzuni kubwa mno, na kwa kipindi kifupi alisahau jinsi gani Bwana alivyokuwa amechukuliana nao, na kwamba manung'uniko yao hayakuwa dhidi yake, bali dhidi ya Mungu. Alijifikiria yeye peke yake jinsi alivyokosewa sana, na ni shukrani ndogo kiasi gani walionesha kama jibu kwa upendo wake wa kina kwao.**{EW 163.1}**

Ulikuwa ni mpango wa Mungu kuwaongoza watu Wake mara kwa mara kwenda mahali penye dhiki, na kisha katika uhitaji wao kuwaokoa kwa uweza Wake, ili waweze kutambua upendo na ulinzi Wake kwao, na hivyo waongozwe katika kumtumikia na kumheshimu Yeye. Lakini Musa alishindwa kumheshimu Mungu na kulitukuza Jina Lake mbele ya watu ili wapate Kumtukuza. Kwa kulitenda hili alileta chuki ya Bwana juu yake yeye mwenyewe.**{EW 163.2}**

Wakati Musa aliposhuka kutoka juu ya mlima akiwa na mbao mbili za mawe na kuwaona Israeli

wakimwabudu ndama wa dhahabu, hasira yake iliwaka sana, na alizitupa chini mbao zile za mawe na kuzivunja. Niliona kuwa Musa hakutenda dhambi katika hili. Alighadhabika kwa ajili ya Mungu, mwenye wivu kwa ajili ya utukufu Wake. Lakini pale aliposalimu amri kwa hisia za kawaida za moyo wake na kujichukulia heshima ambayo ilikuwa ni ya Mungu, alitenda dhambi, kwa sababu ya dhambi ile Mungu hangeweza kumruhusu kuingia katika nchi ya Kanaani.**{EW 163.3}**

Shetani alikuwa akijaribu kupata kitu fulani ambacho kwacho angeweza kumshitaki Musa mbele ya malaika. Alifurahia sana mafanikio yake katika kumwongoza kumchukiza Mungu, na aliwaambia malaika wale kwamba yeye angeweza kumwangusha Mwokozi wa ulimwengu atakapokuja kwa ajili ya kumkomboa mwandamu. Kwa sababu ya dhambi yake, Musa aliingia chini ya nguvu za Shetani—ufalme wa mauti. Kama angelidumu kuwa imara, Bwana angelimfikisha katika Nchi ya Ahadi, na kisha angeweza kumhamisha kwenda mbinguni pasipo kuona mauti.**{EW 164.1}**

Musa alipitia mauti, lakini Mikaeli alikuja chini na kumpa uhai kabla mwili wake haujapata uharibifu.

Shetani alijaribu kuushikilia mwili huu, akidai kuwa ni wake; lakini Mikaeli alimfufua Musa na kumchukua kwenda mbinguni. Shetani alimlaumu Mungu kwa uchungu, akimshutumu kutokuwa mwenye haki kwa kuruhusu windo lake kuchukuliwa kutoka kwake; lakini Kristo hakumkemea adui yake, ingawa ilikuwa ni kwa kupitia majaribu yake ndipo ambapo mtumishi huyu wa Mungu alianguka. Kwa upole alimpeleka kwa Baba, akisema, "Bwana na akukemee." **{EW 164.2}**

Yesu alikuwa amewaambia wanafunzi Wake kwamba kulikuwa na baadhi waliosimama pamoja na Yeye ambao wasingeonja mauti hadi pale watakapouona ufalme wa Mungu ukija kwa nguvu. Katika kubadilika sura kwa Yesu pale mlimani, ahadi hii ilitimizwa. Uso wa Yesu pale ulibadilishwa na kuangaza kama jua. Vazi lake lilikuwa jeupe na lenye kumetameta. Musa alikuwapo ili kuwawakilisha wale ambao watafufuliwa kutoka katika mauti Yesu atakapotokea mara ya pili. Na Eliya, ambaye alihamishwa pasipo kuona mauti, aliwawakilisha wale ambao watabadilishwa na kuingia katika hali ya kutokufa katika ujio wa pili wa Kristo na kuchukuliwa kwenda mbinguni pasipo kuona mauti. Wanafunzi wale walitazama kwa

mshangao na hofu utukufu bora sana wa Yesu na wingu lile lililowafunika, na kusikia sauti ya Mungu katika ukuu wa kuogofya, ikisema, “Huyu ni Mwanangu, mpendwa Wangu, msikieni Yeye.” **{EW 164.3}**

## Sura ya 37 -Kusalitiwa kwa Kristo

Nilichukuliwa hadi wakati ambapo Yesu alikula chakula cha Pasaka pamoja na wanafunzi Wake. Shetani alikuwa amemdanganya Yuda na kumwongoza kufikiri kwamba alikuwa mmoja wa wanafunzi wa kweli wa Kristo; lakini moyo wake siku zote ulikuwa ni wa tamaa za kimwili. Alikuwa ameona matendo makuu ya Yesu, alikuwa pamoja Naye katika huduma Yake, na kuukubali ushahidi wenye nguvu nyingi kwamba alikuwa Ndiye Masihi; lakini Yuda alikuwa ni bahili, msiri na mwenye tamaa (close); alipenda fedha. Alilalamika kwa hasira juu ya manukato ya gharama kubwa yaliyomiminwa kwa Yesu. Mariamu alimpenda Bwana wake. Alikuwa amemsamehe dhambi zake, ambazo zilikuwa nyingi, na alikuwa amemfufua kaka yake aliyempenda sana kutoka kwa wafu, na alihisi kuwa hakuna kitu kilichokuwa na thamani

nyingi kiasi cha kukizuia kutolewa kwa Yesu. Kadiri ambavyo marhamu ingekuwa ya thamani zaidi, ndivyo angeweza kutoa shukrani zake kwa Mwokozi wake kwa kuitoa Kwake. Yuda, kama udhuru kwa tamaa yake, alipendekeza kwamba marhamu hayo yangeuzwa na kutolewa kwa maskini. Lakini haikuwa kwa sababu alikuwa anajali hata kidogo kuhusu watu maskini; kwani alikuwa mtu mbinafsi, na mara nyingi alijitwalia kwa ajili ya matumizi yake mwenyewe kile ambacho alikabidhiwa kusimamia kwa ajili ya maskini. Yuda hakuwa msikivu kwa faraja na hata mahitaji ya Yesu, na kwa kujipa udhuru wa tamaa yake mara nyingi aliwataja maskini. Kitendo hiki cha ukarimu kwa upande wa Mariamu kilikuwa karipio kali sana kwa tabia yake ya tamaa. Njia ilitayarishwa kwa ajili ya majaribu ya Shetani kupata mapokezi mazuri katika moyo wa Yuda.**{EW 165.1}**

Makuhani na watawala wa Kiyahudi walimchukia Yesu; lakini umati wa watu ulisongamana kusikiliza maneno Yake ya hekima na kushuhudia matendo Yake makuu. Watu walichochewa na shauku kubwa na walimfuata Yesu kwa shauku kusikia mafundisho ya mwalimu huyu wa ajabu. Wengi wa watawala walimwamini, lakini hawakuthubutu kukiri

imani yao, ili wasije wakatengwa na sinagogi. Makuhani na wazee waliamua kwamba kitu fulani ni lazima kifanyike ili kuvuta usikivu wa watu kutoka kwa Yesu. Waliogopa kwamba watu wote wangemwamini Yeye. Wasingeona usalama kwa ajili yao wenyewe. Ni lazima wapoteze nafasi zao au wamuue Yesu. Na baada ya kumuua, bado wangekuwapo wale ambao walikuwa ni kumbukumbu hai ya uweza Wake. Yesu alimfufua Lazaro kutoka kwa wafu, nao walihofu kwamba iwapo wangemuua Yesu, Lazaro angeshuhudia kuhusu uweza Wake mkuu. Watu walikuwa wanamiminika kwenda kumwona yeye aliyefufuliwa kutoka kwa wafu, na watawala walidhamiria kumuua Lazaro pia, na kuzima msisimko ule. Ndipo wangeweza kuwageuza watu kwenda katika mapokeo na mafundisho ya wanadamu, kutoa zaka ya mnanaa na bizari na jira, na tena kuwa na mvuto juu yao. Walikubaliana kumchukua Yesu wakati akiwa peke yake; kwa sababu kama wangejaribu kumchukua kutoka kwa watu, wakati akili za watu hao wote zilivutiwa kabisa na Yeye, wangepigwa kwa mawe.**{EW 165.2}**

Yuda alijua jinsi walivyokuwa na shauku ya kumpata Yesu naye alijitolea kumsaliti kwa

makuhani wakuu na wazee kwa vipande vichache vya fedha. Kupenda kwake fedha kulimfanya akubali kumsaliti Bwana wake mikononi mwa maadui zake wabaya kabisa. Shetani alikuwa akifanya kazi moja kwa moja kupitia kwa Yuda, na katikati ya mandhari ya kuvutia ya karamu ya mwisho, msaliti huyu alikuwa akifanya mipango ya kumsaliti Bwana wake. Yesu aliwaambia wanafunzi Wake kwa huzuni kwamba wote wangechukizwa kwa sababu Yake usiku huo. Lakini Petro kwa shauku alithibitisha kwamba ingawa wengine wote wangechukizwa kwa sababu Yake, yeye asingechukizwa kwa ajili Yake. Yesu alimwambia Petro: “Shetani amewataka ninyi apate kuwapepeta kama vile ngano; lakini nimekuombea wewe, ili imani yako isitindike; nawe utakapoongoka, waimarishe ndugu zako.” (Luka 22: 31-32) **{EW 166.1}**

Nilimwona Yesu bustanini akiwa pamoja na wanafunzi Wake. Kwa huzuni kubwa aliwaambia wakeshe na kuomba, wasije wakaingia majaribuni. Alijua kwamba imani yao ingepaswa kuwekwa katika jaribu, na kutindikiwa, na matumaini yao kukatishwa tamaa, na kwamba wangehitaji nguvu zote ambazo wangeweza kupata kwa kukesha kwa

karibu na kuomba kwa bidii. Kwa kulia kaw uchungu na kuomboleza sana Yesu aliomba, “Ee Baba, ikiwa ni mapenzi Yako, uniondolee kikombe hiki; walakini si mapenzi Yangu, bali Yako yatendeke.” Mwana wa Mungu aliomba kwa maumivu makali. Matone makubwa ya damu yalikusanyika juu ya uso Wake na kuanguka chini. Malaika walikuwa wakizungukazunguka juu ya mahali hapo, wakishuhudia tukio hilo, lakini ni mmoja tu aliyeagizwa kwenda kumtia nguvu Mwana wa Mungu katika maumivu Yake makali. Hakukuwa na furaha mbinguni. Malaika walitupa taji zao na vinubi kutoka kwao na kwa shauku ya kina kabisa, kwa kimya walimwangalia Yesu. Walitamani kumzunguka Mwana wa Mungu, lakini malaika viongozi hawakuwaruhusu kufanya hivyo, isije, watakapoona kusalitiwa Kwake, wakamwokoa; kwa sababu mpango ulikuwa umewekwa, na ni lazima utimizwe. **{EW 167.1}**

Baada ya Yesu kuomba, alikuja kwa wanafunzi Wake; lakini walikuwa wamelala. Katika saa hiyo ya kutisha, Yeye hakupata huruma na maombi hata ya wanafunzi Wake. Petro, ambaye alikuwa na ari sana muda mfupi uliopita, alikuwa mzito kwa usingizi. Yesu alimkumbusha juu ya tamko lake dhahiri na

kumwambia, “ Je! Hamkuweza kukesha pamoja Nami hata saa moja?” Mara tatu Mwana wa Mungu aliomba kwa maumivu makali. Ndipo Alijitokeza, akiwa na genge lake la watu wenye silaha. Alimsogelea Bwana wake kama kawaida, ili apate kumsalimu. Kikosi kile kikamzunguka Yesu; lakini pale alionesha uweza wake wa kiungu, aliposema, “Ni nani mnayemtafuta?" "Ni mimi." Walirudi nyuma na kuanguka chini. Yesu aliuliza swali hili ili waweze kushuhudia nguvu Zake na kuwa na ushahidi kwamba angeweza kujiokoa mikononi mwao kama angependa.**{EW 167.2}**

Wanafunzi walianza kuwa na tumaini walipoona umati wakiwa na fimbo zao na panga wakianguka chini haraka kiasi kile. Waliposimama na kumzunguka tena Mwana wa Mungu, Petro aliuchomoa upanga wake, na akampiga mtumishi wa kuhani mkuu, na kumkata sikio. Yesu akamwambia arudishe upanga wake mahali pake, akisema, "Ama wadhani ya kuwa Mimi siwezi kumsihi Baba yangu, Naye ataniletea sasa hivi zaidi ya majeshi kumi na mawili ya malaika?" Niliona kwamba maneno haya yalipokuwa yakisemwa, nyuso za malaika zilihuishwa na tumaini. Walitamani hapo hapo kumzingira Kamanda wao na kulipukutisha lile genge la watu wenye hasira kali. Lakini huzuni iligubila tena mioyo yao, wakati Yesu alipoongeza Maneno haya, "Lakini yatatimizwaje

basi Maandiko ya kwamba ndivyo inavyopaswa kuwa?" Mioyo ya wanafunzi pia ilizama kwa kukata tamaa na kuvunjika moyo kwa uchungu, wakati Yesu alipowaruhusu Mwenyewe maadui Zake, kumchukua.**{EW 167.3}**

Wanafunzi walihofia maisha yao wenyewe, na wote walimtelekeza na kukimbia. Yesu aliachwa peke yake mikononi mwa kundi la wauaji. Lo, ni ushindi ulioje Shetani alikuwa amejipatia, wakati ule! Na ni sikitiko na huzuni iliyoje kwa malaika wa Mungu! Makundi mengi ya malaika watakatifu, kila moja likiwa na malaika mrefu mwenye kuamrisha kama kiongozi wao, walitumwa kushuhudia tukio hilo. Walipaswa kurekodi kila tusi, dhihaka na ukatili uliowekwa juu ya Mwana wa Mungu, na kuandika kila mchomo wa uchungu ambao Yesu angepaswa kuupitia; kwa maana watu wale wale waliojiunga katika tukio hili la kutisha watapaswa kuliona tena lote kwa uthibitisho ulio hai.**{EW 168.1}**

## Sura ya 38-Kushtakiwa kwa Kristo

Malaika walipokuwa wakitoka mbinguni, kwa huzuni walivua taji zao zinazong’aa. Hawakuweza kuzivaa wakati Kamanda wao alikuwa akiteseka na

alikuwa avalishwe taji la miiba. Shetani na malaika zake walikuwa wakishughulika sana katika ukumbi wa hukumu kuharibu hisia na huruma za kibinadamu. Angahewa yenyewe ilikuwa nzito na kuchafuliwa na ushawishi wao. Makuhani wakuu na wazee walichochewa nao kumtukana na kumtendea Yesu vibaya kwa namna ambayo ni vigumu kabisa kwa asili ya mwanadamu kubeba. Shetani alitarajia kwamba dhihaka na vurugu kama hizo zingeleta kutoka kwa Mwana wa Mungu malalamiko au manung'uniko fulani; au kwamba angeweza kudhihirisha nguvu Zake za kiungu, na kujiondoa mwenyewe kutoka katika mikono ya umati, na kwamba kwa kufanya hivyo, mpango wa wokovu mwishowe ungeweza kushindwa.**{EW 169.1}**

Petro alimfuata Bwana wake baada ya kusalitiwa Kwake. Alikuwa na shauku ya kuona ni nini kitafanywa kwa Yesu. Lakini aliposhutumiwa kuwa mmoja wa wanafunzi Wake, hofu ya usalama wake vilimwongoza kutangaza kwamba hakumjua mtu huyo. Wanafunzi walijulikana kwa usafi wa lugha yao, na Petro, ili kuwathibibishia washtaki wake kwamba hakuwa mmoja wa wanafunzi wa Kristo, alilikataa shtaka hilo mara ya tatu kwa kulaani na

kuapa. Yesu, ambaye alikuwa umbali fulani kutoka kwa Petro, aligeuka na kumkazia macho ya huzuni yenye kukemea. Kisha mwanafunzi huyu alikumbuka Maneno ambayo Yesu alikuwa amemwambia kule katika chumba cha juu, na pia dai lake mwenyewe lenye usongo "Wajapochukizwa wote kwa ajili Yako, mimi sitachukizwa kamwe." Alikuwa amemkana Bwana wake, hata kwa kulaani na kuapa; lakini sura ile ya Yesu iliyeyusha moyo wa Petro na kumwokoa. Alilia kwa uchungu na kutubu dhambi yake kubwa, naye aliongoka, na kisha alikuwa tayari kuwaimarisha ndugu zake.**{EW 170.1}**

Umati ulikuwa unapiga kelele kwa ajili ya damu ya Yesu. Walimpiga mijeledi kwa ukatili, na kuweka juu yake vazi la zamani la zambarau la kifalme, na kufunga kichwa Chake kitakatifu na taji ya miiba. Wakaweka mwanzi mkononi Mwake, na kuinama mbele Yake, na kwa dhihaka kumsalimu, “Salamu Mfalme wa Wayahudi!” Kisha wakauchukua mwanzi kutoka mkononi Mwake na kumpiga nao kichwani, na kusababisha miiba kupenya katika paji la uso Wake, na kusababisha damu kutiririka chini ya uso Wake na ndevu.**{EW 170.1}**

Ilikuwa ni vigumu kwa malaika kuvumilia kuona mandhari ile. Wangeweza kumwokoa Yesu, lakini

malaika walioongoza waliwazuia kufanya hivyo, wakisema kwamba ilikuwa ni fidia kubwa iliyopaswa kulipwa kwa ajili ya mwanadamu; lakini ilikuwa ni lazima ikamilike nayo ingesababisha kifo Chake Yeye aliyekuwa na uwezo juu ya kifo. Yesu alijua kwamba malaika walikuwa wakishuhudia tukio la udhalilishaji Wake. Malaika dhaifu kuliko wote angeweza kuusababisha umati ule wenye kudhihaki kuanguka na kukosa nguvu na angeweza kumwokoa Yesu. Alijua kwamba ikiwa angetaka kutoka kwa Baba Yake, malaika wangelimwokoa mara moja. Lakini ilikuwa ni lazima kwamba ateseke kwa ukatili wa watu waovu, ili apate kuutekeleza mpango wa wokovu.**{EW 170.2}**

Yesu alisimama akiwa mpole na mnyenyekevu mbele ya umati uliokasirika, huku wakimtolea matusi mabaya na unyanyasaji wa kutisha. Walitema mate usoni Pake—uso ule ambao siku moja watatamani kujificha wasiuone, ambao utatoa nuru katika mji wa Mungu na kuangaza kwa nuru zaidi ya jua. Kristo hakuwatazama wale wakosaji kwa hasira. Walifunika kichwa Chake kwa vazi la zamani, wakamfunga macho, na kisha wakampiga usoni, na kupaza sauti, "Tabiri, ni nani aliyekupiga?" Kulikuwa na vurugu miongoni mwa malaika.

Wangeliweza kumwokoa mara moja, lakini malaika waliokuwa viongozi wao waliwazuia.**{EW 170.2}**

Baadhi ya wanafunzi walipata ujasiri wa kuingia mahali Yesu alipokuwa na kushuhudia hukumu Yake. Walitarajia kwamba angeweza kudhihirisha nguvu zake za Kiungu, na kujiokoa kutoka mikononi mwa adui Zake, na kuwaadhibu kwa ajili ya ukatili wao Kwake. Matumaini yao yangengepanda na kushuka kadiri matukio tofauti-tofauti yalivyotendeka. Wakati fulani walitia shaka, na kuhofu kwamba walikuwa wamedanganywa. Lakini sauti ile iliyosikika juu ya mlima wa kubadilika sura, na utukufu ambao waliuona pale, viliimarisha imani yao kwamba alikuwa ni Mwana wa Mungu. Waliyakumbuka matukio ambayo walikuwa wameyashuhudia, miujiza ambayo walimwona Yesu akitenda katika kuwaponya wagonjwa, kufungua macho ya vipofu, kufungua masikio ya waliokuwa viziwi, kuyakemea na kuyafukuza mapepo, kuwafufua waliokufa, na hata kukemea na kutuliza upepo na bahari. Hawakuweza kuamini kwamba Yeye angekufa. Walitarajia kwamba bado angeinuka Mwenye nguvu, na kwa sauti Yake ya kuamrisha kuutawanya umati ule wa watu wenye kiu ya damu, kama wakati ule walipokimbia mbele Yake

alipoingia hekaluni na kuwafukuza nje wale waliokuwa wakiifanya nyumba ya Mungu kuwa mahali pa biashara, walipokimbia mbele Yake kana kwamba walikuwa wanafukuzwa na kikosi cha askari wenye silaha. Wanafunzi walitumaini kwamba Yesu angeonesha uweza Wake na kuwathibitishia wote kwamba alikuwa Yeye Ndiye Mfalme wa Israeli.**{EW 171.1}**

Yuda alijawa na majuto makali na aibu kwa kitendo chake cha kukosa uaminifu, hatia na hiana ya kumsaliti Yesu. Na aliposhuhudia matendo mabaya Mwokozi aliyoyavumilia, alilemewa kwa uchungu wa hisia hizi. Yuda alimpenda Yesu, lakini alipenda pesa zaidi. Hakuwa amefikiria kwamba Yesu angelijiruhusu Mwenyewe kuchukuliwa na genge lile  watu ambao alikuwa ameliongoza kumkata Yesu. Alitarajia kuwa angefanya muujiza, na kujiokoa kutoka kwao. Lakini alipoona umati wa watu waliokasirika katika ukumbi wa hukumu, wakiwa na kiu ya damu, alihisi sana hatia yake kwa kina; na wakati wengi walikuwa wakimshutumu Yesu kwa nguvu, Yuda alifanya haraka kupita kwenye umati huo, akiungama kwamba alikuwa ametenda dhambi kwa kuisaliti damu isiyo na hatia. Aliwapa makuhani fedha ambazo walikuwa

wamemlipa, na akawasihi wamwachilie Yesu, akitangaza kwamba hakuwa na hatia kabisa. **{EW 171.2}**

Kwa muda mfupi maudhi, hofu, usumbufu na machafuko yaliwafanya makuhani kukaa kimya. Hawakutaka watu wajue kwamba walikuwa wamemwajiri mmoja wa wale wafuasi bayana wa Yesu, ambaye alijulikana na wengi, ili apate kumsaliti mikononi mwao. Kule kumwinda Yesu na kumchukua kwa siri, walitamani kukuficha. Lakini ungamo la Yuda, na mwonekano wake wa kama mtu mgonjwa, kwaajili ya uchungu, uchovu, wasiwasi, hofu, kukosa furaha, na hatia, viliwafunua wazi makuhani mbele ya umati, vikionesha kuwa ilikuwa ni chuki iliyowafanya wamchukue Yesu. Yuda alipotangaza kwa sauti kubwa kwamba Yesu hana hatia, makuhani wakuu walijibu, "Basi, haya yatupasani sisi? Yaangalie haya wewe mwenyewe." Yesu alikuwa chini ya mamlaka yao, na walikuwa wamedhamiria kuwa na hakika Naye. Yuda, akiwa amelemewa na uchungu, na alizitupa fedha zile ambazo kwa sasa alizidharau miguuni pa wale waliomwajiri, na, kwa uchungu na hofu, alikwenda na kujinyonga. **{EW 172.1}**

Yesu alikuwa na wengi waliomuunga mkono

katika kundi lile lililomzunguka, na kutokujibu Kwake chochote juu ya maswali mengi aliyoulizwa kuliushangaza umati ule. Chini ya dhihaka na vurugu zote za kundi lile la watu wenye ghasia, hakukuwa na kukunja uso, wala udhihirisho wa fadhaa katika uso Wake. Alikuwa ni Mwenye heshima, hadhi na utulivu. Watazamaji walimwangalia kwa mshangao. Walilinganisha umbo Lake kamilifu na mwenendo Wake wa heshima thabiti, na mwonekana wa wale walioketi katika hukumu dhidi Yake, na wakaambiana kwamba Alionekana zaidi kuwa kama Mfalme kuliko yeyote kati ya watawala wale. Yeye hakuwa na alama zozote za kuwa mhalifu. Jicho Lake lilikuwa laini, angavu, na jasiri, paji Lake la uso lilikuwa pana na la refu. Kila sifa ilidhihirisha kwa nguvu ya ukarimu na kanuni bora. Uvumilivu na ustahimilivu Wake ulikuwa tofauti sana na wa mwanadamu kiasi kwamba wengi walitetemeka. Hata Herode na Pilato walifadhaika sana kwa mwenendo, hulka na haiba Yake bora kama wa Mungu. **{EW 172.2}**

Tangu mwanzo, Pilato alisadikishwa kwamba Yesu hakuwa mtu wa kawaida. Alimwamini kuwa mtu mwenye sifa bora sana, na hakuwa na hatia

kabisa juu ya mashtaka yaliyotolewa dhidi Yake. Malaika ambao walikuwa wakishuhudia tukio lile walithibitisha imani ya gavana wa Kirumi, na ili kumwokoa asijihusishe na tendo la kutisha la kumtoa Kristo asulubiwe, malaika alitumwa kwa mke wa Pilato, na akampa habari kupitia ndoto kwamba alikuwa ni Mwana wa Mungu ambaye mumewe alijihusisha katika hukumu Yake, na kwamba alikuwa mtesekaji asiye na hatia. Mara moja alituma ujumbe kwa Pilato, akisema kwamba alikuwa ameteseka sana katika ndoto kwa sababu ya Yesu na kumwonya asifanye jambo lolote na Mtu huyo mtakatifu. Mjumbe, akijipenyeza kwa haraka kupitia kwenye umati wa watu, aliweka barua hiyo mikononi mwa Pilato. Alipokuwa akiisoma, alitetemeka na kupauka uso, na mara moja akaamua kutokujihusisha kabisa na kumhukumu Kristo kifo. Kama Wayahudi wangeitaka damu ya Yesu, yeye asingewekeza ushawishi wake katika hilo, bali angejitahidi kumwokoa. **{EW 173.1}**

Pilato aliposikia kwamba Herode alikuwa Yerusalemu, alipata afueni kwenye hisia, na akafarijika sana; kwa kuwa alitumaini kujiweka huru kutokana na uwajibikaji wote katika kesi na hukumu ya Yesu. Akamtuma mara moja, pamoja na

washtaki Wake, kwa Herode. Mtawala huyu alikuwa sugu katika dhambi. Mauaji ya Yohana Mbatizaji yalikuwa yameacha juu ya dhamiri yake doa ambalo hakuweza kujikomboa kutoka kwalo. Aliposikia habari za Yesu na matendo makuu yaliyofanywa Naye, aliogopa na kutetemeka, akiamini kwamba Yeye ndiye Yohana Mbatizaji aliyefufuka kutoka kwa wafu. Yesu alipowekwa mikononi mwake na Pilato, Herode alichukulia kitendo hicho kama ni kukiri nguvu, mamlaka, na busara zake. Hii ilikuwa na matokeo ya kufanya urafiki baina ya watawala wale wawili, ambao hapo awali walikuwa ni maadui. Herode alifurahi kumwona Yesu, akitarajia afanye miujiza mikubwa kadhaa kumridhisha. Lakini haikuwa kazi ya Yesu kuridhisha udadisi au kutafuta usalama Wake Mwenyewe. Uweza Wake wa Kiungu, wa kimiujiza ulipaswa kutumika kwa ajili ya wokovu wa wengine, lakini si kwa niaba yake Yeye Mwenyewe. **{EW 173.2}**

Yesu hakujibu lolote kwa maswali mengi yaliyoelekezwa Kwake na Herode; wala hakuwajibu maadui Zake, ambao walikuwa wakimshutumu kwa nguvu. Herode alikasirika kwa sababu Yesu hakuonekana kuogopa mamlaka yake, na kwa kuwatumia watu wake wa vita alimkejeli, na

kumdhihaki, na kumdhalilisha Mwana wa Mungu. Lakini bado alishangazwa na mwonekano wa Yesu uliokuwa mzuri, kama wa Mungu alipoteswa na kunyanyaswa kwa aibu, na akiogopa kumhukumu, hivyo alimtuma tena kwenda kwa Pilato.**{EW 174.1}**

Shetani na malaika zake walikuwa wakimjaribu Pilato na kujaribu kumwongoza kwenye uharibifu wake mwenyewe. Walimdokezea kwamba ikiwa hangeshiriki katika kumhukumu Yesu wengine wangefanya hivyo; umati ulikuwa na kiu ya damu Yake; na ikiwa hatamtoa asulubiwe, angepoteza nguvu zake na heshima ya ulimwengu na angeshutumiwa kuwa muumini wa ‘mlaghai’. Kwa kuogopa kupoteza nguvu na mamlaka yake, Pilato alikubali kifo cha Yesu. Na hata ingawa aliweka damu ya Yesu juu ya washitaki Wake, na umati ule ukaipokea, ukipaza sauti, "Damu Yake na iwe juu yetu, na juu ya watoto wetu," lakini bado Pilato hakuwa bila hatia; alikuwa na hatia ya damu ya Kristo. Kwa ajili ya maslahi yake ya ubinafsi, upendo wake wa heshima kutoka kwa watu mashuhuri wa dunia, alimtoa mtu asiye na hatia kufa. Kama Pilato angefuata usadikisho aliopewa mwenyewe, asingefanya lolote katika kumhukumu Yesu kifo. .**{EW 174.2}**

Mwonekano na Maneno ya Yesu wakati wa hukumu Yake uliacha fikra za kina katika akili za wengi waliokuwepo wakati huo wa Alhamisi na Ijumaa. Matokeo ya mvuto uliowekwa kwa jinsi hiyo yalikuwa dhahiri baada ya kufufuka Kwake. Miongoni mwa wale ambao wakati ule walikuwa wakiongezeka kanisani, kulikuwa na wengi ambao imani yao ilianza tangu wakati ule wa kuhukumiwa kwa Yesu..**{EW 174.2}**

Hasira ya Shetani ilikuwa kubwa alipoona kuwa ukatili wote ambao alikuwa amewaongoza Wayahudi kumfanyia Yesu haukusababisha manung'uniko hata kidogo kutoka Kwake. Ingawa alikuwa amechukua juu Yake asili ya mwanadamu, alitegemezwa na ujasiri kama wa Mungu, na hakuondoka hata kidogo katika mapenzi ya Baba Yake. **{EW 175.1}**

## Sura ya 39-Kusulubiwa kwa Kristo

Mwana wa Mungu alikabidhiwa kwa watu ili apate kusulubiwa; kwa kelele za ushindi walimchukua Mwokozi mpendwa na kumwongoza katika safari ya kusulubiwa.  Alikuwa dhaifu na mnyonge kutokana na uchovu, maumivu, na

kupoteza damu kwa mijeledi na mapigo ambayo alikuwa ameyapokea; lakini bado msalaba ule mzito ambao punde tu angepigiliwa juu yake uliwekwa juu Yake. Yesu alizimia chini ya mzigo. Mara tatu msalaba uliwekwa mabegani Mwake, na mara tatu alizimia. Mmoja wa wafuasi Wake, mtu ambaye hakuwa amekiri wazi imani kwa Kristo, lakini bado alimwamini, alikamatwa (Simoni Wa Libya au Mkirene). Juu yake msalaba uliwekwa, na aliubeba hadi mahali pa mauti. Makundi ya malaika yalipangwa angani juu ya mahali hapo. Wanafunzi kadhaa wa Kristo walimfuata kwenda Kalvari, kwa huzuni, na kwa kulia kwa uchungu. Walikumbuka safari Yake ya ushindi kuingia Yerusalemu siku chache tu zilizopita, walipokuwa wamemfuata, wakipaza sauti zao, "Hosana juu mbinguni!" huku wakitupatupa mavazi yao, na matawi mazuri ya mitende njiani. Walidhani kwamba wakati ule angechukua ufalme na kutawala kama mfalme wa dunia juu ya Israeli. Ni jinsi gani sasa, tukio lilikuwa limebadilika! Ni jinsi gani matumaini yao yalifishwa! Si kwa furaha, si kwa matumaini ya uchangamfu, bali kwa mioyo iliyoshikwa na hofu na kukata tamaa sasa polepole, na kwa huzuni walimfuata Yeye ambaye alikuwa amefedheheshwa na kudhalilishwa,

na ambaye alikuwa karibu kufa.**{EW 175.2}**

Mama Yake Yesu alikuwapo pale. Moyo wake ulichomwa na uchungu ule ambao hakuna mwingine ila mama mwenye upendo tu anaweza kuuhisi; lakini, pamoja na wanafunzi, bado alitumaini kwamba Kristo angetenda muujiza fulani mkubwa na kujiokoa kutoka kwa wauaji Wake. Asingeweza kuvumilia wazo kwamba Yeye angejiruhusu Mwenyewe, asulubiwe. Lakini maandalizi yalifanywa, na Yesu alilazwa juu ya msalaba. Nyundo na misumari zililetwa. Mioyo ya wanafunzi ilinyong'onyea. Mama yake Yesu aliinama kwa uchungu mkali mno kuweza kuvumilia. Kabla ya Mwokozi kupigiliwa misumari msalabani, wanafunzi walimchukua kutoka kwenye tukio hilo, ili asiweze kusikia kugongwa kwa misumari ilipokuwa ikipenya katika mifupa na misuli ya mikono na miguu Yake laini. Yesu hakunung'unika, bali aliugua kwa uchungu. Uso Wake ulipauka kwa msongo, na matone makubwa ya jasho yalisimama juu ya paji la uso Wake. Shetani aliyafurahia mateso ambayo Mwana wa Mungu alikuwa akiyapitia, lakini bado alihofu kwamba juhudi zake za kuzuia mpango wa wokovu zilikuwa bure, kwamba ufalme wake umepotea, na kwamba lazima hatimaye

aangamizwe. {**EW 176.1**}

Baada ya Yesu kupigiliwa misumari msalabani, msalaba huu uliinuliwa na kwa nguvu kubwa ulitupwa ndani ya mahali ambapo palikuwa pametayarishwa kwa ajili yake ardhini, ukirarua mwili na kusababisha mateso makali kabisa. Ili kufanya kifo cha Yesu kiwe cha aibu kadiri iwezekanavyo, wezi wawili walisulubiwa pamoja Naye, mmoja kila upande. Wezi wale walichukuliwa kwa nguvu, na baada ya upinzani mkubwa sana kwa upande wao, mikono yao ilisukumwa nyuma na kupigiliwa misumari kwenye misalaba yao. Lakini Yesu alijisalimisha kwa upole. YEYE Hakuhitaji mtu yeyote kulazimisha mikono Yake kwenda juu ya msalaba. Wakati huo wezi walipokuwa wakiwalaani wauaji wao, Mwokozi kwa uchungu mkali aliwaombea maadui Zake, “Baba, uwasamehe, kwa kuwa hawajui watendalo.” Haukuwa uchungu mkali wa mwili peke yake Yesu alioustahimili; dhambi za ulimwengu wote zilikuwa juu Yake.{**EW 176.2**}

Wakati Yesu akiwa juu ya msalaba, baadhi waliokuwa wakipita njiani walimtukana, wakiinamisha vichwa vyao kama kumsujudia mfalme, na kumwambia, “Ewe mwenye kulivunja hekalu na kulijenga kwa siku tatu, jiokoe nafsi Yako;

ukiwa Ndiwe Mwana wa Mungu, shuka msalabani.” Shetani aliyatumia maneno sawa na hayo kwa Kristo jangwani, "Ukiwa Ndiwe Mwana wa Mungu." Nao makuhani wakuu na wazee na waandishi wakamdhihaki wakisema, "Aliokoa wengine; hawezi kujiokoa Mwenyewe. Yeye ni Mfalme wa Israeli, na ashuke sasa msalabani, nasi tutamwamini." Malaika ambao walikuwa wakizungukazunguka juu ya tukio la kusulubiwa kwa Kristo walisukumwa kuwa na hasira wakati watawala walipomdhihaki na kusema, "Ukiwa Ndiwe Mwana wa Mungu, na ujiokoe Mwenyewe." Walitamani pale kuja kumsaidia Yesu na kumwokoa, lakini hawakuruhusiwa kufanya hivyo. Lengo la utume Wake lilikuwa bado halijatimizwa.{**EW 177.1**}

Yesu alipokuwa amening’inia msalabani kwa muda mrefu wa uchungu mkali, Yeye hakumsahau mama Yake. Mama alikuwa amerudi kwenye eneo la tukio la kutisha, kwa kuwa hakuweza tena kuendelea kukaa mbali na Mwanawe. Somo la mwisho la Yesu lilikuwa moja la huruma na ubinadamu. Alitazama uso wa mama Yake uliojaa huzuni, na kisha mwanafunzi Wake mpendwa Yohana. Alimwambia mama Yake, “Mama, tazama, mwanao!” Kisha akamwambia Yohana, “Tazama,

mama yako!” Na tangu saa ile Yohana alimchukua nyumbani kwake.{**EW 177.2**}

Yesu alishikwa na kiu katika maumivu Yake makali, nao walimpa siki na nyongo ili anywe; lakini alipoionja, aliikataa. Malaika waliangalia maumivu makali ya Kamanda wao mpendwa hadi pale ambapo hawakuweza kuendelea kutazama, nao walifunika nyuso zao wasiione mandhari ile. Jua lilikataa kuangalia tukio lile la kuogofya. Yesu alilia kwa sauti kuu, ambayo ilijaza hofu kuu mioyoni mwa wauaji Wake, *“Imekwisha/Tetelestai.”* Ndipo pazia la hekaluni lilipasuka kutoka juu hadi chini, ardhi ikatetemeka, na miamba kupasuka. Giza kuu lilitanda juu ya uso wa dunia. Tumaini la mwisho la wanafunzi lilionekana kufagiliwa mbali pale Yesu alipokufa. Wengi wa wafuasi Wake walilishuhudia tukio la mateso na kifo Chake, na kikombe chao cha huzuni kilikuwa kimejaa. **{EW 177.3}**

Shetani hapo hakufurahi kama ambavyo alifanya hapo awali. Alikuwa na matumaini ya kuuvunja mpango wa wokovu; lakini uliwekwa kwa kina mno. Na sasa kwa kifo cha Kristo alijua kwamba yeye mwenyewe lazima atakufa hatimaye, na ufalme wake atapewa Yesu. Alifanya mkutano na malaika wake. Hakuwa ameshinda chochote dhidi ya

Mwana wa Mungu, na sasa ni lazima waongeze juhudi zao na kwa nguvu zao na werevu wawageukie wafuasi Wake. Ni lazima wawazuie wote ambao wangeweza kupokea wokovu ulionunuliwa kwa ajili yao na Yesu. Kwa kufanya hivyo Shetani bado angeweza kufanya kazi dhidi ya serikali ya Mungu. Pia ingekuwa ni kwa maslahi yake mwenyewe, kuwazuia watu wengi kwenda kwa Yesu kwa kadiri iwezekanavyo. Kwa maana dhambi za wale wanaokombolewa kwa damu ya Kristo hatimaye zitarundikwa juu ya mwanzilishi wa dhambi, na ni lazima huyu adui abebe adhabu yao, wakati huo wale wasioukubali wokovu kupitia Yesu watapata adhabu ya dhambi zao wenyewe. **{EW 178.1}**

Maisha ya Kristo daima yalikuwa bila utajiri, heshima, au maonesho ya dunia. Unyenyekevu na kujikana Kwake vilikuwa na tofauti sana na kiburi na kufurahia na kuendekeza anasa kwa makuhani na wazee. Usafi Wake usio na doa ulikuwa ni karipio la daima kwa dhambi zao. Walimdharau kwa ajili ya unyenyekevu, utakatifu, na usafi Wake. Lakini wale waliomdharau hapa siku moja watamwona katika fahari ya mbinguni na utukufu usio na kifani wa Baba Yake. **{EW 178.2}**

Katika ukumbi wa hukumu, Yeye alikuwa amezungukwa na maadui ambao walikuwa na kiu ya damu Yake; lakini wale watu wakaidi ambao walilia, "Damu Yake na iwe juu yetu, na juu ya watoto wetu," watamtazama akiwa ni Mfalme Mwenye kuheshimiwa. Jeshi lote la mbinguni litamsindikiza njiani Mwake kwa nyimbo za ushindi, wakirindima ukuu, na nguvu Kwake Yeye aliyeuawa, na bado anaishi tena, naam, mshindi Mwenye nguvu. **{EW 178.3}**

Mtu maskini, dhaifu, mnyonge alitema mate usoni pa Mfalme wa utukufu, wakati huo kelele za shangwe ya kikatili ziliibuka kutoka kwa umati kwa sababu ya dhihaka na tusi hilo la kudhalilisha. Waliuharibu kwa mapigo na ukatili uso ule ambao uliijaza mbingu yote kwa kupendeza kwake. Watauona uso huo tena, uking'aa kama jua la adhuhuri, nao watajitahidi kukimbia kutoka mbele Yake. Badala ya kelele ile ya shangwe ya ushindi wa kikatili, wataomboleza kwa sababu Yake Yeye. **{EW 179.1}**

Yesu ataionesha mikono Yake yenye alama za kusulubiwa Kwake. Alama za ukatili huu atazibeba daima. Kila alama na mchoro wa misumari itasimulia kisa cha ukombozi wa ajabu wa

mwanadamu na gharama kubwa ambayo kwayo ulinunuliwa. Watu wale wale ambao walichoma mkuki ubavuni mwa Bwana wa uzima wataona chapa ya mkuki nao wataomboleza kwa uchungu mkubwa kwa ajili ya sehemu ambayo walitenda katika kuuharibu mwili Wake vibaya. **{EW 179.2}**

Wauaji Wake walikasirishwa sana na maandishi ya juu, "Mfalme wa Wayahudi," yaliyowekwa kwenye msalaba juu ya kichwa Chake. Lakini watalazimika kumwona katika utukufu Wake wote na uweza wa Kifalme. Wataona juu ya vazi Lake, na juu ya paja Lake,  Jina lililoandikwa kwa herufi zilizo hai: "Mfalme wa wafalme, na Bwana wa mabwana." Walimlilia kwa dhihaka, alipotundika msalabani, hebu "Kristo, Mfalme wa Israeli, na ashuke sasa msalabani, tupate kuona na kuamini." Watamwona wakati huo akiwa na uweza wa kifalme na mamlaka. Hawatadai ushahidi wowote wa Yeye kuwa Mfalme wa Wayahudi; Lakini kwa kuzidiwa na hisia ya ukuu Wake na utukufu mwingi, watalazimika kukiri, "Amebarikiwa Yeye ajaye kwa  Jina la Bwana." **{EW 179.3}**

Kutetemeka kwa dunia, kupasuka kwa miamba, giza lililoenea juu ya dunia, na kilio kikuu na chenye nguvu cha Yesu, “Imekwisha,“ alipoyatoa maisha

Yake, viliwasumbua adui Zake na kuwafanya wauaji wake kutetemeka. Wanafunzi waliyashangaa maonesho haya ya ajabu; lakini matumaini yao yalikuwa yamepondeka. Walihofu kwamba Wayahudi wangetafuta kuwaangamiza wao pia. Walihisi kuwa na hakika kwamba chuki kama hiyo ambayo ilikuwa imedhihirishwa dhidi ya Mwana wa Mungu haitaishia Kwake. Saa za upweke. Watu hawa walizitumia wakiomboleza juu ya kukatishwa tamaa kwao. Walitarajia kwamba Yesu angetawala akiwa Mfalme wa dunia, lakini matumaini yao yalikufa pamoja Naye. Katika huzuni na kukatishwa tamaa kwao, walitilia shaka kama hakuwa amewadanganya. Hata mama Yake alikuwa na shaka na kuyumba katika imani yake kuhusu Yeye kuwa Masihi.**{EW 179.4}**

Ijapokuwa wanafunzi walikuwa wamekatishwa tamaa katika matumaini yao juu ya Yesu, bado walimpenda na walitamani kuuzika mwili Wake kwa heshima, lakini hawakujua jinsi ya kuupata. Yusufu wa Arimathaya, mtu wa baraza/Sanhedrini, tajiri na mashuhuri wa Wayahudi na mwanafunzi wa kweli wa Yesu, alikwenda kwa faragha lakini kwa ujasiri kwa Pilato na kuomba kutoka kwake mwili wa Mwokozi. Hakuthubutu kwenda waziwazi, kwa

sababu ya chuki ya Wayahudi. Wanafunzi walihofu kwamba juhudi zingefanywa nao kuzuia mwili wa Kristo kuwa na mahali pa heshima pa kupumzika. Pilato alikubali ombi hilo, na wanafunzi waliuchukua mwili usio na uhai kutoka msalabani, wakati huo wakiwa na uchungu mkubwa, nao waliomboleza kuhusu matumaini yao yaliyofishwa. Kwa uangalifu mwili huo ulifunikwa kwa kitani safi, na kuwekwa katika kaburi jipya la Yusufu.**{EW 180.1}**

Wanawake ambao walikuwa wafuasi wanyenyekevu wa Kristo wakati alipokuwa akiishi, hawakuweza kumwacha hadi walipoona amelazwa kaburini na jiwe lenye uzito mkubwa kuwekwa mbele ya mlango, adui Zake wasije wakajaribu kuupata mwili Wake. Lakini hawakupaswa kuwa na haja ya kuogopa; kwa kuwa niliona kwamba jeshi la malaika walitazama kwa shauku isiyoelezeka mahali pale Yesu alipopumzika, wakisubiri kwa ari amri ya kufanya sehemu yao katika kumkomboa Mfalme wa utukufu kutoka katika nyumba Yake ya gereza.**{EW 180.2}**

Wauaji wa Kristo waliogopa kwamba bado angeweza kuwa hai na kuwatoroka. Kwa hiyo walimwomba Pilato awape ulinzi wa kulilinda kaburi mpaka siku ya tatu. Ombi hili lilikubaliwa, na jiwe

lililokuwa mlangoni likapigwa muhuri, ili wanafunzi Wake wasije wakamwiba na kusema kwamba amefufuka kutoka kwa wafu.**{EW 181.1}**

## Sura ya 40-Ufufuo wa Kristo

Wanafunzi walipumzika siku ya Sabato, wakiwa na huzuni kwa ajili ya kifo cha Bwana wao, wakati huo Yesu, Mfalme wa utukufu, alikuwa amelala kaburini. Usiku ulipokaribia, askari waliwekwa kulinda mahali ambapo Mwokozi alipumzika, wakati huo malaika wasioonekana, wakizungukazunguka juu ya mahali hapo Patakatifu. Usiku uliondoka polepole, na wakati kungali giza, malaika wale walinzi walijua kwamba muda wa kuachiliwa kwa Mwana mpendwa wa Mungu, Kamanda wao mpendwa, ulikuwa umekaribia. **{EW 181.2}** Walipokuwa wakingojea kwa hisia kali kabisa saa ya ushindi Wake, malaika mwenye nguvu alikuja akiruka kwa haraka kutoka mbinguni. Uso wake ulikuwa kama umeme, na mavazi yake meupe kama theluji. Nuru yake ilitawanya giza kutoka kwenye njia yake na kuwasababisha malaika waovu, ambao

walikuwa wamedai kwa ushindi umiliki wa mwili wa Yesu, kukimbia kwa hofu kutoka katika mwangaza na utukufu wake. Mmoja wa jeshi la malaika ambaye alikuwa ameshuhudia tukio la kufedheheshwa kwa Kristo, na alikuwa akiangalia mahali Pake pa kupumzika, aliungana na malaika yule aliyetoka mbinguni, na kwa pamoja walishuka hadi kaburini. Dunia ilitetemeka na kutikisika walipokaribia, na kulikuwa na tetemeko kubwa la ardhi.{**EW 182.1**}

Hofu iliwashika walinzi wa Kirumi. Nguvu zao za kuutunza mwili wa Yesu zilikuwa wapi sasa? Hawakufikiri juu ya wajibu wao au wa wanafunzi kumwiba. Nuru ya malaika ilipoangaza pande zote, ing'aayo kuliko jua, kiasi kwamba walinzi wa Kirumi walianguka chini kama wafu. Mmoja wa malaika akalishika lile jiwe kubwa, akalivingirisha kutoka mlangoni pa kaburi, akaketi juu yake. Mwingine aliingia kaburini na kufungua sanda/kitambaa kutoka kwenye kichwa cha Yesu. Ndipo malaika kutoka mbinguni, kwa sauti iliyofanya dunia kutetemeka, alipaza sauti akisema: “Ewe Mwana wa Mungu, Baba Yako anakuita! Toka nje." Kifo hakikuweza kutawala tena juu Yake. Yesu alifufuka kutoka kwa wafu, mshindi wa kushangiliwa. Kwa

kicho makini jeshi la malaika walikaza macho yao kwenye eneo lile la tukio. Na Yesu alipotoka nje ya kaburi, malaika wale waliong'aa walisujudu chini kumwabudu, na kumsifu kwa nyimbo za ushindi na shangwe.{**EW 182.2**}

Malaika wa Shetani walikuwa wamelazimishwa kukimbia mbele ya nuru angavu, inayopenya ya malaika wa mbinguni, na walimlalamikia vikali mfalme wao Shetani kwamba windo lao lilichukuliwa kutoka kwao kwa nguvu, na kwamba Yeye ambaye walimchukia sana alikuwa amefufuka kutoka kwa wafu. Shetani na majeshi yake walikuwa wamefurahi kwamba nguvu zao juu ya mwanadamu aliyeanguka zilikuwa zimemsababisha Bwana wa uzima kulazwa kaburini, lakini ushindi wao wa kuzimu ulikuwa wa kitambo kidogo tu. Kwa kuwa Yesu alipotoka katika nyumba Yake ya gereza akiwa ni mshindi mwenye fahari, Shetani alijua kwamba baada ya kipindi kifupi angekufa, na ufalme wake ungepita kwenda kwa Yeye ambaye ilikuwa ni haki Yake. Aliomboleza na kukasirika kwamba licha ya juhudi zake zote, Yesu hakuwa ameshindwa, bali alikuwa amefungua njia ya wokovu kwa mwanadamu, na yeyote ambaye angependa angeweza kutembea katika hiyo na

kuokolewa.{**EW 182.2**}

Malaika waovu na amiri jeshi wao walikutana katika baraza ili kufikiria jinsi ambavyo bado wangeweza kufanya kazi dhidi ya serikali ya Mungu. Shetani aliwaambia watumishi wake waende kwa makuhani wakuu na wazee. Alisema: "Tulifanikiwa kuwadanganya, na tukayapofusha macho yao, na kuifanya mioyo yao kuwa migumu dhidi ya Yesu. Tuliwafanya waamini kwamba alikuwa ni mtu laghai. Kwamba walinzi wa Kirumi watabeba habari za chuki na kuchukiza kwamba Kristo amefufuka. Tuliwaongoza makuhani na wazee kumchukia Yesu na kumwua. Sasa shikilieni mbele yao kwamba kama ikijulikana kwamba Yesu amefufuka, watapigwa kwa mawe na watu kwa kumwua mtu asiye na hatia.” {**EW 182.3**}

Jeshi la malaika wa mbinguni lilipoondoka kaburini na nuru na utukufu kutoweka, walinzi wa Kirumi walithubutu kuinua vichwa vyao na kuangalia kuwazunguka. Walijawa na mshangao walipoona kwamba lile jiwe kubwa lilikuwa limevingirishwa kutoka kwenye mlango wa kaburi na kwamba mwili wa Yesu ulikuwa umeondoka. Walifanya haraka kwenda mjini ili kuwajulisha makuhani na wazee mambo waliyoyaona. Wauaji

hao walipoisikia habari hiyo ya ajabu, nyuso zao zilisawajika (zikapauka kwa hofu). Hofu iliwashika kwa kufikiria kile walichokuwa wamekitenda. Ikiwa habari hiyo ilikuwa ni sahihi, walikuwa wamepotea. Kwa muda walikaa kimya, wakiangaliana nyuso zao, bila kujua nini cha kufanya au nini cha kusema. Kuikubali ripoti hiyo ingekuwa ni kujihukumu wao wenyewe. Hivyo walikwenda kando ili kushauriana kuhusu jambo gani linapaswa kufanyika. Waliwaza kwamba ikiwa taarifa iliyoletwa na walinzi ingesambazwa miongoni mwa watu, wale waliomuua Kristo wangeuawa kama wauaji Wake. Iliamuliwa kuwalipa askari wale ili kuweka jambo hilo kuwa siri. Makuhani na wazee waliwaahidi kiasi kikubwa cha fedha, wakisema, "Semeni, ya kwamba wanafunzi Wake walikuja usiku, wakamwiba, sisi tulipokuwa tumelala." Wale walinzi walipotaka kujua kuhusu kitu gani kingefanyika kwao kuhusu kulala kwao wakiwa lindoni, viongozi wa Kiyahudi waliahidi kumshawishi liwali na kujipatia usalama wao. Kwa ajili ya fedha, walinzi wa Kirumi waliuza heshima yao, na wakakubali kufuata ushauri wa makuhani na wazee. {**EW 183.1**}

Wakati Yesu, alipokuwa amening’inia juu ya msalaba, Yeye alipopaza sauti, "Imekwisha,"

miamba ilipasuka, nchi ikatetemeka, na baadhi ya makaburi yalifunguliwa. Alipofufuka mshindi juu ya kifo na kaburi, dunia ilipokuwa ikipepesuka na utukufu wa mbingu ukiangaza kuzunguka mahali pale Patakatifu, wengi wa wenye haki waliokufa, watiifu kwa wito Wake, walitoka nje kama mashahidi kwamba alikuwa amefufuka. Watakatifu wale waliopendelewa, waliofufuka walitoka nje wakiwa wametukuzwa. Walikuwa ni wateule na watakatifu wa kila zama/kizazi, tangu uumbaji wa ulimwengu wetu hadi katika siku za Kristo. Hivyo wakati viongozi wa Kiyahudi walikuwa wakijitahidi kuficha Ukweli wa kufufuka kwa Kristo, Mungu alichagua kuleta kundi kutoka katika makaburi kushuhudia kwamba Yesu alikuwa amefufuka, na kuutangaza utukufu Wake. {**EW 184.1**}

Wale waliofufuka walitofautiana katika kimo na umbo, wengine wakiwa bora zaidi katika sura kuliko wengine. Nilijulishwa kwamba wakazi wa dunia walikuwa wakipunguka, wakipoteza nguvu zao na uzuri. Shetani ana nguvu ya magonjwa na kifo, na katika kila zama athari za laana zimekuwa zikionekana zaidi, na nguvu za Shetani zinaonekana wazi zaidi. Wale walioishi katika nyakati za Nuhu na

Ibrahimu walifanana na malaika katika maumbo, uzuri, na nguvu. Lakini kila kizazi kilichofuata kimekuwa kikizidi kuwa dhaifu na wenye kupatwa mara kwa mara na magonjwa, na maisha yao yamekuwa ni ya kudumu kwa kipindi kifupi. Shetani amekuwa akijifunza jinsi ya kuisumbua na kuidhoofisha jamii.**{EW 184.2}**

Wale ambao walitoka baada ya ufufuo wa Yesu waliwatokea wengi, wakiwaambia kwamba dhabihu kwa ajili ya mwanadamu ilikuwa imekamilika, kwamba Yesu, ambaye Wayahudi walimsulubisha, alikuwa amefufuka kutoka kwa wafu; na kwa kuthibitisha Maneno yao walisema, "Sisi Tumefufuka pamoja Naye." Walitoa ushuhuda kwamba ni kwa uweza Wake ndiyo walikuwa wameitwa kutoka makaburini mwao. Licha ya taarifa za uwongo zilizosambazwa, ufufuo wa Kristo usingeweza kufichwa na Shetani, malaika wake, au wakuu wa makuhani; kwani kundi hili takatifu lililofufuka pamoja na Kristo, lilipoletwa kutoka makaburini mwao, lilieneza habari za ajabu, za furaha; pia Yesu alijionesha kwa wanafunzi Wake wenye huzuni, waliovunjika mioyo, akiwaondoa hofu na kuwaletea furaha na shangwe.**{EW 184.3}**

Habari zilipokuwa zikienea kutoka jiji hadi jiji na

kutoka mji hadi mji, Wayahudi kwa upande wao walihofia maisha yao na kuficha chuki waliyokuwa nayo kwa wanafunzi. Tumaini lao pekee lilikuwa ni kueneza habari yao ya uwongo. Na wale waliotamani uongo huu kuwa ndiyo ile Kweli waliukubali. Pilato alitetemeka aliposikia kwamba Kristo amefufuka. Kiongozi huyu hakuweza kutilia shaka ushuhuda uliotolewa, na kutoka saa hiyo amani ilitoweka kwake milele. Kwa sababu ya heshima ya dunia, kwa kuogopa kupoteza mamlaka na maisha yake, alimtoa Yesu afe. Sasa alikuwa na hakika kabisa kwamba hakuwa tu mtu asiye na hatia ambaye damu yake alikuwa na hatia nayo, bali alikuwa Mwana wa Mungu. Hadi mwisho wake maisha ya Pilato yalikuwa ni maisha ya taabu. Kukata tamaa na maumivu makali vilivunjavunja kila hisia ya matumaini, ya furaha. Alikataa kufarijiwa na kufa kifo cha kutisha na chenye taabu mno.**{EW 185.1}**

Herode [Alikuwa ni Herode Antipa aliyemhukumu Kristo na Herode Agripa ndiye aliyemuua Yakobo mtume ambaye alikuwa mkuu wa Baraza la kwanza la mitume (Matendo 12). Agripa alikuwa mpwa na shemejie Antipa. Kwa njama alijipatia kiti cha enzi cha Antipa, na

alipoingia katika mamlaka alifuata mwelekeo ule-ule kwa Wakristo ambao Antipa alikuwa ameufuata. Katika nasaba ya Herode kulikuwa na watu sita ambao waliitwa kwa jina la Herode. Hivyo lilitumika kwa kiasi kama jina la jumla, watu binafsi wakiitwa kwa majina mengine, kama Antipa, Filipo, Agripa, na kadhalika. Kwa mfano wa sasa tunaweza kusema Czar Nicholas, Czar Alexander, na Kaisaria fulani au Malkia au Sultani fulani na kadhalika. Katika mfano wa sasa matumizi haya ya neno hili yanakuwa ya kawaida na ya kufaa zaidi kwa kuwa Agripa, alipomuua Yakobo, alikuwa amekalia kiti cha Antipa, ambaye muda mfupi uliopita alikuwa amehusika katika hukumu ya Kristo; naye alidhihirisha tabia ile ile. Ilikuwa ni roho ile ile ya ki-Herode, isipokuwa katika nafsi ya mtu mwingine, kama vile "joka" la Ufunuo 12:17 alivyo sawa na joka wa aya ya 3, nguvu halisi ya msukumo katika kila mmoja likiwa ni joka wa aya ya 9. Katika mfano mmoja anafanya kazi kupitia Rumi ya kipagani; kwa upande mwingine kupitia serikali yetu wenyewe.] moyo uliendelea kuwa mgumu zaidi; na aliposikia kwamba Kristo amefufuka, hakuhangaika sana. Alimuua Yakobo; na alipoona kuwa hili liliwapendeza Wayahudi, alimchukua Petro naye,

akikusudia kumuua. Lakini Mungu alikuwa na kazi kwa ajili ya Petro kufanya, na akamtuma malaika Wake kumwokoa. Herode alipatilizwa na hukumu za Mungu. Alipokuwa akijitukuza mbele ya umati mkubwa, alipigwa na malaika wa Bwana, akafa kifo cha kutisha mno. **{EW 185.2}**

Mapema asubuhi ya siku ya kwanza ya juma, kabla hakujapambazuka, wanawake watakatifu walikuja kaburini, wakileta manukato mazuri kwa ajili ya kuupaka mwili wa Yesu. Waligundua kwamba lile jiwe zito lilikuwa limevingirishwa mbali na mlango wa kaburi, na mwili wa Yesu haukuwapo. Mioyo yao ilifadhaika, na kuhofia kwamba maadui zao walikuwa wameuchukua mwili ule. Mara wakaona malaika wawili waliovaa mavazi meupe, nyuso zao ziking'aa na kuangaza. Viumbe hawa wa mbinguni walifahamu ni shuguli gani maalumu iliwaleta wanawake wale hapo na mara moja waliwaambia kwamba Yesu hakuwapo pale; Alikuwa amefufuka, lakini wangeweza kuona mahali ambapo alikuwa amelala. Waliwaambia waende kuwaambia wanafunzi Wake kwamba Yeye atawatangulia kwenda Galilaya. Kwa hofu kubwa na furaha, wanawake wale walirudi haraka kwa wale wanafunzi wenye huzuni na kuwaambia yale

waliyoyaona na kuyasikia.**{EW 186.1}**

Wanafunzi hawakuweza kuamini kwamba Kristo alikuwa amefufuka, lakini, pamoja na wanawake ambao walikuwa wameleta habari hii, walikimbia haraka kwenda kaburini. Waliona kwamba Yesu hakuwapo pale: waliona nguo zake za kitani, lakini hawakuweza kuamini habari njema kwamba Yeye alikuwa amefufuka kutoka kwa wafu. Walirudi nyumbani wakistaajabia yale waliyoyaona, na pia habari waliyoletewa na wanawake wale. Lakini Mariamu alichagua kukaa karibu na kaburi, akififikiria kile alichokiona, na kufadhaika na wazo kwamba inawezekana kuwa amedanganywa. Alihisi kwamba majaribu mapya yalikuwa yakimngojea. Huzuni yake ilifanywa upya, naye alianza kulia kwa uchungu. Aliinama na kuangalia tena ndani ya kaburi, na kuwaona malaika wawili waliovaa mavazi meupe. Mmoja alikuwa ameketi mahali ambapo kichwa cha Yesu kilikuwa kimelala, na mwingine mahali ambapo miguu Yake ilikuwa imelala. Walizungumza naye kwa upole, na kumuuliza kwa nini alikuwa analia. Akajibu, “Wamemwondoa Bwana wangu, wala mimi sijui walikomweka.”**{EW 186.2}**

Alipogeuka kutoka kaburini akamwona Yesu

amesimama karibu, lakini hakumjua. Alizungumza naye kwa upole, akiuliza sababu ya huzuni yake na kuuliza ni nani alikuwa akimtafuta. Akidhani kwamba alikuwa ni mtunza bustani, alimwomba, kwamba ikiwa ni Yeye Ndiye alimchukua Bwana wake, amwambie mahali alipomweka, ili amwondoe. Yesu alizungumza naye kwa sauti Yake Mwenyewe ya mbinguni, akisema, "Mariamu!" Aliijua sauti ile ya thamani, na pendwa, na kwa haraka alijibu, "Bwana!" na katika furaha yake alikuwa karibu kumkumbatia; lakini Yesu alisema, "Usinishike; kwa maana sijapaa kwenda kwa Baba. Lakini enenda kwa ndugu zangu, ukawaambie, Ninapaa kwenda kwa Baba Yangu, Naye ni Baba yenu; kwa Mungu Wangu, Naye ni Mungu wenu." Kwa furaha aliharakisha kwenda kwa wanafunzi akiwa na habari njema. Yesu alipaa kwa haraka kwenda Baba Yake apate kusikia kutoka katika midomo Yake kwamba aliikubali dhabihu ile, na kupokea mamlaka yote mbinguni na duniani.**{EW 187.1}**

Malaika kama wingu walimzunguka Mwana wa Mungu na kuyaambia malango ya milele yafunguliwe, ili Mfalme wa utukufu apate kuingia. Niliona kwamba wakati ule Yesu akiwa na jeshi lile angavu la mbinguni, mbele ya Mungu, na

kuzungukwa na utukufu Wake,  Yeye hakuwasahau wanafunzi Wake waliokuwa duniani, bali alipokea uweza kutoka kwa Baba Yake, ili aweze kurudi na kuwapa nguvu. Siku ile ile alirudi na kujionesha kwa wanafunzi Wake. Kisha akawaruhusu wamguse; kwa kuwa alikuwa amepaa kwenda kwa Baba Yake Naye amepokea uweza.**{EW 187.2}**

Wakati huo Tomaso hakuwepo. Hakuweza kupokea taarifa ya wanafunzi kwa unyenyekevu, bali kwa uthabiti na kujiamini alithibitisha kwamba asingeamini isipokuwa angeweka vidole vyake kwenye alama za misumari na mkono wake ubavuni ambapo mkuki wa kikatili ulichoma. Katika hili alionesha kutokuwa na imani na ndugu zake. Kama wote wangepaswa kuhitaji ushahidi sawa na huo, hakuna mtu kufikia wakati huo angekuwa amempokea Yesu na kuamini katika ufufuo wake. Lakini ilikuwa ni mapenzi ya Mungu kwamba taarifa ya wanafunzi iweze kupokelewa na wale ambao wenyewe wasingeweza kumwona na kumsikia Mwokozi aliyefufuka. Mungu hakupendezwa na kutokuamini kwa Tomaso. Yesu alipokutana tena na wanafunzi wake, Tomaso alikuwa pamoja nao; na alipomwona Yesu, aliamini. Lakini alikuwa ametangaza kwamba asingeridhika bila ushahidi

wa kuhisi kuongezwa katika ule wa kuona, na Yesu alimpa ushahidi ule ambao alikuwa ameutaka sana. Tomaso alipaza sauti, “Bwana wangu na Mungu wangu!” Lakini Yesu alimkaripia kwa sababu ya kutokuamini kwake, “Wewe, kwa kuwa umeniona, umesadiki; wa heri wale wasioona, wakasadiki.” **{EW 188.1}**

Vivyo hivyo wale ambao hawajapata uzoefu katika ujumbe wa malaika wa kwanza na wa malaika wa pili wanapaswa kupokea kutoka kwa wengine ambao walikuwa na uzoefu na kuufuatia ujumbe huo. Kama Yesu alivyokataliwa, hivyo niliona kwamba ujumbe huu umekataliwa. Na kama vile wanafunzi walivyotangaza kwamba hapana Jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu liwapasalo kuokolewa kwalo, vivyo hivyo watumishi wa Mungu wanapaswa pia kuwaonya kwa uaminifu na bila woga wale wanaokubali sehemu tu za Kweli zilizounganishwa na ujumbe wa malaika wa tatu, kwamba ni lazima wapokee kwa furaha ujumbe wote kama Mungu alivyowapa, au wasiwe na sehemu katika jambo hilo.**{EW 188.2}**

Wakati ule ambapo wanawake wale watakatifu walikuwa wakitoa habari ile kwamba Yesu alikuwa amefufuka, walinzi wa Kirumi walikuwa

wakivumisha uwongo ambao ulikuwa umetiwa vinywani mwao na wakuu wa makuhani na wazee, kwamba wanafunzi walikuja usiku, wakiwa wamelala, na kuuiba mwili wa Yesu. Shetani alikuwa ameweka uongo huu ndani ya mioyo na vinywa vya wakuu wa makuhani, na watu wakasimama tayari kupokea neno lao. Lakini Mungu alilifanya jambo hili kuwa hakika, na kuliweka tukio hili muhimu, ambalo wokovu wetu unalitegemea, juu ya shaka yoyote; na haikuwezekana kwa makuhani na wazee kulifunika. Mashahidi waliinuka kutoka kwa wafu kushuhudia ufufuo wa Kristo. **{EW 189.1}**

Yesu alidumu kuwa na wanafunzi Wake kwa siku arobaini, akiwafanya wawe na furaha na shangwe ya moyo wakati alipowafungulia kwa ukamilifu zaidi hali halisi ya ufalme wa Mungu. Aliwaagiza kutoa ushuhuda wa yale waliyoyaona na kuyasikia juu ya mateso, kifo, na ufufuo Wake, kwamba alikuwa ametoa dhabihu kwa ajili ya dhambi, na kwamba wote ambao wangependa wangekuja Kwake na kupata uzima. Kwa upole mwaminifu aliwaambia kwamba wangeteswa na kuhuzunishwa; lakini wangepata faraja katika kukumbuka uzoefu wao na kukumbuka maneno ambayo alikuwa amewaambia.

Aliwaambia kwamba alikuwa ameshinda majaribu ya Shetani na kupata ushindi kupitia maonjo na mateso. Shetani asingekuwa na nguvu zaidi juu Yake, lakini angeleta majaribu yake kuwaathiri zaidi moja kwa moja, wote ambao wangeliamini Jina Lake. Lakini wangeweza kushinda kama Yeye alivyoshinda. Yesu aliwapa wanafunzi wake uwezo wa kutenda miujiza, na aliwaambia kwamba ingawa wangeteswa na watu waovu, mara kwa mara angewatuma malaika Zake kuwaokoa; maisha yao yasingeweza kuchukuliwa hadi utume wao umekamilika; ndipo wangeweza kuhitajika kutia muhuri kwa damu yao shuhuda walizozibeba.**{EW 189.2}**

Wafuasi Wake wenye shauku walisikiliza mafundisho Yake kwa furaha, wakifurahia kwa shauku kila Neno lililoanguka kutoka kwenye midomo Yake mitakatifu. Sasa kwa hakika walijua kuwa Yeye Ndiye Mwokozi wa ulimwengu. Maneno Yake yalizama kwa kina ndani ya mioyo yao, na walihuzunika kwamba punde tu ni lazima waachane na Mwalimu wao wa mbinguni na wasisikie tena Maneno ya kufariji, ya ukarimu na neema kutoka katika midomo Yake. Lakini tena mioyo yao ilipatwa na joto kwa upendo na furaha kuu, pale Yesu

alipowaambia kwamba angeenda na kuwaandalia makao na kuja tena na kuwachukua, ili wapate kuwa pamoja Naye milele zote. Pia aliahidi kumtuma Mfariji, Roho Mtakatifu, kuwaongoza katika Ukweli wote. “Akainua mikono Yake akawabariki.”**{EW 190.1}**

## Sura ya 42-Kupaa kwa Kristo

Mbingu yote ilikuwa ikiisubiri saa ile ya ushindi wakati Yesu alipopaswa kupaa kwa Baba Yake. Malaika walikuja kumpokea Mfalme wa utukufu na kumsindikiza kwa shangwe kwenda mbinguni. Baada ya Yesu kuwabariki wanafunzi Wake, aliondoka kwao na kuchukuliwa kwenda juu. Na alipokuwa akipaa kwenda juu, kundi kubwa la watu waliofufuliwa wakati ule alipofufuka lilifuata. Umati mkubwa wa jeshi la mbinguni ulikuwapo, wakati huo mbinguni kundi la malaika wasiohesabika walingojea kuja Kwake. Walipokuwa wakipaa kwenda kwenye Jiji Takatifu, malaika waliomsindikiza Yesu walipaza sauti, "Inueni vichwa vyenu, enyi malango, Inukeni, enyi malango ya

milele, Mfalme wa utukufu apate kuingia." Malaika walioko jijini walipiga kelele kwa furaha nyingi, "Ni nani Mfalme wa utukufu?" Malaika waliosindikiza walipaza sauti kwa shangwe, “Bwana mwenye nguvu, hodari, Bwana hodari wa vita. Inueni vichwa vyenu, enyi malango, Naam, viinueni, enyi malango ya milele, Mfalme wa utukufu apate kuingia” Malaika wale wanaongojea wakauliza tena, "Ni nani Mfalme wa utukufu?" na malaika wale wasindikizaji wakajibu kwa nyimbo zenye sauti tamu, “Bwana wa majeshi, Yeye Ndiye Mfalme wa utukufu” Ndipo jeshi lote la mbinguni lilimzunguka Kamanda wao Mkuu, na kwa ibada ya kina na itokayo moyoni kabisa waliinama mbele Yake na kutupa taji zao zenye kung'aa miguuni Pake. Kisha walivigusa vinubi vyao vya dhahabu, na kwa nyimbo tamu zenye sauti nzuri waliijaza mbingu yote kwa muziki mtamu sana na nyimbo tamu kwa Mwana-Kondoo aliyechinjwa, lakini anaishi tena kwa fahari na utukufu.**{EW 190.2}**

Wanafunzi walipokuwa wakiangalia mbinguni kwa huzuni ili wapate kwa mara ya mwisho kumwona Bwana wao anayepaa, malaika wawili waliovaa mavazi meupe walisimama karibu nao na kuwaambia, "Enyi watu wa Galilaya, mbona

mmesimama mkitazama mbinguni? Huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja jinsi iyo hiyo mlivyomwona akienda Zake mbinguni.” Wanafunzi na mama wa Yesu, ambaye pamoja nao walishuhudia kupaa kwa Mwana wa Mungu, walitumia usiku uliofuata kuzungumza juu ya matendo Yake ya ajabu na matukio ya ajabu na matukufu ambayo yalikuwa yametokea ndani ya muda mfupi.**{EW 191.1}**

Shetani alishauriana tena na malaika wake, na kwa chuki kali dhidi ya serikali ya Mungu aliwaambia kwamba wakati bado ana nguvu na mamlaka yake duniani juhudi zao lazima ziwe na nguvu mara kumi zaidi dhidi ya wafuasi wa Yesu. Hawakuwa wameshinda chochote dhidi ya Kristo lakini ni lazima wawaangushe wafuasi Wake, ikiwezekana. Katika kila kizazi ni lazima wajitahidi kuwanasa wale ambao wangemwamini Yesu. Aliwasimulia malaika wake kwamba Yesu alikuwa amewapa wanafunzi Wake uwezo wa kuwakemea na kuwafukuza, na kuwaponya wale ambao wangewatesa. Kisha malaika wa Shetani wakatoka kama simba angurumaye, wakitafuta kuwaangamiza wafuasi wa Yesu.**{EW 191.2}**

## Sura ya 42- **Wanafunzi wa Kristo**

Kwa nguvu kubwa wanafunzi walimhubiri Mwokozi aliyesulubiwa na kufufuka. Ishara na maajabu vilifanywa na wao kwa Jina la Yesu; wagonjwa waliponywa; na mtu aliyekuwa kiwete tangu kuzaliwa Kwake alirejeshwa kwenye uzima mkamilifu na kuingia pamoja na Petro na Yohana hekaluni, akitembea na kurukaruka na kumsifu Mungu mbele ya watu wote. Habari hizi zilienea, na watu wakaanza kusongamana kuwazunguka wanafunzi. Wengi walikimbia pamoja, wakishangazwa sana na uponyaji ambao ulikuwa umefanywa.**{EW 192.1}**

Yesu alipokufa, makuhani walidhani kwamba hakuna miujiza zaidi ambayo ingefanywa kati yao, kwamba msisimko ule ungekufa na watu wangegeukia tena mapokeo ya wanadamu. Lakini tazama! Miongoni mwao kabisa wanafunzi walikuwa wakitenda miujiza, na watu walijawa na mshangao. Yesu alikuwa amesulubiwa, na walishangaa ni wapi wafuasi Wake walipata nguvu hii. Wakati alipokuwa hai, walidhani kwamba

aliwapa nguvu; lakini alipokufa, walitarajia kuwa miujiza ingekoma. Petro alifahamu mfadhaiko wao na kuwaambia, "Enyi Waisraeli, mbona mnastaajabia haya, au mbona mnatukazia macho sisi, kana kwamba tumemfanya huyu aende kwa nguvu zetu sisi, au kwa utauwa wetu sisi? Mungu wa Ibrahimu na wa Isaka na wa Yakobo, Mungu wa baba zetu, amemtukuza mtumishi Wake Yesu, ambaye ninyi mlimsaliti na kumkana mbele ya Pilato, alipokuwa ametoa hukumu Yake afunguliwe. Bali ninyi mlimkana Yule Mtakatifu, Yule Mwenye haki, mkataka mpewe mwuaji; mkamwua Yule Mkuu wa uzima, ambaye Mungu amemfufua katika wafu; na sisi tu mashahidi Wake. Na kwa imani katika Jina Lake, Jina Lake limemtia nguvu mtu huyu mnayemwona na kumjua; na imani ile iliyo Kwake Yeye imempatia huyu uzima huu mkamilifu mbele yenu ninyi nyote." **{EW 192.2}**

Wakuu wa makuhani na wazee hawakuweza kuyastahimili maneno hayo, kwa hiyo kwa amri yao Petro na Yohana walikamatwa na kuwekwa gerezani. Lakini maelfu walikuwa wameongoka na kuongozwa kuamini ufufuo na kupaa kwa Kristo kwa kusikia hotuba moja tu kutoka kwa wanafunzi. Makuhani na wazee walifadhaika. Walikuwa

wamemwua Yesu ili akili za watu ziweze kugeuzwa kuja kwao; lakini sasa jambo hilo lilikuwa baya kuliko hapo awali. Walituhumiwa waziwazi na wanafunzi kuwa wauaji wa Mwana wa Mungu, na hawakuweza kuonesha ni kiasi gani mambo haya yangeweza kukua au jinsi ambavyo wao wenyewe wangeweza kutazamwa na watu. Kwa furaha wangeweza kuwaua Petro na Yohana, lakini hawakuthubutu, kwa kuwaogopa watu. **{EW 193.1}**

Siku iliyofuata mitume hao walileta mbele ya baraza. Watu wale-wale ambao walikuwa wameililia kwa shauku damu ya Yule Mwenye Haki walikuwapo pale. Walimsikia Petro akimkana Bwana Wake kwa kulaani na kuapa aliposhtakiwa kuwa mmoja wa wanafunzi Wake, na walitumaini kumtisha tena. Lakini Petro alikuwa ameongoka, na sasa aliona fursa ya kuondoa doa la kukana huko kwa haraka, kwa uoga na kulitukuza Jina ambalo alilivunjia heshima. Kwa ujasiri mtakatifu, na kwa nguvu ya Roho, aliwatangazia bila woga, "Kwa Jina la Yesu Kristo wa Nazareti, ambaye ninyi mlimsulibisha, na Mungu akamfufua katika wafu, kwa Jina hilo mtu huyu anasimama ali mzima mbele yenu. Yeye Ndiye Jiwe lile lililodharauliwa na ninyi waashi, nalo limewekwa kuwa jiwe kuu la

pembeni. Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo.” **{EW 193.2}**

Watu walishangazwa na ujasiri wa Petro na Yohana na kujua ya kuwa walikuwa pamoja na Yesu; kwa maana mwenendo wao mzuri, usio na hofu ulikuwa kama ule wa Yesu alipokuwa mbele ya maadui Wake. Yesu, kwa sura moja ya masikitiko na huzuni, alimkemea Petro wakati alipomkana, na sasa anapomkiri Bwana wake kwa ujasiri, Petro alikubaliwa na kubarikiwa. Kama ishara ya kukubaliwa na Yesu, alijazwa na Roho Mtakatifu.**{EW 194.1}**

Makuhani hawakuthubutu kudhihirisha chuki waliyoihisi kwa wanafunzi. Waliwaamuru kutoka katika baraza, wakishauriana wao kwa wao, wakisema, “Tuwafanyie nini watu hawa? Maana ni dhahiri kwa watu wote wakaao Yerusalemu ya kwamba ishara mashuhuri imefanywa nao, wala hatuwezi kuikana.” Wakaogopa sana kuacha habari ya tendo hili jema kuenea miongoni mwa watu. Kama ingejulikana kwa ujumla, makuhani walihisi kwamba nguvu zao wenyewe zingepotea, nao wangetazamwa kama wauaji wa Yesu. Na yote

waliyothubutu kufanya ni kuwatishia mitume, na kuwaamuru wasiseme tena kwa Jina la Yesu, wasije wakafa. Lakini Petro alitamka kwa ujasiri kwamba wangeyasema yale waliyoyaona na kuyasikia.**{EW 194.2}**

Kwa nguvu za Yesu wanafunzi waliendelea kuwaponya watu walioteseka na wagonjwa walioletwa kwao. Mamia walijiandikisha kila siku chini ya bendera ya Mwokozi aliyesulubiwa, aliyefufuka, na kupaa. Makuhani na wazee, na wale ambao walijihusisha nao, walishtuka kwa hofu. Tena waliwaweka mitume gerezani, wakitumaini kwamba taharuki ingepungua. Shetani na malaika zake walifurahi; lakini malaika wa Mungu walifungua milango ya gereza, na, kinyume na amri ya wakuu wa makuhani na wazee, waliwaambia mitume, "Enendeni mkasimame hekaluni mkawaambie watu Maneno yote ya Uzima huu." **{EW 194.3}**

Baraza lilikutana na kutuma wafungwa wao waletwe. Wale maofisa wakafungua milango ya gereza, lakini wale waliokuwa wakiwatafuta hawakuwapo. Walirudi kwa wakuu wa makuhani na wazee, na kusema, “Gereza tumeikuta imefungwa salama, nao walinzi wamesimama mbele ya mlango;

lakini tulipoufungua hatukukuta mtu ndani.” "Mtu mmoja akaja akawapasha habari ya kwamba, Watu wale mliowaweka gerezani wako ndani ya hekalu, wamesimama wakiwafundisha watu. Ndipo yule jemadari akaenda pamoja na watumishi, wakawaleta, lakini si kwa nguvu, kwa maana waliogopa watu wasije wakawapiga kwa mawe. Walipowaleta, wakawaweka katika baraza. Kuhani Mkuu akawauliza, akisema, Je! Hatukuwaamuru ninyi kwa nguvu, msifundishe kwa Jina hili? Nanyi, tazameni, mmeijaza Yerusalemu mafundisho yenu, na mnataka kuileta damu ya mtu yule juu yetu.”**{EW 195.1}**

Viongozi hao wa Kiyahudi walikuwa wanafiki; walipenda sifa za wanadamu kuliko walivyompenda Mungu. Mioyo yao ilishupazwa kiasi kwamba matendo makuu na yenye nguvu kabisa, ya Mungu, yaliyofanywa na mitume yaliwakasirisha tu. Walijua kwamba ikiwa wanafunzi wangelimhubiri Yesu, kusulubiwa Kwake, ufufuo, na kupaa, ingekaza hatia juu yao kama wauaji Wake. Hawakuwa tayari kupokea damu ya Yesu kama wakati ule walipopaza sauti kwa nguvu, "Damu Yake na iwe juu yetu, na juu ya watoto wetu." **{EW 195.2}**

Mitume walitangaza kwa ujasiri kwamba

wanapaswa kumtii Mungu kuliko wanadamu. Petro alisema, “Mungu wa baba zetu alimfufua Yesu, ambaye ninyi mlimwua mkimtundika katika mti. Mtu huyo Mungu amemtukuza kwa mkono Wake wa kuume, awe Mkuu na Mwokozi, awape Waisraeli toba na msamaha wa dhambi. Na sisi tu mashahidi wa mambo haya, pamoja na Roho Mtakatifu ambaye Mungu amewapa wote wamtiio." Kwa Maneno haya ya ujasiri wauaji hao walikasirika, na wakaamua kuchafua tena mikono yao katika damu kwa kuwaua mitume. Walikuwa wanapanga kulifanya hili, wakati malaika kutoka kwa Mungu alipousukuma moyo wa Gamalieli kuwashauri makuhani na watawala: “ Jiepusheni na watu hawa, waacheni; kwa kuwa shauri hili au kazi hii ikiwa imetoka kwa binadamu, itavunjwa, lakini ikiwa imetoka kwa Mungu hamwezi kuivunja; msije mkaonekana kuwa mnapigana na Mungu.” Malaika waovu walikuwa wakiwachochea wakuu wa makuhani na wazee kuwaua mitume; lakini Mungu alimtuma malaika Wake alizuie hili kwa kuinua kutoka miongoni mwa viongozi wa Kiyahudi wenyewe sauti ya kuwatetea watumishi Wake. Kazi ya mitume haikukamilika. Walipaswa kupelekwa mbele ya wafalme ili kulishuhudia  Jina la Yesu na

kushuhudia juu ya mambo waliyoyaona na kuyasikia.**{EW 195.3}**

Makuhani bila kupenda, waliwaachilia wafungwa wao, baada ya kuwapiga na kuwaamuru wasiongee tena kwa Jina la Yesu. “Nao wakatoka katika ile baraza, wakifurahi kwa sababu wamehesabiwa kuwa wamestahili kuaibishwa kwa ajili ya Jina hilo. Na kila siku, ndani ya hekalu na nyumbani mwao, hawakuacha kufundisha na kuhubiri habari njema za Yesu kwamba ni Kristo.” HivyoNeno la Mungu likazidi kuenea na kukua. Wanafunzi walishuhudia kwa ujasiri kuhusu yale waliyoyaona na kuyasikia; na kupitia kwa Jina la Yesu walifanya miujiza mikubwa. Waliidai damu ya Yesu bila woga juu ya wale ambao walikuwa tayari sana kuipokea pale waliporuhusiwa kuwa na nguvu juu ya Mwana wa Mungu.**{EW 196.1}**

Niliona kwamba malaika wa Mungu waliagizwa kulinda kwa uangalifu maalum Kweli takatifu, zilizo muhimu ambazo zingetumika kama nanga kwa wanafunzi wa Kristo kupitia kila kizazi. Roho Mtakatifu alikaa juu ya mitume kwa namna ya pekee, ambao walikuwa ni mashahidi wa kusulubiwa kwa Bwana wetu, ufufuo, na kupaa—Kweli muhimu ambazo zilipaswa kuwa

tumaini la Israeli. Wote walipaswa kumtazama Mwokozi wa ulimwengu kama tumaini lao pekee, na kutembea katika njia ambayo alikuwa ameifungua kwa kafara ya maisha Yake Mwenyewe, na kutunza sheria ya Mungu na kuishi. Niliona hekima na wema wa Yesu katika kuwapa wanafunzi uwezo wa kuendelea na kazi ile ile ambayo kwayo alichukiwa na kuuawa na Wayahudi. Katika Jina Lake walikuwa na uwezo juu ya kazi za Shetani. Duara la nuru na utukufu lilizunguka juu wakati wa kifo na ufufuo wa Yesu, likiupa kutokufa Ukweli ule mtakatifu kwamba Alikuwa ni Mwokozi wa ulimwengu.**{EW 196.2}**

## Sura ya 43 -Kifo cha Stefano

Wanafunzi waliongezeka sana huko Yerusalemu, na makuhani wengi waliitii imani. Stefano, aliyejaa imani, alikuwa akifanya maajabu na miujiza mikubwa miongoni mwa watu. Viongozi wa Kiyahudi walichochewa kwa hasira kubwa walipoona makuhani wakigeuka kutoka katika mapokeo yao, na kutoka katika kafara na sadaka, na kumkubali Yesu kama dhabihu kuu. Kwa nguvu kutoka juu, Stefano aliwakemea makuhani na

wazee wasioamini, na kumtukuza Yesu mbele yao. Hawakuweza kustahimili hekima na nguvu alizozungumza nazo, na walipoona kwamba hawawezi kumshinda kwa chochote, waliajiri watu kuapa kwa uwongo kwamba walikuwa wamemsikia akisema maneno ya kufuru dhidi ya Musa na dhidi ya Mungu. Waliwachochea watu na kumchukua Stefano, na, kupitia kwa mashahidi wa uwongo, walimshtaki kwa kusema kinyume na hekalu na sheria. Walisema huu ni ushuhuda wao kwamba walimsikia akisema kwamba huyu Yesu wa Nazareti angeziharibu desturi ambazo Musa alikuwa amewapa. **{EW 197.1}**

Stefano aliposimama mbele ya wahukumu wake, nuru ya utukufu wa Mungu ilikaa juu ya uso wake. “Watu wote walioketi katika ile baraza wakamkazia macho yao, wakamwona uso wake kuwa kama uso wa malaika.” Alipoitwa kujibu mashtaka yaliyoletwa dhidi yake, alianza kwa Musa na manabii na kupitia historia ya wana wa Israeli na kushughulika kwa Mungu pamoja nao na kuonesha jinsi Kristo alivyokuwa ametabiriwa katika unabii. Alirejelea historia ya hekalu na kutangaza kwamba Mungu hakai katika mahekalu yaliyotengenezwa kwa mikono. Wayahudi waliabudu hekalu na walijawa na

ghadhabu kubwa zaidi kwa kitu chochote kilichosemwa dhidi ya jengo hilo kuliko kama kingesemwa dhidi ya Mungu. Stefano alipokuwa anaongea juu ya Kristo na kurejelea hekalu, aliona kwamba watu walikuwa wakikataa maneno yake; na bila woga akawakemea: “Enyi wenye shingo gumu, msiotahiriwa mioyo wala masikio, siku zote mnampinga Roho Mtakatifu.” Huku wakishika maagizo ya nje ya dini yao, mioyo yao ilipotoka na kujaa uovu wa kufisha. Alirejelea ukatili wa baba zao katika kuwatesa manabii, na kutangaza kwamba wale ambao alikuwa akiwahutubia walikuwa wamefanya dhambi kubwa katika kumkataa na kumsulubisha Kristo. “Ni yupi katika manabii ambaye baba zenu hawakumwudhi? Nao waliwaua wale waliotabiri habari za kuja Kwake Yule Mwenye Haki; ambaye ninyi sasa mmekuwa wasaliti Wake, mkamwua." **{EW 198.1}**

Ukweli huu wa wazi, unaochoma uliponenwa, makuhani na watawala walikasirika, na walimvamia Stefano, wakisaga meno yao. “Lakini yeye akijaa Roho Mtakatifu, akakaza macho yake, akitazama mbinguni, akauona utukufu wa Mungu,” na kusema, “Tazama! Naona mbingu zimefunguka, na Mwana wa Adamu amesimama mkono wa kuume wa

Mungu.” Watu hawakumsikia. “Wakapiga kelele kwa sauti kuu, wakaziba masikio yao, wakamrukia kwa nia moja, wakamtoa nje ya mji, wakampiga kwa mawe.” Naye akapiga magoti, akapaza sauti kuu, 'Bwana, usiwahesabie dhambi hii.” **{EW 198.2}**

Niliona kwamba Stefano alikuwa shujaa hodari wa Mungu, hasa aliyeinuliwa juu ili kujaza nafasi muhimu katika kanisa. Shetani alifurahia kifo chake; kwa kuwa alifahamu kuwa wanafunzi wangehisi sana hasara ya kutokuwapo kwake. Lakini ushindi wa Shetani ulikuwa ni wa muda mfupi; kwa kuwa katika kundi hilo, lililokuwa linashuhudia kifo cha Stefano, alikuwapo mmoja ambaye Yesu mwenyewe angejifunua kwake. Sauli hakushiriki katika kurusha mawe kwa Stefano, lakini bado alikubali kifo chake. Alikuwa na usongo katika kulitesa kanisa la Mungu, akiwawinda, kuwakamata katika nyumba zao, na kuwakabidhi kwa wale ambao wangewaua. Sauli alikuwa mtu mwenye uwezo na elimu; bidii na elimu yake vilimfanya aheshimiwe sana na Wayahudi, huku akiogopwa na wanafunzi wengi wa Kristo. Vipaji vyake vilitumiwa vizuri na Shetani katika kuendeleza uasi wake dhidi ya Mwana wa Mungu, na wale waliomwamini Yeye. Lakini Mungu anaweza kuvunja nguvu za adui

mkubwa na kuwaweka huru wale wanaoongozwa kuwa mateka. Kristo alikuwa amemchagua Sauli kama "chombo kiteule" kulihubiri Jina Lake, kuwaimarisha wanafunzi Wake katika kazi yao, kujaza na kuzidi mahali pa Stefano.**{EW 199.1}**

## Sura ya 44 -Uongofu wa Sauli

Wakati Sauli alipokuwa akisafiri kwenda Dameski, akiwa na barua zilizompa kibali cha kuwachukua wanaume au wanawake ambao walikuwa wakimhubiri Yesu, na kuwaleta Yerusalemu wakiwa wamefungwa, malaika waovu walishangilia sana, na kumzunguka. Lakini ghafla nuru kutoka mbinguni ilimulika pande zote kumzunguka, ambayo iliwafanya malaika wale waovu kukimbia na kumfanya aanguke chini ghafla. Ndipo akasikia sauti ikisema, “Sauli, Sauli, mbona waniudhi?” Sauli aliuliza, "U nani Wewe, Bwana?" Naye Bwana akajibu, “Mimi Ndimi Yesu unayeniudhi wewe: Ni vigumu kwako kuupiga mateke mchokoo.” Na Sauli huku akitetemeka na kustaajabu, aliuliza, “Bwana wataka nifanye nini?” Naye Bwana akasema, “Simama, uingie mjini, nawe utaambiwa yakupasayo kutenda.” **{EW 200.1}**

Wale watu waliokuwa pamoja naye walisimama kimya, wakisikia sauti, lakini wasimwone mtu. Nuru ile ilipopita na Sauli akainuka kutoka ardhini na kufungua macho yake, alijikuta hawezi kuona kabisa. Utukufu wa nuru ya mbinguni ulikuwa umempofusha. Basi wakamwongoza kwa kumshika mkono wakamleta Dameski; naye kwa siku tatu alikuwa haoni, wala hakula, wala kunywa. Kisha Bwana akamtuma malaika Wake kwa mmoja wa wale watu ambao hasa Sauli alitarajia kuwachukua mateka na kumfunulia katika maono kwamba aende katika barabara inayoitwa Nyofu, "ukaulize katika nyumba ya Yuda mtu aitwaye Sauli, wa Tarso; maana, angalia, anaomba; naye amemwona mtu, jina lake Anania, akiingia, na kumwekea mikono juu yake, apate kuona tena." **{EW 200.2}**

Anania aliogopa kwamba kunaweza kuwa na makosa katika jambo hili, na akaanza kumsimulia Bwana kile alichokisikia kuhusu Sauli. Lakini Bwana akamwambia Anania, "Nenda tu; kwa maana huyu ni chombo kiteule Kwangu, alichukue Jina Langu mbele ya Mataifa, na wafalme, na wana wa Israeli. Maana nitamwonyesha yalivyo mengi yatakayompasa kuteswa kwa ajili ya Jina Langu." Anania aliyafuata maelekezo ya Bwana, akaingia

katika nyumba ile, na huku akiweka mikono yake juu yake, alisema, “Ndugu Sauli, Bwana amenituma, Yesu, Yeye aliyekutokea katika njia uliyoijia, upate kuona tena, na ukajazwe Roho Mtakatifu.” **{EW 200.2}**

Mara ile Sauli akapata kuona na akainuka na kubatizwa. Baada ya hapo akawa anafundisha katika masinagogi kwamba Yesu hakika alikuwa ni Mwana wa Mungu. Wote waliomsikia walishangaa na kuuliza, “Siye huyu aliyewaharibu walioliitia Jina hili huko Yerusalemu? Na hapa alikuwa amekuja kwa kusudi hilo, awafunge na kuwapeleka kwa wakuu wa makuhani?” Lakini Sauli akazidi kupata nguvu, na kuwafadhaisha Wayahudi. Kwa mara nyingine tena walikuwa katika shida. Wote walifahamu upinzani wa Sauli kwa Yesu na bidii yake katika kuwatafuta na kuwatoa wapate kuuawa wale wote walioliamini Jina Lake; na uongofu wake wa kustaajabisha uliwashawishi wengi kwamba Yesu alikuwa ni Mwana wa Mungu. Sauli alisimulia kuhusu uzoefu wake katika nguvu za Roho Mtakatifu. Alikuwa akiwatesa hadi kufa, akiwafunga na kuwatupa gerezani wanaume na wanawake, wakati ule, alipokuwa safirini kwenda Dameski, ghafla nuru kubwa kutoka mbinguni ilimmulika

pande zote, na Yesu alijifunua kwake, na kumfundisha kwamba alikuwa ni Mwana wa Mungu.**{EW 201.1}**

Sauli alipokuwa akimhubiri hivyo Yesu kwa ujasiri, alitoa mvuto wenye nguvu. Alikuwa na ujuzi wa Maandiko, na baada ya uongofu wake nuru ya Kiungu iliangaza juu ya unabii kuhusu Yesu, ambayo ilimwezesha kuuwasilisha Ukweli kwa uwazi na kwa ujasiri na kusahihisha upotovu wowote wa Maandiko. Huku Roho wa Mungu akiwa juu yake, kwa namna ya wazi na yenye nguvu angewachukua wasikilizaji wake kupitia unabii hadi wakati wa ujio wa kwanza wa Kristo na kuwaonesha kwamba maandiko yalikuwa yametimizwa ambayo yalirejelea mateso, kifo, na ufufuo Wake.**{EW 201.2}**

## Sura ya 45-Wayahudi Wanaamua Kumuua Paulo

Wakuu wa makuhani na watawala waliposhuhudia matokeo ya maelezo ya uzoefu wa Paulo, walisukumwa kuwa na chuki dhidi yake. Waliona kwamba alimhubiri Yesu kwa ujasiri na kufanya miujiza kwa Jina Lake, kiasi kwamba umati wa watu ulimsikiliza na kuyaacha mapokeo yao na

kuwatazama viongozi wa Kiyahudi kama wauaji wa Mwana wa Mungu. Hasira yao iliwaka, nao wakakusanyika ili wapate kushauriana kuhusu ni nini kilicho bora zaidi kufanyika ili kuiangusha taharuki hiyo. Walikubaliana kwamba njia pekee iliyo salama ilikuwa ni kumuua Paulo. Lakini Mungu alijua nia yao, na malaika waliagizwa kumlinda, ili aweze kuishi na kutimiza utume Wake. **{EW 202.1}**

Wakiongozwa na Shetani, Wayahudi wasioamini waliyalinda malango ya Dameski mchana na usiku, ili Paulo atakapokuwa akipita, waweze kumuua mara moja. Lakini Paulo alikuwa ametaarifiwa kwamba Wayahudi walikuwa wanayatafuta maisha yake, na wanafunzi walimshusha ukutani kwenye kikapu usiku. Katika kushindwa huku kutekeleza malengo yao, Wayahudi waliaibika na kukasirika, na lengo la Shetani likashindwa. **{EW 202.2}**

Baada ya hili, Paulo alikwenda Yerusalemu apate kujiunga na wanafunzi; lakini wote walimwogopa. Hawakuweza kuamini kuwa alikuwa ni mwanafunzi. Maisha yake yalikuwa yanawindwa na Wayahudi huko Dameski, na ndugu zake mwenyewe hawakukubali kumpokea; lakini Barnaba alimchukua na kumleta kwa mitume, na kuwaarifu jinsi alivyokuwa amemwona Bwana njiani na

kwamba alikuwa amehubiri kwa ujasiri huko Dameski kwa Jina la Yesu. **{EW 202.3}**

Lakini Shetani alikuwa akiwachochea Wayahudi wamwangamize Paulo, na Yesu alimwamuru aondoke Yerusalemu. Kwa kushirikiana na Barnaba, alienda katika miji mingine, akimhubiri Yesu na kufanya miujiza, na wengi waliongoka. Mtu mmoja aliponywa ambaye siku zote alikuwa ni kilema, watu walioabudu sanamu walikuwa karibu kutoa kafara kwa wanafunzi. Paulo alihuzunika, na akawaambia kwamba yeye na mfanyakazi mwenzake walikuwa watu tu na kwamba Mungu aliyeumba mbingu na nchi, bahari na vitu vyote vilivyomo, Ndiye peke Yake anapaswa kuabudiwa. Hivyo Paulo alimtukuza Mungu mbele ya watu; lakini aliweza kuwazuia mara chache tu. Dhana ya kwanza ya imani katika Mungu wa Kweli, na ibada na heshima inayostahili Kwake, ilikuwa inaundwa katika akili zao; na walipokuwa wakimsikiliza Paulo, Shetani alikuwa akiwasisitiza Wayahudi wasioamini wa miji mingine kumfuata Paulo na kuharibu kazi nzuri iliyofanywa kupitia kwake. Wayahudi hawa walichochea akili za wale waabudu sanamu kwa taarifa za uongo dhidi ya Paulo. Mshangao na kuvutiwa kwa watu sasa vilibadilika kuwa chuki, na wale ambao muda mfupi

kabla walikuwa tayari kuwaabudu wanafunzi, walimpiga Paulo kwa mawe na kumvuta nje ya mji, wakidhani kwamba alikuwa amekufa. Wanafunzi walipokuwa wamemzunguka Paulo na kumwombolezea, kwa furaha yao Paulo aliinuka na kwenda pamoja nao mjini. **{EW 203.1}**

Tena, Paulo na Sila walipokuwa wakimhubiri Yesu, mwanamke mmoja aliyepagawa na roho ya uaguzi aliwafuata, akisema, "Watu hawa ni watumishi wa Mungu aliye juu, wenye kuwahubiria njia ya wokovu." Kwa jinsi hiyo aliwafuata wanafunzi hawa siku nyingi. Lakini Paulo alihuzunika; kwa kuwa kupiga kelele huku kuligeuza mawazo ya watu kutoka katika ile Kweli. Lengo la Shetani katika kumwongoza kufanya hivi lilikuwa ni kuwachukiza watu na kuharibu mvuto wa wanafunzi. Roho ya Paulo iliamka ndani yake, naye aligeuka, na kumwambia yule roho, "Nakuamuru kwa  Jina la Yesu Kristo mtoke huyu"; yule roho mchafu alikaripiwa, akamwacha yule binti.**{EW 203.2}**

Mabwana zake walifurahi kwa kuwa aliwapigia kelele wanafunzi wale. Lakini yule pepo mchafu alipomwacha, nao wakamwona akiwa mwanafunzi mpole wa Kristo, walikasirika. Walikuwa

wamekusanya pesa nyingi sana kwa sababu ya utabiri wake, na sasa tumaini la faida yao likawa limemekwisha. Lengo la Shetani likashindwa; lakini watumishi wake waliwakamata Paulo na Sila, wakawavuta mpaka sokoni, kwa wakuu na makadhi, wakisema, “Watu hawa wanachafua sana mji wetu, nao ni Wayahudi.” Kundi la watu likainuka pamoja dhidi yao, Wale makadhi wakawavua Paulo na Sila nguo zao, wakaamuru wapigwe viboko. Na baada ya kupewa mapigo mengi, wakawatupa gerezani, wakimwamuru mlinzi wa gereza kuwalinda salama, ambaye, baada ya kupokea agizo kama hilo, aliwatia katika gereza la ndani na kufunga miguu yao kwa mikatale. Lakini malaika wa Bwana walifuatana nao ndani ya kuta za gereza, na kusababisha kifungo chao kuutangaza utukufu wa Mungu, na kuwaonesha watu kwamba Mungu alikuwa katika kazi hiyo, na pamoja na watumishi Wake wateule.**{EW 204.1}**

Panapo usiku wa manane Paulo na Sila walikuwa wakimwomba Mungu na kumwimbia nyimbo za kumsifu. Ghafula pakawa na tetemeko kuu la nchi, hata misingi ya gereza ikatikisika; Nami niliona kwamba mara moja malaika wa Mungu alifungua vifungo vya kila mmoja. Mlinzi wa gereza,

alipoamka na kuona milango ya gereza ikiwa imefunguliwa, aliogopa sana. Alidhani kwamba wafungwa walikuwa wametoroka, na kwamba lazima aadhibiwe kwa kifo. Lakini alipokaribia kujiua, Paulo alipaza sauti kwa nguvu: "Usijidhuru kwa maana sisi sote tuko hapa." **{EW 204.2}**

Nguvu za Mungu zilimsadikisha mlinzi wa gereza. Aliita aletewe taa, akaingia ndani akitetemeka, akaanguka chini mbele ya Paulo na Sila, akawaleta nje, akasema, "Bwana zangu, yanipasa nifanye nini nipate kuokoka?" Wao wakamjibu, "Mwamini Bwana Yesu nawe utaokoka pamoja na nyumba yako." Kisha mlinzi wa gereza aliwaleta pamoja watu wote wa nyumbani mwake, na Paulo aliwahubiria habari za Yesu. Hivyo moyo wa mlinzi wa gereza uliungana na ile ya wale ndugu zake, naye aliosha mapigo yao, na yeye na nyumba yake yote walibatizwa usiku huo. Kisha akawaandalia chakula, akafurahi, akimwamini Mungu pamoja na nyumba yake yote. **{EW 205.1}**

Habari hizi za ajabu za udhihirisho wa uweza wa Mungu katika kufungua milango ya gereza, na katika uongofu wa mlinzi na familia yake, zilienea upesi. Watawala walisikia kuhusu mambo hayo, nao waliogopa, wakamtuma mkuu wa gereza, wakimwomba awaruhusu Paulo na Sila waende zao.

Lakini Paulo hakutaka kuondoka gerezani kwa njia ya siri; hakuwa tayari kwamba udhihirisho wa uweza wa Mungu ufichwe. Aliwaambia, “Wametupiga mbele ya watu wote bila kutuhukumu, na sisi tu Warumi, tena wametutupa gerezani; na sasa wanataka kututoa kwa siri? Sivyo, lakini na waje wenyewe wakatutoe.” Maneno haya yaliposemwa kwa makadhi, na ikajulikana kuwa mitume walikuwa raia wa Kirumi, watawala waliogopa kwa kuogopa kwamba wangelalamika kwa mfalme juu ya kutendewa kinyume cha sheria. Hivyo, walikwenda kuwataka radhi na baada ya kuwatoa ndani waliwaomba watoke katika mji ule.**{EW 205.2}**

## Sura ya 46 -Paulo Anazuru Yerusalemu

Baada ya Paulo kuongoka, alitembelea Yerusalemu na huko alimhubiri Yesu na maajabu ya neema Yake. Alisimulia uongofu wake wa kustaajabisha, ambao uliwakasirisha sana makuhani na watawala kiasi kwamba walitafuta kumuua. Lakini ili aweze kuokolewa, Yesu alimtokea tena katika maono alipokuwa akiomba, na kumwambia, “Hima, utoke Yerusalemu upesi, kwa

sababu hawatakubali ushuhuda wako katika habari Zangu.” Paulo alijibu, "Bwana, wanajua hao ya kuwa mimi nalikuwa nikiwafunga gerezani wale wanaokuamini na kuwapiga katika kila sinagogi. Na damu ya Stefano shahidi Wako ilipomwagwa, mimi nami nilikuwa nikisimama karibu, nikikubali, na kuzitunza nguo zao waliomwua." Paulo alidhani kwamba Wayahudi wa Yerusalemu wasingeweza kuupinga ushuhuda wake; kwamba wangeweza kuona kwamba badiliko lile kubwa ndani yake lingeweza kufanywa kwa nguvu ya Mungu peke yake. Lakini jibu lilikuwa thabiti zaidi kuliko hapo awali: "Enenda zako; kwa kuwa Mimi nitakutuma uende mbali kwa watu wa Mataifa."**{EW 206.1}**

Wakati Paulo hakuwapo Yerusalemu, aliandika barua nyingi kwenda sehemu mbalimbali, akielezea uzoefu wake na kutoa ushuhuda wenye nguvu. Lakini baadhi walijitahidi kuharibu uwezo wa barua hizo. Walilazimika kukubali kwamba barua zake zilikuwa zilikuwa na maneno ya uzito, yenyemaana na nguvu, lakini walitangaza kwamba uwepo wake wa kimwili ulikuwa dhaifu na maneno yake yalikuwa ni za kuchukiza. **{EW 206.2}**

Uhalisia katika jambo hilo ilikuwa kwamba Paulo alikuwa ni mtu mwenye elimu kubwa, na

hekima yake na tabia yake viliwavutia wasikilizaji wake. Wasomi walipendezwa na maarifa yake, na wengi wao walimwamini Yesu. Alipokuwa mbele ya wafalme na mikusanyiko mikubwa, angeongea kwa umbuji ambao ungewavutia wote waliokuwa mbele yake. Jambo hili liliwakasirisha sana makuhani na wazee. Paulo angeweza kuingia kirahisi katika kutoa hoja kwa kina na, na kupembua mambo kwa hekima, pale anapopaa juu, angewabeba watu pamoja naye kwa namna ya mfululizo wa mawazo yaliyoinuliwa mno, akifanya kuonekana utajiri wa kina wa neema ya Mungu na kuonesha mbele yao taswira ya upendo wa kushangaza wa Kristo. Kisha kwa usahili angeshuka chini katika uelewa wa watu wa kawaida na kwa namna yenye nguvu mno kusimulia uzoefu wake, ambao uliotaka kutoka kwao shauku kubwa ya kuwa wanafunzi wa Kristo. **{EW 206.3}**

Kwa mara nyingine Bwana alimtokea Paulo na kumfunulia kwamba ni lazima apande kwenda Yerusalemu, ili apate kufungwa huko na kuteseka kwa ajili ya Jina Lake. Ingawa alikuwa ni mfungwa kwa muda mrefu, lakini Bwana aliendelea na kazi Yake maalum kupitia kwake. Vifungo vyake vilipaswa kuwa njia ya kueneza maarifa juu ya

Kristo na hivyo kumtukuza Mungu. Kadiri alivyotumwa kutoka mji hadi mji kwa ajili ya mashtaka yake, ushuhuda wake juu ya Yesu na matukio ya kuvutia ya uongofu wake mwenyewe vilisimuliwa mbele ya wafalme na maliwali, ili wapate kuachwa bila udhuru kuhusu Yesu. Maelfu walimwamini na kulifurahia Jina Lake. Niliona kwamba kusudi maalum la Mungu lilitimizwa katika safari za Paulo baharini; Alipanga kwamba wafanyakazi wa meli waweze kushuhudia nguvu za Mungu kupitia kwa Paulo na kwamba wapagani pia wapate kusikia Jina la Yesu, na kwamba wengi wapate kuongoka kupitia kwa mafundisho ya Paulo na kwa kushuhudia miujiza aliyoifanya. Wafalme na maliwali walivutiwa na utoaji wake wa hoja, na jinsi ambavyo kwa bidii na kwa nguvu ya Roho Mtakatifu alimhubiri Yesu na kusimulia matukio ya kupendeza ya uzoefu wake, usadikisho uliweka msisitizo kwao kwamba Yesu alikuwa Mwana wa Mungu. Wakati wengine waliona ajabu kwa mshangao walipomsikiliza Paulo, mmoja wao alisema kwa sauti kubwa, “Kwa maneno machache wadhani kunifanya mimi kuwa Mkristo.” Hata hivyo wengi wa wale waliomsikia walidhani kwamba wakati fulani ujao wangeweza kuzingatia kile walichokisikia.

Shetani alitumia vizuri uhairishaji huo, na, walipopuuza fursa ile wakati ambapo mioyo yao ilikuwa imelainishwa,  nafasi hiyoilipotea milele. Mioyo yao ilishupazwa na kuwa migumu.**{EW 207.1}**

Nilioneshwa kazi ya kwanza ya Shetani katika kuwapofusha macho Wayahudi ili wasiweze kumpokea Yesu kama Mwokozi wao; na kilichofuata katika kuwaongoza, kupitia wivu kwa sababu ya matendo Yake makuu, kutaka sana maisha Yake. Shetani aliingia ndani ya mmoja wa wafuasi wa Kristo Mwenyewe na akamwongoza katika kumsaliti mikononi mwa adui Zake, ili wapate kumsulubisha Bwana wa uzima na utukufu.**{EW 208.1}**

Baada ya Yesu kufufuka kutoka kwa wafu, Wayahudi waliongeza dhambi juu ya dhambi pale walipojitahidi kuficha Ukweli wa ufufuo Wake kwa kuwaajiri walinzi wa Kirumi wapate kushuhudia uwongo. Lakini ufufuo wa Yesu ulifanywa kuwa hakika maradufu kwa ufufuo wa mashahidi wengi kwa wakati huo huo. Baada ya kufufuka Kwake, Yesu aliwatokea wanafunzi Wake, na zaidi ya watu mia tano mara moja, wakati huo wale aliowafufua pamoja Naye waliwatokea wengi, wakitangaza kwamba Yesu amefufuka.**{EW 208.2}**

Shetani aliwasababisha Wayahudi kumwasi Mungu kwa kukataa kumpokea Mwanawe, na kwa kutia madoa mikono yao kwa damu Yake ya thamani kubwa. Haidhuru ni ushahidi wenye nguvu kiasi gani unaotolewa sasa kwamba Yesu alikuwa ni Mwana wa Mungu, Mkombozi wa ulimwengu, watu hawa walimuua, na wasingepokea ushahidi wowote kwa ajili ya utetezi Wake. Tumaini lao pekee na faraja, kama lile la Shetani baada ya kuanguka kwake, lilikuwa ni katika kujaribu kumshinda Mwana wa Mungu. Kwa hiyo waliendeleza uasi wao kwa kuwatesa wanafunzi wa Kristo, na kuwaua. Hakuna kitu kilichoanguka kwa kuchukiza masikioni mwao kama Jina la Yesu waliyemsulubisha; nao waliazimia kutokusikiliza ushahidi wowote kwa niaba Yake. Kama wakati Roho Mtakatifu kupitia kwa Stefano alivyotangaza ushahidi mkubwa wa Yesu kuwa Mwana wa Mungu, waliziba masikio yao wasije wakasadikishwa. Shetani aliwakamata kwa nguvu wauaji wale wa Yesu mkononi mwake. Kwa matendo maovu walikuwa wamejisalimisha wenyewe kuwa raia wake watiifu, na kupitia kwao alikuwa kazini akiwasumbua na kuwaudhi waumini wa Kristo. Alifanya kazi kupitia Wayahudi ili kuwachochea watu wa mataifa dhidi ya Yesu na

dhidi ya wale waliomfuata. Lakini Mungu alituma malaika Wake kuwaimarisha wanafunzi katika kazi yao, ili washuhudie mambo waliyoyaona na kuyasikia, na mwishowe kwa uthabiti wao, watie muhuri ushuhuda wao kwa damu yao.**{EW 208.2}**

Shetani alifurahi kwamba Wayahudi walikuwa salama katika mtego wake. Bado waliendelea na desturi zao zisizo na maana, kafara zao, na ibada zao. Yesu alipokuwa ametundikwa msalabani na kupaza sauti, "Imekwisha," pazia la hekalu lilipasuka vipande viwili kutoka juu hadi chini, kuashiria kwamba Mungu hatakutana tena na makuhani hekaluni, kupokea dhabihu kaida na ibada zao, na pia kuonesha kwamba ukuta uliotenga kati ya Wayahudi na Mataifa ulikuwa umevunjwa. Yesu alikuwa amejitoa Mwenyewe kuwa sadaka kwa ajili ya wote, na ikiwa kwa vyovyote wataokolewa, wote ni lazima wamwamini Yeye kama sadaka pekee ya dhambi, Mwokozi wa ulimwengu.**{EW 209.1}**

Askari alipomchoma Yesu ubavuni alipokuwa ametundikwa msalabani, vijito viwili tofauti vilitokea, kimoja cha damu na kingine cha maji. Damu hiyo ilikuwa ni ya kuosha dhambi za wale ambao wangeliamini Jina Lake, na maji yalikuwa yakiwakilisha maji yale yaliyo hai ambayo

yanapatikana kutoka kwa Yesu kwa ajili ya kutoa uzima kwa muumini.**{EW 209.2}**

## Sura ya 47 -Uasi Mkuu

Nilipelekwa mbele hadi wakati ambapo waabudu sanamu wa kipagani waliwatesa kikatili na kuwaua Wakristo. Damu ilitiririka kwa mbubujiko wa nguvu. Wakuu, wenye elimu, na watu wa kawaida waliuawa sawa bila huruma. Familia tajiri zilifanywa kuwa maskini, kwa sababu hazikuweza kuiacha dini yao. Licha ya mateso na maumivu ambayo Wakristo hawa waliyavumilia, hawakukubali kushusha kiwango. Waliidumisha dini yao kuwa safi. Niliona kwamba Shetani alifurahia na kushangilia mateso yao. Lakini Mungu aliwaangalia wafia dini Wake waaminifu kwa ukubali mkuu. Wakristo walioishi katika wakati ule wa kuogofya walipendwa sana na Yeye, kwa sababu walikuwa tayari kuteseka kwa ajili Yake. Kila mateso waliyoyavumilia yaliongeza thawabu yao mbinguni.**{EW 210.1}**

Ingawa Shetani alilifurahi kwa ajili ya mateso ya watakatifu, bado hakuridhika. Alitaka udhibiti wa akili na mwili pia. Mateso ambayo waliyavumilia yaliweza tu kuwaendesha kwenda karibu zaidi na Bwana, yakiwaongoza kupendana kila mtu na mwenzake, na kuwafanya waogope zaidi kuliko wakati wowote ule kumkosea Mungu. Shetani alitaka sana apate kuwaongoza kumchukiza Mungu; kisha wangepoteza nguvu, ujasiri na uthabiti wao. Ingawa maelfu waliuawa, lakini bado wengine walikuwa wakiinuka ili kujaza nafasi zao. Shetani aliona kwamba alikuwa anawapoteza raia wake; kwa maana ingawa walipitia mateso na kifo, lakini bado walikuwa salama kwa Yesu Kristo, kuwa raia wa ufalme Wake. Kwa hiyo Shetani aliweka mipango yake ya kupigana kwa mafanikio zaidi dhidi ya serikali ya Mungu na kulipindua kanisa. Aliwaongoza waabudu sanamu wapagani kukubali sehemu ya imani ya Kikristo. Walidai kuamini katika kusulubiwa na kufufuka kwa Kristo, na wakapendekeza kuungana na wafuasi wa Yesu, pasipokuwa na badiliko la moyo. Lo, hatari ya kutisha ya kanisa. Ulikuwa ni wakati wa maumivu makali ya akili. Wengine walidhani kwamba ikiwa watashuka na kuungana na wale waabudu sanamu

ambao walikuwa wamekubali sehemu ya imani ya Kikristo, ingekuwa ndiyo njia ya uongofu wao kamili. Shetani alikuwa akitafuta kuyapotosha Mafundisho ya Biblia.**{EW 210.2}**

Niliona kwamba mwishowe kiwango kilishushwa, na kwamba wapagani walikuwa wakiungana na Wakristo. Ingawa waabudu hawa wa sanamu walidai kuwa wameongoka, walileta ibada yao ya sanamu ndani ya kanisa, wakibadilisha tu vitu vya ibada yao kuwa sanamu za watakatifu, na hata Kristo na Mariamu mama Yake. Kadiri wafuasi wa Kristo walivyoungana nao kidogo kidogo, dini ya Kikristo iliharibiwa na kanisa lilipoteza usafi na nguvu zake. Wengine walikataa kuungana nao; watu kama hao walilinda usafi wao na kumwabudu Mungu peke Yake. Wasingesujudu sanamu ya kitu chochote kilichoko mbinguni juu au duniani chini!**{EW 211.1}**

Shetani alifurahi juu ya kuanguka kwa wengi kiasi hicho; na kisha akalichochea kanisa lililoanguka lipate kuwalazimisha wale ambao walihifadhi usafi wa dini yao ama kusalimu amri kwa desturi zao na ibada za sanamu au kuuawa. Mioto ya mateso iliwaka tena dhidi ya kanisa la Kweli la Kristo, na mamilioni waliuawa bila

huruma.**{EW 211.2}**

Iliwasilishwa mbele yangu kwa namna ifuatayo: Kundi kubwa la waabudu sanamu wapagani lilibeba bendera nyeusi, ambayo juu yake kulikuwa na maumbo ya jua, mwezi na nyota. Kundi hili lilionekana kuwa wakali na wenye hasira. Kisha nikaoneshwa kundi lingine lililobeba bendera safi nyeupe, ambayo iliandikwa, "Usafi na utakatifu kwa Bwana." Nyuso zao zilikuwa na uthabiti na kukubalika mbinguni. Niliwaona wapagani waabudu sanamu wakiwakaribia, na kulikuwa na mauaji makubwa. Wakristo waliyeyuka mbele yao; lakini kundi la Wakristo lilisongamana kwa karibu zaidi, na kushikilia bendera kwa uthabiti zaidi. Wengi walipoanguka, wengine waliunganika kuizunguka bendera ile na kujaza nafasi zao.**{EW 211.3}**

Niliona kundi la waabudu sanamu wakishauriana pamoja. Wakiwa wameshindwa kuwafanya Wakristo kusalimu amri, walikubaliana kuhusu mpango mwingine. Niliwaona wakishusha bendera yao na kisha kulikaribia kundi hilo thabiti la Wakristo na kutoa mapendekezo kwao. Mwanzoni mapendekezo yao yalikataliwa kabisa. Kisha nikaona kundi lile la Wakristo wakishauriana pamoja. Wengine walisema kwamba wangeishusha

bendera, wakubali mapendekezo yale, na kuokoa maisha yao, na mwishowe wangeweza kupata nguvu ya kuiinua bendera yao miongoni mwa wapagani. Wachache, hata hivyo, hawakusalimu amri kwa mpango huu, bali kwa uthabiti walichagua kufa wakiwa wameishikilia bendera yao badala ya kuishusha. Ndipo nilipowaona wengi wakishusha bendera na kuungana na mataifa; lakini wale walio imara na thabiti wangeishika tena na kuiinua juu. Niliona kwamba watu walikuwa wakiliacha kila wakati kundi lile la wale waliobeba bendera safi, na walikuwa wakiungana na waabudu sanamu chini ya bendera nyeusi, kuwatesa wale waliobeba bendera nyeupe. Wengi waliuawa, lakini bendera nyeupe ilishikiliwa juu, na waumini waliinuliwa kuungana kuizunguka. **{EW 212.1}**

Wayahudi ambao kwanza waliamsha ghadhabu ya wapagani dhidi ya Yesu hawakuepuka kuadhibiwa. Katika ukumbi wa hukumu, wakati Pilato aliposita kumhukumu Yesu kifo, Wayahudi waliokasirika walipaza sauti, "Damu Yake na iwe juu yetu, na juu ya watoto wetu." Kutimilizwa kwa laana hii ya kutisha ambayo waliiita juu ya vichwa vyao wenyewe, taifa la Wayahudi limejipatia huo uzoefu. Wapagani na wale wanaoitwa Wakristo wote sawa

wamekuwa maadui wao. Wale wanaokiri kuwa Wakristo, katika bidii yao kwa Kristo, ambaye Wayahudi walimsulubisha, walidhani kwamba kadiri ambavyo wangeweza kuwaletea mateso zaidi, ndivyo Mungu angependezwa zaidi. Kwa hiyo wengi wa Wayahudi wasioamini waliuawa, wakati wengine walifukuzwa kutoka mahali hadi mahali na waliadhibiwa kwa namna mbalimbali. **{EW 212.2}**

Damu ya Kristo na ya wanafunzi, ambao walikuwa wamewaua, ilikuwa juu yao, nao walipatilizwa kwa hukumu za kutisha. Laana ya Mungu iliwafuata, nao walikuwa ni watu wa kudharauliwa na kudhihakiwa na wapagani na wale wanaoitwa Wakristo. Walidhalilishwa, wakaepukwa, na kuchukiwa, kana kwamba alama ya aibu ya Kaini ilikuwa juu yao. Hata hivyo niliona kwamba Mungu alikuwa amewahifadhi watu hawa kwa njia ya ajabu na kuwatawanya ulimwenguni kote ili waweze kutazamwa kama waliotembelewa hasa na laana ya Mungu. Lakini bado niliona kwamba Mungu alikuwa amewahifadhi watu hawa na kuwatawanya duniani kote ili wapate kuonekana kama watu ambao wamepatilizwa kwa namna ya pekee na laana ya Mungu. Niliona kuwa Mungu alikuwa amewaacha Wayahudi kama taifa; lakini kwamba watu binafsi

kati yao bado wangeongoka na kuwezeshwa kurarua pazia kutoka mioyoni mwao na kuona kwamba unabii uliowahusu ulikuwa umetimizwa; watampokea Yesu kama Mwokozi wa ulimwengu na kuona dhambi kubwa ya taifa lao katika kumkataa na kumsulubisha.**{EW 213.1}**

## Sura ya 48 -Siri ya Uovu

Umekuwa ni mpango wa Shetani kuvuta mawazo ya watu kutoka kwa Yesu kwenda kwa mwanadamu, na kuharibu uwajibikaji wa mtu binafsi. Shetani alishindwa katika kusudi lake alipomjaribu Mwana wa Mungu; lakini alifaulu vizuri zaidi alipokuja kwa mwanadamu aliyeanguka. Ukristo ulipotoshwa na kuharibiwa. Mapapa na makasisi walithubutu kuchukua vyeo vya juu, na kuwafundisha watu kuwategemea kwa ajili ya msamaha wa dhambi zao, badala ya kumtegemea Kristo kwaajili yao wenyewe.**{EW 213.2}**

Watu walidanganywa kabisa. Walifundishwa kwamba mapapa na makasisi walikuwa ni

wawakilishi wa Kristo, wakati kwa kweli walikuwa ni wawakilishi wa Shetani, na wale waliowainamia na kuwasujudu, walimwabudu Shetani. Watu walidai kupewa Biblia; lakini makasisi waliona kuwa ilikuwa ni hatari kuwaruhusu waipate ili waisome wao wenyewe, wasije wakaelimishwa na kufichua dhambi za viongozi wao. Watu walifundishwa kupokea kila neno kutoka kwa wadanganyifu hawa kama vile ni kutoka katika kinywa cha Mungu. Walishikilia nguvu ile juu ya akili ambayo Mungu peke Yake Ndiye anapaswa kuishikilia. Ikiwa mtu yeyote angethubutu kufuata dhamiri yake mwenyewe, chuki ile-ile ambayo Shetani na Wayahudi walitumia kwa Yesu ingewashwa juu yake, na wale wenye mamlaka wangekuwa na kiu ya damu yake.**{EW 214.1}**

Nilioneshwa muda ambapo Shetani hasa alishinda. Umati wa Wakristo waliuawa kwa namna za kutisha, kwa sababu walihifadhi usafi wa dini yao. Biblia ilichukiwa, na jitihada zilifanywa kuiondoa duniani. Watu walikatazwa kuisoma, kwa maumivu ya kifo; na nakala zote ambazo zingeweza kupatikana ziliteketezwa. Lakini niliona kwamba Mungu alikuwa na mpango maalum kwa ajili ya Neno Lake. Alililinda. Katika nyakati tofauti kulikuwa

na nakala chache tu za Biblia zilizokuwepo, lakini bado Yeye asingeliruhusu Neno Lake kupotea, kwani katika siku za mwisho nakala zake zilipaswa kuongezeka kiasi kwamba kila familia ingeweza kuimiliki. Niliona kwamba wakati ule kulipokuwa na nakala chache tu za Biblia, Kitabu hiki kilikuwa ni cha thamani kubwa na chenye kufariji wafuasi wa Yesu walioteswa. Ilisomwa kwa njia ya siri mno, na wale waliokuwa na upendeleo huu uliotukuka walihisi kwamba walikuwa wamekuwa na mahojiano na Mungu, na Mwanawe Yesu, na wanafunzi Wake. Lakini upendeleo huu wenye baraka uliwagharimu wengi wao, maisha yao. Walipogunduliwa, walipelekwa kwenye gongo la kulazia kichwa tayari kukatwa, kwenye mti wa kufungia watu wa kuchomwa moto, au gereza ya chini ya ngome kufa kwa njaa.**{EW 214.2}**

Shetani hakuweza kuzuia mpango wa wokovu. Yesu alisulubiwa, na kufufuka siku ya tatu. Lakini Shetani aliwaambia malaika wake kwamba angefanya kusulubiwa na kufufuka kuwa kwa ajili ya faida yake. Alikuwa tayari kwamba wale waliokiri imani kwa Yesu wangepaswa kuamini kwamba sheria zinazodhibiti dhabihu na sadaka za Kiyahudi zilikoma wakati wa kifo cha Kristo, kama angeweza

kuwasukuma mbali zaidi na kuwafanya waamini kwamba sheria ya amri kumi pia ilikufa pamoja na Kristo.**{EW 215.1}**

Niliona kwamba wengi waliikubali kwa urahisi hila hii ya Shetani. Mbingu zote ziliguswa na hasira walipoona sheria takatifu ya Mungu ikikanyagwa chini ya miguu. Yesu na jeshi lote la mbinguni walijua asili ya sheria ya Mungu; walijua kwamba *Asingeibadilisha* au kuibatilisha. Hali isiyo na tumaini ya mwanadamu baada ya kuanguka ilisababisha huzuni kubwa mno mbinguni, na ilimsukuma Yesu kujitoa kufa kwa ajili ya wavunjaji wa sheria takatifu ya Mungu. Lakini kama sheria hiyo ingeweza kubatilishwa, mwanadamu angeweza kuokolewa bila ya kifo cha Yesu. Kwa hiyo kifo Chake hakikuiharibu sheria ya Baba yake, bali kiliitukuza na kuiheshimu na kusisitiza utii kwa maagizo Yake yote matakatifu.**{EW 215.2}**

Kama kanisa lingebaki safi na thabiti, Shetani asingeweza kuwadanganya, na kuwaongoza kuikanyaga sheria ya Mungu. Katika mpango huu wa ufidhuli wenye ujasiri, Shetani hushambulia moja kwa moja dhidi ya msingi wa serikali ya Mungu mbinguni na duniani. Uasi wake ulisababisha afukuzwe kutoka mbinguni. Baada ya

kuasi, ili kujiokoa mwenyewe alitaka sana Mungu abadilishe sheria Yake, lakini aliambiwa mbele ya jeshi lote la mbinguni kwamba sheria ya Mungu haiwezi kubadilika. Shetani anajua kwamba kama ataweza kuwasababisha wengine kukiuka sheria ya Mungu, atakuwa amewapata kwa ajili ya kusudi lake; kwa kuwa kila mkosaji wa amri za Mungu ni lazima afe.**{EW 215.3}**

Shetani aliamua kwenda mbali zaidi. Aliwaambia malaika zake kwamba wengine wangekuwa na wivu sana juu ya sheria ya Mungu kiasi kwamba hawataweza kunaswa katika mtego huu; amri kumi zilikuwa wazi mno kiasi kwamba wengi wangeamini kwamba bado zilikuwa ni lazima kutiiwa, na kwa hiyo ni lazima ajitahidi kupotosha moja tu ya amri hizo. Ndipo alipowaongoza wawakilishi wake kujaribu kubadilisha amri ya nne, au Sabato, na hivyo kubadilisha ile moja ambayo peke yake katika kumi inamfunua Mungu wa Kweli, Muumba wa mbingu na dunia. Shetani aliwasilisha mbele yao ufufuo mtukufu wa Yesu, na akawaambia kwamba kwa kufufuka kwake siku ya kwanza ya juma, alibadilisha Sabato kutoka siku ya saba hadi siku ya kwanza ya juma.**{EW 215.4}**

Hivyo Shetani alitumia kufufuka kwa Yesu

kutimiza kusudi lake. Yeye na malaika zake walifurahi sana kwamba makosa waliyokuwa wameyaandaa yaliwakamata vizuri sana wale wanaodai kuwa marafiki wa Kristo. Kile ambacho mmoja alikitazama kwa hofu ya kidini, mwingine angekipokea. Hivyo makosa tofauti yalipokelewa na kutetewa kwa bidii. Mapenzi ya Mungu, yaliyofunuliwa wazi sana katika Neno Lake, yalifunikwa na makosa na mapokeo, ambayo yamefundishwa kama amri za Mungu. Ingawa udanganyifu huu wa kuipinga mbingu utaruhusiwa kuendelea hadi kuonekana kwa Yesu mara ya pili, lakini bado katika kipindi hiki chote cha makosa na udanganyifu, Mungu hajaachwa bila mashahidi. Katikati ya giza na mateso ya kanisa daima wamekuwapo watu walio wa kweli na waaminifu ambao walizitunza amri zote za Mungu. **{EW 216.1}**

Niliona kwamba jeshi la malaika lilijawa na mshangao walipoona mateso na kifo cha Mfalme wa utukufu. Lakini niliona kwamba haikuwa ajabu kwao kwamba Bwana wa uzima na utukufu, Yeye aliyejaza mbingu yote kwa furaha na fahari, angepaswa kuvunja vifungo vya mauti, na kutembea nje ya nyumba Yake ya gereza, akiwa ni mshindi Mwenye shangwe. Kwa hiyo, kama

mojawapo ya matukio haya yangepaswa kuadhimishwa kwa sikukuu ya kupumzika, basi ni kusulubiwa. Lakini niliona kwamba hakuna hata tukio moja kati ya haya lilikusudiwa kubadilisha au kufutilia mbali sheria ya Mungu; kinyume chake, yanatoa uthibitisho wenye nguvu wa kutokubadilika Kwake.**{EW 216.2}**

Matukio haya yote mawili yana kumbukumbu zake muhimu. Kwa kushiriki meza ya Bwana, mkate uliovunjwa na matunda ya mzabibu, tunaonesha kifo cha Bwana hadi atakapokuja. Matukio ya mateso na kifo chake kwa hivyo yanaletwa upya akilini mwetu. Ufufuo wa Kristo unaadhimishwa kwa kuzikwa kwetu pamoja Naye katika ubatizo, na kufufuka kutoka katika kaburi la maji, kama mfano wa kufufuka Kwake, ili kuishi katika upya wa uzima.**{EW 217.1}**

Nilioneshwa kwamba sheria ya Mungu ingesimama imara milele, na kuwepo katika dunia mpya milele yote. Wakati wa uumbaji, misingi ya dunia ilipowekwa, wana wa Mungu waliangalia kwa mshangao kazi ya Muumbaji, na jeshi lote la mbinguni lilipiga kelele kwa furaha. Ilikuwa ni wakati huo ndipo msingi wa Sabato uliwekwa. Mwisho wa siku sita za uumbaji, Mungu alipumzika

siku ya saba kutoka katika kazi Yake yote aliyoifanya; na akaibariki siku ya saba na kuitakasa, kwa sababu ndani yake alikuwa amepumzika kutokana na kazi Yake yote. Sabato ilianzishwa katika Edeni kabla ya kuanguka, na ilitunzwa na Adamu na Hawa, na jeshi lote la mbinguni. Mungu alipumzika katika siku ya saba Naye aliibariki na kuitakasa siku hiyo. Niliona kwamba Sabato haitaondolewa kamwe; lakini kwamba watakatifu waliokombolewa, na jeshi lote la malaika, wataishika kwa heshima ya Muumbaji mkuu milele zote.**{EW 217.2}**

## Sura ya 50 -Matengenezo

Licha ya mateso yote ya watakatifu, mashahidi walio hai wa Ukweli wa Mungu waliinuliwa kila upande. Malaika wa Bwana walikuwa wakifanya kazi iliyokabidhiwa katika dhamana yao. Walikuwa wakitafuta katika maeneo ya giza mno na kuchagua

kutoka katika giza hilo watu ambao walikuwa waaminifu moyoni. Hawa wote walikuwa wamezikwa katika makosa, lakini Mungu aliwaita, kama alivyofanya kwa Sauli, kuwa vyombo vilivyochaguliwa kubeba Ukweli Wake na kupaza sauti zao dhidi ya dhambi za watu Wake bayana. Malaika wa Mungu waligusa mioyo ya Martin Luther, Melanchthon, na wengine katika maeneo tofauti, na kuwafanya wawe na kiu ya kutoa ushuhuda hai wa Neno la Mungu. Adui alikuwa amekuja kama mafuriko, na bendera na kiwango ni lazima voinuliwe dhidi yake. Luther ndiye aliyechaguliwa kuikabili dhoruba, kusimama dhidi ya hasira ya kanisa lililoanguka, na kuwaimarisha wale wachache ambao walikuwa waaminifu kwa ungamo lao takatifu. Daima alikuwa anaogopa kumkosea Mungu. Alijaribu kwa njia ya matendo kupata kukubaliwa Naye, lakini hakuridhika hadi pale mng’ao wa nuru kutoka mbinguni ulipofukuza giza kutoka katika akili yake na kumwongoza kuamini, si katika matendo, bali katika ustahili wa damu ya Kristo. Aliweza kuja kwa Mungu kwa ajili yake mwenyewe, si kupitia kwa mapapa au waungamishi, bali kwa kupitia kwa Yesu Kristo peke yake.**{EW 222.1}**

Lo, ilikuwa ni ya thamani kiasi gani kwa Luther nuru hii mpya na tukufu ambayo ilikuwa imepambazuka katika ufahamu wake wa giza na kufukuza ushirikina wake! Aliithamini zaidi kuliko hazina ya dunia yenye fahari kubwa kabisa. Neno la Mungu lilikuwa ni jipya. Kila kitu kilibadilika. Kitabu kile ambacho alikuwa anakiogopa kwa sababu hakuweza kuona uzuri ndani yake, sasa kilikuwa ni uzima, uzima wa milele, kwake. Kilikuwa ni furaha yake, faraja yake, mwalimu wake aliyebarikiwa. Hakuna kitu kilichoweza kumshawishi kuacha kukichunguza. Alikuwa na hofu juu ya kifo; lakini kadiri alivyosoma Neno la Mungu, hofu zake zote zilipotea, na alipendezwa na tabia ya Mungu na kumpenda. Aliichunguza Biblia mwenyewe na kujifurahisha katika hazina nyingi zilizomo ndani yake; kisha aliichunguza kwa ajili ya kanisa. Alichukizwa na dhambi za wale ambao alikuwa amewatumaini kwa ajili ya wokovu, na alipoona wengine wengi wamegubikwa katika giza lile lile ambalo lilikuwa limemfunika, kwa shauku alitafuta fursa ya kuwaelekeza kwa Mwana-Kondoo wa Mungu, ambaye peke yake anachukua dhambi ya ulimwengu.**{EW 223.1}**

Akipaza sauti yake dhidi ya makosa na dhambi

za kanisa la kipapa, alijitahidi kwa ari kuuvunja mnyororo wa giza ambao ulikuwa ukiwafunga maelfu na kuwafanya wategemee matendo kwa ajili ya wokovu. Alitamani kuwezeshwa apate kufungua kwa akili zao utajiri wa Kweli wa neema ya Mungu na ubora wa wokovu unaopatikana kupitia kwa Yesu Kristo. Kwa nguvu za Roho Mtakatifu alipaza sauti dhidi ya dhambi zilizopo za viongozi wa kanisa; na alipokutana na dhoruba ya upinzani kutoka kwa makasisi, ushujaa wake haukuzimia; kwa maana aliutegemea mkono wa Mungu wenye nguvu, na kwa ujasiri alimtegemea Yeye kwa ajili ya ushindi. Kadiri alivyosukuma vita karibu zaidi na zaidi, hasira ya makasisi bado iliwaka dhidi yake kwa joto kali zaidi. Hawakutaka kubadilishwa au kufanya matengenezo. Walichagua kuachwa katika raha, katika starehe ya bure, katika uovu; nao walitamani kanisa pia kuachwa gizani.**{EW 223.2}**

Niliona kwamba Luther alikuwa ni mwenye shauku na ari, asiyeogopa na jasiri katika kuikemea dhambi na kuutetea Ukweli. Hakuwajali watu waovu au mashetani; alijua kuwa alikuwapo pamoja naye Yeye aliye Mwenye nguvu kuwazidi hao wote. Luther alikuwa na ari, ushujaa, na ujasiri na kwa nyakati fulani alikaribia kupitiliza kiasi. Lakini

Mungu alimwinua Melanchthon, ambaye alikuwa ni kinyume kwa tabia, kumsaidia Luther kuendeleza kazi ya matengenezo. Melanchthon alikuwa ni, mtaratibu, mwenye woga, mwangalifu, mwenye uvumilivu mkubwa na alionekana kama vile anakosa ujasiri kwa namna fulani. Mtu huyu alipendwa sana na Mungu. Ujuzi wake wa Maandiko ulikuwa mkubwa, na busara yake na hekima vilikuwa bora. Upendo wake kwa kazi ya Mungu ulikuwa sawa na ule wa Luther. Mioyo ya watu hawa Bwana aliiweka pamoja; walikuwa ni marafiki wasioweza kutenganishwa. Luther alikuwa msaada mkubwa kwa Melanchthon wakati alipokuwa katika hatari ya kuogopa na kwenda taratibu, na Melanchthon naye alikuwa msaada mkubwa kwa Luther wakati alipokuwa katika hatari ya kwenda haraka mno. Uangalifu wa Melanchthon wenye kuona mbele mara nyingi ulizuia shida ambayo ingekuja juu ya kazi ya Mungu  kama kazi ingeachwa kwa Luther peke yake; na mara nyingi kazi isingesukumwa mbele kama ingeachwa kwa Melanchthon peke yake. Nilioneshwa hekima ya Mungu katika kuwachagua watu hawa wawili kuendelea na kazi ya matengenezo ya kanisa.**{EW 223.4}**

Kisha nilirudishwa nyuma katika siku za mitume na kuona kwamba Mungu aliwachagua kama marafiki Petro mwenye shauku nyingi, mwenye bidii na Yohana mpole, mvumilivu. Wakati mwingine Petro alikuwa mkali, na mara nyingi hali hii ilipotokea mwanafunzi mpendwa angemzuia. Hata hivyo, hili halikumbadilisha. Lakini baada ya kumkana Bwana wake, na akatubu, na kuongoka, yote aliyohitaji kwa ajili ya kusimamia shauku na bidii yake ilikuwa ni shauri la upole kutoka kwa Yohana. Kusudi la Kristo mara nyingi lingeshindwa kama lingeachwa kwa Yohana peke yake. Bidii ya Petro ilihitajika. Ujasiri na nguvu zake mara nyingi viliwaokoa kutokana na shida na kuwanyamazisha maadui zao. Yohana alikuwa na karama ya kushawishi mioyo ya watu. Aliwapata wengi kwa ajili ya kazi ya Kristo kwa uvumilivu wake wa subira na kujitoa kwake kwa moyo.**{EW 224.2}**

Mungu aliwainua watu kupaza sauti dhidi ya dhambi zilizopo za kanisa la kipapa na kuendeleza Matengenezo. Shetani alijitahidi kuwaangamiza mashahidi hawa hai; lakini Bwana alifanya boma kuwazunguka. Wengine, kwa ajili ya utukufu wa Jina Lake, waliruhusiwa kutia muhuri kwa damu yao ushuhuda waliokuwa wameubeba; lakini kulikuwa

na watu wengine wenye nguvu, kama vile Luther na Melanchthon, ambao wangeweza kumtukuza Mungu vizuri zaidi kwa kuishi na kuziweka wazi dhambi za makasisi, mapapa, na wafalme. Hawa walitetemeka mbele ya sauti ya Luther, na watenda kazi wenzake. Kupitia kwa watu wale wateule, miale ya nuru ilianza kuitawanya giza, na wengi sana walipokea nuru kwa furaha na kutembea ndani yake. Na pale shahidi mmoja alipouawa, wawili au zaidi waliinuka kuziba nafasi yake.**{EW 225.1}**

Lakini Shetani hakuridhika. Angeweza tu kuwa na nguvu juu ya mwili. Asingeweza kuwafanya waumini kusalimisha imani yao na tumaini. Na hata katika kifo walishangilia ushindi kwa tumaini angavu la kutokufa katika ufufuo wa wenye haki. Walikuwa na nguvu zaidi ya nguvu ya mauti. Hawakuthubutu kulala hata kidogo, bali walijifunga silaha za Mkristo juu yao, wakiwa tayari kwa mapambano, si tu na maadui wa kiroho, bali na Shetani katika umbo la wanadamu ambao kilio chao cha kila wakati kilikuwa, "Kana imani yako, au ufe." Wakristo hawa wachache walikuwa na nguvu katika Mungu, na wa thamani zaidi machoni Pake kuliko nusu ya ulimwengu ambao wanalibeba Jina la Kristo, na bado ni waoga katika kazi Yake. Wakati

huo kanisa likiteswa, washiriki wake walikuwa na umoja na upendo; walikuwa na nguvu katika Mungu. Wenye dhambi hawakuruhusiwa  kujiunga na kanisa. Ni wale tu ambao wako tayari kuacha yote kwa ajili ya Kristo, ndiyo wangeweza kuwa wanafunzi Wake. Hawa walipenda kuwa maskini, wanyenyekevu, na wenye kufanana na Kristo. **{EW 225.2}**

## Sura ya 51-Kanisa  na Ulimwengu Vyaungana

Baada ya hayo nilimwona Shetani akishauriana na malaika zake na wakipima kile walichokuwa wamekipata. Kweli, kwa njia ya hofu ya kifo, walikuwa wamezizuia baadhi ya roho zenye kuogopa kuukubali Ukweli; lakini wengi, hata kati ya waoga mno, walikuwa wameupokea Ukweli, na kwa sababu hii hofu zao na woga viliwaacha mara moja. Hawa waliposhuhudia vifo vya ndugu zao na kuona uthabiti na uvumilivu wao, walijua kuwa Mungu na malaika walikuwa wamewasaidia kuvumilia mateso kama hayo, na wakawa na ujasiri na wasio na hofu. Na walipoitwa kuyatoa maisha yao wenyewe, walidumisha imani yao kwa uvumilivu na uthabiti kiasi kwamba hata wauaji wao walitetemeka.

Shetani na malaika zake waliamua kwamba kulikuwa na njia yenye mafanikio zaidi ya kuangamiza roho, njia ambayo hatimaye ingekuwa ni ya hakika zaidi. Ingawa Wakristo walifanywa kuteseka, uthabiti wao, na tumaini angavu ambalo liliwatia matumaini, liliwafanya wanyonge kuwa na nguvu na kuwawezesha kukiendea chanja ya kutesea na moto bila hofu. Waliuiga mwenendo mzuri wa Kristo wakati alipokuwa mbele ya wauaji Wake, na kwa uthabiti wao na utukufu wa Mungu ambao ulikaa juu yao, waliwashawishi wengine wengi juu ya Ukweli. **{EW 226.1}**

Kwa hiyo Shetani aliamua kwamba ni lazima aje kwa namna ya upole zaidi. Alikuwa tayari amekwisha kuyachafua mafundisho ya Biblia, na mapokeo ambayo yalilenga kuwaharibu mamilioni yalikuwa yakiota mizizi kwa kina. Akizuia chuki yake, aliamua kutosisitiza kwa raia wake mateso yale makali, bali kuliongoza kanisa kushindana juu ya mapokeo tofauti tofauti, badala ya juu ya ile imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu. Alipolishawishi kanisa kupokea fadhila na heshima kutoka kwa ulimwengu, chini ya kisingizio cha kupokea misaada, alianza kupoteza fadhila za Mungu. Likiepuka kutangaza Ukweli ule usiopinda

ambao uliwafungia nje wale wapendao anasa na walio marafiki wa ulimwengu, polepole lilipoteza nguvu zake.**{EW 226.2}**

Kanisa sasa si watu waliojitenga na wa pekee kama lilivyokuwa wakati moto wa mateso ulipowaka dhidi yake. Ni jinsi gani dhahabu imekuwa hafifu! Ni jinsi gani dhahabu safi imebadilika! Niliona kwamba kama kanisa lingekuwa limedumisha tabia yake ya pekee, takatifu, nguvu ya Roho Mtakatifu ambayo ilitolewa kwa wanafunzi bado ingekuwa pamoja nalo. Wagonjwa wangeponywa, mapepo wangekemewa na kufukuzwa, na lingekuwa ni lenye nguvu na tishio kwa adui zake.**{EW 227.1}**

Niliona kundi kubwa sana likikiri Jina la Kristo, lakini Mungu hakuwatambua kama ni watu Wake. Hakupendezwa nao. Shetani alionekana kuchukua tabia ya kidini na alikuwa radhi sana kwamba watu wajifikirie kuwa walikuwa Wakristo. Alikuwa hata na shauku kwamba wangemwamini Yesu, kusulubiwa Kwake, na kufufuka Kwake. Shetani na malaika zake wanayaamini haya, na kutetemeka. Lakini ikiwa imani hii haisababishi matendo mema, na kuwaongoza wale wanaoikiri kuiga maisha ya kujikana nafsi ya Kristo, Shetani hasumbuliwi; kwa

kuwa wanalisadiki tu Jina la Kikristo, wakati huo mioyo yao bado ni ya kimwili, na anaweza kuwatumia katika utumishi Wake hata bora zaidi kuliko kama wasingekiri chochote. Wakificha ulemavu wao chini ya jina la Mkristo, wanaendelea na asili zao zisizotakaswa, na tamaa zao mbaya zisizotiishwa. Hii inatoa fursa kwa wasioamini kumfedhehesha Kristo kwa kasoro zao, na kusababisha wale walio na dini safi na isiyo na mawaa kupoteza sifa njema. **{EW 227.2}**

Wachungaji wanahubiri mambo laini ili kuwafaa wale wanaomkiri, Mungu lakini wanaishi kwa mtindo wa tamaa za mwili. Hawathubutu kumhubiri Yesu na Kweli za Biblia zinazochoma; kwa kuwa kama wangefanya hivyo, watu hawa wanaokiri kimwili wasingebaki kanisani. Na kwa kuwa wengi wao ni matajiri, ni lazima wabakizwe, ingawa hawastahili kuwepo pale kuliko Shetani na malaika wake. Na hivi ndivyo Shetani angependa iwe. Dini ya Yesu inafanywa kuonekana kuwa ya kupendwa, maarufu, na ya kuheshimiwa machoni pa ulimwengu. Watu wanaambiwa kwamba wale wanaokiri dini wataheshimiwa zaidi na ulimwengu. Mafundisho kama hayo yanatofautiana sana na mafundisho ya Kristo. Mafundisho Yake na dunia

haviwezi kupatana. Wale ambao walimfuata walipaswa kuikana dunia. Haya mambo laini yalianza na Shetani na malaika wake walioanguka. Walitengeneza mpango huo, na wale wanaokiri kwa majina tu waliutekeleza. Visa vya kubuni vinavyopendeza vilifundishwa na kupokelewa kwa urahisi, na wanafiki na watenda dhambi dhahiri waliungana na kanisa. Kama Ukweli ungehubiriwa katika usafi wake, punde ungelifungia nje tabaka hili. Lakini hakukuwa na tofauti kati ya wale wafuasi wanaomkiri Kristo na ulimwengu. Niliona kwamba ikiwa kifuniko bandia kingeraruliwa kutoka kwa washiriki wa makanisa, kungekuwa kumefunuliwa uovu, upotovu, na ufisadi ule ambao kwa huo mtoto wa Mungu asiyejiamini kabisa asingesita kuwaita hawa wanaodai kuwa Wakristo kwa jina lao sahihi, watoto wa baba yao, ibilisi; kwa kuwa kazi zake ndizo walizozifanya.**{EW 228.1}**

Yesu pamoja na jeshi lote la mbinguni walilitazama tukio hilo kwa kuchukizwa; lakini bado Mungu alikuwa na ujumbe kwa kanisa ambao ulikuwa mtakatifu na muhimu. Kama ujumbe huu ungepokelewa, ungefanya matengenezo kamili katika kanisa, kufufua ushuhuda ulio hai ambao ungewatakasa wanafiki na wenye dhambi, na

kulirudisha kanisa katika kumpendeza Mungu. **{EW 228.2}**

## Sura ya 52-Sura ya -William Miller

[Angalia Kiambatisho.]

Mungu alimtuma malaika Wake kuugusa moyo wa mkulima ambaye hakuiamini Biblia, kumwongoza kuuchunguza unabii. Malaika wa Mungu walimtembelea mteule huyu mara kwa mara, ili kuiongoza akili yake na kufungua kwa ufahamu wake unabii ambao daima ulikuwa giza kwa watu wa Mungu. Mwanzo wa mnyororo wa Ukweli alipewa, naye aliongozwa kutafuta kiungo kimoja baada ya kingine, mpaka akalitazama Neno la Mungu kwa mshangao na kupendezwa. Aliona pale mfuatano kamili wa Ukweli. Neno hilo ambalo alikuwa ameliona kwamba halikuwa limevuviwa sasa lilifunguka mbele ya maono yake katika uzuri na utukufu wake. Aliona kwamba sehemu moja ya Maandiko inaelezea sehemu nyingine, na wakati fungu moja lilifungwa kwa ufahamu wake, alipata katika sehemu nyingine ya Neno kile ambacho kililielezea. Aliliangalia Neno takatifu la Mungu kwa

furaha na kwa heshima kubwa na kicho.**{EW 229.1}**

Alipokuwa akifuatilia unabii huo, aliona kwamba wakazi wa dunia walikuwa wakiishi katika matukio ya mwisho ya historia ya ulimwengu huu, lakini bado hawakujua. Aliyaangalia makanisa na kuona kwamba yalikuwa yamepotoka; walikuwa wameyaondoa mapenzi yao kutoka kwa Yesu na kuyaweka juu ya ulimwengu; walikuwa wakitafuta heshima ya ulimwengu, badala ya heshima ile inayotoka juu; wakishika utajiri wa ulimwengu, badala ya kuweka hazina yao mbinguni. Aliona unafiki, giza, na kifo kila mahali. Roho yake ilisisimka ndani yake. Mungu alimwita aache shamba lake, kama alivyomwita Elisha aache ng'ombe wake na uwanja wa kazi yake kumfuata Eliya. Kwa kutetemeka, William Miller alianza kuwafunulia watu siri za ufalme wa Mungu, akiwabeba wasikilizaji wake kupitia unabii hadi wakati wa kuja kwa Kristo mara ya pili. Kwa kila juhudi alipata nguvu, Kama Yohana Mbatizaji alivyotangaza ujio wa kwanza wa Yesu na kuandaa njia kwa ajili ya kuja Kwake, ndivyo William Miller na wale waliojiunga naye walivyotangaza ujio wa pili wa Mwana wa Mungu.**{EW 229.2}**

Nilipelekwa nyuma hadi siku za wanafunzi na

kuoneshwa kwamba Mungu alikuwa na kazi maalum kwa Yohana mpendwa kukamilisha. Shetani alikuwa ameazimia kuzuia kazi hii, na aliwaongoza watumishi wake kumwangamiza Yohana. Lakini Mungu alimtuma malaika wake na kumhifadhi kwa namna ya ajabu. Wote walioshuhudia nguvu kubwa ya Mungu iliyodhihirishwa katika ukombozi wa Yohana walistaajabu, na wengi walisadiki kwamba Mungu alikuwa pamoja naye, na kwamba ushuhuda alioutoa juu ya Yesu ulikuwa sahihi. Wale ambao walitaka kumwangamiza waliogopa kujaribu tena kuyachukua maisha yake, na aliruhusiwa kuendelea kuteseka kwa ajili ya Yesu. Alishtakiwa kwa uwongo na maadui zake na muda mfupi alifukuzwa kutoka sehemu aliyoishi kwenda katika kisiwa cha upweke, ambapo Bwana alimtuma malaika wake kumfunulia matukio ambayo yangetokea duniani na hali ya kanisa hadi kufikia mwisho—kurudi kwake nyuma na nafasi ambayo lingepaswa kuchukua ikiwa lingempendeza Mungu na hatimaye kushinda. **{EW 230.1}**

Malaika kutoka mbinguni alimwendea Yohana kwa utukufu, uso wake ukiwa umechangamka kwa utukufu bora wa Mungu. Alimfunulia Yohana

matukio ya kina na ya kusisimua katika historia ya kanisa la Mungu na kuleta mbele yake mapambano ya hatari ambayo wafuasi wa Kristo walipaswa kuyavumilia. Yohana aliwaona watu wakipita katika majaribio makali, wakiwa wamefanywa kuwa weupe na kujaribiwa, na, hatimaye, washindi wenye shangwe, waliookolewa kwa utukufu katika ufalme wa Mungu. Uso wa malaika yule ulizidi kung'aa kwa furaha na ulikuwa na utukufu mwingi, alipomwonesha Yohana ushindi wa mwisho wa kanisa la Mungu. Mtume alipoona ukombozi wa mwisho wa kanisa, alijisahau katika utukufu wa tukio lile na kwa kicho cha kina na hofu alianguka miguuni pa malaika yule kumwabudu. Mjumbe wa mbinguni mara moja alimwinua na kumkemea kwa upole, akisema, "Angalia usifanye hivi: mimi ni mjoli wako, na wa ndugu zako walio na ushuhuda wa Yesu: msujudie Mungu: kwa maana ushuhuda wa Yesu ndio roho ya unabii." Kisha malaika yule alimwonesha Yohana mji wa mbinguni na fahari yake yote na utukufu unaong'aa wenye kutia kiwi, naye, akiwa amefurahishwa sana na kuzidiwa, na kusahau karipio la kwanza la malaika yule, alianguka tena kuabudu miguuni pake. Tena karipio la upole lilitolewa, “Angalia, usifanye hivi; mimi ni

mjoli wako, na wa ndugu zako manabii, na wa wale wayashikao Maneno ya kitabu hiki. Msujudie Mungu.” **{EW 230.2}**

Wahubiri na watu wamekitazama kitabu cha Ufunuo kama fumbo na chenye umuhimu mdogo kuliko sehemu zingine za Maandiko Matakatifu. Lakini niliona kwamba Kitabu hiki kwa Kweli ni ufunuo uliotolewa kwa manufaa maalum ya wale ambao wanapaswa kuishi katika siku za mwisho, ili kuwaongoza katika kuhakikisha msimamo wao halisi na wajibu wao. Mungu alielekeza akili ya William Miller kwenye unabii na kumpa nuru kubwa juu ya kitabu cha Ufunuo. **{EW 231.1}**

Kama maono ya Danieli yangeeleweka, watu wangeweza kuelewa vizuri zaidi maono ya Yohana. Lakini kwa wakati ufaao, Mungu alimgusa mtumishi Wake mteule, ambaye, kwa uwazi na kwa nguvu ya Roho Mtakatifu, alifungua unabii na kuonesha upatanifu wa maono ya Danieli na Yohana na sehemu zingine za Biblia, na kuyasisitiza barabara mioyoni mwa watu maonyo haya matakatifu, yenye kuogofya ya Neno, wapate kujiandaa kwa ajili ya ujio wa Mwana wa Adamu. Usadikisho wa kina na mzito ulikaa kwenye akili za wale waliomsikia, na wachungaji na watu/walei, wenye dhambi na

makafiri, walimgeukia Bwana na kujitahidi kufanya maandalizi ya kusimama katika hukumu. **{EW 231.2}**

Malaika wa Mungu waliandamana na William Miller katika utume wake. Alikuwa thabiti na asiyeogopa, akitangaza bila woga ujumbe ule aliokabidhiwa. Ulimwengu uliolala katika uovu na kanisa baridi, linalopenda dunia vilitosha kuamsha nguvu zake zote na kumwongoza kwa utayari kuvumilia taabu, ufukara, na mateso. Ingawa alipingwa na watu waliodai kuwa Wakristo  na ulimwengu, na kufanyiwa ukatili na Shetani na malaika zake, hakuacha kuihubiri injili ya milele kwa watu popote alipoalikwa, akipaza sauti kwenda mbali na karibu, "Mcheni Mungu, na kumtukuza; kwa maana saa ya hukumu Yake imekuja." **{EW 232.1}**

## Sura ya 53-Ujumbe wa Malaika wa Kwanza

[Angalia Kiambatisho.]

Niliona kwamba Mungu alikuwa akitangaza wakati mnamo mwaka 1843. Ulikuwa mpango Wake kuwaamsha watu na kuwafikisha katika mahali pa

kupimwa, ambapo wangepaswa kuamua kuwa upande wa Ukweli au dhidi yake. Wachungaji waliridhishwa juu ya usahihi wa misimamo iliyochukuliwa kuhusu nyakati za unabii, na wengine walikana kiburi chao, na kuacha mishahara yao na makanisa yao ili wapate kusonga mbele kutoka mahali hadi mahali kuutoa ujumbe. Lakini kwa kuwa ujumbe kutoka mbinguni uliweza kupata nafasi katika mioyo ya wachungaji wachache tu waliomkiri  Kristo, kazi hii iliwekwa juu ya watu wengi ambao hawakuwa wahubiri. Wengine waliacha mashamba yao ili kuutangaza ujumbe huu, wakati huo wengine waliitwa kutoka katika maduka yao na biashara zao. Na hata baadhi ya watu wenye taaluma walilazimika kuacha fani zao ili kujihusisha katika kazi isiyopendwa na wengi ya kutoa ujumbe wa malaika wa kwanza. **{EW 232.3}**

Wachungaji waliweka kando maoni na hisia zao za madhehebu na kuungana katika kutangaza kuja kwa Yesu. Popote ujumbe huu ulipotolewa, uliwagusa watu. Wenye dhambi walitubu, walitoa machozi, na kuomba msamaha, na wale ambao maisha yao yalikuwa ya udanganyifu walikuwa na shauku ya kufanya urejeshaji na kupatanishwa. Wazazi walihisi mashaka ya kina kabisa kwa ajili ya

watoto wao. Wale waliopokea ujumbe walifanya kazi pamoja na marafiki na jamaa zao ambao hawajaongoka, na roho zao zikiwa zimeinamishwa kwa uzito wa ujumbe huo mzito, waliwaonya na kuwasihi wajiandae kwa ajili ya ujio wa Mwana wa Adamu. Mifano ya wale ambao walikuwa wakaidi kabisa kiasi kwamba hawakuweza kujisalimisha kwa uzito kama huo wa ushahidi walirudi nyumbani wakiwa na maonyo ya dhati. Kazi hii inayotakasa roho iliongoza mapenzi mbali na mambo ya dunia kwenda katika kujiwekwa wakfu ambako hakukuwahi kutokea hapo awali.**{EW 232.3}**

Maelfu waliongozwa kuukubali kwa moyo ukweli uliohubiriwa na William Miller, na watumishi wa Mungu waliinuliwa katika roho na nguvu ya Eliya kuutangaza ujumbe. Kama Yohana, mtangulizi wa Yesu, wale waliohubiri ujumbe huu mzito walilazimika kuweka shoka kwenye mzizi wa mti, na kuwataka watu kuzaa matunda yapasayo toba. Ushuhuda wao ulikusudiwa kuyaamsha na kuyagusa makanisa kwa nguvu na kudhihirisha tabia yao halisi. Na pale onyo zito la kuikimbia ghadhabu ijayo liliposikika, wengi ambao walikuwa wamejiunga na makanisa hayo walipokea ujumbe wa uponyaji; waliona kurudi nyuma kwao, na kwa

machozi machungu ya toba na maumivu makubwa ya roho, walijinyenyekesha mbele za Mungu. Na Roho wa Mungu alilipokaa juu yao, walisaidia katika kupiga kelele, "Mcheni Mungu, na kumtukuza; kwa maana saa ya hukumu Yake imekuja." **{EW 233.1}**

Kuhubiriwa kwa wakati halisi kulileta upinzani mkubwa kutoka kwa matabaka yote, kutoka kwa mchungaji aliye kwenye mimbari hadi kwa mtenda dhambi asiyejali kabisa, na anayethubutu kuiipinga mbingu bila hofu. "Habari ya siku ile na saa ile hakuna aijuaye," ilisikika kutoka kwa mchungaji mnafiki na mfanya dhihaka thabiti. Wala haikuweza kufundishwa na kusahihishwa na wale ambao walikuwa wakielekeza katika ule mwaka ambapo waliamini kuwa nyakati za unabii zingetimia, na kwa ishara ambazo zilionesha kuwa Kristo yu karibu, milangoni. Wachungaji wengi wa kundi, ambao walidai kumpenda Yesu, walisema kwamba hawakuwa na upinzani kuhusu kuhubiriwa kwa kuja kwa Kristo, bali walipinga muda halisi. Lakini jicho la Mungu linaloona yote lilisoma mioyo yao. Watu hawakupenda kuja kwa Yesu kuwa karibu. Walijua kwamba maisha yao yasiyo ya Kikristo yasingestahimili jaribio hilo, kwa kuwa hawakuwa wanatembea katika njia dhalili iliyowekewa mipaka

na Yeye. Wachungaji hawa wa uongo walisimama katika njia ya kazi ya Mungu. Ukweli uliozungumzwa katika nguvu yake ya kushawishi uliwaamsha watu, na kama mlinzi wa gereza, walianza kuuliza, "Nifanye nini nipate kuokoka?" Lakini wachungaji hawa waliingilia kati ya Ukweli na watu, na kuhubiri mambo laini ya kuwaongoza kutoka kwenye Ukweli. Waliungana na Shetani na malaika zake, wakipaza sauti, “Amani, amani” wakati hakukuwa na amani. Wale waliopenda raha, na maisha bwerere na kuridhika kuwa mbali kwao na Mungu wasingeweza kuamshwa kutoka katika usalama wao wa matendo ya mwili. Niliona kwamba malaika wa Mungu waliyazingatia na kuyawekea alama yote; mavazi ya wale wachungaji ambao hawajawekwa wakfu yalifunikwa kwa damu ya roho nyingi.**{EW 233.2}**

Wachungaji wale ambao hawakuukubali ujumbe huu wa kuokoa wenyewe waliwazuia wale ambao wangeweza kuupokea. Damu ya roho nyingi iko juu yao. Wahubiri na watu waliungana katika kuupinga ujumbe huu kutoka mbinguni na katika kumtesa William Miller na wale walioungana naye katika kazi hii. Uongo ulisambazwa ili kudhuru ushawishi wake; na kwa nyakati tofauti baada ya

kuutangaza kwa uwazi ushauri wa Mungu, akitumia Ukweli unaochoma mioyo ya wasikilizaji wake, hasira kali iliwaka dhidi yake, na alipokuwa akiondoka mahali pa mkutano, watu wengine walimvizia ili wapate kuyachukua maisha yake. Lakini malaika wa Mungu walitumwa kumlinda, nao walimwongoza salama kutoka katika kundi lenye hasira. Kazi yake bado ilikuwa haijamalizika.**{EW 234.1}**

Watu waliojitoa kabisa waliupokea ujumbe ule kwa furaha. Wanatambua kwa hakika kwamba ulitoka kwa Mungu na kutolewa kwa wakati unaofaa. Malaika walikuwa wakitazama kwa shauku kubwa kuona matokeo ya ujumbe wa mbinguni, na wakati makanisa yalipogeuka kutoka kwake na kuukataa, kwa huzuni walishauriana na Yesu. Kristo Aligeuza uso Wake kutoka kwa makanisa hayo na kuwaambia malaika Wake wawalinde kwa uaminifu wale walio wa thamani ambao hawakuukataa ushuhuda huo, kwa maana nuru nyingine bado ilikuwa iwaangazie.**{EW 235.1}**

Niliona kwamba kama wale wanaodai kuwa wa Wakristo wangependa kuonekana kwa Mwokozi wao, kama wangeweka mapenzi yao Kwake, na kutambua kuwa hakuna mtu yeyote duniani wa

kulinganishwa Naye, wangeikaribisha kwa furaha taarifa ya kwanza ya kuja Kwake. Lakini chuki walioonesha, pale waliposikia kuhusu kuja kwa Bwana wao, ilikuwa ni ushahidi thabiti kwamba hawakumpenda Yeye. Shetani na malaika zake walishangilia, na kudai mbele za Yesu na malaika Zake kwamba watu Wake wanaomkiri walikuwa na upendo kidogo kwa Yesu kiasi kwamba hawakutamani kuja Kwake mara ya pili.**{EW 235.2}**

Niliwaona watu wa Mungu wakiwa na furaha katika mategemeo, wakimtarajia Bwana wao. Lakini Mungu alikusudia kuwathibitisha. Mkono Wake ulifunika kosa katika hesabu ya nyakati za unabii. Wale ambao walikuwa wakimtarajia Bwana wao hawakuligundua kosa hili, na watu wasomi kabisa ambao walipinga wakati ule pia walishindwa kuliona. Mungu alipanga kwamba watu wake wakutane na kukatishwa tamaa. Muda ulipita, na wale ambao walikuwa wametazamia Mwokozi wao kwa mategemeo ya furaha walikuwa na huzuni na kuvunjika moyo, wakati wale ambao hawakupenda kuonekana kwa Yesu, lakini waliukubali ujumbe kupitia hofu, walifurahi kwamba hakuja katika muda ule wa matarajio. Ungamo lao halikuwa limegusa moyo na kuyatakasa maisha. Kupita kwa wakati

kulikusudiwa vyema kudhihirisha mioyo kama hiyo. Walikuwa wa kwanza kugeuka na kuwadhihaki wale wenye huzuni, waliokatishwa tamaa ambao kwa kweli walipenda kuonekana kwa Mwokozi wao. Niliona hekima ya Mungu katika kuwathibitisha watu Wake na kuwapa majaribio ya kuchunguza ili kuwagundua wale ambao wangesita na kurudi nyuma katika saa ya majaribio. **{EW 235.3}**

Yesu pamoja na jeshi lote la mbinguni waliwatazama kwa huruma na upendo wale ambao kwa matarajio matamu walitamani sana kumwona Yeye ambaye roho zao zilimpenda. Malaika walikuwa wakizunguka-zunguka juu yao, ili kuwategemeza katika saa ya kujaribiwa kwao. Wale ambao walipuuza kuupokea ujumbe wa mbinguni waliachwa gizani, na hasira ya Mungu iliwaka dhidi yao, kwa sababu hawakuipokea nuru ambayo alikuwa amewatumia kutoka mbinguni. Wale waaminifu, waliokatishwa tamaa, ambao hawakuweza kufahamu ni kwa nini Bwana wao hakuja, hawakuachwa gizani. Tena waliongozwa katika Biblia zao wapate kuzichunguza nyakati za unabii. Mkono wa Bwana uliondolewa kutoka katika tarakimu, na kosa lile lilielezewa. Waliona kwamba

vipindi vya unabii vilifikia mwaka wa 1844, na kwamba ushahidi ule-ule ambao walikuwa wamewasilisha ili kuonesha kwamba vipindi vya unabii viliishia mwaka 1843, ulithibitisha kwamba vingeishia mwaka 1844. Nuru kutoka katika Neno la Mungu iliangaza juu ya msimamo wao, nao waligundua muda wa kungoja -"Ijapokawia [njozi], ingojee." Katika upendo wao kwa ujio wa mara moja wa Kristo, hawakutilia maanani kukawia kwa maono, ambako kulikusudiwa kuwadhihirisha wale wanaongojea kwa kweli. Tena walikuwa na jambo linalohusu muda. Lakini bado niliona kwamba wengi wao hawakuweza kuinuka juu ya kukatishwa kwao tamaa kwa ukali na kuwa na kiwango kile cha bidii na nguvu ambacho kilikuwa kimedhihirisha imani yao mnamo 1843.**{EW 236.1}**

Shetani na malaika zake walishangilia kwa ushinda juu yao, na wale ambao hawakuupokea ujumbe ule walijipongeza wenyewe kwa kuwa na busara ya kuona mbele na hekima yao kwa kutokupokea udanganyifu ule, kama walivyouita. Hawakutambua kwamba walikuwa wakikataa shauri la Mungu dhidi yao wenyewe, na kwamba walikuwa wakifanya kazi kwa umoja na Shetani na

malaika zake kuwafadhaisha watu wa Mungu, ambao walikuwa wakiishi kulingana na ujumbe uliotumwa na mbingu.**{EW 236.2}**

Waumini katika ujumbe huu walionewa na kunyanyaswa ndani ya makanisa. Kwa muda, wale ambao hawakuupokea ujumbe huu walizuiwa na hofu kudhihirisha hisia za mioyo yao; lakini kupita kwa wakati kulifunua hisia zao za kweli. Walitaka kuunyamazisha ushuhuda ambao wale waliokuwa wakisubiri walijisikia kulazimishwa kuutoa, kwamba nyakati za unabii ziliendelea hadi 1844. Kwa uwazi waumini walielezea makosa yao na kutoa sababu kwa nini walimtarajia Bwana wao katika mwaka 1844. Wapinzani wao hawakuweza kuleta hoja dhidi ya sababu zenye nguvu zilizotolewa. Hata hivyo hasira ya makanisa iliwaka; waliazimia kutokusikiliza ushahidi, na kufungia ushahidi nje ya makanisa, ili wengine wasiweze kuusikia. Wale ambao hawakuthubutu kuzuia kwa wengine nuru ile ambayo Mungu alikuwa amewapa, walifungiwa nje ya makanisa; lakini Yesu alikuwa pamoja nao, na walifurahi katika nuru ya uso Wake. Walikuwa tayari kuupokea ujumbe wa malaika wa pili.**{EW 237.1}**

## Sura ya 54-Ujumbe wa Malaika wa Pili

[angalia kiambatisho.]

Wakati makanisa yalipokataa kuupokea ujumbe wa malaika wa kwanza, walikataa nuru kutoka mbinguni na wakaanguka kutoka katika neema ya Mungu. Walizitumaini nguvu zao wenyewe, na kwa kuupinga ujumbe wa malaika wa kwanza walijiweka mahali ambapo hawakuweza kuona nuru ya ujumbe wa malaika wa pili. Lakini wapendwa wa Mungu, ambao walionewa, waliukubali ujumbe, "Umeanguka Babeli," na kukayaacha makanisa.**{EW 237.2}**

Karibu na mwisho wa ujumbe wa malaika wa pili, [angalia kiambatisho.] niliona nuru kubwa kutoka mbinguni ikimulika juu ya watu wa Mungu. Miale ya nuru hii ilionekana kung'aa kama jua. Kisha nikasikia sauti za malaika zikipazwa, "Haya, Bwana arusi; tokeni mwende kumlaki!"**{EW 238.1}**

Hiki kilikuwa ni kilio cha usiku wa manane, ambacho kilipaswa kuupa nguvu ujumbe wa malaika wa pili. Malaika walitumwa kutoka mbinguni kuwaamsha watakatifu waliokuwa wamevunjika moyo na kuwaandaa kwa ajili ya kazi kubwa iliyokuwa mbele yao. Watu wenye vipaji na

karama kubwa, hawakuwa wa kwanza kuupokea ujumbe huu. Malaika walitumwa kwa wale waliokuwa wanyenyekevu, waliojitoa, na kuwabidisha kupaza sauti wakisema, "Haya, Bwana arusi; tokeni mwende kumlaki!" Wale waliokabidhiwa kupaza sauti walifanya haraka kutoka, na kwa nguvu ya Roho Mtakatifu waliutangaza ujumbe huo, na kuwaamsha ndugu zao waliovunjika moyo. Kazi hii haikusimama juu ya hekima na usomi wa wanadamu, bali juu ya uweza wa Mungu, na watakatifu Wake waliolisikia tangazo hawakuweza kulipinga. Watu wa kiroho zaidi walipokea ujumbe huu wa malaika wa kwanza, na wale ambao hapo awali walikuwa wameongoza katika kazi walikuwa wa mwisho kupokea na kusaidia katika kuzidi kupaza sauti, "Haya, Bwana Arusi; tokeni mwende kumlaki!" **{EW 238.2}**

Katika kila sehemu ya nchi, nuru ilitolewa juu ya ujumbe wa malaika wa pili, na kilio hiki kiliyeyusha mioyo ya maelfu. Kilio hiki kilienda mji mmoja hadi mwingine, na kutoka kijiji hadi kijiji kingine, mpaka watu wa Mungu waliokuwa wakingojea walipoamshwa kabisa. Katika makanisa mengi ujumbe huu haukuruhusiwa kutolewa, na kundi kubwa ambalo lilikuwa na ushuhuda ulio hai

liliyaacha makanisa haya yaliyoanguka. Kazi kubwa ilikamilishwa na kilio cha usiku wa manane. Ujumbe huo ulikuwa ukiichunguza mioyo, ukiwaongoza waumini kutafuta uzoefu wa maisha ulio hai kwa yao wenyewe. Walijua kwamba wasingeweza kutegemeana kila mtu na mwenzake.**{EW 238.3}**

Watakatifu walimngojea Bwana wao kwa shauku, kwa kufunga, kukesha, na walikaribia kuwa na maombi ya daima. Hata wenye dhambi waliutarajia wakati ule kwa hofu; lakini umati mkubwa ulidhihirisha roho ya Shetani katika upinzani kwa ujumbe huu. Walidhihaki na kwa maneno ya dharau, wakafanya futuhi, wakirudiarudia kila mahali, "Hamwijui siku wala saa." Malaika waovu waliwasisitiza wafanye mioyo yao kuwa migumu na kukataa kila mwale wa nuru kutoka mbinguni, ili waweze kufungwa katika mtego wa Shetani. Wengi waliokiri kuwa walikuwa wakimtarajia Kristo hawakuwa na sehemu katika kazi ya ujumbe huo. Utukufu wa Mungu ambao walikuwa wameushuhudia, unyenyekevu na kujitoa kwa kina kwa wale waliokuwa wakingojea, na uzito mkubwa wa ushahidi, uliwafanya kukiri kuupokea Ukweli; lakini walikuwa hawajaongoka; hawakuwa tayari kwa ajili ya kuja kwa Bwana wao.**{EW 238.4}**

Roho ya maombi mazito na ya dhati ilihisiwa kila mahali na watakatifu. Uzito mtakatifu ulikuwa juu yao. Malaika walikuwa wakitazama kwa shauku kubwa mno kuona matokeo ya ujumbe huo, nao walikuwa wakiwainua wale walioupokea, na kuwavuta kutoka kwenye vitu vya dunia ili kupata majaliwa mengi kutoka kwenye chemchemi ya wokovu. Watu wa Mungu wakati ule walikubaliwa Naye. Yesu aliwatazama kwa furaha, kwa kuwa sura yake iliakisiwa ndani yao. Walikuwa wametoa kafara kamili, kujiweka wakfu kikamilifu, nao walitarajia kubadilishwa katika hali ya kutokufa. Lakini walikusudiwa tena kukatishwa tamaa na kujipatia huzuni. Muda ambao waliutazamia, wakitegemea ukombozi, ulipita; bado walikuwapo duniani, na athari za laana kama zilionekana ni nzito, basi ilikuwa wakati huu. Walikuwa wameweka mapenzi yao mbinguni, na kwa matarajio matamu walikuwa wameonja ukombozi wa milele; lakini matumaini yao hayakutimia.**{EW 239.1}**

Hofu ambayo ilikuwa imekaa juu ya watu wengi haikupotea mara moja; hawakupata ushindi mara moja juu ya wale waliovunjika moyo. Lakini kwa kuwa hakukuwa na ishara zinazoonekana za ghadhabu ya Mungu zilizoonekana, walipona

kutoka katika hofu ile ambayo walikuwa wameihisi na kuanza dhihaka zao na maneno ya dharau. Watu wa Mungu tena walijaribiwa na kupimwa. Ulimwengu uliwacheka na kuwadhihaki na kuwashutumu; na wale ambao walikuwa wameamini bila shaka kwamba Yesu angekuja kuwafufua wafu, na kuwabadilisha watakatifu walio hai, na kuchukua ufalme, kuimiliki milele, walihisi kama vile wanafunzi katika kaburi la Kristo walivyojisikia, "Wamemwondoa Bwana wangu, wala mimi sijui walikomweka."**{EW 239.2}**

## Sura ya Sura ya 55 --Vuguvugu la Marejeo Lafafanuliwa

Niliona idadi kadhaa ya makundi ambayo yalionekana kuwa yamefungwa pamoja kwa kamba. Wengi katika makundi haya walikuwa gizani kabisa; macho yao yalielekezwa chini duniani, na ilionekana kuwa hakuna uhusiano wowote kati yao na Yesu. Lakini katika makundi haya mbalimbali walikuwapo watu waliotawanyika ambao nyuso zao zilionekana kuwa nyepesi, na ambao macho yao yaliinuliwa kwenda mbinguni. Miali ya nuru kutoka kwa Yesu, kama mionzi kutoka katika jua, walipewa. Malaika

aliniambia niangalie kwa makini, nami nikamwona malaika akimwangalia kila mmoja wa wale ambaye alikuwa na mwali wa nuru, wakati huo malaika waovu waliwazunguka wale waliokuwa gizani. Nilisikia sauti ya malaika ikisema kwa sauti kuu, “Mcheni Mungu na kumtukuza, kwa maana saa ya hukumu yake imekuja.**{EW 240.1}**

Nuru tukufu ilitua juu ya makundi haya, ili kuwaangazia wote ambao wangeipokea. Baadhi ya wale waliokuwa gizani waliipokea nuru ile na kufurahi. Wengine waliipinga nuru ile kutoka mbinguni, wakisema kwamba ilitumwa kuwapoteza. Nuru ile ilitoweka kwao, nao wakaachwa gizani. Wale ambao walikuwa wamepokea nuru kutoka kwa Yesu walithamini kwa furaha ongezeko la nuru ya thamani ambayo ilitolewa juu yao. Nyuso zao zilichangamka kwa furaha takatifu, wakati huo macho yao yalielekezwa juu kwa Yesu kwa shauku kubwa, na sauti zao zilisikika kwa upatanifu na sauti ya malaika, “Mcheni Mungu, na kumtukuza; kwa maana saa ya hukumu Yake imekuja.” Walipoinua kilio hiki, niliwaona wale waliokuwa gizani wakiwasukuma kwa ubavu na kwa bega. Kisha wengi walioithamini nuru ile takatifu, walivunja kamba zilizowafunga na kusimama wakiwa

wametengwa na makundi hayo. Walipokuwa wakifanya hivyo, watu wa makundi mbalimbali na walioheshimiwa nao sana walipita, wengine wakiwa na maneno ya kupendeza, na wengine wakiwa na sura za ghadhabu na ishara za vitisho, na kufunga kamba zilizokuwa zinalegea. Watu hawa daima walikuwa wanasema, “Mungu Yu pamoja nasi. Tunasimama kwenye nuru. Tunao Ukweli.” Niliuliza watu hawa walikuwa ni akina nani, na niliambiwa kwamba walikuwa ni wachungaji na viongozi ambao walikuwa wameikataa nuru wao wenyewe, na hawakutaka wengine waipokee.**{EW 240.2}**

Niliwaona wale walioihifadhi nuru ile kwa upendo wakitazama juu kwa shauku kubwa, wakimtazamia Yesu aje kuwachukua kwenda Kwake. Punde wingu lilipita juu yao, na nyuso zao zilikuwa na huzuni. Niliuliza sababu ya wingu hili nami nilioneshwa kuwa ni masikitiko yao (Great disappointment). Wakati ambao walimtarajia Mwokozi wao ulikuwa umepita, na Yesu hakuja. Sikitiko lilipotua juu ya wale waliokuwa wakingojea, wachungaji na viongozi ambao nilikuwa nimewaona hapo awali, walifurahi, na wale wote waliokuwa wameikataa nuru ile walishangilia mno, wakati huo Shetani na malaika zake waovu pia walifurahia.**{EW**

**241.1}**

Kisha nilisikia sauti ya malaika mwingine akisema, "Umeanguka, umeanguka Babeli!" Nuru iliwaangazia wale waliokata tamaa, na kwa shauku kubwa ya kuonekana Kwake, walikaza macho yao tena kwa Yesu. Niliona malaika kadhaa wakizungumza na yule aliyepaza sauti akisema, "Umeanguka Babeli," na hawa waliungana naye katika kupaza sauti, "Haya, Bwana arusi; tokeni mwende kumlaki." Sauti tamu kama muziki za malaika hawa zilionekana kufika kila mahali. Nuru angavu mno na tukufu iliwaangazia wale ambao walikuwa wameihifadhi kwa upendo mkuu nuru ile ambayo walikuwa wamepewa. Nyuso zao ziliangaza kwa utukufu mkuu, na waliungana na malaika katika kupaza sauti, "Haya, Bwana arusi." Walipopaza sauti zao kwa upatanifu miongoni mwa makundi mbalimbali, wale walioikataa nuru ile waliwasukuma na kwa sura za hasira waliwadharau na kuwadhihaki. Lakini malaika wa Mungu walipeperusha mabawa yao juu ya wale walioteswa, wakati huo Shetani na malaika zake walikuwa wakijitahidi kushinikiza giza lao kuwazunguka, kuwaongoza kukataa nuru kutoka mbinguni.**{EW 241.2}**

Kisha nikasikia sauti ikiwaambia wale waliokuwa wamesukumwa na kudharauliwa, "Tokeni kati yao, msiguse kitu kilicho kichafu." Kwa kutii sauti hii, idadi kubwa walivunja kamba zilizowafunga, na kuacha makundi yale yaliyokuwa gizani, na kujiunga na wale ambao hapo awali walikuwa wamepata uhuru wao, na kwa furaha wakaunganisha sauti zao pamoja nao. Nilisikia sauti ya maombi ya dhati, yenye uchungu kutoka kwa wachache ambao bado walibaki katika makundi yaliyokuwa gizani. Wachungaji na viongozi walikuwa wakizunguka watu katika makundi haya mbalimbali, wakikaza kamba kwa uthabiti zaidi; lakini bado nilisikia sauti hii ya maombi ya dhati. Kisha nikawaona wale ambao walikuwa wakiomba wakinyosha mikono yao juu kuomba msaada kutoka katika kundi lile lenye umoja ambao walikuwa huru, wakifurahi katika Mungu. Jibu kutoka kwao, walipokuwa wakitazama mbinguni kwa bidii na kuelekea juu, lilikuwa, "Tokeni kati yao, mkatengwe nao." Niliwaona watu binafsi wakipigania uhuru, na mwishowe walizivunja kamba zilizowafunga. Walizipinga juhudi zile ambazo zilifanywa kufunga kamba kwa kukazwa zaidi na kukataa kutii madai ya mara kwa mara:

"Mungu Yu pamoja nasi." “Tunao Ukweli pamoja nasi.” **{EW 242.1}**

Watu walikuwa wakiendelea kuyaacha makundi yale yaliyokuwa gizani na kujiunga na kundi huru, ambao walionekana kuwa katika uwanja wa wazi ulioinuliwa juu ya dunia. Macho yao yalielekezwa juu, utukufu wa Mungu ulitulia juu yao, na walipaza sauti zao kwa furaha kutaja sifa Zake. Walikuwa wameungana kwa karibu na walionekana kufunikwa na nuru ya mbinguni. Kuzunguka kundi hili kulikuwapo na wengine ambao walikuja chini ya mvuto wa nuru ile, lakini ambao hawakuwa wameungana hasa na kundi hilo. Wote walioihifadhi nuru waliyopewa kwa upendo mkubwa walikuwa wakiangalia juu kwa shauku kubwa, na Yesu aliwatazama kwa ukubali kabisa, ulioleta furaha moyoni. Walimtarajia aje na walitamani sana kuonekana Kwake. Hawakuiangalia dunia hata kidogo kwa kukawia. Lakini tena wingu lilitua juu ya wale waliokuwa wanangojea, nami niliwaona wakigeuza macho yao yaliyochoka kuelekea chini. Niliuliza chanzo cha badiliko hili. Malaika aliyeandamana nami akasema, "Wamekatishwa tamaa tena katika matarajio yao. Yesu bado hawezi kuja duniani. Lazima wavumilie majaribu makubwa

kwa ajili Yake. Ni lazima wavumilie majaribu makubwa zaidi kwa ajili Yake. Wanapaswa kuachana na makosa na mapokeo yaliyopokelewa kutoka kwa wanadamu na kumgeukia kabisa Mungu na Neno Lake. Ni lazima watakaswe, wafanywe kuwa weupe, na kupimwa. Wale watakaoyavumilia majaribu hayo machungu watapata ushindi wa milele."**{EW 243.1}**

Yesu hakuja duniani kama vile kundi la waliongojea, kwa furaha lilivyotarajia, kusafisha Patakatifu kwa kuitakasa dunia kwa moto. Niliona kuwa walikuwa sahihi katika hesabu yao ya nyakati za unabii; wakati wa unabii ulifungwa mnamo 1844, na Yesu aliingia katika mahali Patakatifu pa Patakatifu kupatakasa Patakatifu mwishoni mwa mwishoni mwa siku zile. Kosa lao lilikuwa katika kutokuelewa Patakatifu palikuwa ni nini na namna ya kutakaswa kwake. Nilipowatazama tena kundi lililokuwa likisubiri, waliovunjika moyo, walionekana kuwa na huzuni. Walichunguza kwa makini uthibitisho wa imani yao na kufuatilia hesabu ya nyakati za unabii, lakini hawakuweza kugundua kosa lolote. Wakati ulikuwa umetimilika, lakini Mwokozi wao alikuwa wapi? Walikuwa wamempoteza. **{EW 243.2}**

Nilioneshwa sikitiko la wanafunzi pale walipokuja kaburini na hawakuukuta mwili wa Yesu. Mariamu alisema, “Wamemwondoa Bwana wangu, wala mimi sijui walikomweka.” Malaika waliwaambia wanafunzi wenye huzuni kwamba Bwana wao alikuwa amefufuka, Naye angewatangulia kwenda Galilaya.**{EW 244.1}**

Vivyo hivyo niliona kwamba Yesu aliwaangalia kwa huruma kubwa mno wale waliovunjika moyo ambao walikuwa wamengojea kuja Kwake; na aliwatuma malaika Zake kuelekeza akili zao ili waweze kumfuata pale alipokuwa. Aliwaonesha kwamba dunia hii sio Patakatifu, bali kwamba alipaswa kuingia katika Patakatifu pa Patakatifu pa mbinguni kufanya upatanisho kwa ajili ya watu Wake na kupokea ufalme kutoka kwa Baba Yake, na kwamba ndipo atakaporudi duniani na kuwachukua wakae Naye milele. Sikitiko la wanafunzi wa kwanza linawakilisha kwa uzuri sikitiko la wale waliomtazamia Bwana wao mnamo 1844.**{EW 244.2}**

Nilirudishwa nyuma hadi wakati ambapo Kristo alipanda na kuingia kwa shangwe ya ushindi kuingia Yerusalemu. Wanafunzi wenye furaha waliamini kwamba wakati huo angechukua ufalme na kutawala kama mfalme wa dunia hii. Walimfuata

mfalme wao wakiwa na matumaini makuu. Walikata matawi mazuri ya mitende, na kuvua mavazi yao ya nje, na kwa ari yenye shauku waliyatandaza njiani; na wengine walitangulia, na wengine walifuata, wakipiga kelele, “Hosana Mwana wa Daudi: ndiye mbarikiwa, yeye ajaye kwa  Jina la Bwana; Hosana juu mbinguni.”  Shange na msisimko huu uliwasumbua Mafarisayo, nao walitaka Yesu awakemee wanafunzi Wake. Lakini aliwaambia, "Wakinyamaza hawa, mawe yatapiga kelele." Unabii wa Zekaria 9:9 lazima utimizwe; lakini bado wanafunzi walikuwa waliwekwa katika sikitiko kuu. Ndani ya siku chache walimfuata Yesu hadi Kalvari, na kumwona Akitokwa damu na kuraruliwa juu ya msalaba katili. Walishudia kifo Chake cha maumivu makali na kumlaza kaburini. Mioyo yao ilizama kwa huzuni; matazamio yao hayakufikiwa hata kidogo, na matumaini yao yalikufa pamoja na Yesu. Lakini alipofufuka kutoka kwa wafu na kuwatokea wanafunzi wake wenye huzuni, matumaini yao yalifufuliwa. Walikuwa wamempata tena.**{EW 244.3}**

Niliona kwamba kukatishwa tamaa kwa wale walioamini juu ya kuja kwa Bwana mnamo mwaka 1844 halikuwa sawa na kukatishwa tamaa kwa wanafunzi wa kwanza. Unabii ulitimizwa katika

ujumbe wa malaika wa kwanza na malaika wa pili. Ujumbe ulitolewa kwa wakati unaofaa na kutimiza kazi ile ambayo Mungu alipanga kukamilisha kupitia kwao. **{EW 245.1}**

## Sura ya 56 -Ufafanuzi Mwingine (Kielelezo)

Nilioneshwa shauku ambayo mbingu yote ilikuwa nayo katika kazi inayoendelea duniani. Yesu alimwagiza malaika mwenye nguvu kushuka na kuwaonya wakazi wa dunia wapate kujiandaa kwa ajili ya kutokea Kwake mara ya pili. Malaika yule alipoondoka mbele ya Yesu mbinguni, nuru angavu mno pamoja na utukufu vilitangulia mbele yake. Niliambiwa kwamba kazi yake ilikuwa ni kuiangaza dunia kwa utukufu Wake na kumwonya mwanadamu juu ya ghadhabu ya Mungu ijayo. Umati mkubwa wa watu uliipokea nuru. Baadhi ya hawa walionekana kuwa makini sana, wakati huo wengine walikuwa na shangwe na kupendezwa sana. Wale wote walioipokea nuru waligeuza nyuso zao kuelekea mbinguni na kumtukuza Mungu. Ingawa nuru ilitawanywa kwa wote, wengine walikuja kidogo tu chini ya ushawishi wake, lakini hawakuipokea kwa moyo wote. Wengi walijawa na

ghadhabu kubwa. Wachungaji na watu ambao ni walei, waliungana na waovu na kwa uthabiti waliipinga nuru ile iliyoenezwa na malaika yule mwenye nguvu. Lakini wote walioipokea walijitenga na ulimwenguni na kuwa na umoja kamili wao kwa wao.**{EW 245.2}**

Shetani na malaika zake walijihusisha kwa bidii sana katika kujitahidi kuvutia akili za wengi kwa kadri iwezekanavyo kutoka katika ile nuru. Kundi lililoikataa liliachwa gizani. Nilimwona malaika wa Mungu akiwaangalia kwa shauku kubwa sana watu Wake waliomkiri, ili apate kurekodi tabia ambayo waliyoikuza pale ujumbe wenye asili ya mbinguni ulipowasilishwa kwao. Na kwa kuwa wengi sana waliodai kumpenda Yesu waligeuka kutoka katika ujumbe wa mbinguni kwa dharau, dhihaka, na chuki, malaika yule aliyekuwa na karatasi ya ngozi mkononi mwake aliandika rekodi ya aibu. Mbingu zote zilijawa na hasira kwamba Yesu angepuuzwa kwa namna hiyo na wanaodai kuwa wafuasi Wake.**{EW 246.1}**

Niliona masikitiko ya wale wanaotumaini, pale ambapo hawakumwona Bwana wao kwa wakati uliotazamiwa (1844 October 22). Lilikuwa kusudi la Mungu kuficha wakati ujao na kuwaleta watu Wake

katika mahali ambapo walipaswa kufanya uamuzi. Pasipo kuhubiriwa kwa wakati kamili wa kuja kwa Kristo, kazi iliyokusudiwa na Mungu isingetimilizwa. Shetani alikuwa akiwaongoza wengi sana kutazama mbali sana katika siku zijazo kwa ajili ya matukio makubwa yanayohusiana na hukumu na mwisho wa rehema. Ilikuwa ni muhimu kwamba watu waletwe katika kujitahidi kwa ari kufanya maandalizi ya sasa.**{EW 246.2}**

Wakati ule ulipopita, wale ambao walikuwa hawajaipokea kikamilifu nuru ya malaika waliungana na wale ambao walikuwa wameudharau ujumbe huo, na wakawageukia wale waliovunjika moyo kwa dhihaka. Malaika walizingatia hali ya wale wanaodai kuwa wafuasi wa Kristo. Kupita kwa muda maalumu ule mahususi kulikuwa kumewajaribu na kuwathibitisha, na wengi sana walikuwa wamepimwa katika mizani na kuonekana wamepungua. Walidai kwa sauti kubwa kuwa walikuwa Wakristo, lakini karibu katika kila jambo walishindwa kumfuata Kristo. Shetani alifurahi juu ya hali ya wale wanaodai kuwa wafuasi wa Yesu. Alikuwa nao katika mtego wake. Alikuwa amewaongoza walio wengi kuiacha njia iliyonyoka, nao walikuwa wakijaribu kupanda kwenda mbinguni

kwa njia nyingine. Malaika waliona wale walio safi na watakatifu wakiwa wamechanganyika na wenye dhambi huko Sayuni na pamoja wanafiki wanaoupenda ulimwengu. Walikuwa wanawalinda na kuwaangalia wanafunzi wa Kweli wa Yesu; lakini wale waliopotoka walikuwa wakiwaathiri watakatifu. Wale ambao mioyo yao iliwaka kwa shauku kubwa ya kutaka kumwona Yesu walikatazwa na wale waliokiri kuwa ndugu zao kuzungumza juu ya kuja Kwake. Malaika walitazama mandhari ile na kuwahurumia masalio ambao walipenda kuonekana kwa Bwana wao.**{EW 246.3}**

Malaika mwingine mwenye nguvu aliagizwa kushuka duniani. Yesu aliweka mkononi mwake maandishi, na alipokuja duniani, alipaza sauti akisema, "Umeanguka, umeanguka Babeli," Kisha nikaona wale waliokata tamaa wakiinua macho yao tena kuelekea mbinguni, wakiangalia kwa imani na kutumaini kuonekana kwa Bwana wao. Lakini wengi walionekana kubaki katika hali ya ujinga, kana kwamba wamelala; lakini niliweza kuona dalili ya huzuni kubwa kwenye nyuso zao. Wale waliokatishwa tamaa waliona kutoka katika Maandiko kwamba walikuwa katika wakati wa kukawia, na kwamba lazima wangojee kwa subira

utimilifu wa maono. Uthibitisho huo huo ambao uliwaongoza kumtarajia Bwana wao mwaka 1843, huu uliwaongoza kumtazamia mwaka 1844. Hata hivyo niliona kwamba wengi hawakuwa na nguvu ile ambayo iliashiria imani yao katika mwaka 1843. Kukatishwa tamaa kwao kulipunguza imani yao.**{EW 247.1}**

Watu wa Mungu walipoungana katika kilio cha malaika wa pili, jeshi la mbinguni lilionesha kupendezwa zaidi na matokeo ya ujumbe huo. Waliwaona wengi waliobeba jina la kuwa Wakristo wakigeuka kwa dharau na dhihaka juu ya wale ambao walikuwa wamevunjika moyo. Wakati maneno yalipoanguka kutoka katika midomoni ya dhihaka, "Hivi bado hamjapanda kwenda juu!" malaika aliyaandikia. Malaika yule akasema: “wanamdhihaki Mungu.” Nilielekezwa nyuma dhambi kama hiyo iliyofanywa katika nyakati za zamani. Eliya alihamishwa kwenda mbinguni, na vazi lake lilikuwa limemwangukia Elisha. Kisha vijana waovu, ambao walikuwa wamejifunza kutoka kwa wazazi wao kumdharau mtu wa Mungu, walimfuata Elisha, na kwa dhihaka wakipiga kelele, "Paa wewe mwenye upaa; Paa wewe mwenye upaa." Katika kumtukana hivyo mtumishi Wake,

walimtukana Mungu na kukutana na adhabu yao ya papo hapo. Vivyo hivyo, wale ambao wametoa maneno ya dharau na kudhihaki wazo la watakatifu kupanda kwenda juu, watapatilizwa kwa ghadhabu ya Mungu, na watafanywa kuhisi kwamba si jambo dogo kumchezea Muumba wao.**{EW 247.2}**

Yesu aliwaagiza malaika wengine kuruka haraka kufufua na kuimarisha imani iliyokuwa inafifia ya watu Wake na kuwaandaa kwa ajili ya kuelewa ujumbe wa malaika wa pili na jambo muhimu ambalo lilikuwa karibu kutendwa mbinguni. Niliona malaika hawa wakipokea nguvu kubwa na nuru kutoka kwa Yesu na kuruka haraka kwenda duniani kutimiza agizo lao la kumsaidia malaika wa pili katika kazi yake. Nuru kubwa iling'aa juu ya watu wa Mungu wakati malaika walipopaza sauti, " Haya, Bwana arusi; tokeni mwende kumlaki!" Kisha niliwaona hawa waliokata tamaa wakiinuka na kwa upatanifu na malaika wa pili walitangaza, “Haya, Bwana arusi; tokeni mwende kumlaki!” Nuru kutoka kwa malaika wale ilipenya giza kila mahali. Shetani na malaika wake walijitahidi kuzuia nuru hii isienee na kuwa na matokeo yake yaliyopangwa. Walishindana na malaika kutoka mbinguni, wakiwaambia kwamba Mungu alikuwa

amewadanganya watu hawa, na kwamba kwa nuru na nguvu zao zote wasingeweza kuufanya ulimwengu uamini kwamba Kristo anakuja. Lakini licha ya Shetani kujitahidi kuzuia njia na kuvuta mawazo ya watu kutoka katika nuru, malaika wa Mungu waliendelea na kazi yao.**{EW 248.1}**

Wale waliopokea nuru walionekana kuwa na furaha sana. Waliangalia mbinguni kwa uthabiti na kutamani sana kuonekana kwa Yesu. Wengine walikuwa wakiomboleza na kuomba kwa dhiki kuu. Macho yao yalionekana kukazwa kwao wenyewe wala hawakuthubutu kuangalia juu. Nuru kutoka mbinguni iliitawanya giza lile kutoka kwao, na macho yao yaliyokuwa yamekazwa kwao wenyewe, yaligeuzwa kuangalia juu, wakati huo shukrani na furaha takatifu zilioneshwa juu ya kila sura. Yesu na jeshi lote la malaika waliwatazama kwa kuwakubali waaminifu wale waliokuwa wakingojea.**{EW 248.2}**

Wale waliokataa na kuipinga nuru ya ujumbe wa malaika wa kwanza, walipoteza nuru ya malaika wa pili, na hawakuweza kufaidika na nguvu na utukufu ulioandamana na ujumbe huo, “Haya, Bwana arusi.” Yesu aligeuka kutoka kwao kwa kuchukia; kwa sababu walikuwa wamempuuza na kumkataa. Wale walioupokea ujumbe huu walifunikwa na wingu la

utukufu. Waliogopa sana kumkosea Mungu, nao walisubiri na kukesha na kuomba wapate kuyajua mapenzi Yake. Nilimwona Shetani pamoja na malaika zake wakijitahidi kufunga nuru hii ya Kiungu isiwafikie watu wa Mungu; lakini kadiri wale wanaosubiri walivyoithamini nuru ile na kuweka macho yao kuangalia juu kutoka duniani kwenda kwa Yesu, Shetani asingeweza kuwa na uwezo wa kuwanyima miale yake ya thamani. Ujumbe uliotolewa kutoka mbinguni ulimkasirisha Shetani na malaika wake, na kuwaongoza wale waliodai kumpenda Yesu, lakini wakaudharau ujio Wake, kuwadharau na kuwadhihaki wale waaminifu, wenye kutumaini. Lakini malaika akaweka alama kila tusi, kila dharau, kila kosa, ambalo watoto wa Mungu walipokea kutoka kwa wale wanaodai kuwa ndugu zao.**{EW 249.1}**

Wengi sana waliinua sauti zao kulia, "Haya, Bwana arusi anakuja!" na kuwaacha ndugu zao ambao hawakupenda kuonekana kwa Yesu, na ambao wasingeruhusu waeleze sana juu ya kuja Kwake mara ya pili. Nilimwona Yesu akigeuza uso Wake kutoka kwa wale waliokataa na kudharau kuja Kwake, na kisha akawaambia malaika wawaongoze watu Wake kutoka miongoni mwa wale wachafu,

wasije wakachafuliwa. Wale ambao walikuwa watiifu kwa ujumbe walijitokeza wakiwa huru na wenye umoja. Nuru takatifu iliangaza juu yao. Waliuacha ulimwengu, wakatoa kafara masilahi yao ya dunia, wakaachilia hazina zao za dunia, na kukaza macho yao kwa shauku kuelekea mbinguni, wakitarajia kumwona Mkombozi wao mpendwa. Nuru takatifu ilimulika juu ya nyuso zao, ikisema juu ya amani na furaha iliyotawala ndani. Yesu aliwaambia malaika Zake waende na kuwatia nguvu, kwa maana saa ya kujaribiwa kwao ilikuwa karibu. Niliona kwamba hawa waliokuwa wakingojea bado hawakuwa wamejaribiwa kama inavyopasa. Hawakuwa huru kutokana na makosa. Nami niliona rehema na wema wa Mungu katika kutuma onyo kwa watu wa dunia, na ujumbe uliorudiwa mara kwa mara kwa ajili ya kuwaongoza katika kujichunguza moyo kwa bidii, na kujifunza Maandiko, ili waweze kuyavua makosa kutoka kwao yale ambayo yamerithishwa kutoka kwa wapagani na wafuasi wa kanisa la Kirumi. Kupitia kwa maagizo haya, Mungu amekuwa akiwasababisha watu Wake kuonekana katika mahali pale ambapo anaweza kufanya kazi kwa ajili yao katika nguvu kubwa, na ambapo wanaweza kuzishika amri Zake zote.**{EW 249.2}**

## Sura ya 57-Patakatifu

Nilioneshwa masikitiko makubwa ya watu wa Mungu kwamba hawakumwona Yesu kwa wakati uliotarajiwa. Hawakujua kwa nini Mwokozi wao hakuja; kwa kuwa hawakuweza kuona ushahidi kwamba wakati wa unabii ulikuwa haujafika mwisho. Malaika yule akasema, “ Je, Neno la Mungu limeshindwa? Je, Mungu ameshindwa kutimiza ahadi Zake?” Hapana; ametimiza yote aliyoaahidi. Yesu ameinuka na kufunga mlango wa chumba cha Patakatifu katika Patakatifu pa mbinguni na amefungua mlango wa Patakatifu pa Patakatifu na kuingia ndani ili apate kupatakasa Patakatifu. Wale wote ambao wanasubiri kwa uvumilivu watalielewa fumbo hili. Mwanadamu amekosea, lakini hakujatokea kushindwa kwa upande wa Mungu. Yote yalitimizwa ambayo Mungu alikuwa ameahidi; lakini mwanadamu kwa kukosea aliamini kwamba dunia ndio ilikuwa ni patakatifu pa kutakaswa mwishoni mwa nyakati za unabii. Ni matarajio ya mwanadamu, wala si ahadi ya Mungu, ambayo yalishindwa kutimia."**{EW 250.1}**

Yesu aliwatuma malaika Wake kuelekeza akili za wale waliokatishwa tamaa kwenye katika Patakatifu pa Patakatifu, ambapo Alikuwa amekwenda ili apate kupatakasa Patakatifu na kufanya upatanisho maalum kwa Israeli. Yesu aliwaambia malaika kwamba wote ambao wangempata wangeelewa kazi ambayo alipaswa kuifanya. Niliona kwamba wakati ule Yesu alipokuwa katika Patakatifu pa Patakatifu angefunga ndoa na Yerusalemu Mpya; na baada ya kazi Yake kukamilika katika Patakatifu, angeshuka duniani kwa nguvu za kifalme na kuchukua Kwake wale wenye thamani sana ambao walikuwa wakingojea kwa subira kurudi Kwake.**{EW 251.1}**

Nilioneshwa kile kilichotokea mbinguni mwishoni mwa vipindi vya unabii mnamo mwaka 1844. Yesu alipomaliza huduma  Yake katika Patakatifu na kufunga mlango wa chumba hicho, giza kuu likawakalia wale ambao walikuwa wamesikia na kuukataa ujumbe wa kuja Kwake, na macho yao yakaacha kumwona. Kisha Yesu akajivika mavazi ya thamani sana. Upande wa chini wa joho lake kulizungukwa na kengele na komamanga, kengele na komamanga. Deraya ya kifuani kwa ajili ya kazi ya uchunguzi ilining’inizwa

kutoka mabegani Mwake. Aliposogea, hii iling'aa kama almasi, ikikuza herufi zilizoonekana kama majina yaliyoandikwa au kuchongwa kwenye ile deraya ya kifuani. Juu ya kichwa Chake kulikuwa na kitu fulani ambacho kilikuwa na mwonekano wa taji. Alipokwisha kujivika kikamilifu, alizungukwa na malaika, na katika gari la moto alipita kuingia ndani ya pazia au kiwambaza cha pili.**{EW 251.2}**

Kisha niliambiwa kuviangalia vyumba vile viwili vya Patakatifu pa mbinguni. Pazia, au mlango, ulikuwa umefunguliwa, nami nikaruhusiwa kuingia. Katika chumba cha kwanza niliona kinara cha taa saba, meza ya mikate ya wonyesho, madhabahu ya kufukizia uvumba, na chetezo. Samani zote za chumba hiki zilionekana kama dhahabu safi kabisa nazo ziliakisi sura ya yule aliyeingia mahali hapo. Pazia ambalo lilitenganisha vyumba hivi viwili lilikuwa ni lenye rangi na vitambaa tofauti, na pindo zuri, ambalo ndani yake kulikuwa na vielelezo vilivyotengenezwa kwa dhahabu kuwakilisha malaika. Pazia hili liliinuliwa, nami nikatazama katika chumba cha pili. Hapo nikaona Sanduku la Agano ambalo lilikuwa na muonekano wa kuwa la dhahabu nzuri zaidi. Kama mpaka karibu na juu ya

sanduku, lililokuwa na mwonekano wa kuwa ni dhahabu safi kabisa. Ndani ya sanduku hili kulikuwa na mbao za mawe zenye Amri Kumi.**{EW 251.3}**

Makerubi wawili wa kupendeza, mmoja kila upande wa sanduku la agano, walisimama huku mabawa yao yamenyoshwa juu yake, na kugusana juu ya kichwa cha Yesu alipokuwa amesimama mbele ya kiti cha rehema. Nyuso zao zilielekeana, nao waliangalia chini kwenye Sanduku la Agano, ikiwakilisha jeshi lote la malaika wakiiangalia kwa shauku sheria ya Mungu. Kati ya makerubi hawa kulikuwako na chetezo cha dhahabu, na pale maombi ya watakatifu, yaliyotolewa kwa imani, yalipopanda kuja kwa Yesu, Naye akayawasilisha kwa Baba Yake, wingu la harufu nzuri liliinuka kutoka kwenye uvumba, likionekana kama moshi wenye rangi nyingi nzuri mno. Juu ya mahali pale ambapo Yesu alikuwa amesimama, mbele ya sanduku la agano, kulikuwa na utukufu ulioangaza mno kiasi kwamba sikuweza kuutazama; ulionekana kama kiti cha enzi cha Mungu. Wakati uvumba ulipokuwa unapanda kwenda kwa Baba, utukufu bora ulikuja kwa Yesu kutoka katika kiti cha enzi, na kutoka Kwake ulitawanywa juu ya wale

ambao maombi yao yalikuwa yamepanda juu kama uvumba mzuri. Nuru iliyoenezwa juu ya Yesu kwa fahari nyingi ilikitia kivuli kiti cha rehema, na mfululizo wa utukufu ukalijaza hekalu. Sikuweza kuuangalia kwa muda mrefu mwangaza ule usio na kifani. Hakuna lugha inaweza kuielezea. Nilizidiwa na kugeuka kutoka katika ukuu na utukufu wa mandhari ile.**{EW 252.1}**

Pia nilioneshwa Patakatifu palipo juu ya nchi, palipokuwa na vyumba viwili. Palifanana na pale pa mbinguni, na niliambiwa kwamba palikuwa ni kielelezo cha Patakatifu pa mbinguni. Samani iliyokuwa katika chumba cha kwanza cha Patakatifu pa duniani ilikuwa kama ile iliyomo katika chumba cha kwanza cha Patakatifu pa mbinguni. Pazia liliinuliwa, na nikatazama ndani ya Patakatifu pa Patakatifu na kuona kwamba samani iliyokuwamo ilikuwa sawa na ile iliyomo katika patakatifu pa patakatifu pa mbinguni. Kuhani alihudumu katika vyumba vyote viwili vya ulimwengu. Aliingia kila siku katika chumba cha kwanza, bali aliingia katika Patakatifu pa Patakatifu mara moja tu kwa mwaka, ili apate kupatakasa kutokana na dhambi ambazo zilikuwa zimefikishwa hapo. Niliona kwamba Yesu alihudumu katika

vyumba vyote viwili vya Patakatifu pa mbinguni. Makuhani waliingia katika Patakatifu pa duniani wakiwa na damu ya mnyama kama sadaka ya dhambi. Kristo aliingia katika Patakatifu pa mbinguni akiwa na sadaka ya damu Yake Mwenyewe. Makuhani wa duniani waliondolewa kwa kifo; kwa hiyo hawakuweza kuendelea kwa muda mrefu; lakini Yesu alikuwa ni kuhani milele. Kupitia dhabihu na sadaka zilizoletwa katika Patakatifu pa duniani, wana wa Israeli walipaswa kuzishikilia sifa na stahili za Mwokozi ambaye alikuwa anakuja. Na kwa hekima ya Mungu mambo yote yanayohusu kazi hii yalitolewa kwetu ili tuweze, kwa kuyaangalia, kufahamu kazi ya Yesu katika Patakatifu pa mbinguni.**{EW 252.2}**

Yesu alipokufa pale Kalvari, alipaza sauti akisema, "Imekwisha," na pazia la hekalu lilipasuka vipande viwili, kutoka juu hadi chini. Hii ilipaswa kuonesha kwamba huduma za Patakatifu pa duniani zilikuwa zimemalizika milele, na kwamba Mungu asingekutana tena na makuhani katika hekalu lao la duniani, kuzipokea dhabihu zao. Damu ya Yesu ilimwagika wakati huo, ambayo ilipaswa kutolewa na Yeye Mwenyewe katika Patakatifu pa mbinguni. Kama vile kuhani alivyoingia Patakatifu

pa Patakatifu mara moja kwa mwaka kwa ajili ya kupatakasa Patakatifu pa duniani, ndivyo Yesu alivyoingia katika Patakatifu pa mbinguni, mwishoni mwa siku 2300 za Danieli 8, mwaka 1844, ili apate kufanya upatanisho wa mwisho kwa wote ambao wangeweza kufaidika na upatanisho Wake, na hivyo kupatakasa Patakatifu. **{EW 253.1}**

## Sura ya 58-Ujumbe wa Malaika wa Tatu

[Angalia Kiambatisho.]

Wakati huduma ya Yesu ilipokwisha katika Patakatifu, Naye akaingia katika Patakatifu pa Patakatifu, na kusimama mbele ya Sanduku la Agano lililo na sheria ya Mungu, na alimtuma malaika mwingine mwenye nguvu na ujumbe wa tatu kwa ulimwengu. Karatasi iliyotengenezwa kwa ngozi iliwekwa mkononi mwa malaika huyu, na alipokuwa anashuka duniani kwa nguvu na utukufu, alitangaza onyo la kutisha, na ogofyo kubwa ambalo likuwa halijawahi kutolewa kwa mwanadamu. Ujumbe huu ulikusudiwa kuwafanya watoto wa Mungu wajihadhari, wawe kwenye kituo chao cha ulinzi, kwa kuwaonesha saa ya majaribu na maumivu makali iliyokuwa mbele yao. Malaika

alisema, "Wataletwa katika mapambano makali na yule mnyama na sanamu yake. Tumaini lao pekee la uzima wa milele ni kubaki kuwa thabiti. Ingawa maisha yao yako hatarini, lazima washikilie Ukweli kwa nguvu." Malaika wa tatu anahitimisha ujumbe wake hivi: "Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao amri za Mungu, na imani ya Yesu." Alipokuwa anayarudia Maneno haya, alielekeza katika Patakatifu pa mbinguni. Akili za wote wanaoukubali ujumbe huu zinaelekezwa katika Patakatifu pa Patakatifu, ambapo Yesu amesimama mbele ya Sanduku la Agano, akifanya maombezi Yake ya mwisho kwa wale wote ambao kwao rehema bado ilikuwa inadumu na kwa wale ambao wameivunja sheria ya Mungu pasipo kujua. Upatanisho huu unafanyika kwa ajili ya wenye haki waliokufa na pia kwa wale wenye haki walio hai. Unawajumuisha wote waliokufa wakimtumaini Kristo, lakini ambao, kwa kutokupokea nuru juu ya amri za Mungu, walitenda dhambi bila kwa ujinga, yaani bila ya kujua katika kuyakiuka maagizo Yake. . **{EW 254.1}**

Baada ya Yesu kufungua mlango wa Patakatifu pa Patakatifu, nuru ya Sabato ilionekana, na watu wa Mungu walijaribiwa, kama wana wa Israeli

walivyojaribiwa hapo kale, kuona kama wangeishika sheria ya Mungu. Nilimwona malaika wa tatu akielekeza juu, akiwaonesha wale waliokata tamaa njia ya Patakatifu pa Patakatifu pa mbinguni. Pale wanapoingia kwa imani katika Patakatifu pa Patakatifu, wanamkuta Yesu, na tumaini na furaha vinachipuka upya. Niliwaona wakiangalia nyuma, wakiyapitia upya yale yaliyopita, kuanzia kutangazwa kwa ujio wa pili wa Yesu, hadi uzoefu wao katika kupita kwa wakati mnamo 1844. Wanaona kuwa kusikitishwa kwao kunaelezewa, na furaha na uhakika tena vinawahuisha. Malaika wa tatu amemulika wakati uliopita, wakati uliopo, na wakati ujao, na wanajua kwamba Mungu amewaongoza kwa majaliwa Yake ya ajabu. . **{EW 254.2}**

Iliwakilishwa kwangu kwamba masalio/waliosalia walimfuata Yesu kwenda katika Patakatifu pa Patakatifu na kuliona Sanduku la Agano na Kiti cha Rehema, nao walivutiwa na utukufu wao. Kisha Yesu akainua kifuniko cha Sanduku la Agano, na tazama! Mbao za mawe, zikiwa na Amri Kumi zimeandikwa juu yake. Walifuatilia kwenda chini maneno yale ya

kuchangamsha ya kisa hai, lakini wakaanza tena mwanzo kwa kutetemeka wanapoona amri ya nne miongoni mwa Amri Kumi zile takatifu, ikiwa na nuru ikiangaza juu yake iliyo angavu kuliko ya zile tisa nyingine, na duara la utukufu kuizunguka pande zote. Hawapati kitu chochote huko kinachowajulisha kwamba Sabato imefutwa, au kubadilishwa kwenda siku ya kwanza ya juma. Amri inasomeka kama wakati ilipotamkwa na sauti ya Mungu kwa fahari nzito na ya kutisha juu ya mlima, wakati huo umeme ukiwa unamulika na radi zinanguruma; iko vile vile kama ilivyoandikwa wakati ule kwa kidole Chake Mwenyewe kwenye mbao za mawe: "Siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote; lakini siku ya saba ni Sabato ya Bwana, Mungu wako." Wanashangaa wanapoona utunzaji unaofanywa kwa *Amri Kumi*. Wanaziona Amri zikiwa zimewekwa karibu na Yehova, zikiwa zimefunikwa na kulindwa kwa utakatifu Wake. Wanaona kwamba wamekuwa wakiikanyaga amri ya nne ya zile Amri Kumi, nao wameitunza siku iliyorithishwa na wapagani na wafuasi wa kanisa la Kirumi, badala ya siku iliyotakaswa na Yehova. Wanajinyenyekesha mbele za Mungu na kuomboleza juu ya dhambi zao za zamani. **{EW**

**255.1}**

Niliona uvumba katika chetezo ukitoa moshi wakati Yesu alipokuwa anatoa maungamo na maombi yao kwa Baba Yake. Na ulipokuwa unapaa, nuru angavu ilitulia juu ya Yesu na juu ya kiti cha rehema; na wale waliokuwa wakiomba kwa bidii, waliotaabika, kwa sababu walikuwa wamegundua kuwa wao ni wavunjaji wa sheria ya Mungu, walibarikiwa, na nyuso zao ziliangaza kwa tumaini na furaha. Walijiunga katika kazi ya malaika wa tatu na kupaza sauti zao kutangaza onyo hilo zito. Lakini wachache mwanzoni walilipokea; lakini bado wale walio waaminifu waliendelea kwa nguvu kuutangaza ujumbe huu. Kisha nikaona wengi wakiukubali ujumbe wa malaika wa tatu na kuunganisha sauti zao na za wale ambao walikuwa wametoa onyo la kwanza, nao walimheshimu Mungu kwa kuitunza siku Yake ya mapumziko iliyotakaswa. **{EW 256.1}**

Wengi walioukubali ujumbe wa malaika wa tatu hawakuwa na uzoefu katika maagizo mawili ya awali. Shetani alilielewa hili, na jicho lake ovu lilikuwa juu yao kuwaangusha; lakini malaika wa

tatu alikuwa akiwaelekeza mahali palipo Patakatifu zaidi, na wale ambao walikuwa wamepata uzoefu wa maagizo yaliyopita walikuwa wakiwaelekeza njia ya Patakatifu pa mbinguni. Wengi waliona mnyororo mkamilifu wa Ukweli katika maagizo ya malaika hawa, na kwa furaha wakayapokea katika mfuatano wao, na kumfuata Yesu kwa imani hadi Patakatifu pa mbinguni. Ujumbe [maagizo haya] huu uliwasilishwa kwangu kama nanga kwa watu wa Mungu. Wale wanaozielewa na kuzipokea watalindwa wasije wakazolewa na madanganyo mengi ya Shetani.**{EW 256.2}**

Baada ya sikitiko kuu mnamo mwaka 1844, Shetani na malaika wake walijihusisha sana katika kuweka mitego ili kutupilia mbali imani ya kundi. Aligusa akili za watu wale ambao walikuwa wamepata uzoefu katika maagizo haya, na ambao walikuwa na mwonekano wa unyenyekevu. Wengine walielekeza katika wakati ujao kwa ajili ya utimizaji wa ujumbe wa kwanza na wa pili, wakati wengine walionesha nyuma sana katika siku zilizopita, wakitangaza kwamba yalikuwa yametimizwa wakati huo. Hawa walikuwa wakipata ushawishi juu ya akili za wasio na uzoefu na kuvuruga imani yao. Wengine walikuwa

wakiichunguza Biblia ili kujenga imani yao wenyewe, bila ya kulitegemea kundi. Shetani aliyafurahia haya yote; kwa maana alijua kwamba wale waliojitoa katika kifungo cha nanga angeweza kuwaathiri kwa makosa mbalimbali na kuendesha upepo anuwai wa mafundisho. Wengi ambao walikuwa maarufu katika ujumbe wa kwanza na wa pili sasa waliwakataa, na kulikuwa na mgawanyiko na ghasia kote katika kundi lote.**{EW 256.3}**

Kisha umakini wangu ulielekezwa kwa William Miller. Mtu huyu alionekana kufadhaika na alikuwa ameinamishwa kwa wasiwasi na dhiki kwa ajili ya watu Wake. Kundi lile lililokuwa limeungana na kupendana mnamo 1844 walikuwa wakipoteza upendo wao, wakipingana wao kwa wao, na kuanguka katika hali ya ubaridi, ya kurudi nyuma. Alipoliona hili, huzuni ilidhoofisha nguvu yake. Nikawaona watu maarufu wakimwangalia, wakihofu asije akaupokea ujumbe wa malaika wa tatu na amri za Mungu. Na pale ambapo angeweza kuelekea upande wa nuru kutoka mbinguni, watu hawa wangeweka mpango wa kuvuta mawazo yake kwenda mbali. Ushawishi wa kibinadamu ulitumika kumweka gizani na kubakiza ushawishi wake kuwa miongoni mwa wale walioupinga Ukweli. Hatimaye

William Miller aliinua sauti yake dhidi ya nuru kutoka mbinguni. Alishindwa katika kutokupokea ujumbe ambao ungeelezea kikamilifu kukatishwa tamaa kwake na kutoa nuru na utukufu juu ya siku zilizopita, ambao ungefufua nguvu zake zilizokuwa zimetumika zote, kisha ungechangamsha tumaini lake, na kumwongoza katika kumtukuza Mungu. Alitegemea hekima ya kibinadamu badala ya ile ya Bwana, lakini akiwa amevunjika kwa sababu ya bidii katika kusudi la Bwana wake na umri, hakuwajibika kama wale waliomzuilia Ukweli. Hao wanawajibika; dhambi ile iko juu yao.**{EW 257.1}**

Kama William Miller angweza kuona nuru ya ujumbe wa tatu, mambo mengi ambayo yalionekana kuwa giza na fumbo kwake yangeweza kuelezewa. Lakini ndugu zake walikiri kwa mdomo upendo wa kina sana na shauku kwake, kiasi kwamba asingeweza kuwaacha. Moyo wake ungeweza kuuelekea Ukweli, na kisha aliwaangalia ndugu zake; na hawa waliupinga. Je, aachane na wale ambao walikuwa wamesimama pamoja naye bega kwa bega katika kuutangaza ujio wa Yesu? Aliwaza kwamba wasingeweza kumpotosha.**{EW 258.1}**

Mungu aliruhusu aanguke chini ya nguvu za

Shetani, ufalme wa mauti, na kumficha kaburini kutoka kwa wale ambao daima walikuwa wakimvuta kutoka katika Ukweli. Musa alifanya kosa alipokuwa karibu na kuingia katika Nchi ya Ahadi. Hivyo pia, niliona kwamba William Miller alikosea mara tu alipokaribia kuingia Kanaani ya mbinguni, kwa kuruhusu ushawishi wake kwenda kinyume na Ukweli. Wengine walimwongoza katika hili; wengine ni lazima watatoa hesabu juu ya hili. Lakini malaika wanayaangalia mavumbi ya thamani ya mtumishi huyu wa Mungu, na atatoka nje wakati sauti ya tarumbeta ya mwisho itakaposikika.**{EW 258.2}**

## Sura ya 59- Jukwaa Imara

Niliona kundi ambalo lilisimama likiwa limelindwa vyema na likiwa thabiti, pasipo kukubali ushauri wa wale ambao wangeivuruga imani imara ya kundi hili. Mungu aliwaangalia kwa ukubali. Nilioneshwa madaraja matatu - ujumbe wa malaika wa kwanza, wa pili, na wa tatu. Malaika aliyeandamana nami alisema, “Ole wake atakayehamisha tofali moja au kutikisa msumari wa maagizo haya. Uelewa wa kweli wa maagizo haya ni

muhimu sana. Hatima ya roho hutegemea jinsi yanavyopokelewa.” Nilichukuliwa tena kupitia maagizo haya, na nikaona jinsi watu wa Mungu walivyonunua uzoefu wao kwa gharama kubwa. Ulipatikana kupitia mateso mengi na mapambano makubwa. Mungu alikuwa amewaongoza hatua kwa hatua, hadi alipowaweka kwenye jukwaa imara, lisilohamishika. Niliona watu wakija kwenye jukwaa na kuchunguza msingi. Baadhi kwa furaha, na mara moja walipanda juu yake. Wengine walianza kuukosoa msingi. Walitamani maboresho yafanyike, ndipo jukwaa lingekuwa kamilifu zaidi, na watu wangekuwa na furaha zaidi. Wengine walitoka kwenye jukwaa ili wapate kulichunguza nao walitangaza kuwa liliwekwa vibaya. Lakini niliona kwamba karibu wote walisimama imara juu ya jukwaa na kuwasihi wale ambao walikuwa wameteremka kutoka jukwaani kuacha malalamiko yao; kwa kuwa Mungu Ndiye aliyekuwa Mjenzi Mkuu, nao walikuwa wakipigana vita dhidi Yake. Walisimulia kazi ya ajabu ya Mungu, ambayo ilikuwa imewaongoza kwenye jukwaa thabiti, na kwa umoja wakainua macho yao mbinguni na kwa sauti kuu wakamtukuza Mungu.  Jambo hili liliwagusa baadhi ya wale waliokuwa wamelalamika

na kuondoka kwenye jukwaa, na kwa sura ya unyenyekevu walipanda na kulikanyaga juu yake tena.**{EW 258.3}**

Nilielekezwa nyuma katika tangazo la ujio wa kwanza wa Kristo. Yohana alitumwa kwa roho na nguvu ya Eliya kuandaa njia ya Yesu. Wale walioukataa ushuhuda wa Yohana hawakufaidika na mafundisho ya Yesu. Upinzani wao kwa ujumbe ambao ulitabiri kuja Kwake uliwaweka katika mahali ambapo wasingeweza kupokea kwa urahisi ushahidi wenye nguvu kwamba alikuwa ndiye Masihi. Shetani aliwaongoza wale walioukataa ujumbe wa Yohana kwenda mbali zaidi, kumkataa na kumsulubisha Kristo. Kwa kufanya hivi walijiweka katika mahali ambapo wasingeweza kupokea baraka katika siku ya Pentekoste, ambayo ingewafundisha njia ya kuingia katika Patakatifu pa mbinguni. Kupasuka kwa pazia la hekalu kulionesha kwamba dhabihu/kafara na ibada za Kiyahudi zisingepokelewa tena. Dhabihu/kafara kuu ilikuwa imetolewa na kukubaliwa, na Roho Mtakatifu ambaye alishuka siku ya Pentekoste alikuwa amechukua akili za wanafunzi kutoka katika Patakatifu pa duniani kwenda kwa Patakatifu pa mbinguni, ambapo Yesu alikuwa ameingia kwa

damu Yake mwenyewe, kumwaga juu ya wanafunzi Wake faida za upatanisho Wake. Lakini Wayahudi waliachwa katika giza kamili. Walipoteza nuru yote ambayo wangeweza kuwa nayo juu ya mpango wa wokovu, na bado waliamini katika dhabihu/kafara na sadaka zao zisizo na maana. Patakatifu pa mbinguni palikuwa pamechukua nafasi ya Patakatifu pa duniani, lakini hawakuwa na ufahamu kuhusu mabadiliko hayo. Kwa hiyo hawakuweza kufaidika na upatanisho wa Kristo katika mahali Patakatifu.**{EW 259.1}**

Wengi wanaangalia kwa hofu mwenendo wa Wayahudi katika kumkataa na kumsulubisha Kristo; na wanaposoma historia ya kuonewa na kuteswa Kwake kwa aibu, wanafikiri kwamba wanampenda, na wasingemkana kama alivyofanya Petro, au kumsulubisha kama walivyofanya Wayahudi. Lakini Mungu anayesoma mioyo ya wote, ameuleta kwenye jaribio upendo huo ambao walidai kuuhisi kwa Yesu. Mbingu yote ilitazama kwa hamu kubwa upokeaji wa ujumbe wa malaika wa kwanza. Lakini wengi waliokiri kumpenda Yesu, na ambao walitokwa na machozi walipokuwa wanakisoma kisa cha msalaba, walidhihaki habari njema ya kuja Kwake. Badala ya kuupokea ujumbe ule kwa furaha,

walitangaza kwamba ulikuwa ni udanganyifu. Waliwachukia wale ambao walipenda kuonekana Kwake na kuwafungia nje ya makanisa yao. Wale walioukataa ujumbe wa kwanza wasingeweza kufaidika na ule wa pili; wala hawakufaidika na kilio cha usiku wa manane, ambacho kilikuwa kiwaandae kwa ajili ya kuingia pamoja na Yesu kwa imani katika mahali Patakatifu mno pa Patakatifu pa mbinguni. Na kwa kukataa maagizo hayo mawili ya awali, wameweka giza katika ufahamu wao kiasi kwamba hawawezi kuona nuru katika ujumbe wa malaika wa tatu, ambao unaonesha njia ya kuingia katika patakatifu mno. Niliona kwamba kama vile Wayahudi walivyomsulubisha Yesu, ndivyo makanisa ya majina yalivyousulubisha ujumbe huu, na kwa hiyo hawana ujuzi wa njia ya kuingia katika Patakatifu mno, na hawawezi kufaidika na maombezi ya Yesu yanayofanyika mle. Kama Wayahudi, ambao walitoa dhabihu/kafara zao zisizo na maana, wanatoa maombi yao yasiyo na maana katika chumba ambacho Yesu amekwisha kutoka; na Shetani, akifurahishwa na udanganyifu huo, anachukua tabia ya kidini, na anaongoza akili za hawa wanaokiri kuwa Wakristo kwake, akifanya kazi kwa nguvu zake, ishara zake na maajabu ya

uwongo, kuwafunga katika mtego wake. Baadhi anawafunga kwa njia moja, na wengine kwa njia nyingine. Adui huyu ana udanganyifu tofauti ulioandaliwa kuathiri akili tofauti. Wengine huangalia kwa hofu juu ya udanganyifu mmoja, wakati huo wanaupokea mwingine kwa urahisi. Shetani huwadanganya baadhi ya watu kwa Umizimu. Yeye pia huja kama malaika wa nuru na kueneza ushawishi wake juu ya nchi kwa njia ya matengenezo ya bandia. Makanisa yanasisimka, na kudhani kwamba Mungu anafanya kazi kwa namna ya ajabu kwa ajili yao, wakati ni kazi ya roho nyingine. Msisimko utakufa na kuacha ulimwengu na kanisa katika hali mbaya zaidi kuliko hapo awali.**{EW 260.1}**

Niliona kwamba Mungu ana watoto waaminifu miongoni mwa wale walio Waadventista kwa majina tu na makanisa yaliyoanguka, na kabla mapigo hayajamwagwa, wachungaji na watu wataitwa kutoka katika makanisa haya nao wataupokea Ukweli kwa furaha. Shetani analijua hili; na kabla kilio kikuu cha malaika wa tatu hakijatolewa, atainua msisimko katika jamii hizi za kidini, ili wale walioukataa Ukweli wafikirie kuwa Mungu yuko pamoja nao. Anatarajia kuwadanganya

waaminifu na kuwaongoza kufikiri kwamba Mungu bado anafanya kazi kwa ajili ya makanisa haya. Lakini nuru itang'aa, na wote walio waaminifu watayaacha makanisa yaliyoanguka, na kusimama pamoja na masalio/waliosalia.**{EW 261.1}**

## Sura ya 60-Umizimu-Kubisha-bisha hodi kwa njia ya Kushangaza

Udanganyifu wa kubisha hodi kwa njia ya kushangaza (Mysterious rappings) uliwasilishwa mbele yangu, na nikaona kwamba Shetani ana uwezo wa kuleta mbele yetu kuonekana kwa sura zinazodaiwa kuwa jamaa zetu au marafiki wanaolala katika Yesu. Itafanywa ionekane kana kwamba marafiki hawa walikuwepo hasa; maneno ambayo waliyatamka walipokuwa hapa, ambayo tuliyazoea, yatasemwa, na toni ile ile ya sauti waliyokuwa nayo wakiwa hai itaanguka kwenye sikio. Yote haya ni kwa ajili ya kuidanganya duniana kuwanasa katika imani ya udanganyifu huu. **{EW 262.1}**

Niliona kwamba watakatifu ni lazima wapate ufahamu kamili wa Ukweli wa sasa, ambao watalazimika kuudumisha kutoka katika Maandiko.

Ni lazima waelewe hali ya wafu; kwani roho za mashetani bado zitaonekana kwao, zikidai kuwa ni jamaa zao au marafiki wao wapendwa, ambao watawatangazia mafundisho yasiyo ya Kimaandiko. Watafanya yote yaliyo katika uwezo wao wapate kuchochea huruma nao watafanya miujiza mbele yao ili kuthibitisha kile wanachotangaza. Watu wa Mungu lazima wawe tayari kuzihimili roho hizi kwa Ukweli wa Biblia kwamba wafu hawajui jambo lolote, na kwamba wale wanaoonekana kwao kwa jinsi hiyo ni roho za mashetani.**{EW 262.2}**

Ni lazima tuchunguze vyema msingi wa tumaini letu, kwa kuwa itabidi tutoe sababu kuhusu hilo kutoka katika Maandiko. Udanganyifu huu utaenea, nasi tutalazimika kushindana nao mieleka uso kwa uso; na tusipokuwa tayari kwa hilo, tutanaswa na kushindwa. Lakini ikiwa tunafanya kile tunachoweza kufanya kwa upande wetu kwa ajili ya mapambano ambavyo yako mbele yetu, Mungu atafanya sehemu Yake, na mkono Wake wenye nguvu zote utatulinda. Yeye angetuma mara moja kila malaika kutoka kwenye utukufu kutengeneza ua kuzunguka ya roho waaminifu, kuliko kuwaacha wadanganywe na kupotoshwa na maajabu ya uwongo ya Shetani.

Niliona wepesi ambao kwa huo udanganyifu huu ulikuwa ukienea. Treni yenye mabehewa ilioneshwa kwangu, ikienda kwa kasi ya umeme. Malaika aliniambia niangalie kwa makini. Nikakaza macho yangu kwenye treni ile. Ilionekana kwamba dunia yote ilikuwa ndani ya hiyo treni. Kisha akanionesha kondakta, ambaye alionekana kuwa ni mtu mzuri, adhimu, ambaye abiria wote walimwangalia na kumheshimu sana. Nilishangazwa na kumuuliza malaika aliyeandamana nami huyu alikuwa ni nani. Alisema, "Huyu ni Shetani. Yeye Ndiye kondakta katika umbo la malaika mwenye nuru. Ameichukua dunia mateka. Wamekabidhiwa kwa udanganyifu wenye nguvu, kuamini uwongo, ili wapate kuangamia. Wakala wake huyu, anayefuata kwake kwa ukuu, ni mhandisi/injinia, na wengine katika mawakala wake wamewekwa kutumika katika madaraka mbalimbali kama atakavyowahitaji, na wote wanakwenda kwa mwendo wa umeme kufikia kuangamia kabisa."**{EW 263.1}**

Nilimuuliza malaika kama hakukuwapo na mtu hata mmoja aliyebaki. Aliniambia niangalie upande mwingine, na nikaona kundi dogo wakisafiri katika njia nyembamba. Wote walionekana kuwa na umoja

thabiti, wamefungwa pamoja kwa Ukweli. Kundi hili dogo walionekana kuwa wamechoka kwa taabu, kana kwamba walikuwa wamepitia majaribio na mapambano makali sana. Na ilionekana kana kwamba jua lilikuwa ndio tu limechomoza kutoka nyuma ya wingu na kuangaza nyuso zao, na kuwafanya waonekane kuwa washindi, kana kwamba ushindi wao ulikuwa karibu kupatikana.**{EW 263.2}**

Niliona kwamba Bwana ameupa ulimwengu fursa ya kuugundua mtego ule.  Jambo hili moja ni ushahidi wa kutosha kwa Mkristo, kama hakukuwapo na lingine; yaani, kwamba hakuna tofauti inayowekwa kati ya vyenye thamani na vilivyo viovu. Thomas Paine, ambaye mwili wake sasa umefinyangwa kuwa mavumbi na ambaye ataitwa mwishoni mwa ile miaka elfu moja, katika ufufuo wa pili, kwa ajili ya kupokea thawabu yake na kupata mauti ya pili, anawakilishwa na Shetani kuwa yuko mbinguni, na kuinuliwa sana huko. Shetani alimtumia duniani kwa kadiri alivyoweza, na sasa anaendelea na kazi ile ile kupitia kujifanya kuwa na Thomas Paine aliyeinuliwa sana na kuheshimiwa mbinguni; kama alivyokuwa akifundisha hapa, Shetani angefanya ionekane

kwamba anafundisha mbinguni. Wapo baadhi ambao waliyatazama maisha na kifo chake Paine, kwa hofu kuu, na mafundisho yake yaliyopotoka wakati alipokuwa akiishi, lakini ambao sasa wanakubali kufundishwa naye, mmoja wa watu waovu kabisa na waliopotoka mno, ambaye alimdharau Mungu na sheria Yake.**{EW 263.3}**

Yeye ambaye ni baba wa uongo, anaupofusha na kuudanganya ulimwengu, kwa kuwatuma malaika zake kutoa maneno kwa niaba ya mitume, na kufanya ionekane kwamba wanapingana na yale waliyoyaandika wakiongozwa na Roho Mtakatifu walipokuwa duniani. Malaika hawa wa uongo huwafanya mitume kupotosha mafundisho yao wenyewe na kuyatangaza kuwa yamepotoshwa. Kwa kufanya hivyo Shetani hufurahia kuwatupa Wakristo wanaokiri kwa mdomo tu, na ulimwengu wote katika kutokuwa na hakika juu ya Neno la Mungu. Kitabu hicho Kitakatifu kinakata moja kwa moja kwenye njia yake na kuzuia mipango yake; kwa hiyo anawaongoza kutilia mashaka asili yake, kiasi kwamba ni jambo rahisi kwake kuyajua maneno yale hasa ya kiungu ya Biblia. Kisha anamweka kafiri, Thomas Paine, kana kwamba aliiongozwa kuingia mbinguni wakati alipokufa, na

sasa, akiungana na mitume watakatifu ambao aliwachukia duniani, walikuwa wakijihusisha katika kuufundisha ulimwengu.**{EW 264.1}**

Shetani anampa kila mmoja wa malaika wake sehemu ya kutenda. Anawaamuru wote kuwa wenye hila, stadi, na werevu. Anawaagiza baadhi yao kuigiza nafasi ya mitume na kuzungumza kwa niaba yao, wakati ambapo wengine watapaswa kuigiza nafasi ya makafiri na watu waovu ambao walikufa wakimlaani Mungu, lakini sasa wanaonekana kuwa watu wa kidini sana. Hakuna tofauti inayowekwa kati ya mitume watakatifu mno na makafiri waovu kabisa. Wote wawili wanaoneshwa wakifundisha kitu kile kile. Haijalishi ni nani Shetani anamfanya azungumze, maadam lengo lake linatimizwa. Alikuwa ameunganishwa kwa karibu sana na Paine duniani, akimsaidia katika kazi Paine aliyoyatumia na mwandiko hasa wa yule aliyemtumikia kwa uaminifu kiasi kile na kutimiza makusudi yake vizuri kiasi kile. Shetani aliamuru mengi ya yale aliyoyaandika Paine, na ni jambo rahisi kwake kuamuru hisia kupitia kwa malaika zake sasa na kufanya ionekane kwamba yanatoka katika kazi za Thomas Paine, ambaye, wakati alipokuwa hai, alikuwa mtumishi aliyejitoa wa yule

mwovu. Hii ndio kazi bora ya Shetani (Master Piece). Mafundisho haya yote, yatokayo kwenye Fundisho la umizimu, yanayodaiwa kuwa yanatoka kwa mitume na watakatifu na watu waovu ambao wamekufa, huja moja kwa moja kutoka katika enzi yake ya kishetani. **{EW 264.2}**

Ukweli kwamba Shetani anadai kwamba yule ambaye yeye alimpenda sana, na huyo ambaye alimchukia Mungu kikamilifu, sasa yuko pamoja na mitume watakatifu na malaika katika utukufu, unapaswa kutosha kuondoa pazia kutoka katika akili zote na kuwafunulia kazi za giza, za fumbo za Shetani. Kwa kweli huwa anauambia ulimwengu na makafiri, "Haijalishi wewe ni mwovu kiasi gani, haijalishi kama unamwamini au unamkataa Mungu au Biblia, ishi unavyopenda, mbinguni ni nyumbani kwenu; kwa kuwa wote wanajua kwamba kama Thomas Paine yuko mbinguni, na ameinuliwa kiasi kile, basi, hakika watafika huko." Kosa hili ni dhahiri kiasi kwamba wote wanaweza kuliona kama wanataka. Shetani sasa anatenda kupitia kwa watu kama Thomas Paine kile ambacho amekuwa akijaribu kukifanya tangu anguko lake. Yeye, kupitia katika uwezo wake na maajabu yake ya uongo, anararua msingi wa tumaini la Mkristo na kuliondoa

jua lile ambalo linapaswa kuiangazia njia nyembamba ya kwenda mbinguni. Anaufanya ulimwengu uamini kwamba Biblia haijavuviwa, zaidi ya kitabu chochote cha hadithi, huku akishikilia kitu fulani cha kuchukua nafasi yake; yaani, *udhihirisho wa umizimu!* **{EW 265.1}**

Hii ni njia iliyotengwa kabisa kwa ajili yake mwenyewe na kuwa chini ya udhibiti wake, na anaweza kuifanya dunia kuamini chochote atakacho. Kitabu kile ambacho kitamhukumu yeye pamoja na wafuasi wake anakisogeza nyuma gizani, mahali pale hasa anapotaka kiwepo. Mwokozi wa ulimwengu huu, yeye Paine anamfanya kuwa si zaidi ya mtu wa kawaida; na kama walinzi wa Kirumi waliolilinda kaburi la Yesu walivyoeneza habari ya uwongo ambayo makuhani wakuu na wazee walizitia vinywani mwao, ndivyo wafuasi maskini, wa Paine, ambao wamedanganywa wa udhihirisho huu wa umizimu wa kujisingizia, watarudia na kujaribu kuifanya ionekane kwamba hakuna chochote cha kimuujiza kuhusu kuzaliwa, kufa, na kufufuka kwa Mwokozi wetu. Baada ya kumweka Yesu katika usuli, wanavuta usikivu wa ulimwengu kwao wenyewe na kwa miujiza yao na maajabu ya uongo, ambayo, wanatangaza, kuwa ni

zaidi sana kuliko kazi za Kristo. Hivyo ulimwengu unachukuliwa katika mtego na kutulizwa kujisikia kuwa katika usalama, na wala wasigundue udanganyifu wao mbaya hadi pale mapigo saba ya mwisho yanopomiminwa. Shetani anangua kicheko anapoona mpango wake unafanikiwa vizuri sana na ulimwengu wote ukiwa umekamatwa kwenye mtego na hila hizo.**{EW 265.2}**

## Sura ya  61-Tamaa

Niliona kwamba Shetani aliwaambia malaika wake kuweka mitego yao hasa kwa wale ambao walikuwa wakitazamia kuonekana kwa Kristo mara ya pili na kuzishika amri zote za Mungu. Shetani aliwaambia malaika zake kwamba makanisa yalikuwa yamelala. Angeweza kuongeza nguvu zake na maajabu ya uongo, na angeweza kuyashikilia. "Lakini," alisema, "kikundi cha watunza Sabato tunawachukia; daima wanafanya kazi dhidi yetu, na kuchukua raia wetu, wapate kushika sheria ya Mungu tunayoichukia. Nendeni, mkawafanye, wamiliki wa ardhi na pesa, walewe kwa masumbufu

ya maisha haya. Kama mtaweza kuwafanya waweke mapenzi yao juu ya vitu hivi, bado tutakuwa nao. Wanaweza kukiri chochote wanachopenda, ila wafanyeni kujali zaidi juu ya fedha kuliko juu ya mafanikio ya ufalme wa Kristo au kuenea kwa Ukweli tunaouchukia. Wasilisha ulimwengu mbele yao katika nuru ya kuvutia mno, ili waupende na kuuabudu na hata kuushabikia. Ni lazima tuweke katika safu yetu njia zote ambazo kwa hizo tunaweza kupata udhibiti. Kadiri wafuasi wa Kristo wanavyokuwa na njia nyingi za kutenga maalum kwa madhumuni ya huduma Yake, ndivyo watakavyoudhuru ufalme wetu kwa kuwapata raia wetu. Kadiri wanavyopanga mikutano katika maeneo mbalimbali, tuko katika hatari. Hivyo kaeni macho sana, mkikesha. Sababisheni ghasia na mkanganyiko ikiwezekana. Haribuni upendo wa mtu kwa mwingine. Wawekeeni vikwazo na kuwavunja mioyo wachungaji wao; kwa maana tunawachukia. Toeni kila hoja ya kukubalika kwa hao wenye mali kuwa udhuru, ili wasije wakaitoa. Dhibitini mambo yahusuyo pesa ikiwa mtaweza, na kuwaweka wachungaji wao katika hali ngumu ya uhaba na dhiki. Hii itapunguza ujasiri na ari yao. Pigana vita katika kila sentimeta ya ardhi. Fanya tamaa na

upendo wa hazina za dunia kuwa sifa bainifu zinazotawala za tabia zao. Maadam sifa hizi zinatawala, wokovu na neema vinarudi nyuma.

Lundika kila vivutio kuwazunguka, nao kwa hakika watakuwa wetu, na si tu kwamba tuna uhakika nao, bali ushawishi wao wa kuchukiza hautatumika kuwaongoza wengine kwenda mbinguni. Na pale yeyote atakapojaribu kutoa, weka ndani yao tabia ya ubahili, uchoyo na kinyongo, ili kwamba utoaji wao uwe mchache (utoaji wa huduma, mali, msamaha upendo nk)." **{EW 266.1}**

Niliona kwamba Shetani anatekeleza mipango yake vizuri. Wakati watumishi wa Mungu wanapopanga mikutano, Shetani na malaika wake wanakuwapo katika uwanja ule kuzuia kazi hiyo. Yeye daima anaweka mapendekezo katika akili za watu wa Mungu. Anawaongoza wengine kwa njia moja na wengine kwa njia nyingine, daima akitumia kwa faida yake zile sifa bainifu mbaya za tabia zilizopo ndani ya ndugu na dada, kusisimua na kuchochea hisia zao za asili. Kama wanataka kuwa wabinafsi na wenye tamaa, Shetani husimama kando yao, na kwa nguvu zake zote anajitahidi kuwaongoza kuendekeza dhambi zao zinazowazonga. Neema ya Mungu na mwanga wa

Ukweli vinaweza kuyeyusha hisia zao za kutamani, na ubinafsi kwa muda kidogo, lakini ikiwa hawatapata ushindi kamili, Shetani huja wakati hawako chini ya uwezo wa kuokoa na kunyausha kila kanuni bora, ya ukarimu, na wanafikiri kwamba mengi sana yanahitajika kutoka kwao. Wanachoka na kunyong'onyea katika kutenda mema na kusahau dhabihu kuu ambayo Yesu aliitoa ili kuwakomboa kutoka katika nguvu za Shetani na kutoka katika taabu isiyo na matumaini. **{EW 267.1}**

Shetani alitumia kwa manufaa yake tabia ile ya tamaa, ubinafsi ya Yuda na kumwongoza kunung'unika wakati ule Mariamu alipomimina juu ya Yesu manukato yale ya gharama kubwa. Yuda aliliona tendo hili kama ufujaji mkubwa, na akatangaza kwamba manukato yale yangeweza kuuzwa na kutolewa kwa maskini. Hakuwajali maskini, lakini aliiona sadaka ile ya ukarimu kwa Yesu ilikuwa ni ubadhirifu. Yuda alimthamini Bwana wake kiasi cha kutosha kumuuza kwa vipande vichache tu vya fedha. Na niliwaona baadhi ya watu waliokiri kuwa wanamngojea Bwana wao. Shetani anawatawala, na wala hawajui. Mungu hawezi kukubali hata kiwango kidogo kabisa cha tamaa au ubinafsi, Naye anachukia maombi na kusihi kwa

wale wanaojiingiza katika hizi sifa bainifu za tabia mbaya. Pale Shetani anapoona kuwa muda wake ni mfupi, huwaongoza watu kuwa wabinafsi na wenye uchoyo na tamaa zaidi na zaidi, na kisha hufurahi kwa kuwaona wakiwa wamejifungia ndani yao wenyewe, wachoyo, bahili, na wabinafsi, na wenye kujipenda. Kama macho ya watu kama hao yangeweza kufunguliwa, wangemwona Shetani akiwa katika shangwe ya ushindi wa kishetani, akiwafurahia na kuucheka upumbavu wa wale wanaokubali mapendekezo yake na kuingia kwenye mitego yake ya hila.**{EW 268.1}**

Shetani na malaika wake wanazingatia matendo yote ya ubahili na ya tamaa ya watu hawa na kuyawasilisha kwa Yesu na malaika Wake watakatifu, wakisema kwa kushutumu, "Hawa ni wafuasi wa Kristo! Wanajiandaa kwa ajili ya kuhamishwa." Shetani analinganisha mwelekeo wao na mafungu ya Maandiko ambayo yanakemea waziwazi na kisha anawadhihaki malaika wa mbinguni, akisema, "Hawa wanamfuata Kristo na Neno Lake! Hawa ndio matunda ya kafara na ukombozi wa Kristo!" Malaika hugeuka kwa kuchukizwa, kutoka katika mandhari hiyo. Mungu anataka utendaji thabiti kwa upande wa watu Wake;

na pale wanapochoka kutenda mema, Yeye naye huwachoka. Niliona kwamba hapendezwi mno na udhihirisho mdogo kabisa wa ubinafsi kwa upande wa wale watu Wake bayana, ambao kwa ajili yao Yesu hakuacha kuyaanganiza maisha Yake ya thamani kubwa. Kila mtu mwenye ubinafsi, na mwenye tamaa ataanguka kando ya njia. Kama Yuda aliyemuuza Bwana wake, watauza kanuni njema na tabia bora ya ukarimu kwa pato dogo tu la dunia. Watu wote wlio kama hao watapepetwa kutoka kwa watu wa Mungu. Wale wanaoitaka mbingu ni lazima, kwa nguvu zote walizonazo, watasisiza kanuni za mbinguni. Badala ya kunyauka kwa ubinafsi, roho zao zinapaswa kuwa zinapanuka kwa ukarimu. Kila fursa inapaswa kutumika vizuri katika kutendeana mema kila mtu na mwenzake na hivyo kuhifadhi kanuni za mbinguni. Yesu aliwasilishwa kwangu kama Mfano mkamilifu. Maisha Yake hayakuwa na masilahi ya ubinafsi, bali daima yalikuwa na ukarimu usiopendelea, ukarimu unaojikana nafsi.**{EW 268.2}**

## Sura ya 62 -Kupepetwa

Niliwaona wengine, wakiwa na imani thabiti na kilio cha maumivu makubwa, wakimsihi Mungu. Nyuso zao zilikuwa zimepauka kwa msongo, na kuashiriwa na mfadhaiko na wasiwasi kubwa, ikielezea mapambano yao ya ndani. Uthabiti na ari kubwa vilioneshwa katika nyuso zao; jasho kubwa lilianguka kutoka kwenye mapaji ya nyuso zao. Mara kwa mara nyuso zao zingeangaza kwa alama za ukubali wa Mungu, na tena sura ile ile ya dhati, ya ari, ya wasiwasi ingekaa juu yao.**{EW 269.1}**

Malaika waovu walisongamana kuzunguka, wakisukumiza giza juu yao ili wamfungie Yesu mbali nje wasiweze kumwona, ili macho yao yaweze kuvutwa na giza lililowazunguka, na kwa hiyo waongozwe katika kutokumwamini Mungu na kunung'unika dhidi Yake. Usalama wao pekee ulikuwa ni katika kukaza macho yao kuelekea juu. Malaika wa Mungu walikuwa na jukumu juu ya watu Wake, na wakati angahewa yenye sumu ya malaika waovu iliposukumizwa karibu na hawa waliofadhaishwa, malaika wa mbinguni walikuwa wakizungusha mabawa yao juu yao kila wakati kulitawanya lile giza nene.**{EW 269.2}**

Wakati waliokuwa wakiomba walipokuwa wakiendelea na vilio vyao vya dhati, mara zingine mwangaza wa nuru kutoka kwa Yesu uliwajia, ili kutia moyo mioyo yao na kumulika nyuso zao. Wengine, niliwaona, hawakuwa wanashiriki katika kazi hii ya kuhisi na kuonesha uchungu na kusihi. Walionekana kuwa wasiojali na wazembe. Hawakuwa wanalipinga giza lililowazunguka, nalo liliwafunga kama wingu zito. Malaika wa Mungu waliwaacha hawa na kwenda kuwasaidia wale walio dhati na bidii kusali. Niliwaona malaika wa Mungu wakifanya haraka kwenda kuwasaidia wote ambao walikuwa wakipambana kwa nguvu zao zote kuwapinga malaika waovu na kujaribu kujisaidia kwa kumwita Mungu kwa uvumilivu. Lakini malaika Wake waliwaacha wale ambao hawakujitahidi kujisaidia, na nilipoteza kuwaona. **{EW 270.1}**

Niliuliza nini maana ya kupepetwa nilikokuona na nilioneshwa kwamba kungesababishwa na ushuhuda usiopinda unaotokana na ushauri wa Shahidi wa Kweli kwa Walaodikia (Straight Testimony). Kuchekechwa huku kungekuwa na matokeo yake katika moyo wa mpokeaji, na kungemwongoza kuinua kiwango na kuutoa kwa wingi Ukweli usiopinda. Wengine hawataubeba

ushuhuda mnyoofu. Watainuka dhidi yake. Na hili ndilo litakalosababisha kuchekechwa miongoni mwa watu wa Mungu.**{EW 270.2}**

Niliona kwamba ushuhuda wa Shahidi wa Kweli haujasikilizwa hata nusu. Ushuhuda mzito ambao hatima ya kanisa inategemea umeheshimiwa kidogo, kama si kupuuzwa kabisa. Ushuhuda huu ni lazima ufanye toba ya kina; wote wanaoupokea kwa Kweli watautii na kutakaswa.**{EW 270.3}**

Malaika yule alisema, “Sikieni!” Punde nilisikia sauti kama ya vyombo vingi vya muziki vyote vikisikika kwa wimbo mkamilifu, mtamu na wenye upatanifu. Ulipita muziki wowote niliowahi kuusikia, ukionekana kujaa rehema, huruma, na wa kuinua furaha takatifu. Nilisisimka nafsi yangu yote, Malaika alisema, "Angalieni!" Shauku yangu iliwageukia kundi lile ambalo nilikuwa nimeliona hapo awali, ambao walitikiswa kwa nguvu. Nilioneshwa wale hapo nyuma nilioneshwa wakilia na kuomba kwa maumivu makubwa ya roho. Kundi la malaika walinzi waliowazunguka waliongezwa maradufu, nao walikuwa wamevaa silaha kutoka vichwani mpaka miguuni. Walitembea kwa utaratibu halisi, kama kundi la askari. Nyuso zao zilionesha vita kali ambayo walikuwa wameivumilia, pambano

kali ambalo walikuwa wamelipitia. Hata hivyo sura zao, zikiashiria maumivu makubwa ya ndani, sasa ziling'aa kwa nuru na utukufu wa mbinguni. Walikuwa wamepata ushindi, nao uliita kutoka ndani yao shukrani ya kina na furaha tukufu, takatifu. **{EW 270.4}**

Idadi ya watu katika kundi hili ilikuwa imepungua. Wengine walikuwa wametikiswa na kuachwa njiani. Wale wazembe na wasiojali, ambao hawakujiunga na wale waliothamini ushindi na wokovu kiasi cha kutosha kuwafanya kusihi kwa uvumilivu na kujitaabisha kwa ajili yake, hawakuupata, na waliachwa nyuma gizani, na nafasi zao zilijazwa mara moja na wengine walioshikilia Ukweli na kujiunga katika safu ya Jeshi la Bwana. Malaika waovu bado walisongamana kuwazunguka, lakini hawakuweza kuwa na nguvu juu yao.**{EW 271.1}**

Niliwasikia wale waliovikwa silaha hizo wakiutangaza Ukweli kwa nguvu nyingi. Ilikuwa na matokeo. Wengi walikuwa wamefungwa; baadhi ya wanawake walifungwa na waume zao, na baadhi ya watoto na wazazi wao. Watu waaminifu ambao walikuwa wamezuiwa kuusikia Ukweli wa sasa waliushikilia kwa shauku. Hofu zote za ndugu na

jamaa zao zilikuwa zimeondoka, na ni Ukweli peke yake uliwafurahisha. Walikuwa wakiona njaa na kiu ya Ukweli; ulikuwa ni wa kupendeza na wa thamani kuliko maisha. Niliuliza ni kitu gani kilichosababisha badiliko hili kubwa. Malaika alijibu, "Ni mvua ya masika, burudisho kutoka uso wa Bwana, kilio kikuu cha malaika wa tatu." **{EW 271.2}**

Nguvu kubwa ilikuwa pamoja na wateule hawa. Malaika alisema, "Angalieni!" Shauku yangu iligeuzwa kwenda kwa waovu, au wasioamini. Wote walikuwa wamesisimkwa. Ari na nguvu wakiyokuwa nayo watu wa Mungu viliwaamsha na kuwakasirisha. Ghasia, ghasia, ilikuwa kila upande. Niliona hatua zikichukuliwa dhidi ya kundi lile lililokuwa na nuru na uweza wa Mungu. Giza lilizidi kuwa nene kuwazunguka; lakini bado walisimama imara, waliokubaliwa na Mungu, na wenye kumtumaini Yeye. Niliwaona wakiwa wamefadhaishwa; kilichofuata ni kuwa, niliwasikia wakimlilia Mungu kwa bidii. Mchana na usiku vilio vyao havikukoma: “Mapenzi Ee Mungu, yatimizwe! Kama itaweza kulikuza Jina Lako Hebu fanya njia ya wokovu kwa watu Wako! Tuokoe na Wapagani waliotuzunguka pande zote. Wametupangia mauti; Laikini mkono Wako unaweza kuleta wokovu.” Haya

ndio maneno ambayo ninaweza kuyaleta akilini. Wote walionekana kuwa na hisia ya kina ya kutokustahili kwao na walionesha kujisalimisha kikamilifu katika mapenzi ya Mungu; lakini bado, kama Yakobo, kila mmoja, bila kukosa, alikuwa akisihi kwa dhati na kupigana mweleka kwa ajili ya ukombozi.**{EW 272.1}**

Mara tu baada ya kuanza kilio chao cha dhati, malaika, kwa huruma, walitamani kwenda kuwakomboa. Lakini malaika mrefu, mwenye kuamuru, hakuwaruhusu. Alisema, "Mapenzi ya Mungu bado hayajatimizwa." Ni lazima wakinywee kikombe kile, Ni lazima wabatizwe kwa ubatizo ule." **{EW 272.2}**

Punde nilisikia sauti ya Mungu ambayo ilitikisa mbingu na nchi. Kulikuwako na tetemeko kubwa la nchi. Majengo yaliangushwa kwa mtikisiko kila upande. Kisha nilisikia kelele za shangwe ya ushindi, sauti kubwa, ya muziki, na dhahiri. Niliangalia kundi hilo, ambalo, muda mfupi uliopita, walikuwa katika dhiki, kifungo na huzuni kubwa kiasi kile. Utumwa wao uligeuzwa. Nuru tukufu iliangaza juu yao. Ni jinsi gani walionekana kuwa wazuri ajabu! Alama zote za masumbufu na uchovu ziliondoka, na afya na uzuri zilionekana katika kila uso. Adui zao,

wapagani waliowazunguka, walianguka kama wafu; hawakuweza kuvumilia nuru iliyowaangazia wale watakatifu, waliokombolewa. Nuru na utukufu huu vilibaki juu yao, hadi pale Yesu alipoonekana katika mawingu ya mbinguni, na kundi hili la waaminifu, waliojaribiwa lilibadilishwa kwa dakika moja, kufumba na kufumbua, kutoka utukufu hadi utukufu. Na makaburi yalifunguliwa, na watakatifu walitoka nje, wamevikwa kutokufa, wakipaza sauti zao, "Ushindi juu ya mauti na kaburi"; nao kwa pamoja na watakatifu walio hai walinyakuliwa kwenda kumlaki Bwana wao hewani, wakati kelele tamu, za muziki wa utukufu na ushindi zilikuwa katika kila ulimi wa asiweza kufa.**{EW 272.3}**

## Sura ya 63-Dhambi za Babeli

Niliona kwamba tangu malaika wa pili alipotangaza kuanguka kwa makanisa, yamekuwa yakiongezeka kuwa machafu, na uovu zaidi na zaidi. Wanabeba jina la kuwa wafuasi wa Kristo; lakini bado haiwezekani kuwatenganisha na ulimwengu. Wachungaji huchukua maandiko yao kutoka katika Neno la Mungu, lakini huhubiri mambo laini. Kwa

hili moyo wa asili hauhisi pingamizi lolote. Ni roho na nguvu ya Ukweli peke yake na wokovu wa Kristo ndivyo vinavyochukiza kwa moyo wa kimwili (moyo wenye tamaa ya kimwili). Hakuna kitu chochote katika huduma maarufu na inayopendwa na watu wengi ambacho kinachochea ghadhabu ya Shetani, ambacho kinamfanya mwenye dhambi atetemeke, au kinatia katika moyo na dhamiri hali halisi ya kuogofya ya hukumu inayokuja hivi karibuni. Watu waovu kwa ujumla wanafurahishwa na mfano wa uchaji usio na utauwa wa Kweli, nao wataisaidia na kuiunga mkono dini kama hiyo.**{EW 273.2}**

Malaika alisema, "Hakuna chochote kilicho pungufu ya silaha zote za haki kinachoweza kumwezesha mwanadamu kuzishinda nguvu za giza na kubakiza ushindi juu yake. Shetani amechukua umiliki kamili wa makanisa kama kundi la jamii ya watu. Kauli na matendo ya wanadamu yanaelezewa sana badala ya Ukweli dhahiri, unaochoma wa Neno la Mungu. Roho na urafiki wa ulimwengu ni uadui kwa Mungu. Wakati Ukweli katika usahili na nguvu Zake, kama ulivyo katika Yesu, unapoletwa kushuhudia dhidi ya roho ya ulimwengu, mara moja huamsha roho ya mateso. Watu wengi wanaokiri kuwa ni Wakristo bado

hawajamjua Mungu. Moyo wa asili haujabadilishwa, na akili ya kimwili inabakia kuwa na uadui na Mungu. Wao ni watumishi waaminifu wa Shetani, licha ya kwamba wamejitwalia jina lingine." **{EW 273.2}**

Niliona kwamba tangu Yesu alipoondoka katika chumba cha Patakatifu pa Patakatifu pa mbinguni na kuingia ndani ya pazia la pili, makanisa yamekuwa yakijazwa na kila ndege mchafu na mwenye kuchukiza. Niliona uovu mkubwa na ubaya katika makanisa; lakini bado washiriki wao wanakiri kuwa ni Wakristo. Maungamo yao, sala zao, na kusihi kwao ni chukizo mbele za Mungu. Malaika yule akasema, "Mungu hatanusa makusanyiko yao. Ubinafsi, ulaghai, na udanganyifu hufanywa nao bila hata, dhamiri kujilaumu au kujikosoa. Na juu ya sifa zote bainifu za uovu wanavaa joho la dini." Nilioneshwa kiburi na fahari ya makanisa yaliyo kwa majina tu. Mungu hayuko katika mawazo yao; akili zao za kimwili hufikiri sana juu yao wenyewe; wanaipamba miili yao yenye kustahili huruma, iliyo masikini na iliyo ya kufa, na kisha hujiangalia kwa kuridhika na kupendezwa. Yesu pamoja na malika wanawaangalia kwa hasira. Malaika yule alisema,

“Dhambi na kiburi chao vimefika mbinguni. Fungu lao limeandaliwa. Haki na hukumu zimesinzia kwa muda mrefu, lakini punde zitaamka. Kisasi ni juu Yangu Mimi; Mimi nitalipa, anena Bwana.” Vitisho vya kuogofya vya malaika wa tatu vitapatikana, na waovu wote watainywa ghadhabu ya Mungu. Kundi lisilohesabika la malaika waovu linaenea juu ya nchi nzima na kujazana na kubanana katika makanisa. Mawakala hawa wa Shetani huziangalia jamii hizi za kidini kwa furaha kubwa, kwa kuwa joho la dini linafunika uhalifu mkubwa na uovu.**{EW 274.1}**

Mbingu yote inawatazama wanadamu kwa hasira, kazi ya mikono ya Mungu, waliopunguzwa hadhi na wanadamu wenzao hadi kufikia kina cha chini kabisa cha kushushwa hadhi na kuwekwa kwenye kiwango sawa na viumbe hayawani, yaani wanyama tu. Wafuasi bayana wanaomkiri kwa mdomo Mwokozi huyo Mpendwa, ambaye siku zote huruma Yake iliguswa kwa kuona shida na huzuni za wanadamu, hawajihusishi kabisa na moyo wote katika dhambi hii kubwa na nzito, na kushughulika na biashara ya watumwa na roho za wanadamu. Maumivu makubwa ya binadamu yanabebwa kutoka sehemu moja hadi nyingine na watu hawa hununuliwa na kuuzwa. Malaika wamerekodi yote

haya; yameandikwa katika kitabu. Machozi ya watumwa wachamungu, wajakazi wachamungu, ya baba, ya mama, na ya watoto, ndugu na dada, yote yamewekwa ndani ya chupa mbinguni. Mungu atazuia hasira Yake kwa kitambo kidogo tu. Hasira Yake itawaka dhidi ya taifa hili na hasa dhidi ya jamii za kidini ambazo zimeidhinisha biashara hii ya usafirishaji huu wa kutisha na wao wenyewe wamejihusisha nao (human trafficking). Udhalimu kama huo, uonevu kama huo, mateso kama hayo, hutazamwa kwa kutokujali kusiko na huruma na wengi walio wafuasi bayana wa Yesu mpole na mnyenyekevu. Na wengi kati ya hao wamiliki wa watumwa, au wapiga debe wa biashara hii, binafsi wanaweza kujipa moyo wa kuridhika, na hisia hizi za kuchukiza na haya maumivu makubwa yasiyoelezeka; lakini bado wanathubutu kumwabudu Mungu. Hii ni dhihaka kuu; Shetani hufurahia jambo hili na kumshutumu Yesu pamoja na malaika Wake kwa kutokupatana huko kwa Waumini, Maandiko, matendo na hisia zao, akisema, kwa shangwe ya kishetani, " Jamani watu kama hao, ndio wafuasi wa Kristo!"**{EW 275.1}**

Hawa wanaodai kuwa Wakristo walisoma juu ya mateso ya wafia dini, na machozi yalitiririka

mashavuni mwao. Na kisha wakashtuka na kushangaa kwamba wanadamu wangeweza kuwa wakatili na wenye ukali kiasi cha kufanya ukatili kama huo kwa wanadamu wenzao. Lakini bado wale wanaofikiri na kusema hivyo wakati huo huo wanawashikilia wanadamu katika utumwa. Na hii si yote; wanakata na kuviachanisha vifungo vya asili na kuwaonea kikatili wanadamu wenzao (Wanatenganisha familia, baba na watoto, na mke, na kuwapeleka kwa mmili wa watumwa mahali pengine mbali). Wanaweza kuwapiga kwa mateso ya kinyama mno kwa ukatili ule ule usiokoma ulioonesha na wafuasi wa dini ya Kirumi na wapagani kwa wafuasi wa Kristo. Malaika alisema, “Watavumilika zaidi wale wapagani na wafuasi wa dini ya Kirumi katika siku ile ya utekelezaji wa hukumu ya Mungu kuliko kwa watu kama hao.” Kilio cha walioonewa kimefika mbinguni, na malaika wanasimama wakishangazwa na mateso yasiyoelezeka, yenye maumivu makali ambayo mwanadamu, aliyeumbwa kwa mfano wa Muumbaji wake, humsababishia mwanadamu mwenzake. Alisema malaika, "Majina ya wadhalimu yameandikwa kwa damu, iliyokatwa kwa mistari kwa mapigo, na kufurika kwa machozi ya maumivu

makali yenye moto, na yanayochoma ya mateso. Hasira ya Mungu haitakoma hadi pale atakapoifanya nchi hii ya nuru kunywa makapi ya kikombe cha ghadhabu Yake, hadi atakapoilipa Babeli maradufu. Mlipeni kama alivyowalipa ninyi; mlipeni maradufu kulingana na kazi yake. Katika kikombe ambacho amekijaza, mjazieni mara mbili.” **{EW 275.2}**

Niliona kwamba bwana wa mtumwa huyo [angalia kiambatisho] atalazimika kujibu kwa ajili ya roho ya mtumwa wake ambaye amemwacha akae katika hali ya ujinga, kutojua na kumshusha hadhi; mmiliki wa mtumwa, amemfanya sijue chochote kuhusu Mungu au Biblia, asiyeogopa chochote isipokuwa mjeledi wa bwana wake, na kushikilia nafasi ya chini kuliko hayawani wa porini. Ila Mungu anafanya jambo jema kabisa kwa ajili yake mtumwa, kile ambacho Mungu Mwenye huruma anaweza kufanya katika hali ambayo mwanadamu ameileta. Anamruhusu kuwa kana kwamba hajawahi kuwapo, kana kwamba hajawahi kuzaliwa, wakati huo bwana anayemiliki mtumwa, ni lazima ayavumilie mapigo saba ya mwisho na kisha aje katika ufufuo wa pili na kuteseka kwa kifo cha pili, kifo ambacho ni cha kutisha mno. Hapo ndipo haki ya Mungu

itakaporidhishwa.**{EW 276.1}**

## Sura ya 64- Kilio Kikuu

Niliwaona malaika wakiharakisha kwenda huku na kule mbinguni, wakishuka duniani, na tena wakipanda mbinguni, wakijiandaa kwa ajili ya kutekeleza tukio fulani muhimu. Kisha nilimwona malaika mwingine mwenye nguvu aliyeagizwa kushuka juu ya nchi, ili apate kuunganisha sauti yake pamoja na malaika yule wa tatu, na kuupa nguvu ujumbe wake. Uwezo mkuu na utukufu vilitolewa kwa malaika huyu, na aliposhuka, dunia iliangazwa kwa utukufu wake. Nuru iliyoambatana na malaika huyu ilipenya kila mahali, alipopiga kelele kwa nguvu (mefafoni), kwa sauti yenye nguvu, “, Umeanguka, umeanguka Babeli ule mkuu; umekuwa maskani ya mashetani, na ngome ya kila roho mchafu, na ngome ya kila ndege mchafu mwenye kuchukiza.” Ujumbe wa kuanguka kwa Babeli, kama ulivyotolewa na malaika wa pili,

unarudiwa, pamoja na kutajwa zaidi kwa ufisadi ambao umekuwa ukiingia makanisani tangu 1844. Kazi ya malaika huyu inakuja kwa wakati unaofaa ili kujiunga katika kazi kubwa ya mwisho ya ujumbe wa malaika wa tatu kadiri inavyoongezeka na kuwa kilio kikuu. Na watu wa Mungu kwa jinsi hiyo wanaandaliwa kusimama katika saa ya majaribu, ambayo watakutana nayo punde. Niliona nuru kuu imekaa juu yao, nao walijiunga katika kutangaza kwa ujasiri ujumbe wa malaika wa tatu.**{EW 277.1}**

Malaika walitumwa kuja kumsaidia malaika yule mwenye nguvu kutoka mbinguni, nami nilisikia sauti ambazo zilielekea kuwa zilisikika kila mahali, "Tokeni kwake, enyi watu Wangu, msishiriki dhambi zake, wala msipokee mapigo yake. Kwa maana dhambi zake zimefika hata mbinguni, na Mungu amekumbuka maovu yake." Ujumbe huu ulionekana kuwa ni nyongeza kwa ujumbe wa tatu, ukiungana nao kama vile kilio cha usiku wa manane kilivyoungana na ujumbe wa malaika wa pili mwaka 1844. Utukufu wa Mungu ulikaa juu ya watakatifu wenye subira, wanaosubiri, na bila woga walitoa onyo zito la mwisho, wakitangaza kuanguka kwa Babeli na kuwaita watu wa Mungu watoke ndani yake ili wapate kuiepuka adhabu yake ya

kutisha.**{EW 277.2}**

Nuru iliyomwagwa juu ya wale waliokuwa wakisubiri ilipenya kila mahali, na wale walio katika makanisa ambao walikuwa na nuru yoyote, ambao hawakuwa wamesikia na kukataa ujumbe malaika hao watatu, waliutii wito ule na kuondoka katika makanisa yale yaliyoanguka. Wengi walikuwa wamekuja kwa miaka mingi ya uwajibikaji tangu ujumbe huu ulipotolewa, na nuru kuwaangazia, na walikuwa na haki ya kuchagua uzima au kifo. Baadhi walichagua uzima na kusimama pamoja na wale waliokuwa wakimtarajia Bwana wao na kutunza amri Zake zote. Ujumbe wa tatu ulipaswa kufanya kazi yake; wote walipaswa kujaribiwa juu yake, na wale walio wa thamani walipaswa kuitwa kutoka kwenye jamii za kidini. Nguvu ya kubidisha iliwagusa waaminifu, wakati huo udhihirisho wa nguvu za Mungu ulileta hofu na kizuizi juu ya jamaa na marafiki zao wasioamini kiasi kwamba hawakuthubutu, wala hawakuwa na nguvu ya, kuwazuia wale ambao walihisi kazi ya Roho wa Mungu juu yao. Wito wa mwisho ulipelekwa hata kwa watumwa maskini, na wacha Mungu miongoni mwao walitoa nyimbo zao za furaha kuu kwa matarajio ya ukombozi wao wa kufurahisha.

Mabwana zao hawakuweza kuwazuia; hofu na mshangao viliwafanya kuwa kimya. Miujiza mikubwa ilifanyika, wagonjwa waliponywa, na ishara na maajabu yaliandamana na waumini. Mungu alikuwa katika kazi hiyo, na kila mtakatifu, bila kuogopa matokeo, alifuata usadikisho wa dhamiri yake mwenyewe na kuungana na wale ambao walikuwa wakishika amri zote za Mungu; na kwa nguvu waliutangaza ujumbe wa Malaika wa tatu. Niliona kwamba ujumbe huu ungefungwa kwa uweza na nguvu unaozidi sana kilio cha usiku wa manane.**{EW 278.1}**

Watumishi wa Mungu, wakiwa wamepewa nguvu kutoka juu na nyuso zao zikiwa zimeangazwa, na kung'aa kwa kujiweka wakfu, walitoka kwenda kuutangaza ujumbe uliotoka mbinguni. Roho ambazo zilitawanyika kotekote katika jamii za kidini ziliitikia wito huo, na roho za thamani ziliharakisha kutoka katika makanisa haya yaliyoangamia, kama Lutu alivyoharakisha kutoka Sodoma kabla ya uharibifu wake. Watu wa Mungu walitiwa nguvu kwa utukufu ule bora ambao ulitulia juu yao kwa wingi na kuwaandaa kwa ajili ya kuvumilia saa ya majaribu. Nilisikia kila mahali umati wa sauti nyingi zikisema,"Hapa ndipo penye

subira ya watakatifu, hao wazishikao amri za Mungu, na imani ya Yesu." **{EW 278.2}**

## Sura ya  -Ujumbe wa Malaika wa Tatu Wafungwa

Nilioneshwa hadi kufikia wakati ujumbe wa malaika wa tatu ulipokuwa unafungwa. Nguvu ya Mungu ilikuwa imekaa juu ya watu Wake; hawa walikuwa wameikamilisha kazi yao na walikuwa tayari kwa ajili ya saa ya kujaribiwa iliyokuwa mbele yao. Walikuwa wamepokea mvua za masika, au za kuburudishwa kutokana na uwepo wa Bwana, na ushuhuda ulio hai ulikuwa umehuishwa. Onyo kuu la mwisho lilikuwa limetangazwa kila mahali, nalo liliwasisimua na kuwakasirisha wakazi wa dunia ambao hawakuweza kuupokea ujumbe huo.**{EW 279.1}**

Niliwaona malaika wakiharakisha kwenda huku na huko mbinguni. Malaika aliye na kidau cha wino wa mwandishi kando yake alirudi kutoka duniani na kumwambia Yesu kwamba kazi Yake imekamilika, na watakatifu walihesabiwa na kutiwa muhuri. Kisha nilimwona Yesu, ambaye alikuwa akihudumu mbele ya sanduku la agano lililokuwa na amri kumi, akikitupa chetezo chini. Aliinua mikono Yake juu na

kusema sauti kubwa, “Imekwisha.” Na jeshi lote la malaika liliweka taji zao wakati Yesu alitoa tangazo kuu, "Mwenye kudhulumu na azidi kudhulumu; na mwenye uchafu na azidi kuwa mchafu; na mwenye haki na azidi kufanya haki; na mtakatifu na azidi kutakaswa."**{EW 279.2}**

Kila kesi imeamuliwa kwa ajili ya uzima au mauti. Wakati Yesu alipokuwa anahudumu katika Patakatifu, hukumu ilikuwa ikiendelea juu ya wafu wenye haki, na kisha juu ya wenye haki walio hai. Kristo alipokea ufalme Wake, baada ya kufanya upatanisho kwa ajili ya watu Wake na kufuta dhambi zao. Raia wa ufalme walikuwa wamekwishateuliwa. Ndoa ya Mwana-Kondoo ilikamilishwa. Na ufalme, na ukuu wa ufalme chini ya mbingu zote, alipewa Yesu pamoja na warithi wa wokovu, na Yesu alikuwa atawale kama Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana.**{EW 280.1}**

Yesu alipokuwa akitoka mahali Patakatifu pa Patakatifu, nilisikia mlio wa njuga juu ya vazi Lake; na alipoondoka, wingu la giza likawafunika wakazi wa dunia. Basi kukawa hakuna mpatanishi, kati ya mwanadamu mwenye hatia na Mungu aliyekosewa. Wakati ule Yesu alipokuwa amesimama kati ya Mungu na mwanadamu mwenye hatia, kizuizi

kilikuwa juu ya watu; lakini alipoondoka kati ya mwanadamu na Baba, kizuizi kiliondolewa na Shetani alikuwa na udhibiti kamili wa wale wasiotubu hatimaye. Haikuwezekana kwa mapigo kumiminwa wakati Yesu alipokuwa anahudumu katika Patakatifu; lakini kazi Yake ilipomalizika, na maombezi yake kufungwa, hakuna kitu cha kuzuia ghadhabu ya Mungu, nayo itaanza kwa ghadhabu juu ya kichwa kisicho na hifadhi cha mwenye dhambi mwenye hatia, ambaye amedharau wokovu na kuchukia karipio. Katika wakati huo wa kuogofya, baada ya mwisho wa upatanishi wa Yesu, watakatifu walikuwa wanaishi mbele za Mungu mtakatifu bila mwombezi. Kila kesi iliamuliwa, kila kito cha thamani kikawa kimehesabiwa. Yesu alikaa kwa muda katika chumba cha nje cha Patakatifu pa mbinguni, na dhambi ambazo ziliungamwa wakati alipokuwa katika Patakatifu pa watakatifu ziliwekwa juu ya Shetani, Mwasisi/mwanzilishi wa dhambi, ambaye lazima apate adhabu ya hizo.**{EW 280.2}**

Kisha nikamwona Yesu akivua mavazi Yake ya ukuhani na kujivika mavazi Yake ya kifalme mno. Juu ya kichwa Chake kulikuwapo mataji mengi, taji ndani ya taji. Akiwa amezungukwa na jeshi la malaika, aliondoka mbinguni. Mapigo yalikuwa

yakianguka juu ya wakazi wa dunia. Baadhi ya watu walikuwa wanamkana Mungu na kumlaani. Wengine walikimbilia kwa watu wa Mungu na kuomba kufundishwa jinsi wanavyoweza kuepuka hukumu Zake. Lakini watakatifu hawakuwa na chochote kwa ajili yao. Chozi la mwisho kwa ajili ya wenye dhambi lilikuwa limemwagika, ombi la mwisho kwa uchungu lilikuwa limetolewa, mzigo wa mwisho ulikuwa umebebwa, onyo la mwisho lilikuwa limetolewa. Sauti tamu ya rehema haikuwapo tena kuwaalika. Wakati ambapo watakatifu, na mbingu yote, walikuwa na shauku kwa ajili ya wokovu wao, hawakuwa na shauku kwa ajili yao wenyewe. Uzima na mauti viliwekwa mbele yao kiume wakafa mapema kabla yake. Wengi walitamani uzima, lakini hawakujitahidi kuupata. Hawakuchagua uzima, na sasa hakukuwa na damu ya upatanisho ya kuwatakasa wenye hatia, hakuna Mwokozi mwenye huruma wa kuwaombea, na kulia, "Mhurumie, mhurumie mtu huyu mwenye dhambi tena kidogo." Mbingu yote waliungana na Yesu, waliposikia Maneno ya kutisha, “Imekwisha kuwa. Imekwisha!” Mpango wa wokovu ulikuwa umetimizwa, lakini wachache walikuwa wamechagua kuukubali. Na wakati pale sauti tamu

ya rehema ilipokuwa inafifia, hofu na ogofyo viliwashika waovu. Kwa udhahiri wa kuogofya walisikia Maneno,"Umechelewa mno! umechelewa mno!” **{EW 281.1}**

Wale ambao hawakuwa wamethamini Neno la Mungu walikuwa wakiharakisha huku na huko, wakitangatanga kutoka bahari hadi bahari, na kutoka kaskazini hadi mashariki, kutafuta Neno la Bwana. Malaika alisema, “Hawatalipata, kuna njaa katika nchi, si njaa ya kukosa chakula, wala kiu ya kukosa maji, bali ni ya kukosa kuyasikia Maneno ya Bwana. Je, ni kitu gani hawatakitoa kwa ajili ya Neno moja tu la ukubali kutoka kwa Mungu! (Amos 8) Lakini hapana, ni lazima waendelee kuwa na njaa na kiu. Siku hadi siku waliudharau wokovu. Wakithamini utajiri wa dunia na anasa za dunia juu kuliko kila hazina au kivutio cha mbinguni. Wamemkataa Yesu na kuwadharau watakatifu Wake. Wakiwa ni wenye uchafu wataendelea kuzidi kuwa wachafu milele.” **{EW 281.2}**

Wengi wa waovu walikasirika sana walipokuwa wanapata athari za mapigo. Ilikuwa ni mandhari ya maumivu makubwa ya kutisha. Wazazi walikuwa wakiwalaumu watoto wao vikali, na watoto walikuwa wakiwalaumu wazazi wao, akina kaka

wanawalaumu dada zao, na akina dada wanawalaumu kaka zao. Vilio vikubwa, na mayowe ya kuomboleza vilisikika kila upande, "Ni wewe ndiye uliyenizuia kupokea Ukweli ambao ungeniokoa kutokana na saa hii ya kuogofya." Watu waliwageukia wachungaji wao kwa chuki kali na kuwalaumu, wakisema, "Hamjatuonya. Mlituambia kwamba ulimwengu wote ulipaswa kuongolewa, na kulia, Amani, amani, ili kutuliza kila hofu iliyoamshwa. Hamkutuambia habari za saa hii; na wale waliotuonya juu ya jambo hili mliwatangaza kuwa ni wazushi, wanafiki na waovu, ambao wangetuangamiza." Lakini niliona kwamba wachungaji wale hawakuepuka ghadhabu ya Mungu. Mateso yao yalikuwa ni makubwa mara kumi zaidi kuliko yale ya watu wao (walei au washiriki).**{EW 282.1}**

## Sura ya 66 -Wakati wa Taabu

Niliwaona watakatifu wakiondoka katika miji na vijiji, na kuungana pamoja katika makundi, na kuishi katika maeneo ya upweke mno. Malaika

waliwapatia chakula na maji, wakati waovu walikuwa wakiteseka na njaa na kiu. Kisha niliwaona watu wakuu duniani, wanashauriana, na Shetani na malaika wake wakijishughulisha kuwazunguka. Niliona maandishi, ambayo nakala zake zilitawanywa katika sehemu mbalimbali za nchi, yakitoa amri kwamba isipokuwa watakatifu wameisalimisha imani yao ya pekee, na kuachana na Sabato, na kuishika siku ya kwanza ya juma, watu walikuwa huru baada ya muda fulani kuwaua. Lakini katika saa hii ya majaribio watakatifu walikuwa kimya na watulivu, wakimtumaini Mungu na kutegemea ahadi Yake kwamba njia ya kuokoka ingetengenezwa kwa ajili yao. Katika baadhi ya maeneo, kabla ya wakati wa amri hiyo kutekelezwa, waovu waliwavamia watakatifu ili wapate kuwaua; lakini malaika wakiwa katika mfano wa askari wa vita wanaoonekana kama wanadamu waliwapigania. Shetani alitamani kuwa na fursa ya kuwaangamiza watakatifu wa Aliye Juu; lakini Yesu aliwaambia malaika Wake wawalinde. Mungu angeheshimiwa kwa kufanya agano na wale ambao walikuwa wameshika sheria Yake, mbele ya wapagani wanaowazunguka; na Yesu angeheshimiwa kwa kuwahamisha, pasipo kuona kifo, waaminifu wale,

wanaosubiri ambao walikuwa wamemtarajia kwa muda mrefu sana.**{EW 282.2}**

Punde niliwaona watakatifu wakiteseka kwa maumivu makubwa ya akili. Walionekana kuwa wamezungukwa na wakazi waovu wa dunia. Kila mwonekano ulikuwa dhidi/kinyume chao. Baadhi yao walianza kuwa na hofu kwamba Mungu hatimaye aliwaacha waangamie mikononi mwa waovu. Lakini kama macho yao yangefunguliwa, wangeliona kuwa walikuwa wamezungukwa na malaika wa Mungu. Kisha umati wa waovu wenye hasira ukaja, na baadaye umati wa malaika waovu, wakiwaharakisha waovu kuwaua watakatifu. Lakini kabla hawajawakaribia watu wa Mungu, waovu hawa ni lazima kwanza walipite kundi hili la malaika watakatifu, wenye nguvu nyingi. Hili lilikuwa haliwezekani. Malaika wa Mungu walikuwa wakiwafanya warudi nyuma na pia kuwafanya malaika waovu ambao waliwasonga na kuwazunguka, warudi nyuma. **{EW 283.1}**

Ilikuwa saa ya maumivu makubwa mno, ya kutisha kwa watakatifu. Mchana na usiku wanamlilia Mungu kwa ajili ya ukombozi. Kwa mwonekano wa nje, hakukuwa na uwezekano wa kuokoka kwao. Waovu walikuwa tayari wameanza

kushinda, wakipiga kelele, "Kwa nini Mungu wako hakuokoi kutoka mikononi mwetu? Kwa nini hampandi juu na kuokoa maisha yenu?” Lakini watakatifu hawakuwasikiliza, Kama Yakobo, walikuwa wakipigana mweleka na Mungu (Mwanzo 32 na 33). Malaika walitamani sana kuwaokoa, lakini ni lazima wasubiri kidogo; watu wa Mungu ni lazima wakinywee kikombe kile na kubatizwa kwa ubatizo ule. Malaika, waaminifu kwa dhamana yao, waliendelea na ulinzi wao. Mungu hataruhusu Jina Lake litukanwe miongoni mwa mataifa. Muda ulikuwa umekaribia wakati ambapo ilibidi adhihirisha uweza Wake mkuu na kwa utukufu awaokoe watakatifu Wake. Kwa ajili ya utukufu wa Jina Lake angemwokoa kila mmoja wa wale ambao walimngoja kwa subira na ambao majina yao yaliandikwa kitabuni.**{EW 283.2}**

Nilielekezwa nyuma katika wakati wa Nuhu. Wakati mvua iliposhuka na gharika ikaja, Nuhu na familia yake walikuwa wamekwisha kuingia ndani ya safina, na Mungu alikuwa amewafungia ndani. Nuhu alikuwa amewaonya kwa uaminifu wakazi wa ulimwengu ule uliotangulia gharika kuu (antedeluvia), wakati huo wakimdhihaki na kumdharau kwa maneno. Na maji yaliposhuka juu

ya nchi, na mmoja baada ya mwingine alikuwa akizama majini, waliiona safina ile, ambayo waliifanyia mizaha sana, ikielea salama juu ya maji salama salimini, ikiwahifadhi Nuhu mwaminifu pamoja na familia yake. Hivyo niliona kwamba watu wa Mungu, ambao walikuwa wameuonya ulimwengu kwa uaminifu kuhusu ghadhabu Yake inayokuja, wangeokolewa. Mungu hangewaruhusu waovu kuwaangamiza wale ambao walikuwa wanatarajia kuhamishwa kwenda mbiguni, na ambao hawakuweza kuinama kwa amri ya mnyama au kupokea alama yake. Niliona kwamba ikiwa waovu wangeruhusiwa kuwaua watakatifu, Shetani na jeshi lake lote ovu, na wote wanaomchukia Mungu, wangeridhika. Na lo, ungekuwa ushindi mkubwa ulioje kwa ukuu wake wa kishetani kuwa na mamlaka, katika pambano la mwisho, juu ya wale ambao walikuwa wamesubiri kwa muda mrefu kumwona Yeye ambaye walimpenda! Wale ambao walikejeli wazo la watakatifu, kupaa juu watashuhudia utunzaji wa Mungu kwa watu wake na kuona ukombozi wao kwa utukufu.**{EW 284.1}**

Watakatifu walipoondoka katika miji na vijiji, walifukuziwa na waovu, ambao walitaka kuwaua. Lakini mapanga yaliyoinuliwa ili kuwaua watu wa

Mungu yalivunjika na kuanguka chini kama majani makavu yasiyo na nguvu. Malaika wa Mungu waliwalinda watakatifu. Walipokuwa wanalia mchana na usiku kwa ajili ya ukombozi, kilio chao kilifika juu mbele za Bwana.**{EW 284.2}**

## Sura ya 67 -Kuokolewa kwa Watakatifu

Ilikuwa usiku wa manane, wakati ambapo Mungu alichagua kuwaokoa watu Wake. Wakati waovu walipokuwa wakiwadhihaki, ghafla jua lilitokea, likiangaza katika nguvu zake, na mwezi ulisimama. Waovu waliiangalia mandhari hiyo kwa mshangao, wakati huo watakatifu walizitazama kwa furaha ya dhati ishara za ukombozi wao. Ishara na maajabu yalifuatana kwa mfululizo wa haraka. Kila kitu kilionekana kuwa kimegeuzwa kutoka katika njia yake ya asili. Mito ilikoma kutiririka. Giza, na mawingu mazito yalitokea na kugongana. Lakini palikuwa na mahali palipo dhahiri ambapo palikuwa na utukufu mtulivu, ambapo kutoka hapo sauti ya Mungu ilisikika kama maji mengi, na kuzitikisa mbingu na nchi. Kulikuwa na tetemeko kubwa la ardhi. Makaburi yalifunguliwa, na wale ambao walikufa katika imani chini ya ujumbe wa malaika

wa tatu, wakiitunza Sabato, walitoka nje kutoka katika vitanda vyao vya mavumbi, wakiwa wametukuzwa, wapate kusikia agano la amani ambalo Mungu angeifanya na wale ambao walikuwa wameishika sheria Yake.**{EW 285.1}**

Mbingu zilifunguka na kufungwa na zilikuwa katika vurugu. Milima ilitikisika kama mwanzi katika upepo, na ikatupa miamba iliyochongoka na rafurafu, pande zote. Bahari ilichemka kama chungu nayo ikarusha mawe juu ya nchi. Na pale Mungu alipotamka siku na saa ya kuja kwa Yesu na kutoa Agano la Milele kwa watu Wake, alisema sentensi moja, na kisha akatua kwa muda, wakati huo Maneno yakivuma kupita juu ya nchi. Israeli wa Mungu walisimama macho yao yakiwa yamekazwa kuelekea juu, wakisikiliza Maneno hayo yakitoka katika kinywa cha Yehova, na kufuliza sauti mithili ya ngurumo ya radi kubwa mno yakipita juu ya nchi. Kulikuwa na kicho cha kuogofya. Mwisho wa kila sentensi watakatifu walipaza sauti, “Utukufu! Haleluya!” Nyuso zao ziliangazwa kwa utukufu wa Mungu; na waling'aa kwa utukufu, kama ile uso wa Musa ulivyong’aa aliposhuka kutoka Sinai. Waovu hawakuweza kuwaangalia kwa sababu ya utukufu ule. Na pale baraka zisizo na mwisho zilipotamkwa

juu ya wale ambao walimheshimu Mungu kwa kuitunza Sabato Yake kuwa takatifu kulitokea kelele kubwa ya shangwe ya ushindi juu ya mnyama na juu ya sanamu yake.**{EW 285.2}**

Ndipo ilipoanza yubile/ Jubilii, wakati ambapo nchi itakapopaswa kupumzika. Nilimwona mtumwa mcha Mungu akiinuka kwa ushindi na shangwe na kuiondoa minyororo iliyomfunga, wakati huo bwana wake aliye mwovu alikuwa amechanganyikiwa na hakujua la kufanya; kwani waovu hawakuweza kuelewa Maneno ya sauti ya Mungu.**{EW 286.1}**

Mara wingu kubwa jeupe lilionekana, ambalo Mwana wa Adamu alikuwa ameketi juu yake. Lilipoonekana kwa mara ya kwanza kwa mbali, wingu hili lilionekana dogo sana. Malaika alisema kwamba lilikuwa ni ishara ya Mwana wa Adamu. Kadiri lilivyoikaribia dunia, tuliweza kuona utukufu na ukuu wa Yesu aliposonga mbele kushinda. Msafara wa malaika watakatifu, wakiwa na taji angavu, zinazometameta juu ya vichwa vyao, walimsindikiza kwenye njia Yake. Hakuna lugha inayoweza kuelezea utukufu wa mandhari ile. Wingu hai la ukuu wa enzi na utukufu usio kifani lilisogea karibu zaidi na zaidi, na tungeweza kuona

wazi nafsi nzuri ya Yesu. Hakuwa amevaa taji ya miiba, bali taji ya utukufu ilikaa juu ya paji Lake takatifu. Juu ya vazi Lake, na juu ya paja Lake, lilikuwa limeandikwa Jina: Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana. Uso Wake uling'aa kama jua la adhuhuri, macho Yake yalikuwa kama mwali wa moto, na miguu Yake ilikuwa na mwonekano wa shaba laini. Sauti Yake ilisikika kama sauti ya vyombo vingi vya muziki. Nchi ilitetemeka mbele Yake, mbingu ziliondoka kama karatasi iliyokunjwa, na kila mlima na kisiwa kilihamishwa kutoka mahali pake. "Na wafalme wa dunia, na wakuu, na majemadari, na matajiri, na wenye nguvu, na kila mtumwa, na mwungwana, wakajificha katika pango na chini ya miamba ya milima, na wakiiambia milima na miamba, Tuangukieni, tusitirini, mbele za uso wake yeye aketiye juu ya kiti cha enzi, na hasira ya Mwana-Kondoo. Kwa maana siku iliyo kuu, ya hasira yao, imekuja; naye ni nani awezaye kusimama?" Wale ambao muda mfupi tu kabla wangewaangamiza watoto waaminifu wa Mungu kutoka duniani, sasa walishuhudia utukufu wa Mungu ambao ulikaa juu yao. Na katikati ya hofu yao yote hii waliisikia sauti za watakatifu, katika nyimbo za furaha, wakisema, "Tazama, huyu Ndiye

Mungu wetu, Ndiye tuliyemngoja atusaidie.” **{EW 286.2}**

Nchi ilitetemeka kwa nguvu wakati ule sauti ya Mwana wa Mungu ilipowaita watakatifu waliolala. Waliuitikia wito ule na kutoka nje wakiwa wamevikwa hali ya kutokufa yenye utukufu, wakipaza sauti iliyosambaa kote kwa muda mrefu, “Ushindi, ushindi, juu ya mauti na kuzimu! U wapi, ewe mauti kushinda kwako, Ewe mauti uchungu wako? " Ndipo watakatifu walio hai na wale waliofufuka walipopaza sauti zao kwa kelele kubwa ya furaha ya ushindi. Miili ile ambayo ilikuwa imeshuka kaburini ikiwa na alama za ugonjwa na kifo iliinuka katika hali ya kutokufa yenye afya na nguvu. Watakatifu walio hai wanabadilishwa kwa dakika moja, kufumba na kufumbua, na kunyakuliwa pamoja na wale waliofufuka, na kwa pamoja wanakutana na Bwana wao hewani. Lo! ni mkutano mkubwa kiasi gani! Marafiki ambao kifo kilikuwa kimewatenganisha waliungana, wasitengane tena kamwe.**{EW 287.1}**

Katika kila upande wa gari hili la wingu kulikuwako na mabawa, na chini yake kulikuwako na magurudumu yaliyo hai; na gari lilipojiviringisha juu, magurudumu yale yalitoa sauti, "Mtakatifu," na

mabawa, yaliposonga, yalitoa sauti, "Mtakatifu," na msafara wa malaika watakatifu kuzunguka wingu lile walipaza sauti, "Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, Bwana Mungu Mwenyezi!" Watakatifu katika wingu wakalia, "Utukufu! Alleluia!" Na gari lilijongea kwenda juu katika Mji Mtakatifu. Kabla ya kuingia mjini, watakatifu walipangwa katika mraba kamili, Yesu akiwa katikati. Alisimama kichwa na mabega juu ya watakatifu na juu ya malaika. Umbo Lake adhimu na uso wa kupendeza viliweza kuonekana kwa wote waliokuwa katika mraba ule. **{EW 287.2}**

## Sura ya 68-Thawabu ya Watakatifu

Kisha niliona idadi kubwa ya malaika wakileta kutoka mjini taji za kupendeza - taji kwa kila mtakatifu, jina lake likiwa limeandikwa juu yake. Yesu alipoagiza apelekewe taji hizo, malaika waliziwasilisha Kwake, na kwa mkono wake wa kulia, Yesu mpendwa aliweka taji juu ya vichwa vya watakatifu. Vivyo hivyo malaika walileta vinubi, na Yesu aliviwasilisha pia kwa watakatifu. Malaika viongozi kwanza walipiga noti, na kisha kila sauti iliinuliwa kwa sifa za furaha, yenye kushuru, na kila mkono ulipita upesi kwa ustadi juu ya nyuzi za

kinubi, ukirindima muziki mtamu katika nyimbo tamu sana na kamilifu. Kisha nilimwona Yesu akiongoza kundi lile lililokombolewa hadi katika lango la mji. Alilishika lango na kulirudisha nyuma kwenye bawaba zake zinazong'aa na kuwaambia mataifa yale ambayo yalikuwa yameushika Ukweli kuingia ndani. Ndani ya mji ule kulikuwa na vitu vyote vya kufurahisha macho kwa kuangalia. Utajiri wa utukufu waliuona kila mahali. Kisha Yesu aliwatazama watakatifu Wake waliokombolewa; nyuso zao ziling'aa kwa utukufu; na alipokaza macho Yake ya upendo kwao, alisema, kwa sauti Yake tamu sana, ya muziki, "Ninaona taabu ya roho yangu, na kuridhika. Utukufu huu mwingi ni kwa ajili yenu kufurahia milele. Huzuni zenu zimekwisha. Hakutakuwapo na kifo tena, wala huzuni, wala kilio, wala hakutakuwa na maumivu tena." Nililiona jeshi la waliokombolewa wakiinama na kuweka taji zao zinazometameta miguuni pa Yesu, na kisha, pale mkono Wake wa kupendeza ulipowainua, waligusa vinubi vyao vya dhahabu na kuijaza mbingu yote kwa muziki wao mtamu sana na nyimbo kwa Mwana-Kondoo. **{EW 288.1}**

Kisha nikamwona Yesu akiwaongoza watu Wake kwenda katika mti wa uzima, na tena tulisikia

sauti Yake ya kupendeza, tamu sana kuliko muziki wowote ambao umewahi kuanguka kwenye sikio la kufa, akisema, "Majani ya mti huu ni kwa ajili ya uponyaji wa mataifa. Kuleni matunda yote." Juu ya mti wa uzima kulikuwako na matunda mazuri mno, ambayo watakatifu wangeweza kuyala kwa uhuru. Katika mji huo kulikuwako na kiti cha enzi kitukufu mno, ambacho kutoka Kwake kulitoka mto safi wa maji ya uzima, safi kama kioo. Kwenye kila upande wa mto huu kulikuwako na mti wa uzima, na kwenye kingo za mto huu kulikuwako na miti mingine mizuri iliyozaa matunda ambayo yaliyofaa kuwa chakula.**{EW 289.1}**

Lugha kwa jumla ni dhaifu mno kuweza kujaribu kuielezea mbingu. Mandhari hii inapoinuliwa mbele yangu, ninajawa na mshangao. Nikiwa nimependezwa mno na fahari kuu na utukufu wa hali ya juu, ninaiweka kalamu chini, na kusema kwa mshangao, “Lo, ni upendo ulioje! ni upendo wa ajabu jinsi gani!” Lugha iliyotukuka mno inashindwa kuelezea utukufu wa mbinguni au kina kisicho na kifani cha upendo wa Mwokozi.**{EW 289.2}**

## Sura ya 69 -Dunia Yaachwa Ukiwa

Shauku yangu tena ilielekezwa duniani. Waovu walikuwa wameangamizwa, na maiti zao zilikuwa zimelala juu yake. Hasira ya Mungu katika mapigo saba ya mwisho ilikuwa ilipatilizwa juu ya wakazi wa dunia, ikiwasababisha kutafuna ndimi zao kutokana na maumivu na kumlaani Mungu. Wachungaji wa uongo walikuwa ni lengo kuu la ghadhabu ya Yehova. Macho yao yalikuwa yameliwa, na hivyo hayakuwepo katika mashimo yake, na ndimi zao vinywani mwao, wakiwa wamesimama kwa miguu yao. Baada ya watakatifu kuokolewa kwa sauti ya Mungu, umati ule wa waovu waligeuza hasira yao juu ya kwa kila mmoja na mwenzake. Dunia ilionekana kuwa imegharikishwa na damu, na maiti zilikuwa kutoka mwisho mmoja hadi mwingine.**{EW 289.3}**

Dunia ilionekana kama jangwa lililotelekezwa. Miji na vijiji, vilivyobomolewa na tetemeko la ardhi, vilikuwa vimekaa mafungu mafungu. Milima ilikuwa imehamishwa kutoka mahali pao, na kuacha mapango makubwa. Miamba yenye kuchongoka na rafurafu, iliyotupwa na bahari, au iliyoraruliwa kutoka katika nchi yenyewe, ilitawanyika kila mahali. Miti mikubwa ilikuwa imeng'olewa na

kutupwatupwa juu ya ardhi. Hapa ndipo patakuwa ni nyumba ya Shetani pamoja na malaika wake waovu kwa muda wa miaka elfu moja. Hapa atafungwa/atawekwa, apate kutangatanga juu na chini katika uso wa dunia uliovunjika vunjika na kuona matokeo ya uasi wake dhidi ya sheria ya Mungu. Kwa miaka elfu moja anaweza kufurahia matunda ya laana ambayo ameisababisha. Akiwa amewekewa mipaka yake duniani tu, hatakuwa na fursa ya kutembelea sayari zingine, kuwajaribu na kuwasumbua wale ambao hawajaanguka. Katika kipindi hiki, Shetani anateseka mno. Tangu kuanguka kwake sifa bainishi za tabia yake mbaya zimekuwa katika utendaji wa mara kwa mara. Lakini wakati huo atanyang'anywa uwezo huu, na kuachwa apate kutafakari juu ya sehemu ambayo ametenda tangu kuanguka kwake, na kutazama mbele kwa kutetemeka na hofu katika mustakabali wa kuogofya siku za usoni, wakati atakapolazimika kuteseka kwa ajili ya uovu wote ambao ameufanya na kuadhibiwa kwa ajili ya dhambi zote ambazo amesababisha kufanywa.**{EW 290.1}**

Nilisikia kelele za shangwe ya ushindi kutoka kwa malaika na kutoka kwa watakatifu waliokombolewa, ambazo zilisikika kama sauti za

vyombo vya muziki elfu kumi, kwa sababu wasingesumbuliwa tena na kujaribiwa na Shetani na kwa sababu wakazi wa malimwengu mengine walikuwa wameokolewa kutokana na uwepo wake na majaribu yake. **{EW 290.2}**

Kisha niliona viti vya enzi, Naye Yesu pamoja watakatifu waliokombolewa waliketi juu yao; nao watakatifu wakatawala kama wafalme na makuhani kwa Mungu. Kristo, kwa kuungana na watu Wake, aliwahukumu wafu waovu, akiyalinganisha matendo yao na kitabu cha sheria, Neno la Mungu, na kuamua kila kesi kulingana na matendo yaliyofanywa katika mwili. Ndipo wakawagawia waovu fungu ambalo ni lazima wapitie, sawasawa na matendo yao; na kama ambavyo imeandikwa mbele ya majina yao katika kitabu cha mauti. Shetani na malaika wake pia walihukumiwa na Yesu na watakatifu. Adhabu ya Shetani ilipaswa kuwa kubwa kuliko ya wale aliowadanganya. Mateso yake yatazidi ya kwao kwa mbali kiasi cha kutoweza kulinganishwa nayo. Baada ya wale wote ambao alikuwa amewadanganya kuangamia, Shetani ilikuwa bado aendelee kuishi na kuteseka kwa muda mrefu zaidi.**{EW 290.3}**

Baada ya hukumu ya wafu waovu kukamilika,

mwishoni mwa miaka elfu moja, Yesu aliondoka mjini, na watakatifu na msafara wa jeshi la malaika walimfuata. Yesu alishuka juu ya mlima mkubwa, ambao mara tu miguu yake ilipougusa, ulivunjika vipande vipande na kuwa uwanda mkubwa. Kisha tuliangalia juu, na kuuona, mji ule mkubwa na mzuri, wenye misingi kumi na miwili, na milango kumi na miwili, kila upande milango mitatu, na malaika akiwa katika kila mlango. Nasi Tulipaza sauti, " Jiji! jiji kuu! Linashuka kutoka kwa Mungu kutoka mbinguni!” Nalo jiji likashuka katika fahari yake yote na utukufu unaong'aa, likakaa katika uwanda mkuu alioutayarisha Yesu kwa ajili yake.**{EW 291.1}**

## Sura ya 70 - Ufufuo wa Pili

Kisha Yesu na msafara wote wa malaika watakatifu, na watakatifu wote waliokombolewa, waliondoka mjini. Malaika walimzunguka Kamanda wao na kumsindikiza alikoelekea, na msafara wa watakatifu waliokombolewa ulifuata. Ndipo, kwa utukufu wa kuogofya na wa kutia hofu, Yesu aliwaita wafu waovu, nao wakatoka nje wakiwa na

miili ile dhaifu, migonjwa, milegevu, iliyoingia kaburini. Ni tamasha kubwa ilioje! Mandhari ya jinsi gani! Wakati wa ufufuo wa kwanza wote walitoka nje wakiwa katika ukamilifu wa mtu asiyeweza kufa; lakini wakati wa huu wa pili alama za laana zinaonekana kwa wote. Wafalme na watu mashuhuri wa dunia, walio maskini na wa hali ya chini, waliosoma na wasio na elimu, walitoka nje pamoja. Wote wanamwona Mwana wa Adamu; na watu wale wale waliomdharau na kumdhihaki, walioweka taji la miiba juu ya paji Lake takatifu, na kumpiga kwa mwanzi, wanamtazama katika fahari Yake yote ya kifalme. Wale waliomtemea mate katika saa ya kujaribiwa Kwake sasa wanageuka wasiyaone macho Yake ya yanyopenya na kutoka katika utukufu wa uso wake. Wale waliopigilia misumari katika mikono na miguu Yake sasa wanaangalia alama za kusulubiwa Kwake. Wale ambao walichoma mkuki ubavuni Mwake wanaona alama za ukatili wao katika mwili Wake. Na wanajua fika kwamba Yeye Ndiye Yule-Yule waliyemsulubisha na kumdhihaki wakati wa maumivu Yake makali ya kufa. Ndipo palizuka kilio kimoja kirefu cha maumivu makali, pale wanapokimbia ili wapate kujificha kutoka katika uso

wa Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana.**{EW 292.1}**

Wote wanatafuta kujificha katika miamba, kujikinga na utukufu wa kutisha wa Yeye ambaye walimdharau hapo awali. Na, wakiwa wameelemewa na kuumizwa na ukuu Wake na utukufu mwingi, wanapaza sauti zao kwa kuptana, na kwa udhahiri wa kutisha wanapaza sauti, "Amebarikiwa Yeye ajaye kwa Jina la Bwana!"**{EW 292.2}**

Kisha Yesu na malaika watakatifu, wakifuatana na watakatifu wote, wanakwenda tena mjini, na maombolezo na vilio vya waovu walioangamia vinaijaza hewa. Kisha nikaona kwamba Shetani tena alianza kazi yake. Alipita kati ya raia wake, na kuwafanya wadhaifu na wanyonge kuwa na nguvu, na kuwaambia kwamba yeye na malaika wake walikuwa na nguvu. Aliwaelekeza kwa mamilioni ya watu ambao walikuwa wamefufuliwa. Kulikuwa na mashujaa na wafalme ambao walikuwa hodari vitani na ambao walikuwa wameshinda falme. Na kulikuwapo na majitu makubwa yenye nguvu na mashujaa watu ambao hawakuwahi kupoteza vita. Kulikuwa na Napoleon mwenye kiburi, mwenye tamaa ya makuu, ambaye mbinu yake ilisababisha

falme kutetemeka. Walisimama pale wanaume wenye kimo kirefu na mwenendo wa kuheshimika, ambao walikuwa wameanguka vitani huku wakiwa na kiu ya kushinda. Wanapotoka makaburini wanarudia mkondo wa mawazo yao pale ulipokomea wakati wa kufa. Wanayo hamu ile ile ya kushinda ambayo ilitawala wakati walipoanguka. Shetani anashauriana na malaika zake, na kisha na wafalme hawa na washindi na watu wenye nguvu. Kisha analiangalia jeshi kubwa, na kuwaambia kwamba kundi lililomo katika mji ni dogo na dhaifu, na kwamba wanaweza kwenda juu na kuuchukua, na kuwatupa nje wakazi wake, na kumiliki utajiri wake na utukufu wao wenyewe.**{EW 293.1}**

Shetani anafanikiwa katika kuwadanganya, na wote mara moja wanaanza kujitayarisha kwa vita. Kuna watu wengi wenye ustadi katika jeshi hilo kubwa, na wanatengeneza kila aina ya vifaa vya vita. Ndipo Shetani akiwa ndiye kiongozi wao, umati huu unasonga mbele. Wafalme na mashujaa wanamfuata Shetani kwa karibu, na umati unafuata katika vikosi. Kila kikosi kina kiongozi wake, na utaratibu unazingatiwa wakati wanapotembea juu ya uso wa dunia uliovunjika-vunjika kwenda kwenye Jiji Takatifu. Yesu anafunga malango ya mji, na

jeshi hili kubwa linauzunguka, na kujiweka katika safu za vita, wakitarajia pambano kali. Yesu na jeshi lote la malaika na wanametameta juu ya vichwa vyao, wanapanda juu ya ukuta wa jiji. Yesu anaongea kwa ukuu, akisema, “Angalieni enyi wenye dhambi, thawabu ya wenye haki! Nanyi angalieni, enyi mliokombolewa Wangu, zawadi ya waovu!” Umati ule mkubwa unawatazama kundi lile lenye utukufu walioko juu ya kuta za mji. Na wanashuhudia fahari ya taji zao zinazometameta na kuona nyuso zao zikimulika kwa utukufu, zikiakisi sura ya Yesu, na kisha wanaona utukufu na ukuu usio na kifani wa Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana, ujasiri wao unatoweka. Wazo la hazina na utukufu ambavyo wamevipoteza linawakumba kwa haraka, nao wanatambua kuwa mshahara wa dhambi ni mauti. Wanawaona watu wa kundi lile takatifu, lenye furaha ambao walikuwa wamewadharau, wakiwa wamevikwa utukufu, heshima, kutokufa, na uzima wa milele, wakati huo wakiwa wako nje ya mji, pamoja kila kitu kibaya cha kuchukiza.**{EW 293.2}**

## Sura ya 71 -Mauti ya Pili

Shetani anakimbia katikati ya wafuasi wake na kujaribu kuchochea umati wa watu wapate kuchukua hatua. Lakini moto kutoka kwa Mungu kutoka mbinguni unanyesha juu yao, na watu mashuhuri, na wakuu, na mashujaa, na waungwana, maskini na wanyonge wote kwa pamoja wanateketezwa. Niliona kwamba baadhi yao waliangamizwa mapema, wakati huo wengine waliteseka kwa muda mrefu zaidi. Waliadhibiwa kulingana na matendo yaliyotendwa katika mwili. Wengine waliungua kwa siku nyingi, na maadamu palikuwapo na sehemu yao ambayo ilikuwa haijateketezwa, dhana ya mateso ilibakia. Malaika alisema, "Funza wao hatakufa, wala moto wao hautazimika maadamu kulikuwako na chembe hata ndogo tu ya kuunguzwa."**{EW 294.1}**

Shetani na malaika wake waliteseka kwa kwa muda mrefu. Shetani hakubeba tu uzito na adhabu ya dhambi zake mwenyewe, bali pia za dhambi za jeshi lililokombolewa, ambazo zilikuwa zimewekwa juu yake; na ni lazima pia ateseke kwa uharibifu wa roho ambao alikuwa amesababisha. Kisha nikaona kwamba Shetani na jeshi lote ovu waliangamizwa, na haki ya Mungu iliridhishwa; na jeshi lote la

malaika, na watakatifu wote waliokombolewa, kwa sauti kuu walisema, "Amina!"**{EW 294.2}**

Malaika akasema, "Shetani ni mzizi, watoto wake ni matawi. Sasa wameteketezwa mzizi na tawi. Sasa wamekufa kifo cha milele. Hawatakuwa na ufufuo kamwe, na Mungu atakuwa na ulimwengu safi, uliotakaswa." Kisha nilitazama na kuona moto ule uliokuwa umewateketeza waovu, ukiunguza takataka na kuitakasa dunia. Tena nilitazama na kuona dunia iliyotakaswa. Hapakuwepo na alama hata moja ya laana. Uso wa dunia uliovunjika, usio sawa sasa ulionekana kama uwanda mpana ulio usawa. Ulimwengu wote wa Mungu ulikuwa ni safi, na pambano kuu lilikuwa limemalizika milele. Popote tulipotazama, kila kitu ambacho macho yetu yalitua juu yake kilikuwa ni kizuri na kitakatifu. Na jeshi lote lililokombolewa, wazee na vijana, wakubwa na wadogo, walitupa taji zao zinazometaneta miguuni pa Mkombozi wao, na kusujudu kwa ibada mbele Yake, na kumwabudu Yeye aishiye milele na milele. Dunia mpya nzuri, pamoja na utukufu wake wote, ilikuwa ni urithi wa milele wa watakatifu. Ufalme na mamlaka, na ukuu wa ufalme chini ya mbingu zote, ulipewa watakatifu wa Aliye Juu, ambao wangeimiliki milele, hata

milele na milele.**{EW 295.1}**

## Kiambatisho

Kurasa 13-20: “*Njozi Yangu ya Kwanza.*”- Hayo ambayo yametolewa katika sura hii yalichapishwa kwa mara ya kwanza na mhariri wa gazeti la *The Day-Star,* Januari 24, 1846, kama “Barua kutoka kwa Dada Harmon” yenye tarehe “Portland, Maine, Desemba 20, 1845.” Kisha yalichapishwa tena mnamo 1846, 1847, na 1851 chini ya kichwa "To The Remnant Scattered Abroad. - Kwa Masalio Waliotawanyika Nje ya Nchi ya Marekani". Kichwa cha sasa kilitolewa mwaka wa 1882 wakati wa kuchapishwa tena kwa Experience and Views - Uzoefu na Maoni.

Maelezo ya kina ya tawasifu kama yalivyochapishwa mwaka 1860 na 1885 yanawasilisha yale yanayoonekana hapa kama maono mawili tofauti. Tazama "Njozi Yangu ya Kwanza" katika *Spiritual Gifts* 2:30-35; *Testimonies for the Church* 1:58-61; na "“Vision of the New Earth,”

katika *Spiritual Gifts*," 2:52-55; *Testimonies* 1, 67-70.**{EW 297.2}**

Kurasa15-20: *Taswira ya Matukio ya Baadaye* -. Mama White alipokuwa akielezea kile ambacho Bwana alikuwa amemfunulia kuhusu matukio ya siku zijazo, alifanya hivyo, nyakati zingine kama mtu anayeshiriki katika matukio haya, kama yalikuwa katika siku zilizopita au zilizopo au za baadaye. Akijibu maswali kuhusu hali yake anapokuwa katika maono, aliandika: **{EW 297.3}**

"Bwana anapoona kuwa inafaa kutoa njozi, ninachukuliwa mbele ya Yesu na malaika, na ninakuwa nimepotea kabisa kwa mambo ya dunia.... Usikivu wangu mara nyingi huelekezwa kwenye matukio yanayoendelea duniani. Wakati mwingine ninapelekwa mbele sana katika siku zijazo na kuoneshwa kile kitakachotendeka. Halafu tena ninaoneshwa mambo kama yalivyotokea katika siku za nyuma."—*Spiritual Gifts* 2:292.**{EW 297.4}**

Ellen White, mwenyewe akiwa ni Mwadventista, aliandika kama mtu aliyepo, ambaye aliona na kusikia kile ambacho bado hakijafanyika; E. G., *Early Writings*: **{EW 297.5}**

"Mara tulisikia sauti ya Mungu kama maji mengi,

ambayo ilitupa siku na saa ya kuja kwa Yesu."- Ukurasa wa 15. **{EW 297.5}**

"Sote pamoja tuliingia ndani ya wingu, tukakaa ndani yake siku saba, tukipanda kwenda katika bahari ya kioo, wakati Yesu alipozileta zile taji, na kuziweka juu ya vichwa vyetu kwa mkono wake wa kuume."- ukurasa wa 16. **{EW 297.7}**

"Sote tulitembea kuingia ndani na tulijisikia kwamba tulikuwa na haki kamili katika jiji." **{EW 297.8}**

"Tuliuona mti wa uzima na kiti cha enzi cha Mungu." **{EW 297.9}**

"Yesu akiwa kiongozi wetu sote, nasi tulishuka kutoka katika mji hadi chini duniani" – Ukurasa wa 17. **{EW 297.10}**

"Tulipokuwa tunakaribia kuingia katika hekalu takatifu..." **{EW 297.11}**

"Mambo ya ajabu niliyoyaona huko siwezi kuyaelezea." – Ukurasa wa 19. **{EW 297.12}**

Baada ya maono, aliweza kukumbuka mengi ya yale ambayo yalikuwa yameoneshwa kwake, lakini yale ambayo yalikuwa ya siri, na yasiyopaswa kufunuliwa, hayo hakuweza kuyakumbuka. Kama

sehemu ya tukio la kile kitakachotendeka wakati watu wa Mungu watakapookolewa (ukurasa wa 285), alisikia ikitangazwa "siku na saa ya kuja kwa Yesu" (ukurasa wa 15; angalia pia ukurasa wa 34). Lakini kuhusu jambo hili baadaye aliandika: **{EW 297.13}**

“Sina maarifa hata kidogo kuhusu wakati ulionenwa kwa sauti ya Mungu. Nalisikia saa ile ikitangazwa, lakini sikuikumbuka saa ile baada ya kutoka katika njozi. Matukio ya kusisimua, yenye maslahi mazito kama haya yalipita mbele yangu, kwa namna ambayo hakuna lugha ambayo inatosha kuyaelezea. Haya yote yalikuwa Ukweli ulio hai kwangu.” - Ellen G. White, *Letter* ya 38, ya mwaka wa 1888, iliyochapishwa katika *Selected Messages* 1, 76. **{EW 298.1}**

Ukweli kwamba alionekana kushiriki katika matukio fulani haukutoa uhakikisho kwamba angekuwa mshiriki wakati matukio hayo yalipotokea. **{EW 298.2}**

Ukurasa wa 17: *Ndugu Fitch na Stockman.*- Katika simulizi ya maono yake ya kwanza, Mama White anawataja “Ndugu Fitch na Stockman” kama watu aliokutana nao na kuongea nao katika

Yerusalemu Mpya. Wote wawili walikuwa ni wachungaji ambao Ellen White alikuwa anawafahamu na ambao walikuwa wameshiriki sana katika kutangaza ujumbe wa Marejeo ya Kristo yaliotarajiwa, lakini ambao walikufa muda mfupi kabla ya kukatishwa tamaa kwa Oktoba 22, 1844. **{EW 298.3}**

Charles Fitch, mchungaji wa Presbyteriani, aliukubali ujumbe wa Marejeo kutokana na kusoma hotuba za William Miller na kupitia kukutana kwake na Josiah Litch. Alijitupa kwa moyo wote katika kutangaza Marejeo yaliyotarajiwa ya Kristo mwishoni mwa kipindi cha miaka 2300, na akawa kiongozi maarufu katika Mwamko wa Marejeo. Katika mwaka wa 1842 alibuni chati ya unabii iliyotumiwa kwa ufanisi na kutajwa katika *Early Writings*, 74. Alikufa zaidi kidogo ya juma moja kabla ya Oktoba 22, 1844. Kifo chake kilitokana na ugonjwa alioambukizwa kutokana na kujiweka hatarini kwa muda mrefu zaidi, kwa kufanya huduma tatu za ubatizo katika siku ya baridi ya majira ya kuchipua. (Angalia *Prophetic Faith of our Fathers*, Vol. 4, 533-545.)**{EW 298.3}**

Levi F. Stockman alikuwa mchungaji kijana wa Methodisti wa jimbo la Maine ambaye katika

mwaka 1842, yeye pamoja na wachungaji wengine Wamethodisti takribani thelathini, waliukubali na kuanza kuuhubiri ujio wa pili wa Kristo. Stockman alikuwa akifanya kazi huko Portland, Maine, ambapo mnamo mwaka wa 1843 afya yake ilidhoofika. Alikufa kwa ugonjwa wa kifua kikuu tarehe 25 Juni 1844. Huyu ndiye Mchungaji ambaye Mama White, alipokuwa msichana, alikwenda kwake kwa ajili ya ushauri pale ambapo katika kuvunjika moyo kwake Mungu alisema naye katika ndoto mbili. (Angalia *Early writings*, Early Writings, 12, 78-81; *Prophetic Faith of our Fathers*, Vol. 4, 780 -782.)**{EW 298.5}**

Ukurasa wa 21: *Kiinimacho* - Ili kuthibitisha upinzani wao, baadhi ya maadui wa awali wa maono walipendekeza kwamba uzoefu wa Ellen White ulileta kupitia kiinimacho, jambo linalojulikana leo kama hiponozi. Hiponozi ni hali inayofanana na usingizi, inayosababishwa na nguvu ya ushauri, mhusika aliyefanyiwa hiponozi huwa katika maelewano na yule anayesababisha hali hiyo na kuwa msikivu kwa kupitiliza kwa mapendekezo yake (kama anayevutwa na sumaku-hyponotism and mesmerism). Hata hivyo, kama Mama White anavyotoa taarifa hapa, wakati daktari wa

kiinimacho alipojaribu kumfanyia hiponozi, hakujiweza mbele yake. **{EW 298.6}**

Ellen White mapema katika uzoefu wake alionywa kuhusu hatari ya hiponozi, na katika miaka ya baadaye, katika matukio kadhaa, alipokea maelekezo kuhusiana nayo. Alionya juu ya hatari kubwa inayoambatana na utendaji wowote ambapo akili moja inaweza kuwa na mamlaka ya kuongoza, kuamuru au kuzuia akili nyingine. (Angalia The Ministry of Healing, 242-244; Medical Ministry, 110-112; , *Patriarchs and Prophets*, 349, 350, 353.) **{EW 298.3}**

Ukurasa wa 33: Waadventista wa Jina - Wale walioungana katika kutoa ujumbe wa malaika wa kwanza na wa pili lakini ambao walikataa ujumbe wa malaika wa tatu pamoja na Ukweli wake wa Sabato, lakini hata hivyo waliendelea kuunga mkono tumaini la Marejeo, wanatajwa na Mama White kama “waadventista wa majina,” au wale “wanaoukataa Ukweli wa sasa” (Ukurasa wa 69), pia “vyama/makundi tofauti vya waumini bayana wa Marejeo” (Ukurasa wa 124). Katika maandiko yetu ya awali watu hawa pia walijulikana kama "Waadventista wa siku ya Kwanza."**{EW 299.1}**

Idadi kubwa ya Wakristo walivunjika moyo katika majira ya kupukutika kwa majani ya 1844 wakati Kristo hakuja kama walivyotarajia. Waadventista waligawanyika katika makundi kadhaa, ambao masalio wake hadi leoni sehemu ya Kanisa la Kikristo la Marejeo, kikundi kidogo, na Waadventista wa Sabato.**{EW 299.2}**

Ni wachache tu miongoni mwa Waadventista walidumisha imani yao juu ya utimilizwaji wa unabii mnamo 1844, lakini wale waliofanya hivyo walisonga mbele katika ujumbe wa malaika wa tatu, na ukiwa na Sabato  Yake ya siku ya Saba. Kuhusu uzoefu katika kipindi hicho kigumu Ellen White baadaye aliandika:**{EW 299.3}**

"Laiti Waadventista, baada ya Sikitiko Kuu mnamo 1844, wangeshikilia imani yao, na kufuata kwa umoja katika majaliwa ya Mungu yaliyokuwa yanafunguliwa, wakipokea ujumbe wa malaika wa tatu na kwa nguvu ya Roho Mtakatifu kuutangaza kwa ulimwengu, wangeuona wokovu wa Mungu, Bwana angetenda kwa nguvu kwa juhudi zao, kazi ingekuwa imekamilika, na Kristo angekuja kabla ya hii, ili kuwapokea watu Wake wapate kupokea thawabu yao.**{EW 299.4}**

“Lakini katika kipindi cha mashaka na kutokuwa na uhakika kilichofuatia Sikitiko lile waumini wengi wa Marejeo walitoa imani yao. Mifarakano na migawanyiko iliingia. Wengi walipinga kwa sauti na kalamu za wale wachache ambao, wakifuata majaliwa ya Mungu, walipokea matengenezo ya Sabato na kuanza kutangaza ujumbe wa malaika wa tatu. Wengi ambao wangepaswa kutumia muda na talanta zao kwa kusudi moja la kutangaza onyo kwa ulimwengu, walijishughulisha na kuupinga Ukweli wa Sabato, na kufuatia hili, kazi ya watetezi wake ilitumika kama kanuni katika kuwajibu wapinzani hawa na kuutetea Ukweli. Hivyo kazi ilicheleweshwa, na ulimwengu uliachwa gizani. Kama jamii yote ya Waadventista ingeunganishwa juu ya amri za Mungu na imani ya Yesu, ni jinsi gani historia yetu ingekuwa tofauti!” — *Selected Messages* 1:68.**{EW 299.5}**

Ukurasa 42-45 *lango Uliofunguliwa na Mlango Uliofungwa.* - Mama White alijadili vuguvugu kuu la Marejeo na Sikitiko la Oktoba 22, 1844, katika *Great Controversy-Pambano Kuu* na kurejelea misimamo iliyochukuliwa mara moja baada ya kuvunjika moyo, anataja juu ya hitimisho lisiloepukika ambalo lililoshikiliwa kwa muda mfupi kwamba "mlango wa

rehema ulifungwa." Lakini kama anavyosema, "nuru iliyo wazi zaidi ilikuja kutokana na uchunguzi wa suala la Patakatifu." Tazama “Utangulizi wa Kihistoria” katika hiki na *The Great Controversy,* 429, na sura yote “In the Holy of Holies - Katika Patakatifu pa Patakatifu,” ukurasa wa 423-432.**{EW 299.6}**

Kuhusu uhusiano wake binafsi na suala hili, aliandika mnamo mwaka 1874 kwamba “kamwe hakuwa amepata maono kwamba hakuna tena wenye dhambi watakaoongoka”. Wala yeye pia kufundisha msimamo huo. "Ilikuwa ni nuru niliyopewa na Mungu," aliandika hivi wakati mwingine, "ambayo ilisahihisha makosa yetu, na kutuwezesha kuona msimamo wa Kweli." (*Selected Messages* 1:74, 63.)**{EW 300.1}**

Kurasa 43, 44, na 86: *Ubishaji Hodi wa Kimiujiza huko New York, na Ubishaji Hodi wa Rochester*. Hapa marejeo yanafanywa Mnamo mwaka 1848 ubishaji hodi wa kimiujiza ulisikika katika nyumba ya familia ya Fox huko Hydesville, jamii iliyo umbali wa takribani maili thelathini na tano mashariki mwa jiji la Rochester, New York. Katika wakati ambapo kulikuwa na dhana mbalimbali kuhusu sababu za ubishaji hodi huu, Ellen White alitangaza, kwa

mamlaka ya maono aliyopewa, kwamba, huu ulikuwa ni udhihirisho wa umizimu, kwamba jambo hili lingekua haraka, na kwa jina la dini lingepata umaarufu na kuwadanganya watu wengi, kujitokeza kuwa kazi bora ya udanganyifu ya Shetani katika siku za mwisho. (Mysterious tappings) **{EW 300.2}**

Ukurasa wa 50: *Wajumbe Wasiokuwa na Ujumbe.* - Maneno haya yanaonekana katika maelezo ya maoni yaliyotolewa kwa Ellen White tarehe 26 Januari 1850. Kwa wakati huu Waadventista wa Sabato hawakuwa na mfumo wa kanisa. Karibu wote walikuwa na hofu kwamba aina yoyote ya mfumo ingeleta urasimu miongoni mwa waumini. Lakini kadiri muda ulivyoendelea, vipengele vya kutokupatana vilianza kuingia kwenye safu. Ujumbe wa maonyo ulitoka kwa Ellen White, na Waadventista wa Sabato waliongozwa hatua kwa hatua kupitisha aina fulani ya mfumo wa kanisa. Matokeo yake, makundi ya waumini yaliunganishwa pamoja kwa karibu zaidi kuliko hapo awali; njia ilibuniwa ya kutoa utambuzi kwa wachungaji ambao walitoa ushahidi kwamba wangeweza kuhubiri ujumbe huo na kuunga mkono kwa maisha yao; na maafikiano yalifanyika kwa ajili ya kuwafukuza wale ambao, chini ya kisingizio cha

kuwasilisha Ukweli, walifundisha makosa. “Angalia Utangulizi wa Kihistoria.” **{EW 300.3}**

Kurasa 61, 62: *Umoja wa Wachungaji.*-Tazama ukurasa wa 50, *Wajumbe wasio na Ujumbe.***{EW 300.4}**

Ukurasa 75: *Wajibu wa kwenda Yerusalemu ya Kale.*-Mama White inarejelea maoni yenye makosa yaliyoshikiliwa na wachache sana wakati ule. Mwaka uliofuata, katika *The Review and Herald*, Oktoba 7, 1851, James White anaandika kuhusu “maoni yanayovuruga mawazo, yasiyo na faida kuhusiana na Yerusalemu ya kale na Wayahudi, n.k., ambayo yameenea kwa wakati wa sasa,” na kuhusu “mawazo ya ajabu ambayo wengine wameyakimbilia, kwamba watakatifu bado hawajaenda Yerusalemu ya zamani. Nk, nk." **{EW 300.5}**

Ukurasa wa 77: Mhariri wa Day-Star. Enoch Jacobs aliishi Cincinnati, Ohio, na kuchapisha gazeti la Day-Star, mojawapo ya majarida ya kwanza yaliyotangaza ujio wa pili wa Kristo. Ilikuwa ni kwa Enoch Jacobs ambako Ellen Harmon mnamo Desemba, 1845, alituma maelezo ya maono yake ya kwanza, akitumaini kumwimarisha. Alikuwa

ameona kwamba alikuwa anayumba katika imani yake katika uongozi wa Mungu, katika uzoefu wa Marejeo. Ilikuwa ni katika Day-Star ambapo mhariri alichapisha maono ya kwanza ya Mama White, katika toleo la Januari 24, 1846. Katika toleo maalum la jarida lake, *The Day-Star Extra*, Februari 7, 1846, makala ya kukumbukwa kuhusu Patakatifu pa mbinguni na utakaso wake, iliyotayarishwa na Hiram Edson, Dk. Hahn, na O.R.L Crozier, ilichapishwa. Iliweka mafundisho ya Maandiko yanayohusiana na huduma ya Kristo katika mahali Patakatifu pa Patakatifu pa mbinguni kuanzia Oktoba 22, 1844. Katika jarida hili pia mnamo Machi 14, 1846, mawasiliano ya pili kutoka kwa kalamu ya Ellen Harmon yalichapishwa. (angalia *Early Writings*, 32-35.) Marejeleo katika aya inayojadiliwa ni maoni ya baadaye yaliyoshikiliwa na Bwana Jacobs na udanganyifu wa umizimu aliouunga mkono.

Ukurasa wa 86: Angalia maoni katika kiambatisho juu ya ukurasa wa 43, 44. **{EW 301.1}**

Ukurasa wa 89: *Thomas Paine*. - Maandishi ya Thomas Paine yalijulikana sana na kusomwa sana nchini Marekani katika miaka ya 1840. Kitabu chake *Age of Reason* = Enzi ya Mantiki kilikuwa ni kazi ya imani ile kwamba Mungu Yupo lakini hakuna

ufunuo ambayo ni Wenye matunda/madhara kwa imani na matendo ya Kikristo. Kitabu hiki kilianza na maneno “Ninamwamini Mungu Mmoja na wala hakuna tena mwingine.” Paine hakumwamini Kristo, na alitumiwa kwa mafanikio na Shetani katika mashambulizi yake juu ya kanisa. Kama Mama White alivyoonesha, ikiwa mtu kama Paine angeweza kuingia mbinguni na kuheshimiwa sana huko, basi mwenye dhambi yeyote, bila matengenezo ya maisha na bila kumwamini Yesu Kristo, basi angeweza kupata haki ya kuingia. Aliufunua uwongo huu kwa lugha ya nguvu na kuonesha kutokuwa na sababu kwa umizimu. **{EW 301.2}**

Ukurasa wa 101: *Ukamilifu*. -Baadhi ya Waadventista wa awali, muda mfupi baada ya uzoefu wa 1844, walipoteza kumshikilia Mungu na kuzama katika ushupavu wa dini. Ellen White aliwakabili watu hawa wenye msimamo mkali na "Bwana asema." Aliwakemea wale waliofundisha hali ya ukamilifu katika mwili na kwa hiyo wasingeweza kutenda dhambi. Kuhusu watu kama hao, baadaye Mama White aliandika, **{EW 301.3}**

“Walishikilia kwamba wale waliotakaswa hawawezi kutenda dhambi. Na hii kwa urahisi

iliongoza katika imani kwamba mapenzi na matamanio ya watakatifu yalikuwa sahihi kila wakati, na kamwe hayako katika hatari ya kuwaongoza katika dhambi. Kwa kupatana na madanganyo haya, walikuwa wakitenda dhambi mbaya mno chini ya vazi la utakaso, na kutokana na ushawishi wao wa kiinimacho udanganyao, walikuwa wakipata nguvu ya ajabu juu ya baadhi ya washirika wao, ambao hawakuona uovu wa nadharia hizi zinazoonekana kuwa nzuri lakini potovu.... **{EW 301.4}**

“Kwa wazi kabisa udanganyifu wa walimu hawa wa uongo ulidhihirishwa mbele yangu, nami niliona maelezo ya kutisha yaliyosimama dhidi yao katika kitabu cha kumbukumbu, na hatia ya kuogofya iliyokuwa juu yao kwa sababu ya kukiri utakatifu kamili wakati matendo yao ya kila siku yalikuwa ni ya kuchukiza mbele za Mungu.”—*Life Sketches, Life Sketches*, 83, 84. **{EW 301.5}**

Kurasa 116 na 117: *Meza ya Bwana*; *Wanawake Kuosha Miguu ya Wanaume, na Busu Takatifu*. - Watangulizi wa Kanisa la Waadventista wa Sabato, baada ya kuukubali Ukweli wa Sabato, walijitahidi

kwa shauku kulifuata Neno la Mungu katika kila hali, na wakati uo huo walikuwa waangalifu kujilinda dhidi ya tafsiri zinazopotosha Ukweli wa Neno na msimamo yoyote ya kuzidi kiasi au ushupavu wa dini. Waliona wazi upendeleo na wajibu wa Meza ya Bwana iliyoanzishwa kwa kanisa na Bwana wetu. Kulikuwapo na maswali kuhusu kuosha miguu na busu takatifu. Katika maono haya Bwana aliweka wazi mambo fulani nyeti ambayo yangeongoza na kulilinda kanisa ambalo lilikuwa ndio linajitokeza.**{EW 302.1}**

Kuhusiana na suala la idadi ya marudio ambayo ibada hii ilipaswa kufuata, Baadhi walisisitiza iwe mara moja kwa mwaka; lakini maagizo yalitolewa kwamba Meza ya Bwana inapaswa kufanywa mara nyingi zaidi. Leo kanisa linafuata mpango wa kuishika ibada hii mara nne kila mwaka. **{EW 302.2}**

Ushauri ulitolewa kuhusu kuosha miguu. Inaonekana kulikuwa na tofauti katika maoni kuhusu utaratibu unaopaswa kufuatwa. Baadhi walitenda pasipo busara na matokeo yalikuwa ni "machafuko." Ushauri ulitolewa kwamba ibada hii ilipaswa kufanywa kwa uangalifu na hadhari, kwa namna ambayo isingeweza kuamsha chuki. Kulikuwa na swali kuhusu usahihi wa wanaume na

wanawake kuoshana miguu. Kuhusu jambo hili Ellen White alileta ushahidi wa maandiko ambao ulionesha kwamba ingekuwa sahihi kwa mwanamke - itakavyoonekana katika hali fulani - kuosha miguu ya mwanaume, lakini alitoa ushauri dhidi ya mwanaume kuosha miguu ya mwanamke. **{EW 302.3}**

Kuhusu busu takatifu, SDA Bible Commentary inasema:**{EW 302.4}**

“Katika Mashariki, kwa namna ya pekee, busu lilikuwa ni njia ya kawaida ya kuonesha upendo na urafiki katika salamu. (Angalia Luka 7:45; Matendo ya Mitume 20:37.) ‘Busu takatifu,’ au ‘busu la upendo’ (1 Petro 5:14), lilikuwa ni ishara ya upendo wa Kikristo. Inaonekana kuwa ilikuja kuwa desturi kwa Wakristo wa awali kubadilishana salamu hii wakati wa Meza ya Bwana (Justin Martyr *First Apology* 65). Maandiko ya baadaye yanaonesha kwamba haikuwa desturi kutoa busu hili takatifu kwa mtu aliye wa jinsia tofauti (*Apostolic Constitutions* II. 57; viii. 11).”—*The S.D.A. Bible Commentary*, 7, 257, 258. **{EW 302.5}**

Ilikuwa ni desturi kati ya Waadventista wa awali walioitunza Sabato kubadilishana busu takatifu

katika ibada hii ya unyenyekevu. Hakuna kumbukumbu lolote lililopo kuhusu kubadilishana busu takatifu kati ya wanaume na wanawake kuwa jambo lisilofaa, lakini kuna wito kwa wote kujiepusha na mwonekano wote wa uovu (Pengine busu hili lilikuwa kama lile la Waethiopia, yaani salam ya kawaida kama kushikana mikono). **{EW 302.6}**

Ukurasa wa 118: Kutengeneza Kelele. — Wavu wa injili huvuta kila aina ya watu kuja kanisani. Kulikuwa na wengine ambao walihisi kwamba uzoefu wao wa kidini haukuwa wa Kweli isipokuwa umeashiriwa na upazaji sauti kwa kelele, kuonesha sifa kwa Mungu, maombi ya sauti kubwa na ya msisimko, na amina hai. Hapa tena kanisa katika uzoefu wake wa awali ambalo lilipewa onyo, na lililohitaji staha na heshima katika kumwabudu Mungu.**{EW 302.7}**

Kurasa za 229-232: *William Miller*. - Kwa kurejelea mwamko mkuu wa marejeo huko Marekani katika miaka ya 1830 na 1840, William Miller anatajwa mara nyingi. Katika kitabu *The Great Controvesy* - Pambano Kuu sura nzima imetengwa kwa ajili ya maisha na huduma ya William Miller chini ya kichwa " An American Reformer -

Mwanamatengenezo wa Marekani" (Kurasa 317-342). William Miller alizaliwa Pittsfield, Massachusetts, mwaka 1782 na kufa akiwa Low Hampton, New York, mwaka 1849. Alipokuwa na umri wa miaka minne alihama pamoja na wazazi wake kwenda huko Low Hampton, New York, karibu na Ziwa Champlain na alikulia kwenye shamba la mpakani. Daima alikuwa ni msomaji mwenye bidii ya mafunzo na makini. Alikuwa kiongozi katika jumuia yake. Mnamo mwaka wa 1816 alianza kujifunza Neno la Mungu kwa uangalifu, na kujifunza kwake kulimwongoza kwenye unabii wa muda mrefu/mkubwa na unabii unaohusiana na ujio wa pili. Alihitimisha kwamba kuja kwa Kristo mara ya pili kulikuwa karibu. Baada ya kuchunguza msimamo wake kwa kipindi cha miaka mingi na kujihakikishia kwamba una uhakika, aliitikia mwanzoni mwa Agosti, 1831, mwaliko wa kuwasilisha hadharani maoni yake kuhusu unabii huo. Kuanzia wakati huo na kuendelea, muda wake mwingi ulitumika katika kuutangaza ujumbe wa Marejeo. Kwa wakati upasao mamia ya wachungaji wengine wa Kiprotestanti walijiunga naye ambao walishiriki katika Mwamko mkuu wa Marejeo wa miaka ya 1840.**{EW 303.1}**

Wakati wa kukatishwa tamaa mnamo Oktoba 22, 1844, Miller alikuwa amechoka sana na kisha alikuwa mgonjwa. Aliwategemea sana washirika wake vijana waliosimama naye katika kutangaza ujumbe wa Marejeo baada ya kuvunjika moyo. Walimwongoza Miller kuukataa Ukweli wa Sabato ulipokuja mbele yake, baada tu ya kukatishwa tamaa (the Great Disappointment) Kwa ajili ya hili, wao na wala si William Miller, watawajibika. Ellen White anaandika kuhusu uzoefu huu katika ukurasa wa 258, na anatuhakikishia kuwa Miller atakuwa miongoni mwa wale watakaoitwa kutoka makaburini mwao kwa sauti ya parapanda ya mwisho (Anaandika kwamba kaburi lake linalindwa na malaika hadi leo!).**{EW 303.2}**

Kurasa 232-240, 254-258: *Ujumbe wa Malaika Watatu wa Ufunuo 14*. - Katika mfululizo wa sura tatu, kuanzia ukurasa wa 232, Ellen White anajadili ujumbe wa malaika wa kwanza, wa pili, na wa tatu. Alikuwa akiwaandikia wale ambao pamoja naye walikuwa wamepitia Mwamko mkuu wa Marejeo na masikitiko ya majira ya kuchipua na ya majani kupukutisha majani, ya mwaka 1844 (Great Awakening). Hakujaribu kuingia katika ufafanuzi wa maagizo haya matatu, bali alichukulia kwamba

wasomaji wake walikuwa na ufahamu kamili wa uzoefu huu. Aliwasilisha kile ambacho kingeleta ujasiri na ufahamu kwa waumini wenzake katika nuru ya uzoefu wao. Lazima tugeukie kitabu chake Pambano Kuu kwa ajili ya maelezo ya kina ya mzigo wa maagizo haya. Ujumbe wa malaika wa kwanza ulitoa onyo la kukaribia kwa saa ya hukumu ya Mungu. The Great Controversy - Pambano Kuu, sura "Heralds of the Morning - Mpiga Mbiu wa Asubuhi," Kurasa 299-316; "An American

Reformer, - Mwanamatengenezo wa Marekani," ukurasa wa 317-342; na "A Great Religious Awakening - Mwamko Mkuu wa Kidini," ukurasa wa 355-374. Kwa uwasilishaji wa ujumbe wa malaika wa pili, angalia sura ""A Warning Rejected, - Onyo Lakataliwa," kuanzia ukurasa wa 375. Masimulizi ya kukatishwa tamaa yanawasilishwa katika sura " "Prophecies Fulfilled - Unabii Watimizwa," Kurasa 391-408; " What is the Sanctuary? - Patakatifu ni Nini?" ukurasa wa 409-422; na "The Holy of Holies - Patakatifu pa Patakatifu," ukurasa wa 423-432. Ujumbe wa malaika wa tatu umetangazwa katika sura ya " God's Law Immutable - Sheria ya Mungu Haibadiliki," ukurasa wa 433-450; na "A Work of Reform - Kazi ya Matengenezo," ukurasa wa 451-

460.**{EW 303.3}**

Ukurasa wa 238: *Mwisho wa Ujumbe wa Malaika wa Pili* - Wakati tunaelewa wazi kwamba ujumbe wa malaika wa kwanza, na wa malaika wa pili, na wa malaika wa tatu, ni ujumbe ambao matumizi yake ni leo, tunatambua pia kwamba katika tangazo lao la kwanza sauti ya ujumbe wa malaika wa kwanza na tamko lake kwamba "saa ya hukumu ya Mungu imekuja" inahusishwa na tangazo la ujio wa Kristo uliotarajiwa katika miaka ya 1830 na mwanzoni mwa miaka ya 1840. Ujumbe wa malaika wa pili ulitangazwa kwa mara ya kwanza mapema katika majira ya joto ya 1844 katika wito kwa waumini wa Marejeo kutoka nje ya makanisa yaliyo kwa majina tu ambayo yalikuwa yamekataa tangazo la ujumbe wa malaika wa kwanza. Na ingawa ni kweli kwamba ujumbe wa malaika wa pili unaendelea kuwa Ukweli wa sasa, kulikuwa na kilele cha kufunga ujumbe wa malaika wa pili mara tu kabla ya Oktoba 22, 1844. Wakati ujumbe wa malaika hawa watatu unapojulikana wazi mbele ya ulimwengu tena kabla ya ujio wa pili wa Kristo, malaika wa Ufunuo 18:1 anajiunga katika tangazo la malaika wa pili katika ujumbe kwamba "Umeanguka Babeli." “Tokeni kwake Enyi watu

Wangu! Angalia sura ya “The last Warning - Onyo la Mwisho” katika The Great Controversy - Pambano Kuu, 603-612.**{EW 304.1}**

Ukurasa wa 254: Angalia maelezo ya kiambatisho kwa ajili kurasa 232-240. **{EW 304.2}**

Ukurasa 276: *Watumwa na Mabwana*. - Kulingana na Ufunuo 6:15, 16 kutakuwa na utumwa wakati wa ujio wa pili wa Kristo. Hapa tunapata maneno "kila mtumwa, na mwungwana." Tamko la Ellen White chini ya majadiliano hayo linaonesha kwamba alioneshwa katika maono mtumwa na bwana wa mtumwa wakati wa ujio wa pili wa Kristo. Katika hili anapatana kikamilifu na Biblia. Yohana na Mama White wote wawili walioneshwa hali ambazo zingekuwepo wakati wa ujio wa pili wa Bwana wetu. Wakati anbapo ni kweli kwamba watumwa weusi nchini Marekani waliachiwa huru kwa tangazo la kuachiwa huru watumwa, ambalo lilianza kutumika miaka sita baada ya taarifa inayojadiliwa hapa kuandikwa, ujumbe huo haukufanywa kuwa batili, kwa kuwa hata leo kuna mamilioni ya wanaume na wanawake ambao wako katika utumwa halisi au ule ulio wa kweli lakini si bayana katika sehemu mbalimbali za ulimwengu. Haiwezekani kupitisha hukumu juu ya unabii wa wakati ujao mpaka

tumefikia wakati wa kutimilizwa kwa unabii huo.**{EW 304.3}**